NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

# BUNGE LA TANZANIA

______

# MAJADILIANO YA BUNGE

______

## MKUTANO WA KUMI NA NNE

## Kikao cha Saba – Tarehe 5 Februari, 2019

*(Bunge lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu.

**NDG. MOSSY LUKUVI – KATIBU MEZANI:**

## HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

**MWENYEKITI:** Hati za Kuwasilisha Mezani, tunaanza na Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, karibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:-**

Taarifa ya Serikali kuhusu Tathmini ya Hali ya Uchumi na Utekelezaji wa Bajeti kwa kipindi cha Julai hadi Desemba, 2018 na Mwelekeo hadi Juni, 2019.

**MHE. DKT. JASMINE T. BUNGA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII:-**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2018.

**MHE. ENG. EDWIN A. NGONYANI (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI:-**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2018.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Katibu, tunaendelea.

**NDG. MOSSY LUKUVI – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu na swali la Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 69

### Miradi ya MIVARF Kuwawezesha Wananchi Kimtaji

**MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH** aliuliza:-

Miradi ya *MIVARF* ina malengo mapana ya kuwaendeleza wakulima wa vijiji kibiashara na kimtaji; na hatua za awali kama vile ujenzi wa barabara za vijijini umekamilika lakini pia masoko ya kuongeza thamani yapo katika hatua za kukamilika:-

Je, ni lini hatua za mwisho za kuwawezesha wananchi kimtaji zitaanza rasmi kwa upande wa Zanzibar?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, VIJANA NA AJIRA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni azma ya Serikali kuhakikisha inaunga mkono juhudi za wananchi kushiriki katika uchumi wa kilimo kwa kusaidia upatikanaji wa mitaji na kuwapatia mafunzo stahiki. Mpango wa Kuwawezesha Wananchi Kimtaji umezingatia hatua zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Mradi wa *MIVARF,* imevijengea uwezo wa kiutawala na kiutendaji Vyama vya Kuweka na Kukopa *(SACCOS)* na vikundi vingine vya uzalishaji Tanzania Bara na Visiwani ili viweze kuratibu na kusimamia kwa ufanisi matumizi ya mitaji yatakayopatikana kupitia mikopo inayotolewa na taasisi za kifedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 3 Novemba, 2017, Ofisi ya Waziri Mkuu, Wizara ya Fedha na Mipango na Benki ya Maendelea ya Kilimo Tanzania *(TADB)* walisaini makubaliano ya uendeshaji wa Mfuko wa Dhamana. Kwa kupitia makubaliano hayo, Serikali tayari imetoa shilingi bilioni 22 kwa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania ili kuanza utekelezaji kwa kushirikisha benki za biashara kufikisha huduma ya mikopo kwa makundi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania walishatangaza utaratibu wa namna benki mbalimbali za biashara zinavyoweza kushiriki katika Mfuko wa Udhamini ambapo Benki za *CRDB, NMB, TPB* na *PBZ* zilionesha nia. Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania ilishakutana na benki zote zilizoonesha nia ya kushiriki katika Mfuko wa Dhamana na kufafanua jinsi Mfuko wa Udhamini unavyofanya kazi. Benki za *NMB* na *TPB* wameshakubaliana na Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania kushiriki katika utoaji wa mikopo kwa vikundi vya wakulima kupitia Mfuko wa Dhamana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa hatua ya mwisho ya kuwawezesha wananchi kimtaji imeshafikiwa baina ya Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania na Benki za *NMB* na *TPB* kama ilivyoelezwa hapo juu, napenda kutoa wito kwa Vyama vya Kuweka na Kukopa *(SACCOS)* na vikundi vingine

vya uwezeshaji Zanzibar kuwasiliana na Benki za *NMB* na *TPB* kwa upande wa Zanzibar ili kupata utaratibu wa kukopa fedha kwa ajili ya shughuli za kilimo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Maida.

**MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza kabisa, niipongeze Serikali kwa juhudi zake katika kuwaendeleza wananchi kiuchumi na niwapongeze pia kwa kutoa shilingi bilioni 22 kwa ajili ya kuendeleza *SACCOS* hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuipongeza Serikali lakini pia ninayo maswali mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri lakini niseme kwamba pamoja na Serikali kuingia mikataba na benki na kufikia uamuzi wa kusaini kwa ajili ya kuwaendeleza wakulima hawa kwa kuwapatia mikopo lakini bado benki za Zanzibar zimekuwa zikisuasua kuhusiana na suala la mikopo hiyo. Je, Serikali iko tayari kuzisimamia benki hizi ili kuweza kufikia utekelezaji ili wananchi hawa waweze kupata mikopo hiyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, nataka kusisitiza tu Serikali kwamba *SACCOS* zetu mara nyingi hazina elimu za kuendeleza biashara zao kimitaji na kimasoko. Kwa hiyo, naiomba Serikali kufika Zanzibar kuwapa elimu wananchi wa Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya maswali hayo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, VIJANA NA AJIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza na swali la kwanza, ni kweli Benki ya Kilimo *(TADB)* ilikwishaingia makubaliano na benki nilizoziainisha pale awali ikiwemo Benki ya Watu ya Zanzibar. Kwa hiyo, rai yangu ni kuziomba taasisi za fedha kwa upande wa Tanzania Visiwani kwa maana ya Zanzibar kuichangamkia fursa hii ili wakulima wengi zaidi wa Zanzibar waweze kunufaika na mikopo inayotolewa na benki hii kwa sababu ipo kwa ajili yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ufupi tu niseme kwamba kwa upande wa Zanzibar tunaendelea pia na hatua za kuviwezesha vikundi hivi. Hivi sasa tayari vikundi kwa maana ya *SACCOS* 231 zimeshafikiwa na tayari zaidi ya shilingi bilioni 24 ziko katika mzunguko kwa ajili ya ukopeshaji. Kwa hiyo, nichukue fursa hii kuziomba na kuzitaka benki za Zanzibar kuchangamkia fursa hii ili wananchi wengi zaidi waweze kunufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye swali la pili kuhusu elimu, katika Programu hii ya *MIVARF,* kabla ya kuanza utoaji wa fedha na uwezeshaji iko *package* ambayo inahusisha masuala ya mafunzo hasa nidhamu ya matumizi ya fedha na utunzaji wa fedha. Kwa hiyo, ombi kuhusu suala la elimu ni kwamba ni sehemu ya mradi huu na imekuwa ikifanyika na ninavyozungumza hivi sasa tayari vikundi 57 vya uzalishaji mali kule Zanzibar wameshapewa elimu ya kutosha juu ya matumizi bora ya fedha na namna ya kukopa.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa *Chief Whip.*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba tu niongeze majibu ya ziada kwenye swali zuri sana la Mheshimiwa Maida na hasa faida ambazo wanaweza wakazipata wenzetu wa upande wa pili wa Muungano yaani kule Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulichokifanya mpaka sasa ni kuhakikisha kwamba Mradi huu wa *MIVARF* unakuwa ni

kielelezo kizuri cha Muungano wetu katika nchi yetu. Kwa sababu inaonekana upande wa pili wa wenzetu bado mikopo hii hawajaifahamu vizuri na bado hawajanufaika nayo, naomba niliahidi Bunge lako Tukufu, tutafanya ushirikiano na mawasiliano ya karibu na Waziri mwenye dhamana ya Vijana na Uwezeshaji kule Zanzibar ajue uwepo wa mikopo hii ili aweze kutusaidia kusimamia na kuhakikisha kwamba wenzetu wa upande wa pili wa Zanzibar na wao wanafaidika na wanajua uwepo wa mikopo hii kupitia benki yao ambayo itawahudumia kupitia Mpango wa *MIVARF.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu. Mheshimiwa Khadija Nassir swali la nyongeza.

**MHE. KHADIJA NASSIR ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniona. Kumekuwa na masharti magumu sana katika kupata mikopo ukizingatia vikundi vya vijana wengi wanakuwa bado hawana zile dhamana ambazo zinahitajika. Serikali inatuambia nini ili na sisi vijana ambao hatukidhi vigezo hivyo tuweze kufaidika na mikopo hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, VIJANA NA AJIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Khadija Nassir Ali, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa namna ambavyo anashughulikia masuala ya vijana na kuwa mstari wa mbele kuwatetea vijana wa Taifa hili la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua kwamba ipo changamoto kubwa sana ya upatikanaji wa mikopo katika kundi hili kubwa la vijana, Serikali kupitia Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na mifuko mbalimbali ya uwezeshaji wananchi kiuchumi, imedhamiria kidhati kabisa kuwasaidia vijana wa Taifa letu kwa kuwakopesha fedha pasipo masharti magumu kama ambavyo wanayapata kupitia taasisi za kifedha. Tunao Mfuko wa Maendeleo ya Vijana ambao mpaka hivi sasa umeshakopesha zaidi ya shilingi bilioni 4.5 katika vikundi 237 vya vijana nchi nzima. Kwa hiyo, ni fursa ambayo vijana wanayo kupitia mfuko huu ambapo wanaweza kukopa bila masharti mengi ambayo yapo katika taasisi nyingine za kifedha. Kwa hiyo, nitoe rai kwa vijana wote nchi nzima ambao wanapenda kufanya shughuli za uzalishaji mali kuutumia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana kwa ajili ya uwezeshaji.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Ofisi ya Rais, TAMISEMI na swali la Mheshimiwa Ignas Aloyce Malocha, Mbunge wa Kwela.

Na. 70

**Kukamilisha Ujenzi wa Kituo cha Afya Ilemba Sumbawanga**

**MHE. IGNAS A. MALOCHA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatoa fedha za kukamilisha ujenzi wa Kituo cha Afya kilichopo Kata ya Ilemba katika Halmashauri ya Sumbawanga?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la

Mheshimiwa Ignas Aloyce Malocha, Mbunge wa Kwela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuboresha huduma za afya katika Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga na Mkoa wa Rukwa kwa ujumla, Serikali inaendelea na ujenzi na ukarabati wa vituo vya afya saba kwa gharama ya shilingi bilioni 3.3 ikiwemo Kituo cha Afya Milepa katika Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga. Vilevile Serikali imeweka kipaumbele cha kujenga hospitali tatu za Halmashauri katika Halmashauri tatu za Wilaya ambazo ni Sumbawanga, Nkasi na Kalambo kwa jumla ya shilingi bilioni 1.5 kila moja na fedha hizo zimepelekwa kwenye Halmashauri husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga ina vituo vya kutolea huduma za afya saba, viwili vikiwa binafsi na vitano vya Serikali vinavyohudumia watu takribani 369,471. Ujenzi wa Kituo cha Afya Ilemba ulianza mwaka 2011 kwa kujenga Jengo la *OPD* na nyumba mbili za watumishi kwa kushirikisha wananchi. Mpaka sasa majengo hayo yamefikia hatua ya upauaji na kiasi cha Sh.82,805,611 ambapo ruzuku kutoka Serikali Kuu ni Sh.54,116,121 na nguvu za wananchi Sh.28,789,490 imetumika. Halmashauri inaelekezwa kuzingatia na kuweka kipaumbele kwenye bajeti kuhusu ukamilishaji wa mradi huo kabla ya kuanzisha miradi mipya.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ignas Malocha, swali la nyongeza.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza kabisa, naipongeza Serikali kwa kutoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa hospitali za wilaya, vilevile upanuzi wa vituo vya afya, tunapongeza sana jitihada hizo za Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pamoja na majibu hayo ninayo maswali mawili ya nyongeza. Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga ni kweli imekuwa ikitenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya Ilemba lakini katika bajeti

zake mfululizo imekuwa ikitenga fedha kwa maana ya kumalizia jengo hilo lakini mfululizo wa miaka karibu minne Serikali haijatoa fedha. Mheshimiwa Waziri atakubaliana na mimi kwamba eneo hilo lina mwingiliano mkubwa sana wa watu kutokana na biashara ya mpunga na samaki na kunakuwa na milipuko mingi ya magonjwa, wananchi wanakufa, wanapata taabu sana. Naomba Serikali sasa itambue kilio hicho iweze kutupatia fedha kumalizia kituo hicho cha afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na ujenzi wa Kituo cha Afya Ilemba, vipo vituo vingine vilishaanza kujengwa katika maeneo ya Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga, Vituo vya Afya vya Muze, Kaoze, Kiteta, Kalambanzite pia zahanati 12 na hii yote inatokana na sera ya kila kata kuwa na kituo cha afya na kila kijiji kuwa na zahanati, jambo ambalo Serikali yenyewe imepanga na tumewahamasisha wananchi. Ni nini kauli ya Serikali katika kukamilisha majengo haya? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya maswali hayo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Ignas Aloyce Malocha, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kujibu, naomba uniruhusu kipekee nimpongeze Mheshimiwa Malocha na wananchi wake wa Jimbo la Kwela kwa jinsi ambavyo wameitikia wito mkubwa wa kuhakikisha kwamba ujenzi unafanyika. Kipekee, naomba nimpongeze hata Mkuu wa Mkoa, nilimuona akishiriki yeye mwenyewe katika kuchimba msingi katika ujenzi wa hospitali ya wilaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo, naomba niendelee kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge, kwanza tunathamini sana jitihada ambazo zinafanywa na yeye binafsi na wananchi wake. Kwa kadri bajeti ya Serikali

inavyoruhusu, maeneo yote ambayo ameyataja, pia hajataja Kituo cha Afya Mpui, naomba nimhakikishie, kwa kadri bajeti itakavyoruhusu hatuwezi tukaacha nguvu za wananchi zikapotea bure. Iko kwenye Ilani yetu ya CCM, tumeahidi, tutatekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hongoli.

**MHE. JORAM I. HONGOLI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Lupembe, Halmashauri ya Wilaya ya Njombe tuliomba fedha kwa ajili ya vituo vya afya hasa ikizingatiwa kwamba hatujapata hata kituo kimoja mpaka leo na tuliomba kwa ajili ya Kituo cha Afya Kichiwa ili kiweze kutoa huduma ya upasuaji lakini pia Kituo cha Afya cha Lupembe ambapo tumejenga huduma ya upasuaji kupitia mapato ya halmashauri na tumejenga jengo dogo la akina mama kupitia mchango wa Mbunge na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wanataka kujua ni lini Serikali italeta hizo fedha kama zilivyopelekwa kwenye halmashauri nyingine na sisi Jimbo la Lupembe tuweze kupata angalau zile shilingi milioni 500 kwa ajili ya kuwa na vituo angalau viwili vitakavyotoka huduma ya upasuaji? Sasa hivi akina mama wanapata shida sana na wanatembea umbali mrefu kwa ajili ya kutafuta huduma hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tumetoka Sumbawanga tumekwenda Lupembe.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli, katika maeneo ambayo hatukujenga kituo cha afya ni pamoja na Jimboni kwake Mheshimiwa kule Lupembe. Mheshimiwa hajataja kuwa miongoni mwa wilaya ambazo zinakwenda kujengewa hospitali za wilaya ni pamoja na wilayani kwake. Pia amewahi kupata fursa ya kuongea na Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana akamuahidi kwamba ikipatikana fursa ya kupata vituo hata viwili au kimoja, hatutasahau kituo chake. Naomba wananchi waendelee kuunga mkono Serikali, tumeahidi, tutatekeleza.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Willy Qambalo.

**MHE. QAMBALO W. QULWI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Wilaya ya Karatu ina zaidi ya umri wa miaka 20 na haina hospitali ya wilaya badala yake wananchi wamekuwa wakipata huduma hiyo katika vituo vya afya binafsi na hata vile vya chini. Tayari kama Halmashauri tumeshatenga eneo la kutosha la kujenga Hospitali ya Wilaya. Je, ni lini Serikali sasa itatenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa hospitali hiyo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri Jafo majibu ya swali hilo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la kaka yangu, Mheshimiwa Mbunge wa Karatu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya ujenzi wa vile Vituo vya Afya 350 ambavyo tunaendelea navyo kama tunavyofahamu mpango wa Serikali katika mwaka huu wa fedha tunajenga hospitali mpya 67. Hata hivyo, mwaka huu wa fedha tena 2019/2020 bajeti tunayoenda nayo tutachukua maelekezo jinsi gani tufanye zile wilaya ambazo hazina hospitali za wilaya twende tukamalize tatizo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu Mkoa wa Arusha tulielekeza nguvu kazi kule maeneo ya Ngorongoro na

Longido hata hivyo katika bajeti ya mwaka huu ambao tunaenda kuipanga, si muda mrefu Aprili, 2019 tuka-*take consideration* ya maeneo hayo. Lengo ni kwamba wananchi wote wapate huduma kama inavyokusudiwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mhehimiwa Jafo. Tunaendelea na Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa Dkt. Shukuru Jumanne Kawambwa, Mbunge wa Bagamoyo sasa aulize swali lake.

Na. 71

**Fedha za Kunusuru Kaya Maskini-Bagamoyo**

**MHE. DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA** aliuliza:-

Vitongoji vingi katika Jimbo la Bagamoyo havijafikiwa na mpango wa *TASAF* wa kunusuru kaya maskini nchini:-

Je, ni lini *TASAF* itaviingiza vitongoji hivyo katika mpango wake wa kunusuru kaya maskini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Manajimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora), naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa, Mbunge wa Jimbo la Bagamoyo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini Wilayani Bagamoyo ulianza mwaka 2013 ambapo vijiji/mitaa 66 vilijumuishwa katika mpango huo. Hadi sasa jumla ya walengwa katika kaya 12,081 wamenufaika na mpango huo. Aidha, jumla ya fedha zilizotumika katika mpango huo ni kama ifuatavyo:-

(a) Uhaulishaji fedha kwa (*conditional cash transfer)* Sh.9,709,631,300.

(b) Miradi ya kutoa ajira za muda 277 yenye thamani ya Sh.3,560,991,100 imetekelezwa.

(c) Vikundi 536 vya kuweka akiba na kuwekeza vyenye jumla ya wanachama 7,591 vimewezeshwa na hadi sasa wanachama wa vikundi hivyo wameweza kuweka akiba ya Sh.27,277,100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Sehemu ya Pili ya Utekelezaji wa Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini Wilayani Bagamoyo inatarajia kuanza kabla ya Juni, 2019 kwa maana ya mwaka huu ambapo jumla ya vijiji na mitaa 44 vitafikiwa. Hivyo, jumla ya vijiji na mitaa 110 katika Wilaya ya Bagamoyo vitakuwa vimenufaika na mpango huo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa.

**MHE. DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri. Pia nichukue fursa hii kumpa pongezi sana kwa namna anavyowajibika tangu amepata nafasi hii, anamsaidia vizuri Mheshimiwa Mkuchika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina swali moja la nyongeza, kwa kutambua kwamba Awamu ya Pili itakapoanza mwezi Juni, 2019 na Wilaya ya Bagamoyo ina majimbo mawili, Chalinze na Bagamoyo, haitoweza kuzifikia kaya zote maskini katika Wilaya ya Bagamoyo kwani ni zaidi ya vijiji na mitaa hii 110. Je, nini tamko la Serikali kuhusu kaya maskini zile ambazo zitakuwa zimeachwa wakati Awamu ya Pili inaanza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Bagamoyo, kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa kwa jinsi ambavyo amekuwa akifuatilia kwa ukaribu sana wananchi wa Jimbo lake la Bagamoyo hususani wale ambao wanaishi katika kaya maskini sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nilieleze Bunge Tukufu kwamba Mpango wetu huu au Mradi wetu huu wa *TASAF* unahudumia na umezingatia sana Muungano kwa maana unahudumia Tanzania Bara na Tanzania Visiwani. Kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi mpaka dakika hii katika Jimbo la Bagamoyo au Wilaya ya Bagamoyo tumeshafikia zaidi ya vijiji 66 awamu ya kwanza na vijiji 44 vitafikiwa katika awamu ya pili hivyo kufanya jumla ya vijiji 110.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema tena kwenye jibu langu la awali kwamba mpaka dakika hii tumeshafikisha asilimia 70 kwa kaya maskini zote nchini tumebakiza asilimia 30. Naomba nimwambie Mheshimiwa Mbunge, Waheshimiwa Wabunge wote na Watanzania wote kwamba katika Sehemu ya Pili ya Mpango wetu ule wa *TASAF* tumehakikisha kwamba tunauboresha zaidi kwa kutumia njia za kielektroniki kwa maana ya *GPS* ili kuweza kuboresha yale madodoso ili kuhakikisha kwamba tunaepuka zile kaya hewa. Vilevile tutafanya uhakiki kuhakikisha kwamba yale madodoso ambayo tumeyaboresha kweli yanafikiwa katika kaya zile maskini ili kila Mtanzania ambaye anaitwa yuko kwenye kaya masikini aweze kunufaika na mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo, naomba niliambie Bunge lako Tukufu kwamba katika asilimia 30 iliyobaki kwa mpango na mradi wetu wa *TASAF* tutahudumia kaya maskini zote Tanzania na tutarudia tena kuhudumia zile kaya zingine za mpango wa kwanza ambazo zilikuwa ni asilimia 70. Kwa hiyo, naomba Watanzania wote wafahamu

kwamba tumeboresha Mpango huu na kuanzisha mfumo wa kielektroniki ili tuweze kuhakikisha tunafikia malengo na wale wote wanaoitwa wako kwenye kaya maskini waweze kunufaika. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shekilindi.

**MHE. SHAABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona. Vitongoji vingi katika Jimbo la Lushoto havijafikiwa na Mpango wa *TASAF* wa kunusuru kaya maskini nchini. Je, ni lini *TASAF* itavifikia vitongoji hivyo katika Mpango wake wa Kunusuru Kaya Maskini nchini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii kujibu swali moja dogo la nyongeza la Mheshimiwa Shekilindi, Mbunge wa Jimbo la Lushoto, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema kwamba Awamu ya Pili ya Mpango na Mradi huu wa *TASAF* tunaanza kuutekeleza Juni, 2019. Nimezungumza hapa kwamba tulikuwa tumebakiza asilimia 30 ya kuhudumia zile kaya maskini sana. Pia nimesema tumeboresha madodoso na tutayafanya kielektroniki na tutahakiki ili kupunguza zile kaya hewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimwambie Mheshimiwa Shekilindi kwamba zile asilimia 30 ambazo nimezisema hapa kwamba zimebaki basi na Jimbo la Lushoto litakuwa mojawapo pamoja na majimbo yote na Watanzania wote ambao wanaishi katika kaya maskini wote tutawafikia. Halmashauri zile 185, vijiji, shehia na mitaa zaidi ya 15,000 vyote tutavifikia. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Naibu Waziri, majimbo yote yatafikiwa, kuna swali lingine bado? Mheshimiwa Mwamoto.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri sana ya Naibu Waziri, pamoja na kazi nzuri inayofanywa na *TASAF,* naomba niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa katika Mpango mzima wa *TASAF,* moja ya kazi kubwa ni kuzisaidia kaya maskini angalau zipate mlo. Hata hivyo, kuna watu ambao walisahaulika hasa wenye ulemavu, sehemu nyingi walikuwa wameachwa. Je, katika huo Mpango ujao, Serikali itakuwa tayari kuzingatia watu wenye ulemavu wote wakiwepo wa Kilolo na sehemu nyingine? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali moja dogo la nyongeza la kaka yangu Mheshimiwa Venance Mwamoto, Mbunge wa Jimbo la Kilolo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza katika kutambua kaya maskini, naomba niliambie Bunge lako Tukufu kwamba tunazingatia vitu vingi wakiwemo na walemavu wenye watoto na wasio na watoto; wazee wenye watoto na wasio na watoto wakiwemo hata na watoto wenyewe ambao pia wote hao tunawapa *category* ya kwamba ni kaya maskini sana. Kwa hiyo, naomba nimwambie Mheshimiwa Mbunge kaka yangu wa Jimbo la Kilolo kwamba walemavu wako katika kundi ambalo tunasema ni kundi la kaya maskini na wenyewe wataangaliwa na kuhudumiwa. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Lubeleje, swali la mwisho la nyongeza.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa niko kwenye Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa na ndiyo tunayekagua miradi hii; na kwa kuwa tulishatoa maelekezo kwa Serikali kwamba wale wote walioandikishwa na kupata msaada wa *TASAF* na siyo kaya maskini wafutwe kwenye orodha lakini mpaka sasa bado wanapata zile fedha. Je, sasa Serikali imeshawafuta wale ambao wana uwezo?

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Lubeleje. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali moja dogo la nyongeza la mzee wangu Mheshimiwa Lubeleje, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama yeye mwenyewe alivyosema ni Mjumbe wa Kamati yetu inayosimamia Utawala pamoja na Serikali za Mitaa na sisi kama Serikali mara nyingi huwa tunazingatia sana ushauri wa Kamati. Naomba nilieleze Bunge lako Tukufu kwamba ni kweli siku za nyuma kulikuwa na makosa ambayo sisi kama Serikali tumeshayarekebisha na ndiyo maana nimesema sasa tunaendelea kuboresha mfumo na tutaanza kutumia mfumo wa kielektroniki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Janeth Maurice Masaburi, Mbunge wa Kuteuliwa uliza swali lako.

Na. 72

**Hitaji la Mafunzo kwa Watumishi wa Umma**

**MHE. JANETH M. MASABURI** aliuliza:-

Kumekuwa na upungufu wa rasilimali watu katika taasisi za umma na baadhi ya watumishi kushindwa kufanya maamuzi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutenga fedha kwa ajili ya mafunzo ndani na nje ya nchi kwa watumishi wa umma ili kuwajengea uwezo na kuleta tija kwa Taifa?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo**.**

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Janeth Maurice Masaburi, Mbunge wa Kuteuliwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa kuwapatia mafunzo watumishi wa umma ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa weledi na ufanisi. Kwa kutambua hilo, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora huandaa sera, kanuni na miongozo inayohusiana na mafunzo katika utumishi wa umma na kufuatilia utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Menejimenti ya Ajira ya mwaka 1999 na marekebisho yake ya mwaka 2008 kifungu 4.8; Sera ya Mafunzo katika Utumishi wa Umma ya mwaka 2013 kifungu 4.2; na Kanuni za Kudumu katika Utumishi wa Umma za mwaka 2009 kifungu G 1 (vifungu vidogo 7, 9, 10 na 11) zinasisitiza kuhusu umuhimu wa kila mwajiri katika utumishi wa umma kuandaa na kutekeleza Mpango wa Mafunzo kwa mujibu wa tathimini ya mahitaji ya mafunzo kwa maana ya (*Training Needs Assessment*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2017/2018 kupitia Wizara, Idara zinazojitegemea pamoja na Wakala, Serikali ilitenga jumla ya Sh.54,470,327,822 kwa ajili ya kugharamia mafunzo ya ndani na nje kwa watumishi wa umma. Aidha, katika mwaka wa fedha 2018/2019, jumla ya Sh.39,839,347,632 zimetengwa kwa ajili hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeimarisha ushirikiano na wadau mbalimbali wa maendeleo hususani Australia, India, Japan, China, Indonesia na Jamhuri ya Korea ambapo katika mwaka ule wa 2016/2017 kupitia wadau hao jumla ya watumishi wa umma 654 walipatiwa mafunzo ya muda mfupi na mrefu katika nchi hizo. Aidha, katika mwaka ule wa 2017/2018, fursa za mafunzo zilizotolewa na washirika hao ziliongezeka hadi kufikia 827. Fursa hizo zimewezesha watumishi wa umma kupata uelewa, ujuzi na maarifa mapya ya kumudu majukumu yao katika kutekeleza malengo ya Taifa. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Janeth Masaburi.

**MHE. JANETH M. MASABURI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, kwa kuwa Serikali ya Awamu ya Tano imefanya mabadiliko makubwa ya kiutendaji kwa watumishi wa umma na ambayo yana mwelekeo wa kuifikisha Tanzania kwenye kipato cha kati ifikapo mwaka 2025. Je, Serikali imejipanga vipi kikanuni kuwa na mfumo endelevu na madhubuti wa uwajibikaji na uwajibishaji kwa awamu zote za utawala zinazofuata? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Serikali haioni umuhimu wa kuajiri vijana waliopo kwenye *private sector* na wale wanaoshi nchi za nje (*Diaspora)* kwa kuwashirikisha pamoja ili tuweze kupata chachu ya maendeleo kwa kutumia ujuzi mbalimbali walionao? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya maswali hayo.

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali madogo mawili ya

nyongeza ya Mbunge wa Kuteuliwa ambaye pia ni wifi yangu Mheshimiwa Janeth Masaburi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza ameulizia kuhusu mfumo. Naomba nimueleze Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kwamba sisi kama Serikali sasa hivi tumejipanga kuboresha mfumo mzuri zaidi tofauti na ule tuliokuwa nao ambao tulikuwa tunatumia *LAWSON version 9* ambapo sasa hivi tuna mfumo mpya wa utumishi pamoja na mishahara. Mfumo huu unatengenezwa na vijana wetu wa Kitazania na wazalendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo huu wa utumishi na mishahara wenyewe utakuwa na uwezo mkubwa sana wa *capture* taasisi zote za umma nchini tofauti na ule ambao tunautumia sasa na ndiyo maana kumekuwa na malalamiko mengi. Mfumo huo tunategemea uanze rasmi Juni, 2019 ambao utahusisha taasisi zote za umma na utaboresha hata mifumo mengine ya utendaji kazi wa mtumishi wa umma mfano *OPRAS*. Kwa maana hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali tumejipanga na mfumo huu ambao utakuwa mpya na uwezo mkubwa utaweza kuhakikisha unapata taarifa za kila mtumishi wa umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili amezungumzia juu ya kuajiri watumishi ambao watatoka katika taasisi binafsi. Naomba nimweleze Mheshimiwa Mbunge kwamba sisi kama Serikali kwa wale wote ambao wanaomba ajira kwa mara ya kwanza hatuna *restriction* yoyote wala hatubagui na huwa tunatoa matangazo ya kazi na sasa hivi tumejiongeza zaidi tunatumia *online* kwa maana ya *Ajira Portal*. Kwa hiyo, mtu yeyote ambaye anataka kuomba kazi Serikalini anakaribishwa mradi sifa, vigezo na mienendo yake na michakato inayotakiwa itafanyika. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Selasini.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mimi niko Kamati ya Utawala, Mheshimiwa

Mzee Mkuchika na Waziri na Naibu Waziri wanafanya kazi na sisi vizuri nawapongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuuliza ni kweli kwamba sasa hivi katika nchi yetu wako watumishi ambao hawatoi maamuzi kwa kisingizio maagizo kutoka juu, tumekuja hapa kwa kazi maalum, ushirikiano hafifu katika Idara mbalimbali na siku za karibuni tumesikia hata vipigo vinatokea maofisini na kadhalika. Pamoja na kazi nzuri ya Mheshimiwa Mzee Mkuchika, Waziri na Naibu wake hivi Serikali inafanya *vetting* kama zamani ili kupata watumishi wanaofaa au mnachukua tu kwa sababu ya ukabila, ya undugu, ya kulipana hisani kwa sababu watu kama hawa wanaaibisha Taifa hili? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali moja dogo la nyongeza la shemeji yangu Mheshimiwa Selasini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naomba niseme tu kwamba Ofisi yangu ndiyo inayoshughulikia pia suala la maadili ya watumishi na viongozi na tumejipanga na linaendelea kufanyika vizuri. Kama tunavyoelewa sasa hivi kwamba utendaji kazi na maadili Serikalini yameongezeka kwa kiwango kikubwa. Ofisi yangu haijasita, bado tunaendelea kulipigania kuhakikisha kwamba wale wote wanaotumia madaraka yao vibaya wanachukuliwa hatua kwa vitendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *vetting,* naomba nilieleze Bunge lako Tukufu kwamba *vetting* ipo na inaendelea. Ndiyo maana katika majibu yangu nilipokuwa namjibu Mheshimiwa Masaburi nilisema wananchi wote wanaruhusiwa kuomba kazi lakini utaratibu na mchakato maalum huwa unafanyika. Kwa maana hiyo, nazungumzia hili katika kusisitiza kwamba watumishi wote wa umma

wanapaswa kuhakikisha wanatii, wanafuata na wanaheshimu miiko yote ya utumishi wa umma. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, napenda kuongezea majibu ya swali la ndugu yangu Mheshimiwa Selasini, Mbunge wa Rombo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya CCM inaajiri watumishi wa umma kwa sifa zilizotangazwa. Hatuajiri kuangalia mkoa, wala ukabila, wala dini, sisi Chama chetu kwenye mambo hayo ya ukabila na dini tumehama huko; sisi tunashughulika na Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine aligusia kwamba wako watu wana kigugumizi kufanya maamuzi. Nataka nimhakikishie Serikali hii ya Awamu ya Tano inafanya maamuzi kwa wakati *(promptly).* Ametoa mfano, ingawa hakutaka kusema, nadhani amerudi nyumbani kwake Moshi kule, watu wamepigana ni kweli, waliohusika tayari tumewachukulia hatua, mmoja hayupo kazini na mwingine anachunguzwa. Hiyo inaonesha namna ni gani Serikali ya CCM inachukua hatua kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, amezungumza suala la *vetting;* huo ni utaratibu wa Serikali. Huwezi ukamteua mtu kufanya kazi ya umma hasa nafasi ya uongozi bila kumfanyia *vetting* lakini wanaofanya *vetting* ni binadamu. Leo Mheshimiwa Selasini anaweza akawa Mbunge mzuri sana siku nyingine akateleza. Sasa husemi kwamba kwa kuwa alikuwa mzuri siku za nyuma aendelee tu. Ndiyo maana mnasikia tunafanya mabadiliko na tunatengua uteuzi. Kwa hiyo, nimhakikishie ndugu yangu Mheshimiwa Selasini tuko pamoja. Nilidhani mwishoni utasema napenda nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali ya CCM kwa hatua mlizochukua Mkoa wa Kilimanjaro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi/ Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Wizara ya Utumishi na Utawala Bora imetuchukulia muda, tunaendelea na Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Abdallah Haji Ali, Mbunge wa Kiwani, sasa aulize swali lake.

Na. 73

**Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Majimbo Zanzibar**

**MHE. ABDALLAH HAJI ALI** aliuliza:-

Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo *(CDCF)* hutolewa kila mwaka kwa Majimbo yote ya Uchaguzi Tanzania lakini fedha hizi zimekuwa zikichelewa sana kutolewa kwa upande wa Zanzibar tofauti na Tanzania Bara:-

Je, ni sababu zipi za msingi zinazofanya fedha za mfuko huo kuchelewa kupelekwa Zanzibar?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Muungano na Mazingira, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, naomba nichukue fursa hii kujibu swali la Mheshimiwa Abdallah Haji Ali, Mbunge wa Kiwani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo ulianzishwa kwa lengo la kuchochea maendeleo ya Majimbo ya Uchaguzi ya Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kutokana na makubaliano hayo, Sheria Na.16 ya mwaka 2009 ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo katika kifungu cha 3 inamtaja Waziri anayehusika na Mfuko huo kuwa ni Waziri anayehusika na masuala ya Serikali za Mitaa.

Aidha, kifungu cha 4(2) cha Sheria kinasema kwamba, kwa upande wa Tanzania Bara ni Waziri anayehusika na Serikali za Mitaa na kwa upande wa Zanzibar ni Waziri anayehusika na masuala ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzia mwaka 2010, Ofisi ya Makamu wa Rais ameratibu na kufuatilia miradi ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo kwa upande wa Zanzibar. Mchanganuo wa mgawanyo wa fedha kwa kila Jimbo kulingana na vigezo vilivyoainishwa vya idadi ya watu katika Jimbo, ukubwa wa eneo na kiwango cha umaskini hufanywa na Ofisi ya Makamu wa Rais na kuwasilishwa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar kwa utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi zinatakiwa kufuata utaratibu wa mgawanyo kama nilivyoeleza. Utaratibu huo ni kama ifuatavyo: Fedha zinatolewa na Wizara ya Fedha na Mipango (SMT), baada ya kutolewa, Ofisi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hufanya mchanganuo wa kila Jimbo, mchanganuo huo huwasilishwa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar ambapo huwasilishwa Wizara ya Fedha na Mipango ya SMZ. Wizara ya Fedha na Mipango ya SMZ ndiyo inayoingiza fedha kwenye akaunti za majimbo ya Zanzibar. Hivyo, ni dhahiri kuwa hatua hizo zinaweza kusababisha ucheleweshaji wa fedha ikilinganishwa na fedha zinazotolewa katika majimbo ya Tanzania Bara. Hata hivyo, jitihada za makusudi zinafanyika ili kuhakikisha fedha hizo zinaingia kwenye akaunti za majimbo ya Zanzibar kwa wakati.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Abdallah Ali Haji.

**MHE. ABDALLAH HAJI ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Niseme tu kwamba urasimu huu kwa kweli umekuwa ukitupa usumbufu mkubwa sana sana kwa majimbo ya Zanzibar. Nilikuwa naomba ikiwa hili suala halipo kisheria bora lifutwe ili na sisi hizi pesa tuzipate kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nina maswali ya nyongeza mawili madogo kabisa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, Mfuko huu wa Maendeleo ya Jimbo umeanzishwa mwaka 2009, takribani sasa ni miaka 10. Majimbo yamekua, watu wameongezeka na mahitaji yameongezeka vilevile lakini kiwango kinachotolewa hadi sasa ni kilekile. Je, Serikali ina mpango gani wa kuuongezea Mfuko huu fedha ili upate uweze wa kuendana na mahitaji ya majimbo yetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kumekuwa na malalamiko kwa utendaji wa baadhi ya Wakurugenzi katika Halmashauri; wanakuwa hawatendi vizuri. Je, Waziri yuko tayari kuzitembelea Halmashauri hususani Halmashauri zetu za Zanzibar kukaa na Wabunge na Wakurugenzi wa Halmashauri ili kulizungumzia au kupeana uzoefu juu ya suala hili ili twende sambamba?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya maswali hayo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hi kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Abdallah Haji, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikiri kabisa kweli kuna ongezeko la watu, mahitaji na vitu vingine lakini nimuahidi tu kwamba kuna haja ya kufanya tathmini ili kubaini hayo ambayo tunayasema sasa. Baada ya tathmini hiyo tutajua nini kifanyike kuhusiana na ongezeko la kiwango kinachotolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, kwa kweli nimshukuru na mimi wakati wowote nitakuwa tayari kwenda Zanzibar na nimuahidi tu kwa sababu nakwenda Zanzibar mara

nyingi, nitakuja tukae nanyi pamoja na Wakurugenzi wote kama ambavyo ameshauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Masoud.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nina swali moja dogo sana kwa Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la msingi lilikuwa kuhusu ucheleweshaji wa fedha za Mfuko huu upande Zanzibar. Nimefuatilia majibu kwa makini sana, Mheshimiwa Naibu Waziri amejaribu kujibu kwa kiasi alichoweza. Kwa kuwa fedha hizi zinatoka kwenye Serikali ya Muungano na inachukua zaidi ya miezi sita, saba au nane, ametoa mlolongo wa taratibu jinsi fedha hizi zinavyokwenda Zanzibar, naomba atuambie mkakati gani wa ziada walio nao kurekebisha utaratibu huu ili kasoro hii iweze kuondoka?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kumjibu Mheshimiwa Masoud swali lake la nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeeleza utaratibu wa kisheria ambao tuna kila sababu ya kuufuata. Kwenye majibu yangu ya msingi nimesema pia kama ziko changamoto zingine za ucheleweshwaji tutafanya kila jitihada tunavyoweza ili fedha hizi zisichelewe. Niwahakikishie tu ndugu zangu na nichukue fursa hii kuipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hususani Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa namna inavyoratibu zoezi hili la kuhakikisha fedha hizi za Mfuko wa Jimbo zinafika kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Wizara ya Madini, Mheshimiwa Maryam Salum Msabaha, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 74

**Wachimbaji Wadogo wadogo Kupoteza Maisha Migodini.**

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA** aliuliza:-

Wachimbaji wadogo wadogo wa madini nchini wamekuwa wakipoteza maisha mara kwa mara kwenye mgodi:-

Je, ni lini Serikali itawapatia zana za kisasa pamoja na elimu ya kutosha wachimbaji hao?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Madini, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Maryam Salum Msabaha, Mbunge wa Viti Maalum; kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha kwamba uchimbaji wa madini nchini unafuata taratibu za usalama, afya na utunzaji wa mazingira, Serikali imeanzisha Tume ya Madini ambayo ina Ofisi za Afisa Madini Wakaazi *(RMO's)* takribani mikoa yote nchini. Vilevile kila eneo lenye shughuli za uchimbaji madini, Wizara imeanzisha Ofisi za Maafisa Migodi Wakaazi kwa lengo la kuimarisha shughuli za utoaji elimu kwa wachimbaji wadogo, ukaguzi wa migodi na ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wachimbaji wengi katika migodi ya wachimbaji wadogo wamekuwa hawazingatii tahadhari za usalama wakati wa shughuli za za uchimbaji. Serikali itazidi kuweka msisitizo kwa wachimbaji wadogo

kuzingatia Sheria ya Madini ya mwaka 2010 na marekebisho yake ya mwaka 2017 na Kanuni zake za Usalama, Afya na Utunzaji wa Mazingira wakati wa uchimbaji. Aidha, Serikali haitasita kuyafunga maeneo yatakayobainika kuwa ni hatarishi na yanakiuka kanuni za usalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Madini ilikuwa ikitoa ruzuku kwa wachimbaji wadogo wa madini. Hata hivyo, ilibainika kuwa baadhi ya wachimbaji waliopatiwa ruzuku walitumia ruzuku hiyo kinyume cha maelekezo na makubaliano. Serikali inaanglia utaratibu mzuri wa kuwasaidia wachimbaji wadogo, ikiwa ni pamoja na kuzishawishi taasisi za fedha kuwakopesha wachimbaji wadogo. Wachimbaji wadogo wanashauriwa kutunza kumbukumbu za uzalishaji na mauzo ya madini ili kuzishawishi taasisi za fedha kuweza kuwakopesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Maryam Msabaha.

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, kwa kuwa wachimbaji wadogo wadogo wanachangia sana pato la Taifa kwa kulipa kodi na Wizara ya Madini kwa kuongeza kukusanya maduhuli. Je, Serikali ina mikakati gani kurudisha maduhuli haya katika Wizara ya Madini ili kutatua changamoto hasa hizi za wachimbaji wadogo wadogo kupata zana za kisasa za uchimbaji ili waweze kuliingizia tena Serikali pato la Taifa?

Mheshimiwa Mwnyekiti, swali la pili, kwa kuwa wale ambao walikopeshwa ruzuku kwenye sekta ya madini kama mikopo na wakaitumia sivyo. Je, Serikali ina mikakati gani kuhakikisha wale waliochukua mikopo ile wanachukuliwa hatua na mikopo ile kurudishwa tena kwa wachimbaji wale wadogo wadogo ili waweze kuendeleza sekta hizo za madini za wachimbaji wadogo wadogo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya maswali hayo ya nyongeza.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Maryam Msabaha, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli wachimbaji wadogo tunawategemea sana katika kukusanya maduhuli. Wachimbaji wakubwa walikuwa wanachangia zaidi ya asilimia 95 za michango yote ambayo ilikuwa inakwenda Serikalini na wachimbaji wadogo walikuwa wanachangia asilimia 4 mpaka 5. Sisi kama Serikali tunatambua umuhimu wa wachimbaji wadogo, tukiwawezesha tutapata maduhuli mengi ya kutosha. Kwa hiyo, sisi kama Serikali tulikuta katika Wizara ya Madini walikuwa tayari wachimbaji wadogo wanapewa ruzuku kutoka Serikalini. Ruzuku ile walipewa wanaostahili na wasiostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Wizara ya Madini tumewafuatilia wale maafisa wote waliokuwa wanawawezesha wachimbaji wadogo wasiostahili kupata ruzuku zile. Tumeshawafuatilia na wengine tumeshawaondoa katika nafasi zao za kazi. Vilevile kwa wale wachimbaji wa madini waliopewa fedha kinyume na taratibu na hawana sifa ya kupewa fedha hizo tumewafikisha katika vyombo vya sheria na sasa hivi kuna kesi zinaendelea ziko chini ya *PCCB* na zingine zimepelekwa Mahakamani. Tunachotaka ni kwamba warudishe fedha hizo na tuangalie namna bora ya kuwawezesha wachimbaji wadogo. Nia yetu kama Serikali tunataka wachimbaji wadogo tuwawezeshe, wawe wengi kwa sababu tunatambua kabisa kwamba tukiwawezesha tutaweza kupata kipato kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais tarehe 22 alikaa na wachimbaji wadogo na walizungumza changamoto zao. Changamoto nyingine ilikuwa ni za kodi ambazo tunawatoza katika uchimbaji huo. Kwa hiyo, hatua tunachukua kuangalia namna ya kuwasaidia wachimbaji hao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali la pili ni kwamba changamoto za wachimbaji zipo na sisi kama Serikali tunaendelea kutoa elimu kuhakikisha kwamba wachimbaji hao wadogo wanapata elimu ya kutosha katika uchimbaji huo na wanatunza kumbukumbu ili wawe na sifa za kupata mikopo katika benki na vyombo mbalimbali ambavyo vinakopesha *(financial institutions)* na sisi kama Serikali tutashawishi vyombo hivyo kuwakopesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Wizara hiyohiyo, Mheshimiwa Agness Mathew Marwa, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake. Kwa niaba yake Mheshimiwa Getere.

Na.75

**Mgodi wa ACACIA Kuwalipa Fidia Wananchi**

**MHE. BONIFACE M. GETERE (K.n.y. MHE. AGNESS M. MARWA)** aliuliza:-

Wananchi wengi walibomolewa nyumba zao na Mgodi wa *ACACIA* uliopo Nyamongo, Mkoani Tarime na wengine hawajalipwa fidia ya maeneo yao mpaka sasa. Aidha, Mgodi huo pia umeanza kuchimba chini ya ardhi ya maeneo ya watu *(underground mining):-*

Je, ni lini Mgodi wa *ACACIA* uliopo Nyamongo utalipa fidia kwa wananchi hao?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Madini, naomba sasa nijibu swali la Mheshimiwa Agness

Mathew Marwa ambalo limeulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Getere, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kusimamia sekta ya madini kwa kuhakikisha uwekezaji unafanyika kwa mujibu wa sheria na taratibu za nchi ikiwemo kuhakikisha kuwa wananchi wanaoishi katika maeneo ambayo miradi na uendelezaji wa migodi inatake kufanyika na kulazimika kupisha maeneo yao wanalipwa fidia stahiki kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi na wanapewa makazi mbadala ambayo yana hali bora kuliko makazi waliyokuwa nayo awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uthaminishaji katika maeneo yanayozunguka Mgodi wa North Mara na ulipaji wa fidia umegawanyika katika awamu nyingi kwa kuzingatia vijiji husika kuridhia. Kijiji cha Nyabirama wakazi wake waliothaminiwa wote walilipwa fedha zao isipokuwa wakazi 138 ambao fidia yao iliyoidhinishwa ya shilingi bilioni 3 waliikataa na hundi zao zilitolewa na mgodi na ziko kwa Mkurugenzi wa Wilaya ya Tarime. Eneo la Kijiji cha Nyabichune lilithaminiwa katika awamu ya 47 lakini wananchi walikataa fidia husika iliyoidhinishwa. Aidha, eneo la Mrwambe lilithaminiwa katika awamu ya 30, 32, 32A na 32B na taarifa yake bado haijaridhiwa na Mthamini Mkuu wa Serikali. Taarifa hiyo ikisharidhiwa itawasilishwa kwa mwekezaji ili aweze kufidia wahusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kijiji cha Nyamichele ambacho nacho kina waathirika ambao wanatakiwa kufidiwa kuna changamoto ya uwepo wa taarifa mbili tofauti za uthaminishaji. Katika kutafuta ufumbuzi wa changamoto hiyo, Wizara ya Madini kwa kushirikiana na uongozi wa Mkoa wa Mara tumekubaliana ifanyike tathmini mpya katika eneo hilo. Pia uthaminishaji utafanyika katika eneo tengefu la mita 200 *(buffer zone 200 meters)* lililotengwa kwa ajili ya uhifadhi wa maji ya kemikali na mabaki yanayotokana na shughuli ya uchenjuaji wa madini unaofanyika mgodini hapo. Kazi hii ikikamilika wahusika watalipwa stahiki zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na suala la mgodi kubadilisha aina ya uchimbaji kutoka uchimbaji wa wazi *(open pit)* kwenda kwenye uchimbaji wa chini *(underground mining),* uamuzi huo ulifanyika baada ya mgodi kufanya utafiti uliioonesha kuwa ilikuwa ni rahisi kutumia njia hiyo badala ya kuendelea na mgodi wa wazi. Niwatoe shaka wananchi wa Tarime kuwa Wizara yangu inafuatilia kwa karibu uchimbaji wa *underground* unaofanyika hivi leo. Uchimbaji huo unafanyika katika eneo la Gokona kuelekea Nyabigena ndani ya maeneo yao ya zamani ambayo walikuwa wameshachimba toka awali. Hivyo, hakuna eneo ambalo mgodi wa *underground* unachimba kwenye makazi ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwita Getere.

**MHE. BONIFACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeze tu Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri ya Serikali kwa jinsi wanavyoshughulikia suala hili katika Mgodi ule wa *ACACIA* Nyamongo kule. Nina maswali mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa tatizo la fidia katika eneo la Nyamongo limekuwa la muda mrefu; na ni miaka mingi kila siku watu wanadai na wengine wanadai malipo hewa na wengine malipo halali: Ni lini sasa Serikali itamaliza hili tatizo kwa muda muafaka ili kutufa kabisa tatizo la kudai madai ya Nyamongo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, matatizo yanayotokea Nyamongo, yanafanana sana na matatizo yanayotokea katika kijiji changu cha Nyabuzume Jimbo la Bunda Kata ya Nyamang'uta; na kwa bahati nzuri Mheshimiwa Naibu Waziri wewe ulifika kenye kile kijiji, kuna

wachimbaji wako pale, wanapiga yowe za muda mrefu, wanasumbua wananchi na hawawezi kushirikiana nao katika kupeana zile kazi za kijiji; nawe uliahidi kumaliza hilo tatizo. Ni lini tatizo la Nyabuzume wale wachimbaji wasio halali au walio halali ambao hawatekelezi suala la kuondoa matatizo ya wanakijiji katika kijiji kile? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa maswali hayo.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali ya nyongeza Mheshimiwa Getere, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa madai ya Nyamongo kule *North Mara* katika ile kampuni ya *Acacia* yamechukua muda mrefu. Yamechukua muda mrefu kwa sababu mbili. Sababu ya kwanza ni kampuni yenyewe ya *Acacia* ilichelewa kulipa malipo kwa muda uliostahili. Sababu ya pili ni kwa wananchi wenyewe ambao baada ya *evaluation* ya kwanza ku-*expire, evaluation* ya pili kuna watu walifanya *speculation,* yaani walifanya kutegesha, kwa maana waliongeza majengo, wakaongeza mazao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli limetupa shida sana suala hili kwa sababu *evaluation* ya mwanzo ilikuwa inaonekana ni ndogo, kuja kufanya *evaluation* ya pili imeonekana ni kubwa sana. Mfano kuna sehemu ya Nyabichele. Wao walithaminishiwa kwenye mazao yao; gharama ilikuwa ni shilingi bilioni 1.6, lakini baada ya *evaluation* ya pili kuja kufanyika, gharama yake ikaonekana ni shilingi bilioni 12. Hili limefanya kampuni kusita kuweza kulipa fedha hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika majibu yangu ya msingi nilisema kwamba hili suala lipo kwa *Chief Valuer* na leo nimeongea na *Chief Valuer* amefanya *evaluation* na ameandika barua kwa *North Mara* kwa maana ya Kampuni ya *Acacia,* ile *evaluation* ambayo wameandikiwa na *Chief Valuer* wailipe *immediately.* Wailipe mara moja, wasipoteze

muda ili kuondoa manung'uniko. Vilevile kupitia Serikali ya Mkoa wa Mara, tumeelewana na Kampuni ya *Acacia* kwa maana ya *North Mara,* walipe fidia kwa wale wananchi wanaodai wanaona kabisa kwamba wananchi hawa wana madai yao ya haki, hawana *dispute* yoyote, hawana mgogoro wowote, hao walipwe mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna wananchi wengine ambao ni 138 toka mwaka 2016 kuna *cheque* ya thamani ya shilingi bilioni 3.2 wamegoma kwenda kuchukua kwa sababu wanalishana maneno, wanasema kwamba wanacholipwa ni kidogo. Nawaasa na ninawaomba, wananchi ambao *cheque* zao ziko tayari, waende wakachukue *cheque* zao mara moja ndani ya wiki hii. Wasipochukua ina maana sasa Serikali ya Mkoa itachukua hatua nyingine na itakuwa vinginevyo. Kwa hiyo, itazidi kuwacheleweshea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, nawaomba wananchi wa Mkoa wa Mara na maeneo ya *North Mara* tusilishane maneno. Watu ambao wana haki, wanatakiwa kulipwa na *cheque* zao ziko kihalali, waende wakachukue *cheque* zao mara moja. Kampuni ya *North Mara,* ndani ya wiki hii tumeshawaambia, yale maeneo ambayo hakuna *dispute,* walipe mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuhusiana na suala la Bunda kule ambako Mheshimiwa Mbunge amelielezea, kwa wale watu wanaomiliki *PLs* na hawazitumii, nimezungumza hapa hata jana, kwamba kwa wamiliki wa *PLs* wasiozitumia, hawafanyi tafiti, sisi tunapitia *PL* moja baada ya nyingine. Tunakwenda kufuta hizo *PL* na tunakwenda kuwapa wachimbaji wadogo wachimbe ili waweze kujipatia kipato na Serikali iweze kupata mapato kupitia uchimbaji mdogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Naibu Waziri wa Madini, Mheshimiwa Stanslaus Nyongo. Tunaendelea na Wizara ya

Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Ally Seif Ungando, Mbunge wa Kibiti sasa aulize swali lake.

Na. 76

**Kuboresha Mazingira ya Ufugaji Kibiti**

**MHE. ALLY S. UNGANDO** aliuliza:-

Katika Jimbo la Kibiti kuna mifugo mingi kama ng'ombe, mbuzi na kondoo, hivyo kusababisha mtafaruku baina ya wakulima na wafugaji, kwani wafugaji hawajawekewa mazingira rafiki kwa mifugo yao:-

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuboresha mazingira rafiki kwa mfugaji?

(b) Je, ni lini mazingira hayo yataboreshwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ally Seif Ungando, Mbunge wa Kibiti, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Kibiti ni moja ya Wilaya nane zilizopo katika Mkoa wa Pwani. Wilaya hii ina mifugo takribani Ng'ombe 50,000, Mbuzi 8,852 na Kondoo 4,877. Serikali inao mkakati wa kuboresha mazingira rafiki kwa wafugaji wa Wilaya ya Kibiti kwa kufanya mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imetenga jumla ya shilingi milioni 80 kwa ajili ya kuanzisha minada miwili ya awali ambapo wafugaji watapata mahali pa kuuzia mifugo yao, Shilingi milioni 18 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa machinjio;

na jumla ya shilingi milioni sita zimetengwa kwa ajili ya ukarabati wa josho. Aidha, Wilaya ya Kibiti kupitia Serikali za Vijiji imetenga takribani hecta 22,000 kwa ajili ya wafugaji katika vijiji18.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo yaliyotengwa yatawezesha wafugaji kupata malisho na machunga. Wataalam wameendelea kuwahamasisha wafugaji kushiriki katika kuboresha maeneo yaliyotengwa na kusisitiza wakulima wasivamie maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya wafugaji. Pia, mifugo ifugwe kulingana na ukubwa wa eneo na pale inapozidi, basi ivunwe ili kuendana na hali halisi ya ukubwa wa eneo.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeandaa mikakati ya kuendeleza sekta ya mifugo nchini katika Wilaya ya Kibiti ikihusisha uboreshaji wa malisho, ujenzi wa majosho, minada ya awali, machinjio na miundombinu ya maji kwa mifugo na utekelezaji wake, unatarajiwa kuanza hivi karibuni kulingana na upatikanaji wa fedha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ungando, swali la nyongeza.

**MHE. ALLY S. UNGANDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, je, Serikali ina mpango gani wa kujenga machinjio ya kisasa ili kuwaletea tija wananchi wa kibiti ambao sasa hivi wana mifugo mingi katika maeneo ya Makima, Nyatanga, Mwambao, Nyambunda, Msala na Muyuyu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, je, Wizara sasa haioni ina kila sababu ya kukaa na wakulima na wafugaji ili kubaini changamoto zao kutatua kama ilivyofanya katika Wizara ya Madini? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo la nyongeza.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Ungando, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza, Mheshimiwa Ally Seif Ungando anataka kujua mkakati wa Serikali juu ya ujenzi wa machinjio ya kisasa kulingana na idadi ya mifugo iliyopo katika ukanda huu wa Wilaya ya Kibiti na jirani zake Mkuranga, Rufiji mpaka Kilwa. Jambo hili ni jema na Serikali imekuwa na mkakati huu ambapo baadhi ya maeneo katika Halmashauri mbalimbali nchini zimejengewa machinjio ya kisasa. Hivyo basi, ni wakati muafaka kwa Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti kuibua mradi huu wa kimkakati na nina hakika Serikali itakuwa pamoja kulingana na ukweli kwamba maeneo haya niliyoyataja hivi sasa yana fursa hii kubwa na nzuri ya Uhamiaji wa mifugo kwa wingi ambapo itakwenda kusababisha upatikanaji wa uhakika wa ajira vilevile kuongeza kipato cha Halmashauri zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili Mheshimiwa Ungando amenihimiza na kututaka Wizara yetu kukaa na wadau hasa wa ufugaji na wakulima, sawa na walivyofanya wenzetu wa Wizara ya Madini. Ni wazo jema na ni zuri sana. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Ungando na Waheshimiwa Wabunge wote, Wizara ya Mifugo na Uvuvi imekuwa na utaratibu huo. Mara nyingi tumekuwa tukikutana na wadau wetu na hata sasa ninavyozungumza wako wataalam wetu kwa maana ya timu maalum inayoshughulika na migogoro ya wakulima na wafugaji, timu ambayo imeundwa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi inayojumuisha wataalam kutoka Wizara ya TAMISEMI, Wizara ya Ardhi na Wizara yetu ya Mifugo na Uvuvi inayokwenda kusikiliza wakulima, kuwasikiliza wafugaji vijijini kwa ajili ya kuweza kupata suluhu ya migogoro yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi leo ninavyozungumza, timu ile ya wataalam iko katika Wilaya ya Kibiti ikifanya mazungumzo na wafugaji na wakulima kwa ajili ya kutafuta suluhu ya kudumu ya matatizo ya migogoro ya wakulima na wafugaji. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Salma Kikwete.

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona. Ng'ombe ni muhimu sana katika ustawi wa Taifa letu la Tanzania na hulipatia Taifa takribani 7% kutokana na ng'ombe hao. Kwa kuwa makundi makubwa yanaingia ndani ya Mkoa wa Pwani na Mkoa wa Lindi; na kwa kuwa ng'ombe wanapoingia ndani ya mikoa hiyo huleta uharibifu mkubwa sana wa mazingira; na tunafahamu mazingira ndiyo kila kitu katika uhai wa binadamu; natahadharisha hii ili yasije yakatokea kama yale yaliyotokea kule Ihefu hatimaye yakasababisha mabwawa kukauka na maji yakakosekana ndani ya nchi yetu. Je, nini kauli ya Serikali au mkakati wa Serikali katika kuhakikisha kwamba mazingira yanaboreshwa ili yasije yakaleta athari kwa Watanzania na nchi kwa ujumla? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza ya Mheshimiwa mama Salma Kikwete, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza mama yangu Mheshimiwa Salma Kikwete kwa kukiri na kukubali kuwa ng'ombe ni fursa kubwa sana kwa uchumi na ustawi wa Taifa letu. Kwa mtazamo huu wa kwamba ng'ombe ni fursa kubwa ya uchumi kwa Taifa letu, hivyo basi, ng'ombe ni fursa kubwa ya ustawi katika mikoa aliyoitaja ya Pwani na Lindi pia vilevile kwa uhamiaji wa ng'ombe wengi wanaoingia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tahadhari yake juu ya ulinzi wa mazingira, sisi Wizara ya Mifugo, tumeizingatia sana. Ndiyo

maana mkakati wetu wa kuhakikisha kuwa tunalinda maeneo yanayotengwa mahususi kwa ajili ya wafugaji na kutoyasababishia kuhamishiwa kwa shughuli nyingine zozote za kibinadamu ikiwemo shughuli za kilimo, tutaendelea nao ili kuhakikisha tunalinda mazingira ya nchi yetu yasiharibiwe na vilevile kwa ustawi wa shughuli hizi za mifugo na shughuli nyingine za wananchi wetu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge na Waheshimiwa Mawaziri, naomba maswali yawe mafupi na majibu yawe mafupi ya kueleweka ili tuende na muda. Mheshimiwa Julius Kalanga, swali fupi la nyongeza.

**MHE. JULIUS K. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kumekuwepo na operesheni inayofanywa na Wizara ya Mifugo katika mipaka yetu ya Tanzania hasa eneo la Namanga na ambapo wafugaji wetu wamekuwa wakipata matatizo makubwa ya kunyang'anywa mifugo na wakati huo huo sheria hairuhusu mifugo kutaifishwa lakini ipigwe faini; na operesheni hii haishirikishi wananchi wanaohusika wala viongozi wa maeneo husika na imesababisha madhara makubwa sana kwa wafuaji wetu. Nini kauli ya Serikali kuhakikisha kwamba wafugaji wanaoenda kutafuta masoko nje ya nchi kwa sababu hakuna viwanda huku ndani, hawapati madhara na madhila wanayopata katika mipaka yetu ya Tanzania, hasa Namanga?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo kwa ufupi. Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza ya Mheshimiwa Laizer, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafugaji wetu wanapofanya shughuli zao za biashara wanashauriwa kuzingatia sheria za nchi zilizowekwa ili wasiweze kupata usumbufu wowote ambao unaweza kujitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua Mheshimiwa Mbunge anazungumzia kama mifugo imekamatwa halafu ikakosa mwenyewe, sheria inawaelekeza wale waliokamata mifugo kuitafisha na baadaye kuipiga mnada hadi pale yule mwenyewe atakapokuwa amepatikana. Nimhakikishie kwamba operesheni hizi haziendi hivyo. Kwa hiyo, wananchi wanachotakiwa ni kutoa ushirikiano tu wa kuhakikisha kwamba wanafuata sheria na taratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado sasa hivi soko la nje ni kubwa kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge mwenyewe kwamba tuna tatizo la viwanda hapa nchini, lakini Waheshimiwa Wabunge kwa sababu baadaye taarifa ya Kamati itawasilishwa, niwahakikishie kwamba mipango tuliyoipanga ni mizuri, viwanda vyetu vingi vitakamilika hivi karibuni na suala la wananchi wetu kuhangaika kutafuta masoko nje litakuwa limekoma kwa sababu karibia kila kona tutakuwa na viwanda vikubwa vyenye uwezo wa kuzalisha na tutakuwa na uwezo mkubwa wa kuuza mpaka nje ya nchi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dau, swali fupi la nyongeza.

**MHE. MBARAKA K. DAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa fursa. Kufuatia operesheni ya kijeshi iliyoendelea pale Mafia na kupelekea madhila na hasara kubwa sana kwa wavuvi ambao walinyang'anywa zana zao halali za kuvulia, wengine mashine zao za boti zimezuiwa; wengine *compressor*s zao, wangine magenereta yao yamezuiwa na hifadhi ya bahari. Mheshimiwa Waziri alitoa taarifa hapa kwamba vitu vyote hivi viachiwe. Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana atakuwa tayari kufuatana nami twende Mafia, Jibondo, Tumbuju na Kilimnoni akaonane na wavuvi ili awaelezee kiuhalisia zoezi hili lilivyokwenda?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, uko tayari?

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza ya Mheshimiwa Dau, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, niko tayari kwenda na nimeshamkubalia Mheshimiwa Mbunge, tukimaliza tu Bunge hapa kuanzia Jumapili, nitakuwa ukanda huo kutembelea maeneo hayo yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kukiweka sawa ni kwamba saa nyingine tunapozungumzia wananchi wetu, wanaweza kuwa wako sahihi kulingana na malalamiko yao, lakini wanaweza kuwa wahalifu. Sasa ni vizuri pia tukawa makini na hilo kwa sababu kama ni wahalifu halafu wanazungmziwa kupata unafuu hapa Bungeni, nadhani itakuwa ni utaratibu ambao haukubaliliki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninachotaka niseme, mimi niko tayari. Waheshimiwa Wabunge, hakuna hata sababu kwa mfano mhalifu mmoja wa kumzungumzia hapa Bungeni. Sisi tuko hapa kama ofisi, kama kuna mtu yoyote ameonewa mahali popote, lete tushughulikie, hakuna hata sababu ya kuhangaika kuuliza swali hapa. Kwa sababu wengine ni wahalifu. Sasa Bunge likigeuka kuwa linazungumzia wahalifu kila siku, litakuwa linapoteza muda wake mwingi. Saa nyingine wengine wanataka huruma ya Mheshimiwa Waziri, sasa huwezi kuipata huruma kwa kuvunja sheria halafu unataka utetewe na Bunge. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwakajoka, swali la mwisho.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nilikuwa nataka nipate ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri. Wanatumia kigezo gani katika kupanga ushuru wa dagaa hasa dagaa zinazotokea bahari ya Hindi? Wafanyabiashara walikuwa wanalipwa kwa gunia la kilo 100 shilingi 10,000/=, lakini sasa hivi kilo moja wanalipisha dola moja. Kwa hiyo, gunia hilo sasa hivi limefika mpaka shilingi 250,000/=. Wafanyabiashara wameshindwa

kufanya biashara hiyo. Serikali inasema nini kuhusiana na jambo hilo kwa sababu linaathiri biashara katika mpaka wa Tunduma? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo kwa ufupi.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza ya Mheshimiwa Mwakajoka, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Mbunge kwa swali lake. Vigezo vya kupanga ushuru wa dagaa au wa bidhaa au wa mazao yoyote ya uvuvi, hutegemeana na thamani ya zao lenyewe linalohusika. Kwa hiyo, hiyo ndiyo hasa zana yake, thamani yake ili Taifa liweze kunufaika na mazao yake hasa yanapotokea kuuzwa nje. Kwa hiyo, kama kuna shida yoyote ambayo katika kubadilisha tozo aidha, zimeweza kuleta mkwamo mkubwa wa biashara, sisi tutatathmini, tutaangalia. Mheshimiwa Mbunge, kama hilo limeleta shida, tutaangalia kwa sababu sasa hivi tunaingilia tunaanza kuzitazama tozo zetu upya kama unavyojua tunaingia kwenye bajeti, kama kuna mahali itaonekena tozo hizi zimewekwa kubwa sana kuliko biashara ilivyo, tutazipunguza na hilo halina matatizo yoyote.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Wizara ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Allan Joseph Kiula, Mbunge wa Iramba Mashariki, sasa aulize swali lake.

Na. 77

**Ujenzi wa Mahakama ya Wilaya – Mkalama**

**MHE. ALLAN J. KIULA** aliuliza:-

Wakazi wa Jimbo la Mkalama wanapata shida sana kufuata huduma za Mahakama katika Wilaya ya Iramba – Kiomboi, umbali mrefu kutoka Mkalama:-

(a) Je, ni lini Serikali itajenga Mahakama ya Wilaya yalipo Makao Makuu ya Wilaya ya Mkalama?

(b) Je, Serikali ipo tayari kuanzisha Mahakama ya muda ya Wilaya katika majengo ya Mahakama ya Mwanzo Nduguti?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Allan Joseph Kiula, Mbunge wa Iramba Mashariki, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakama imejiwekea mkakati wa kujenga na kukarabati majengo ya Mahakama kwa awamu, lengo likiwa ni kuwa na majengo katika wilaya zote ifikapo mwaka 2021. Katika mkakati huo, jengo la Mahakama ya Wilaya ya Mkalama limepangwa kujengwa mwaka 2019 na 2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepokea mapendekezo ya Mheshimiwa Mbunge kuhusu kutumia jengo la Mahakama ya Mwanzo Nduguti kuanzisha huduma za Mahakama ya Wilaya. Hata hivyo, tumefanya tathmini na kubaini kuwa jengo linalotumika sasa kwa Mahakama ya Mwanzo ya Nduguti halitoshelezi kuendesha Mahakama ya Wilaya na ya Mwanzo kwa kuwa mahitaji ya huduma za Mahakama za Mwanzo bado ni makubwa. Mpango tulionao ni kuanzisha Mahakama ya Wilaya katika Mahakama ya Mwanzo Iguguno, ujenzi wa jengo jipya katika Mahakama ya Mwanzo Iguguno umekamilika na kwa tathmini iliyofanyika linaweza kutumika kwa Mahakama ya Wilaya ya Mkalama na Mahakama ya Mwanzo Iguguno kwa muda wakati mipango ya kujenga ya ujenzi wa jengo la Mahakama ya Wilaya inaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa tunaendelea kukamilisha taratibu za upatikanaji wa vifaa, watumishi,

pamoja na taratibu za kisheria ili kuweza kuanzisha Mahakama hiyo kabla ya mwisho wa mwezi Juni, 2019.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kiula, swali la nyongeza.

**MHE. ALLAN J. KIULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwanza niipongeze Serikali ya Awamu ya Tano kwa kuweza kujenga hiyo Mahakama ya Mwanzo, ni Mahakama nzuri na ya kisasa. Swali la nyongeza, kwa kuwa, Mheshimiwa Waziri amesema Mahakama ya muda itaanza kabla ya mwisho wa mwezi Juni. Je, ni lini maandalizi ya kuhamisha mafaili ya kesi zilizopo Kiomboi kwenda Iguguno yataanza ili wakati wa uzinduzi na mafaili yawepo? Tusije tukapeleka wafanyakazi halafu kukawa hamna mashauri ya kusikiliza?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Kiula, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeyapokea mapendekezo yake ya kuhakikisha kuwa kabla ya mwezi Juni, 2019 mafaili yawe yamehama kutoka Mahakama ya Kiomboi kwenda Iguguno. Nami nimhakikishie kuwa, ushauri huo tumeuchukua, tutaufanyia kazi na tutahakikisha kabla ya tarehe hiyo, mafaili hayo yatakuwa yamekwishahamia katika Mahakama ambayo imepangwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Alhaji Abdallah Bulembo.

**MHE. ALHAJI ABDALLAH M. BULEMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Wilaya ya Misenyi katika Mkoa wa Kagera ni wilaya iliyoanza mwaka 2007 mpaka leo ina miaka 11, lakini haina Mahakama ya Wilaya. Wilaya ile ni ya mpakani, kuna wahamiaji haramu, kuna nyarubanja kahawa, kuna matatizo mengi sana. Sasa nataka kuiuliza

Serikali yangu, ni lini wilaya hii itapata haki ya kuwa na Mahakama ya Wilaya ili kuwapunguzia adha wananchi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza ya Mheshimiwa Alhaji Bulembo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua kabisa kwamba, Wilaya ya Misenyi inayo mashauri mengi hasa yanayohusu masuala ya ardhi na mimi mwenyewe binafsi mwaka jana nilitembelea Wilaya ya Misenyi na nilifika na kuoneshwa eneo ambalo limetengwa ili kujenga Mahakama ya Wilaya ya Misenyi. Kwa hiyo, niahidi kwamba, tulikuwa tumepanga kuanza kujenga Mahakama ya Wilaya ya Misenyi mwaka 2017/2018, tunabadilisha mipango ili tuweze kuiwezesha Mahakama hiyo kuanza kujengwa mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Mbunge avute subira wakati wa bajeti tunaweza kuwa na maelezo mazuri zaidi ni lini ujenzi wa Mahakama ya Misenyi utaanza na kama nilivyosema mimi mwenyewe nimefika na kweli Misenyi kuna mashauri mengi sana ya ardhi.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria kwa majibu mazuri na mafupi. Sasa tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Ester Bulaya, Mbunge wa Bunda Mjini, kwa niaba yake Mheshimiwa Paresso.

Na. 78

**Ulipaji Fidia kwa Wananchi Waliopisha Mradi wa Ujenzi wa Barabara Wilaya ya Bunda**

**MHE. CECILIA D. PARESSO (K.n.y. MHE. ESTHER A. BULAYA)** aliuliza:-

Wananchi wa Vijiji vya Manyamanyama, Nyasura, Bunda Mjini na Balili, mwezi Julai, 2003 walivunjiwa nyumba zao kupisha hifadhi ya barabara baada ya *TANROADS* kuongeza umiliki wa hifadhi toka mita 16 hadi mita 22.5:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwalipa wananchi hao fidia na ni lini itafanya hivyo?

(b) Je, ni tathmini ipi itatumika kuwalipa kwani kumekuwepo na mserereko mkubwa wa thamani ya shilingi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Esther Amos Bulaya, Mbunge wa Bunda Mjini, lenye Sehemu (a) na (b) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Jedwali la Kwanza la Sheria ya Barabara ya Mwaka 1932 pamoja na Marekebisho yake, yaani *The Highways Ordinance* ya Mwaka 1932 Barabara ya Mwanza – Bunda – Tarime – Kenya *Border,* yaani Sirari, imeainishwa kama barabara kuu yaani *Territorial Main Road.* Kwa mujibu wa kanuni zilizotungwa chini ya sheria hiyo upana wa hifadhi ya barabara kuu ikiwemo sehemu ya Balili – Bunda – Manyamanyama yenye urefu wa kilometa 9.8 zilikuwa futi 75 kila upande kutoka katikati ya barabara ambayo ni sawa na mita 22.5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu mwaka 1932 barabara hii ilipoainishwa kuwa barabara kuu imeendelea kuwa na hadhi hiyo hadi mwaka 2007. Upana wa hifadhi ya barabara hiyo ulibadilika kutoka mita 22.5 kuwa mita 30 kila upande kwa mujibu wa Sheria ya Barabara Namba 13 ya Mwaka 2007 na sio mita 16 kwenda mita 30, kama alivyodai Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na maelezo hayo, Serikali itawalipa fidia wananchi waliokuwa nje ya hifadhi ya barabara ya mita 22.5 wakati eneo hilo litakapohitajika kutokana na mabadiliko ya Sheria Namba 13 ya Barabara ya Mwaka 2007 kwa vile wamefuatwa na barabara. Aidha, ulipaji wa fidia utazingatia Sheria ya Ardhi Namba 4 ya Mwaka 2001 na Sheria ya Ardhi ya Vijiji Namba 5 ya Mwaka 2001 na Kanuni zake.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Paresso, swali la nyongeza.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, kuna ujenzi wa kiwango cha lami unaendelea kutoka Kisolya, Jimbo la Mwibara inapita Bunda Mjini na kuishia Nyamswa, Jimbo la Bunda Vijijini; na kwa kuwa, katika Jimbo la Bunda Mjini barabara hiyo imeingia kwenye makazi ya wananchi na wananchi hao wamewekewa alama ya *X*, maana yake wanapaswa kulipwa fidia. Je, ni lini na kwa uhakika Serikali itawalipa Wananchi hao fidia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Serikali ya Awamu ya Nne ilitoa ahadi ya ujenzi wa kilometa nane katika Mji wa Bunda zijengwe kwa kiwango cha lami lakini mpaka leo ahadi hiyo haijatekelezwa na barabara hizo hazijaanza kujengwa. Je, ni lini Serikali itajenga barabara hii kwa kiwango cha lami?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya maswali hayo mafupi ya nyongeza.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Paresso, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimfahamishe tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, mradi wa ujenzi wa barabara ya lami unaoendelea sasa ni kati ya Bulamba na Kisolya, lakini nimfahamishe pia Mheshimiwa Mbunge kwamba, tuko kwenye hatua ya manunuzi ya kujenga barabara kutoka Bulamba kupita Bunda kwenda Nyamswa, kilometa 56 na wakati wowote mkandarasi atapatikana barabara hii itaanza kujengwa, lakini Mheshimiwa Mbunge afahamu pia kwamba, harakati za ujenzi wa barabara zitaanza pindi ambapo wananchi watalipwa fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti,Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Mbunge na wananchi wawe na subira kwamba, sasa mkakati wa kujenga barabara hii kilometa 56 utaanza na hii itakuwa kwa kweli, ni neema kwa wananchi wa Bunda na Musoma kwa ujumla kwa sababu, itaungana na barabara inatoka Makutano kwenda hadi Mugumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuhusu swali lake la pili kuhusu ahadi za kilometa nane, ahadi za viongozi wakuu; nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, sisi kama Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi tumejipanga kuhakikisha kwamba, tunatekeleza ahadi zote za viongozi. Kwa hiyo, wananchi wavute subira, kama wanavyoona sasa tunajenga barabara hii kubwa kupita katika mji wa Bunda, kwa hiyo, sina mashaka pia kilometa nane hizi zitajengwa na wananchi wataendelea kunufaika na barabara.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nape.

**MHE. NAPE M. NNAUYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Kwa kuwa ujenzi wa reli ya Mtwara ambao ulipangwa kupita kwenye baadhi ya maeneo ya Jimbo la Mtama, Kata ya Nyangao, Mtama, Kiwalala, Mnolela kuelekea Mtwara maeneo ambayo reli imepangwa kupita wananchi walizuiwa kufanya uendelezaji mpaka pale watakapofidiwa; na kwa

kuwa, sasa huu ni mwaka karibu wa nne na hatuoni dalili za ujenzi wa reli hiyo, kwa nini wananchi hawa sasa wasiruhusiwe kuendeleza maeneo yao mpaka pale Serikali itakapokuwa tayari kuyachukua kwa ajili ya ujenzi wa reli na ikafanya tathmini upya na kufidia?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti naomba kujibu swali la nyongeza ya Mheshimiwa Nape, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza Mheshimiwa Mbunge, Mheshimiwa Nape atakubaliana nami kwamba, ujenzi wa reli hii ni kitu muhimu sana kwa ajili ya maendeleo ya nchi na ni muhimu kwa ajili ya wananchi wenyewe. Kwa hiyo, nataka nimwombe tu avute subira kwa sababu, tunavyotambua kwamba, kuna mradi utapita hapa, ni vema sasa kwamba, wananchi wakaona wasije wakaweka vitu ambavyo vitakuwa na gharama kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiuchumi kama tutawaruhusu wafanye vitu vya maendeleo halafu baadaye tukabomoa kwa ajili ya kuweka miundombinu muhimu kama hii ya reli, tutakuwa tunabomoa ile dhana nzima ya ukuaji wa uchumi. Kwa hiyo, niwaombe tu wananchi wasiweke vitu vya thamani kubwa, reli ni kwa ajili yao, reli ni kwa ajili ya maendeleo ya nchi. Kwa hiyo, tushirikiane tu, lakini Serikali inaendelea kusukuma jambo hili ili tuweze kupata hii reli ambayo itatupa manufaa makubwa katika nchi yetu.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Ramo Matala Makani, Mbunge wa Tunduru Kaskazini, sasa aulize swali lake.

Na. 79

**Changamoto za Matengenezo ya Miundombinu Nchini**

**MHE. ENG. RAMO M. MAKANI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mipango ipi ya muda mfupi, wa kati na mrefu ya kushughulikia changamoto zinazojitokeza katika matengenezo ya miundombinu nchini baada ya ujenzi wake kukamilika?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ramo Matala Makani, Mbunge wa Tunduru Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukabiliana na changamoto ya matengenezo ya miundombinu ya barabara na madaraja, Serikali ilianzisha Bodi ya Mfuko wa Barabara mwezi Julai, 2000 kwa lengo la kufanya matengenezo mbalimbali ya barabara ya kawaida, matengenezo ya muda maalum, matengenezo ya maeneo korofi na matengenezo ya madaraja. Ili kukabiliana na changamoto za matengenezo ya miundombinu ya barabara baada ya kukamilika kwa ujenzi, Serikali imekuwa ikiongeza bajeti ya matengenezo kila mwaka kupitia Mfuko wa Barabara kwa ajili ya kufanya matengenezo mbalimbali ya barabara nchini. Bajeti ya matengenezo ambayo imekuwa ikiongezeka kila mwaka inatumika kufanya matengenezo ya kawaida, matangenezo ya muda maalum, matengenezo ya maeneo korofi na matengenezo ya madaraja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu ilivyoanzishwa Bodi ya Mfuko wa Barabara bajeti ya matengenezo imekuwa

ikiongezeka kila mwaka. Kwa mfano, katika bajeti ya mwaka 2000/2001 zilitengwa Sh.44,436,708,674 na Mwaka wa Fedha 2010/2011 zilitengwa Sh.286,907,000,000 na Mwaka wa Fedha 2018/2019 zimetengwa jumla ya Sh.908,808,000,000. Mfuko huu unaimarishwa kila mwaka ili miundombinu ya barabara na madaraja iweze kutengenezwa na kupitika majira yote ya mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali pia inaendelea kudhibiti uzito wa magari kwa kujenga mizani na kupima uzito wa magari kwenye barabara zote za lami zilizokamilika na zinazopendelea kujengwa nchi nzima ili kuzinusuru barabara hizo kutokana na uharibifu mkubwa unaosababishwa na magari yanayozidisha uzito. Mizani inajumuisha mizani ya kudumu, mizani inayohamishika na mizani inayopima magari yakiwa kwenye mwendo, yaani *Weigh in Motion.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)* unaendelea kufanya tafiti mbalimbali kupitia Maabara Kuu ya Vifaa vya Ujenzi kwa kushirikiana na Taasisi ya Utafiti ya Afrika Kusini, lengo ni kubaini sababu za baadhi ya barabara hapa nchini kuharibika katika kipindi kifupi mara baada ya kukamilika. Wizara kupitia *TANROADS* tayari imekwishatoa mwongozo wa usanifu wa uchanganyaji wa lami, yaani *Guideline for Asphalt Mix Design,* unaozingatia mabadiliko ya mifumo ya miundo na vyombo vya usafiri, hali ya hewa na viwango sahihi vya vifaa vya ujenzi wa barabara. Mwongozo huu ulianza kutumika Mwezi Novemba mwaka 2018.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Makani, swali la nyongeza.

**MHE. ENG. RAMO M. MAKANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Taarifa zinaeleza wazi na takwimu zinaonesha kwamba, takribani asilimia 45 ya bajeti ya Serikali iko upande wa miundombinu, lakini kati ya hizo asilimia 45 za bajeti nzima ya Serikali karibu asilimia 40 inakwenda kwenye *maintenance. Maintenance* ambayo ni matengenezo ya barabara baada ya kuwa zimekamilika na

kuanza kutumia ni eneo ambalo kama Taifa tunatakiwa kuliangalia vizuri zaidi ili tuweze kuokoa fedha zinazokwenda huko kutumika kwa *maintenance* ziweze kutumika katika miradi mingine ya sekta mbalimbali kwa ajili ya maendeleo ya jamii. Nikisema bajeti ya maendeleo kwa upande wa miundombinu, nazungumza ile bajeti ambayo iko Wizara ya Miundombinu pekee, lakini miundombinu pia, iko kwenye miradi mingine kama ya umeme, maji, mifugo, kilimo, elimu, afya, kote kuna miradi ya miundombinu ambayo tafsiri yake ni...

**MWENYEKITI:** Uliza swali Mheshimiwa muda unakwenda.

**MHE. ENG. RAMO M. MAKANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, sasa nataka kuuliza swali, nilikuwa najenga mazingira ya kuuliza swali. Sasa kutoka na ukweli huo wa kwamba, fedha nyingi zinakwenda kwenye *maintenance.* Je, Serikali inajipanga namna gani licha ya hizi njia walizozieleza kwenye swali za kimaabara, upande wa watalaam Serikali inajipangaje kuhakikisha kwamba, wataalam wanaoshiriki katika kufanya kazi hizo wakati wa matengenezo ya barabara wanazingatia misingi ya kuwa na miundombinu bora ili isije ikasababisha kuwa na gharama kubwa upande wa *maintenance*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, katika Jimbo la Tunduru Kaskazini iko miradi ambayo nasisitiza kwamba, katika mipango yake Serikali inapokwenda kutekeleza iitekeleze miradi hiyo kwa kuzingatia viwango. Miradi hiyo ni pamoja na Barabara ya Mji Mwema kupitia Ngapa kwenda Nachingwea kwa kiwango cha lami, Barabara ya Mironde kwenda Kalulu mpaka Selou kwenye Hifadhi ya Taifa kule kwa kiwango cha changarawe, Barabara ya Nandembwe – Nampungu mpaka Mbatamira kwa kiwango cha changarawe na Barabara ya Kangomba kupitia Kidodoma mpaka Machemba na kule Chiwana kwa kiwango cha changarawe na pia mwisho kabisa Daraja la Fundi Mbanga. Je, Serikali itatekeleza lini mipango hii ya kutengeneza miradi hii kwa viwango?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa ufupi, ingawa maswali ni marefu sana.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Makani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba uniruhusu nitoe shukrani sana kwa Mheshimiwa Rais wetu kwa kuendelea kusukuma tuweze kupata fedha nyingi kwa ajili ya kuendeleza hii miundombinu muhimu. Pia nimshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa sababu mara nyingi tumezungumza na ushauri wake tunaendelea kuuchukua, lakini nilishukuru Bunge kwa sababu limeendelea kututengea fedha za kutosha. Katika mwaka tu wa Fedha huu ambao tunaendelea nao Wizara yetu imetengewa trilioni 4.2, sasa hii ni fedha nyingi sana kuonesha *concern* ya Bunge nalo lipo pamoja na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kujibu swali lake la kwanza niseme kwamba, yako mambo mengi kama Serikali kupitia Wizara hii ya Ujenzi tunafanya ili kuhakikisha kwamba, tunafanya kazi vizuri na kuboresha miundombinu. Kama unavyoshuhudia Mheshimiwa Makani sheria zimekuwa zikifanyiwa mabadiliko mbalimbali, kumekuwa na miongozo mingi inatolewa, lakini ziko programu nyingi sana ambazo hapa siwezi kuzitaja kwa ajili ya kuhakikisha kwamba, kazi inafanyika kwa weledi. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, kupitia Bodi ya Wahandisi *(ERB)* tunaendelea kusimamia maadili ya wataalam wetu, tunaendelea kukuza namba ya wataalam katika nchi hii ili kuweza kusimamia miradi hii. Pia tutaendelea kuchukua hatua kwa wataalam hawa ambao watakwenda kinyume na utaratibu ambao tunautaka, lengo tu ni kuhakikisha kwamba, utaalam unatumika vizuri na miundombinu yetu inajengwa vizuri, lakini pia, tunaisimamia vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu viwango vya ujenzi wa barabara, amezungumza barabara hizi alizozitaja

Mheshimiwa Mbunge. Natambua kwamba, barabara hizi karibu zote ziko kwenye upande wa TAMISEMI, lakini sisi kama Serikali, tunashirikiana na TAMISEMI kuhakikisha kwamba, barabara hizi zinaenda kuwahudumia wananchi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge usiwe na wasiwasi, natambua kwamba, liko Daraja hili la Fundi Mbangai, hili daraja tayari upande wa Serikali za Mitaa kwa maana ya kupitia Halmashauri ya kwake waliomba utaalam kutoka kwenye Serikali na daraja hili limetengenezwa, isipokuwa zile *approach road* ndio zinahitajika kufanyiwa matengenezo. Naamini kutokana na *concern* ya Halmashauri yake hizi barabara zitatengenezwa, lakini Barabara hii ya Mji Mwema – Ngapa kwenda Nachingwea itaenda kutuunga na Mkoa wa Lindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Ruvuma, upande huu wa Tunduru, hii Barabara kutoka Mji Mwema kwenda Ngapa tumeshaichukua na eneo la Ngapa pale tutahitaji kujenga daraja. Kwa hiyo, wananchi wa Tunduru wawe na imani kwamba, tutakwenda kujenga daraja hili ambalo litatuunga na Mkoa wa Lindi. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ahsante kwa majibu. Tunaendelea na Mheshimiwa Pauline Gekul, Mbunge wa Babati Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 80

**Barabara za Arusha – Singida na Arusha – Dodoma**

**MHE. PAULINE P. GEKUL** aliuliza:-

(a) Je, ni lini wananchi wanaodai fidia kutokana na barabara ya mchepuo kutoka Arusha – Singida na Arusha – Dodoma katika Mji wa Babati watalipwa fidia?

(b) Je, ni lini ujenzi wa barabara hizo utaanza?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Pauline Philip Gekul, Mbunge wa Babati Mjini, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa mchepuo kutoka barabara za Arusha – Singida na Arusha – Dodoma kwa Babati Mjini (*Babati Baypass*) unatekelezwa kwa pamoja na mradi wa barabara ya mchepuo wa Bwawa la Mtera *(Mtera Baypass)* katika barabara ya Iringa – Dodoma chini ya ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB). Aidha, taratibu za ununuzi wa kumpata Mhandisi Mshauri atakayefanya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina upo katika hatua za mwisho ambapo kazi ya upembuzi yakini na usanifu wa kina itakayotekelezwa na Mhandisi Mshauri itahusisha pia usanifu wa mwelekeo ulio bora na sahihi wa barabara ya mchepuo kwa kuzingatia vigezo vya kitaalam kama vile gharama za ujenzi, uhifadhi wa mazingira pamoja na usalama wa watumiaji wa barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulingana na hadidu za rejea alizopewa Mhandisi Mshauri ni pamoja na kutambua watu na mali zao watakaoathiriwa na mradi. Baada ya Mhandisi Mshauri kukamilisha jukumu la kitaalam; tathmini ya mali za wananchi zitakazoathiriwa na mradi itafanyika kwa kufuata sheria na taratibu na hatimaye fidia kulipwa kwa walengwa kwa kuzingatia sheria zilizopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kukamilisha kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina pamoja na maandalizi ya nyaraka za zabuni, kazi hii itatangazwa ili kumpata mkandarasi wa kujenga barabara hiyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Gekul, swali la nyongeza.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niishukuru sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi, Serikali ya chama changu... *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuunganisha jimbo letu na miradi barabara ya lami. Tumeunganishwa na Arusha Dodoma na Singida lakini tuna kilomita 10 za lami ambazo zinaendelea na taa za barabarani zinawekwa. Kwa hiyo, nashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, huu mchakato wa kumpata Mhandishi Mshauri umechukua zaidi ya miaka mine. Naomba nifahamu Wizara yako ipo tayari kuwasiliana na *African Development Bank* ili huu mchakato ufike mwisho na wale wananchi wapate fidia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa hizi barabara za lami zilivyopita mita 7.5 ziliongezeka tangu 2007 kwa mujibu wa Sheria ya Barabara lakini wananchi hao hawajafidiwa na wameshindwa kujenga nyumba zao. Naomba nifahamu kwa nini Serikali isipitie kanuni hii ya fidia muone wananchi hawa ambao wapo kwenye *road reserve* walipwe *at least* wale ambao wamejenga nyumba zao kwa sababu sasa wanashindwa hata kuzikarabati?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri kwa ufupi kama maswali yalivyo ya Kibunge.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Gekul, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda uniruhusu nitumie muda mfupi huu nimkaribishe sana Mheshimiwa Gekul upande huu. Nimpongeze sana kwa sababu anapigania kweli maendeleo ya Mji wa Babati. Nami namuahidi kwamba tutaendelea kushirikiana kama tunavyoshirikiana na Waheshimiwa Wabunge wote ili

kuhakikisha kwamba maendeleo yanawafikia wananchi wetu kwa ujumla wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake la kwanza ametoa ushauri, kwa hiyo, nikubali kuwa ushauri wake tutauchukua na tutaufanyia kazi. Kikubwa ni kwamba tunaendelea kushirikiana na wafadhili kwa sababu wamekuwa na imani na Serikali yetu na nimuahidi kwamba AfDB tutaendelea kuwasiliana nao ili kuhakikisha kwamba yale yote yanayohitajika kuweza kutekeleza mradi huu tunaweza kutekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili kuhusu fidia ya wananchi ambao walipisha eneo la mradi, nakubaliana naye kwamba tutaendelea kulitazama. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba maeneo yote tunaendelea kulipa kwa kasi na maeneo yote ambayo miradi inapita tutaendelea kufanya malipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niseme kwamba jambo hili nimelichukuwa, nitaendelea kuzungumza na wenzetu ili tuweze kuhakikisha kwamba wale wanaostahili fidia wanalipwa kulingana na taratibu ambazo zipo. Kwa hiyo, nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge na wananchi wote wa Babati kwamba tutaliangalia suala lao kwamba wamepisha eneo la mradi na wanastahili kulipwa kama sheria inavyotaka.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Asha AbdullahJuma, swali fupi la nyongeza.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kunipa nafasi. Naomba kuuliza swali moja la nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ni lini Serikali itaandaa jedwali la kuonyesha miradi mikubwa ya barabara zinazounganisha miji mikuu ya mikoa ili kuonyesha hali ilivyo na hivyo kuweza kuwaanika wakandarasi wanaochelewesha kazi hiyo kwa makusudi na kuwapa wananchi dhiki mfano

barabara ya Nyakanazi – Kabingo - Kidahwe - Kasulu ambazo kwa muda mrefu hazikamiliki? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Asha, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, iko miradi mingi sana ya ujenzi wa barabara inatekelezwa kote nchini. Nawaona Waheshimiwa wa Kigoma wanatabasamu kwa sababu wanafahamu fika kwamba miradi hii ambayo ilikuwa inatekelezwa katika Mkoa wa Kigoma ukianzia Nyakanazi – Kibondo - Kidahwe – Kasulu inaendelea vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaambie wananchi wa Kigoma kwa ujumla kwamba ipo miradi mingi sana ambayo kwa hapa siwezi kuitaja inaendelea vizuri. Mheshimiwa Nsanzugwanko na Mheshimiwa Zitto wanafahamu kwamba sasa *appetite* ya matengenezo ya barabara kwenye Mkoa wa Kigoma ipo juu sana na barabara karibu zote zina fedha kwa ajili ya ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Asha asiwe na wasiwasi. Hata eneo hili lililokuwa linasuasua kutoka Nyakanazi - Kakonko tumeendelea kulisimamia. Mimi mwenyewe nimekwenda mara kadhaa na tumezungumza na mkandarasi na zile changamoto zilizokuwa zinamkabili kama Serikali tumezitatua. Tunaendelea kusukuma na nitahakikisha barabara hii inakamilika ili wananchi wa Kigoma nao wapate faraja ya kuwa na miundombinu kwa ajili ya kuchochea maendeleo ya mkoa wao.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na swali la Mheshimiwa Daniel Nichodemus Nsanzugwanko, Mbunge wa Kasulu Mjini.

Na. 81

**Kubadilishana Wafungwa Wakimbizi na Nchi Jirani**

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO** aliuliza:-

Wafungwa wakimbizi toka nchi za Burundi na DRC wamekuwa wakijaza mahabusu na magereza yetu:-

(a) Je, kwa nini Serikali isikubaliane na nchi za Burundi na DRC kubadilishana wafungwa ili wakimbizi hao wafungwe katika nchi zao?

(b) Je, wafungwa wa aina hiyo wanapokuwa mahabusu na magereza, Shirika la *UNHCR* linachangia gharama kwa kiasi gani?

(c) Je, *UNHCR* imechangia fedha kiasi gani kwa wafungwa wakimbizi waliofungwa au kuwekwa mahabusu nchini kuanzia mwaka 2017/2018?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Alhaj Masauni, karibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Daniel Nichodemus Nsanzugwanko, Mbunge wa Kasulu Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimwa Mwenyekiti, suala la kubadilishana wafungwa baina ya nchi moja na nyingine huongozwa na mkataba wa makubaliano ulioingiwa baina ya nchi moja na nyingine. Lengo la mkataba huo ni kumpa fursa mfungwa anayetumikia kifungo chake gerezani kutumikia sehemu ya kifungo chake kilichobaki katika nchi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ieleweke kuwa ni utamaduni wa kisheria duniani kwamba mahabusu na mfungwa bila

kujali kama ana hadhi ya ukimbizi, wanapopokelewa na kuhifadhiwa katika magereza, jukumu la kuwatunza hufanywa na Serikali ya nchi husika. Serikali yetu imekuwa ikifanya hivyo kwa kufuata Sheria na Kanuni za Magereza zilizopo ambazo kimsingi zimeipa Serikali jukumu hilo. Aidha, ifahamike kuwa kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Magereza hakuna mahabusu au mfungwa mkimbizi kwani wahalifu wote hupokelewa kwa hati kutoka Mahakama zetu zenye utambulisho wa hadhi ya mahabusu au mfungwa tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, kwa misingi hiyo suala la Shirika la *UNHCR* kuchangia gharama za kuwatunza wafungwa na mahabusu wanaodaiwa kuwa ni wakimbizi huwa halipo na halifanyiki kwa sababu kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Magereza zilizopo hazijaainisha kumtambua mahabusu au mfungwa mkimbizi katika magereza yetu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nsanzugwanko, swali fupi la nyongeza.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maelezo ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msingi wa hoja ni Serikali ianze mchakato wa kimkataba wa makubaliano, ndiyo msingi wa hoja. Kama kubadilishana wafungwa kunaongozwa na mkataba, ni lini Serikali yetu itaanza mchakato huo kati ya nchi ya DRC na Burundi ambazo zina wafungwa wengi Kasulu na Kigoma?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Mheshimiwa Naibu Waziri anataka kuniambia wale wafungwa wa Kongo na Burundi waliopo Kibondo, Kasulu na Kigoma kwa ujumla wanatoka Taifa gani kama siyo wakimbizi toka nchi hizo nilizozisema? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya maswali hayo kwa ufupi sana.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Daniel Nsanzungwanko, Mbunge wa Kasulu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza ni ushauri ambao tumeuchukuwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ni kweli wale ni wakimbizi lakini kwa maana ya tafsiri ya kisheria wamefanya makosa wamekuwa ni wafungwa. Kwa hiyo, kimsingi kwa tafsiri ya kisheria wale ni wafungwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Maftaha na Mheshimiwa Zitto, maswali mafupi sana ya nyongeza.

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kuuliza swali la nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa kumekuwa na operesheni ambayo inafanywa na Jeshi la Polisi ya kusaka watu ambao wanasema hawana kazi mtaani. Cha ajabu hawa watu wanakamatwa kipindi kile cha jioni tayari wamesharudi makazini wakiwa wamepumzika barazani huko Dar es Salaam na maeneo mengine ya Tanzania hali ambayo inapelekea kujaza mahabusu zetu katika maeneo mengi ya nchi hii. Serikali inatoa tamko gani kuhusu operesheni hii inayofanywa na Jeshi la Polisi ambayo inapelekea kujaza mahabusu bila sababu? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo fupi la nyongeza.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Maftaha, Mbunge wa Mtwara Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina taarifa ya maelezo ambayo ametoa Mheshimiwa Mbunge kwamba Polisi wanachukuwa mtu yeyote. Nachojua katika utaratibu wa kawaida wa Jeshi la Polisi ni kufanya doria na pale wanapoona watu wanaojihusisha na uhalifu ama wana viashiria vya uhalifu kuwachukuwa na kufanya uchunguzi wao ili hatua zaidi zichukuliwe. Taarifa za ziada kwamba kuna watu ambao anadhani yeye hawakupaswa kuchukuliwa na Jeshi la Polisi kutokana na shughuli hiyo, labda angetupatia taarifa mahsusi ili tuweze kuzifanyia kazi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zitto, swali fupi la nyongeza.

**MHE. KABWE Z.R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ukienda Segerea utakuta idadi ya mahabusu ni wengi zaidi kuliko watu ambao wameshahukumiwa na hii inatokana na sheria kandamizi ambazo zinanyima watu dhamana kama zilivyonyima dhamana Wabunge wetu wawili; Mheshimiwa Mbowe na Mheshimiwa Matiko na Sheria ya *Anti Money Laundering* ambayo makosa yanawekwa tu ili kuweza kuwaweka ndani watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali haioni kwamba imefikia wakati kwa watu ambao umri wao ni kuanzia miaka 75 na kuendelea kama ilivyokuwa kwa Mheshimiwa William Shelukindo ambaye aliwekwa kwenye Gereza la Maweni kwa kukosa dhamana tu, kuweka utaratibu watu hawa wawe wanafungwa kifungo cha nyumbani kwao badala ya kuwajaza magerezani bila sababu kutokana na umri wao kama ambavyo nchi nchi nyingine wanafanya?

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Zitto. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo fupi la nyongeza.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Zitto Kabwe, Mbunge wa Kigoma Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Zitto amezungumza vitu viwili kwa pamoja suala la mahabusu na wafungwa. Suala la wafungwa siku zote nimekuwa nikieleza mikakati ya Serikali ya jinsi ya kupunguza msongamano kwenye magereza kupitia njia mbalimbali. Tumeona Mheshimiwa Rais akitoa msamaha kwa wafungwa, tuna sheria za *parole,* sheria za huduma za jamii na nyinginezo. Pia tunafanya jitihada ya kujenga magereza ili kupunguza ule msongamano. Kwa hiyo, kimsingi kwa wafungwa huo ndiyo mkakati wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo la mahabusu ni suala la kisheria zaidi, kumchukua mahabusu na kumpa kifungo cha nje anakuwa bado hajahukumiwa. Kwa hiyo, cha msingi ni kufuata sheria za dhamana ili aweze kupata dhamana wakati huo huo sisi tukifanya jitihada za kuboresha mahabusu zetu ili kuepusha msongamano na madhara yanayoweza kujitokeza.

**MWENYEKITI:** Tunamalizia na Mheshimiwa Lucy Simon Magereli, Mbunge Viti Maalum.

Na. 82

**Utaratibu wa Kutoza Faini za Magari**

**MHE. LUCY S. MAGERELI** aliuliza:-

Tangazo la Serikali Namba 257 kifungu cha 6 kinaelekeza faini za makosa ya barabarani kulipwa kwa Askari aliyeandika faini au kwa *OCD* au Ofisi ya Mhasibu aliyeko karibu. GN hiyo imetoa nafasi ya kulipa ndani ya siku saba (7) na iwapo faini haitalipwa ndani ya siku saba (7) mkosaji atafikishwa Mahakamani ndani ya siku 10:-

(a) Kwa nini Askari wa Usalama Barabarani huamua kushikilia magari ya wanaokamatwa wakati huohuo, wakati sheria inasema walipe ndani ya siku saba (7)?

(b) Katika Mkoa wa Dar es Salaam kuna mashine za kielektroniki *(POS)* za kulipia faini na *ANPR* ambayo husaidia kufuatilia ambao wanakwepa kulipa faini walizoandikiwa. Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza upatikanaji wa *POS* na *ANPR* ili kuepusha mifarakano na usumbufu unaojitokeza?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lucy Simon Magereli, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba kifungu cha 6 cha Tangazo la Serikali Namba 257 alichokinukuu kilishafanyiwa marejeo mwaka 2015 na kutangazwa katika Gazeti la Serikali mnamo tarehe 30/01/2015 na kuwa Kanuni namba 30/2015 ya Sheria ya Usalama Barabarani ambayo imelenga kutengeneza mfumo wa ulipaji wa tozo za papo kwa papo kwa njia ya kielektroniki. Kanuni hii pia inasomwa pamoja na Sheria ya Usalama Barabarani, Sura ya 168 iliyorejewa mwaka 2002, kifungu cha 95.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukamataji wa magari na kisha kuyashikilia upo kisheria, kifungu cha 87, kifungu kidogo cha (a), (b) (c) na (d) cha Sheria ya Usalama Barabarani, Sura ya 168 iliyorejewa mwaka 2002, magari haya hushikiliwa kulingana na uzito wa kosa alilofanya dereva mfano makosa hatarishi kama ubovu wa gari ambapo gari linatakiwa likafanyiwe ukaguzi na Mkaguzi wa Magari, makosa ambayo dereva au mmiliki anatakiwa apelekwe Mahakamani na kadhalika.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo wa ulipaji tozo za papo kwa papo kwa njia ya mtandao ulianza kutekelezwa kwa majaribio katika Mikoa mitatu ya Kipolisi ya Ilala, Kinondoni na Temeke ambapo jumla ya mashine za kielektroniki *(POS)* 360 na kamera za kufuatilia magari yanayodaiwa faini *(ANPR)* 3 zilizotumika na kuonyesha ufanisi na mafanikio makubwa. Kuanzia Apili, 2018, mfumo huu ulianza kutumika nchini kote ambapo mashine hizi za kielekroniki *(POS)* zipatazo 3,000 zilipelekwa mikoa yote nchini na mashine za ufuatiliaji wa magari *(ANPR)* zipatazo 400 zinatarajia kusambazwa mikoa yote nchini kuondoa usumbufu usio wa lazima.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lucy Magereli, swali la nyongeza.

**MHE. LUCY S. MAGERELI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza na nieleze masikitiko yangu kwamba swali langu nilileta mwaka 2016 lakini kwa bahati mbaya limekuja 2019. Nishukuru kwa maendeleo ambayo yamefanywa ya kusambaza hizo mashine za kielektroniki nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kusambazwa mashine hizo sasa hivi Jeshi la Polisi limekuwa sehemu ya chanzo kikuu cha mapato ya Serikali na wanapangiwa viwango vya fedha za kukusanya. Kwa hiyo, uwepo wa mashine hizi pamoja na kwamba tulidhani ingekuwa ni suluhisho lakini imekuwa chanzo cha kuwabambika makosa watumia barabara ili kuzalisha mapatao. Je, Serikali ina mpango gani wa kuwanusuru watumia barabara kwa makosa haya ya kubambikizwa na kulazimishwa kulipa faini ili tu kufikia viwango za fedha walizokubaliana vitendo vinavyofanywa na askari wa usalama barabarani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, hivi karibuni Mheshimiwa Kangi Lugola, Waziri mwenye dhamana ya Mambo ya Ndani alitoa maelekezo kwamba gari

linapokamatwa hata kama litakuwa na makosa zaidi ya moja basi liandikiwe kosa moja lakini hadi tunavyozungumza, magari mengi yanaandikiwa faini zaidi ya kosa moja na kutozwa faini na *penalties* kinyume na maelekezo ya Mheshimiwa Waziri. Je, Serikali inaweza kurejea tena agizo lake kupitia Bunge letu Tukufu ili liwe maelekezo rasmi ya Serikali kwa watekeleza sharia? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi kwa maswali hayo mawili ya nyongeza.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lucy Magereli, Mbunge wa Viti Maalum, kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na hoja ya kubambikiwa kesi ambayo ametuhumu Askari wa Usalama wa Barabarani, nimwambie tu kwamba yanapotokea matukio kama haya kwa baadhi ya askari wetu tunachukua hatua na hata hili agizo la Mheshimiwa Waziri lilikuwa linalenga kuziba mianya ya aina kama hiyo. Kwa hiyo, nimhakikishie Mbunge kwamba Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nchi ndiye mwenye dhamana ya mwisho ya Wizara hii na maagizo yake ni lazima yatekelezwe. Maagizo haya yanatekelezwa ikiwa kuna upungufu katika utekelezaji wake, kama labda kuna watu ambao hawatekelezi, hiyo taarifa hatujaipata rasmi lakini kimsingi Mheshimiwa Waziri ametoa agizo na linapaswa kutekelezwa kwa maslahi ya wananchi wa nchi yetu ambao wanatumia barabara.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Tunaendelea na Wizara ya Maji, Mheshimiwa Haroon Mulla Pirmohamed, Mbunge wa Mbarali, sasa aulize swali lake. Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, kwa niaba ya Mheshimiwa Haroon Mulla Pirmohamed. *(Makofi)*

Na.83

**Tatizo la Maji – Jimbo la Mbarali**

**MHE. DKT. TULIA ACKSON** (**K.n.y HAROON M. PIRMOHAMED**) aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itapeleka maji maeneo katika maeneo ya Kata za Mahongele katika vijiji (6), Kata ya Mwatenga vijiji (4), Kata ya Kongoro/Mswiswi vijiji (2), Kata ya Utengule - Usangu vijiji (6), Kata ya Luhanga vijiji (4), Kata ya Itambo vijiji (4), Kata ya Chimala vijiji (7), Kata ya Ihahi vijiji (3), Kata ya Imalilo – Songwe vijiji (5), Kata ya Igaua vijiji (5), Kata ya Miyombweni vijiji (5), Kata ya Mapogoro vijiji (9) na Mji wa Rujewa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Haroon Mulla, Mbunge wa Jimbo Mbarali, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali kupitia Progamu ya Maji Vijiji tangu mwaka 2012 imefanya usanifu katika vijiji 16 na kujenga miradi ya maji katika vijiji Simike-Kata ya Utengule Usangu, Udindilwa - Kata ya Ruiwa, Igurusi - Kata ya Igurusi, Chimala - Kata ya Chimala, Mkunywa -Kata ya Madibira na Ubaruku - Kata Ubaruku. Pia Halmashauri kupitia kwa wadau wa maelendeleo (*UNICEF*) imechimba visima 25 katika vijiji mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kukamilisha miradi hiyo, Halmashuri inaendelea na utekelezaji wa ujenzi wa mradi wa Luduga Mawindi ambao hadi utapokamilika utagharima shilingi bilioni 9 na utahudumia vijiji sita vya Kata ya Mawindi na Ipwani. Mradi huu utatekelezwa kwa awamu

tano na kwa sasa utelezaji unaendelea katika awamu ya kwanza ambayo imefikia asilimia 98 na awamu ya pili imefikia asilimia 75. Hadi sasa mradi huu umegharimu shilingi bilioni 2.9. Taratibu za kutangaza awamu ya 3 zinaendelea na awamu ya 4 na 5 zitatangazwa baada awamu ya 3 kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa lengo la kuboresha huduma ya maji katika Mji wa Rujewa mji huo pia umejumuishwa katika miji itakayonufaika kupitia fedha za mkopo kiasi cha Dola za Kimarekani milioni 500 kutoka Serikali ya India ambazo zitatumika katika ujenzi na ukarabati wa miradi ya maji katika maeneo mbalimbali nchini.

**MWENYEKITI:** Mhe Dkt. Tulia Ackson, maswali la nyongeza.

**MHE. DKT. TULIA ACKSON:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, changamoto zilizopo Wilaya Mbarali zipo pia Wilaya ya Rungwe hususani kwenye eneo la Bonde la Mwakaleli lakini pia Kata ya Ikuti. Maeneo haya yanazungukwa na mito lakini hayana miundombinu ya kupelekea wananchi maji. Nataka kujua ni lini Serikali itapekeza miradi ili wananchi waweze kupata maji? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, changamoto hizi pia zipo kwenye kata mbalimbali ya Mbeya Jiji. Baadhi ya kata hizo zenye changamoto ni pamoja na Kata ya Mwasekwa, Mtaa wa Ilembo na Mengo; Kata ya Iganjo, Mtaa Mayombo na Rumbila; Kata ya Iduda, Mtaa wa Muhala; Kata ya Uyolem, Mtaa wa Hasanga; Kata ya Msalaga, Mtaa wa Ntundu na Itezi Mashariki; Kata Iwambi, Mtaa Mayombo na Lumbila, Itagano kwenye mtaa mingi, Itenda baadhi ya mitaa.

**WABUNGE FULANI:** Uliza swali.

**MHE. DKT. TULIA ACKSON:** Mheshimiwa Mwenyekiti nataka kujua ni lini Serikali itapeleka maji kwa wananchi Kata hizi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya maswali hayo mawili.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda tutambue kwamba maji ni uhai. Nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Naibu Spika kwa kutetea uhai wa wananchi wa Mbeya. Kama Wizara ya Maji jukumu letu ni kuhakikisha Watanzania wakiwemo wananchi wa Mbeya wanapata maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu la Bonde la Mwakaleli tuna mradi pale wa zaidi ya shilingi bilioni 6 ambao utaweza kunufaisha wananchi wa Kata ya Masebe pamoja na Suma. Kwa Kata ya Ikuti katika Jimbo lile la Rungwe, tunamuagiza Mhandisi wa Maji wa Wilaya ya Rungwe afanye usanifu haraka ili wananchi wale waweze kupata maji safi, salama na yenye kutosheleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala zima la Jiji la Mbeya, uzalishaji wa Mamlaka ya Maji ya Mbeya ni lita milioni 48, 45 kwa siku. Mkakati wa muda mfupi ni kuhakisha tunatumia miundombinu ya sasa iliyopo ili wananchi wa Iwambi, Iganzo, Iduda, Itende, Uyole na Isesya nao wanapata maji. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Naibu Spika hata maeneo yenye miinuko kwa maana Mwansekwa pamoja na Itagano nao tutawapelekea maji kwa sababu sisi siyo Wizara ya ukame. Kwa hiyo, nataka nimhakikshie Mheshimiwa Naibu Spika sisi kama Wizara ya Maji hatutakuwa kikwazo kwa wananchi wa Jiji la Mbeya kupata maji safi, salama na yenye kutosheleza. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Kutokana na muda, tunamalizia na Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Benardetha Kasabago Mushashu, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na.84

**Kuinua Bei ya Zao la Kahawa**

**MHE. BENARDETHA K. MUSHASHU** aliuliza:-

Kahawa ni zao la biashara na la kimkakati ingawa kwa miaka kadhaa bei ya zao hilo imeendelea kuwa chini:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuinua zao hilo Mkoani Kagera ikiwemo kupandisha bei ili kumnufaisha mkulima?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Benardetha Kasabago Mushashu, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, zao la kahawa ni miongoni mwa mazao ya kimkakati ambayo Serikali imeamua kuboresha mazingira ya uzalishaji pamoja na masoko ili kumnufaisha mkulima.

*(Hapa king'ora cha kuashiria hatari kililia)*

**WABUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, dharura, dharura.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba nisitishe shughuli za Bunge kwa muda mfupi.

*(Saa 5.16 Asubuhi Bunge lilisitishwa)*

*(Saa 06.02 Mchana Bunge lilirudia)*

*Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alikalia Kiti*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba, tukae. Poleni sana kwa yaliyotokea. Wataalam wetu wanaendelea kufanyika kazi na tutakapojua sababu ilikuwa nini tutaambia. Mpaka sasa hivi hakuna sababu ambayo ipo *obvious* ya ving'ora vile kuweza kulia kwa kiasi hicho.

Waheshimiwa Wabunge, kipindi cha maswali kimepita na muda wake umepita, kama kuna swali lilibaki basi tutalifanyia utaratibu baadaye kidogo. Ili tuweze kuokoa muda, sasa tunaendelea moja kwa moja katika hatua inayofuata, Katibu.

**NDG. MOSSY LUKUVI - KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA KAMATI**

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii Kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2018**

**na**

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2018**

**SPIKA:** Ahsante. Mwenyekiti wa Kamati, tafadhali na nitaomba *presentation* iwe ya robo saa, kwa sababu kila Mbunge ana nakala. Mheshimwa Kiruswa, tafadhali jitahidi sana kwenda moja kwa moja kwenye maoni na mapendekezo, karibu.

**MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII):** Mheshimwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi, nitajitahidi kutumia hiyo robo saa kuwasilisha yale mambo ya msingi yaliyopo kwenye taarifa ya shughuli za Kamati ya

Ardhi, Maliasili na Utalii kwa mwaka 2018. Taarifa hii imetolewa chini ya Kanuni ya 117(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016.

Mheshimwa Spika, naomba ripoti yetu hii yote iingie katika *Hansard*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kwanza, ni maelezo ya jumla, utangulizi. Kwa mujibu wa Kanuni ya 117(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo Januari 2016, naomba kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Kamati kwa kipindi cha kuanzia Januari 2018 hadi Januari, 2019 ili iweze kujadiliwa na kuridhiwa Bunge.

Mheshimwia Spika, taarifa hii ina sehemu kuu nne. Sehemu ya Kwanza, inaelezea utangulizi; Sehemu ya Pili, inaelezea utekelezaji wa majukumu ya Kamati kwa kipindi cha mwaka 2018/2019 na matokeo yaliyobainishwa; Sehemu ya Tatu, inaelezea maoni na mapendekezo ya Kamati; na Sehemu ya Nne na mwisho ni hitimisho.

Mheshimiwa Spika, majukumu ya Kamati. Majukumu ya Kamati yameainishwa katika Nyongeza ya Nane chini ya Kanuni ya 118, kifungu cha 6(6) cha Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo 2016, kuwa nanukuu: "Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii itasimamia shughuli za Wizara mbili nazo ni:-

(a) Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; na

(b) Wizara ya Maliasili na Utalii".

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa majukumu yaliyotekelezwa na Kamati. Kamati ilifanya ziara katika maeneo mbalimbali kwa lengo la kujiridhisha na hali halisi ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya baadhi ya Taasisi zilizo chini ya Wizara inazozisimamia. Nitataja tu hizo ziara bila kutoa maelezo marefu kwamba tulifanya ziara katika Mapori ya Akiba ya Biharamulo, Burigi na Kimisi. Pia tulifanya

ziara katika Hifadhi ya Taifa ya Serengeti ambapo Makamu wa Rais, Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan alizindua Jeshi USU ambalo sasa linakwenda kusimamia shughuli za uhifadhi kwa kudhibiti ujangili katika Hifadhi zetu za Taifa, Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania.

Mheshimiwa Spika, tulifanya ziara pia katika Hifadhi ya Taifa ya Mikumi. Katika hifadhi hii tulipata mfano hai wa hifadhi moja ambayo imeweza kumaliza migogoro yote kati yake na vijiji vinavyoizunguka. Tunaziomba hifadhi nyingine zote ziende kujifunza kutoka kwako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia tulifanya ziara katika Hifadhi ya Taifa ya Ruaha. Kamati ilifanya ziara hiyo tarehe 22 Januari, 2019 na kubaini miongoni mwa changamoto mbalimbali ni tishio la kukauka kwa Mto Ruaha Mkuu na mgogoro wa mpaka kati ya hifadhi na vijiji vinavyopaka navyo na ubovu na miundombinu hususani ya barabara na uhaba wa sehemu ya malazi kwa watalii.

Mheshimiwa Spika, pia tulifanya ziara katika Shamba la Miti la Sao Hill ambapo Kamati baada ya kupata taarifa inashauri Serikali kuongeza kazi ya upandaji wa miti kwa kufungua mashamba ya miti sehemu nyingine nchini. Aidha, Kamati inashauri Serikali kukuhakisha kwamba inajenga mahusiano mazuri na jamii inayozunguka mashamba ya miti ili kuwa na ulinzi shirikishi na kupunguza matukio ya wananchi kuchoma moto misitu ya Serikali kutokana na sababu mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, tulifanya ziara pia katika Makumbusho ya Taifa ya Kalenga. Kamati ya Bunge inapenda kumpongeza Mkuu wa Kituo hicho Bwana Eric Jordan kwa umahiri wake wa kuelezea historia ya Kabila la Wahehe na ushujaa wa Chifu Mkwawa aliyewasambaratisha Wajerumani walipojaribu kuwateka Wahehe kwa mara ya kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Kamati ilifanya ziara katika maeneo yafuatayo: Ziara katika mpaka wa Tanzania na Uganda; ziara katika Miradi ya Shirika la Nyumba la Taifa (NHC); ziara katika Programu ya Urasimishaji Makazi Holela katika Mkoa wa Dar es Salaam; na ziara katika Programu ya Upimaji na Umilikishaji Ardhi katika Wilaya za Kilombero, Malinyi na Ulanga.

Mheshimiwa Spika, pia tulifanya mikutano mbalimbali ikiwepo Mikutano na Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi ambapo pamoja na taarifa zingine tulipata taarifa kuhusu maendeleo ya mashamba makubwa na hatua zinazochukuliwa na Serikali kwa mashamba yaliyotelekezwa. Pia tulipata taarifa kuhusu migogoro ya ardhi nchini. Kumekuwepo na ongezeko kubwa la migogoro ya ardhi inayotokana na sehemu kubwa ya ardhi ya nchi yetu kutokupimwa na kupangiwa matumizi na hivyo kusababisha mgongano baina ya watumiaji mbalimbali wa ardhi. Aidha, mashamba makubwa yaliyotelekezwa yamekuwa kichocheo cha migogoro kwa sababu wakulima na wafugaji wasio na ardhi wamekuwa wakiyavamia na kuyatumia bila kuwa na kibali maalum.

Mheshimiwa Spika, kipekee Kamati inatumia fursa hii kusema kwamba tunampongeza Rais Dkt. John Joseph Magufuli kwa tamko lake la karibuni la kuwataka Mawaziri wa sekta husika kuhakikisha wanamaliza migogoro katika muda aliowapangia. Kamati inaamini kuwa hii ni hatua muhimu ya kumaliza migogoro ya ardhi hapa nchini. Hivyo, Kamati inashauri zoezi hilo zoezi hili liratibiwe vizuri ili kupata matokeo yaliyotarajiwa. *(Makofi)*

Mheshimimiwa Spika, pia Kamati ilipokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa Fedha 2017/18, pamoja na mapendekezo ya mapato na matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka 2018/2019 na kuiwasilisha Bungeni.

Mheshimwa Spika, Kamati ilipata fursa ya kukutana na Wizara ya Maliasili na Utalii na kupokea na kujadili taarifa mbalimbali. Miongoni mwa taarifa hizo kuna taarifa za utekelezaji wa Mradi wa Kuendeleza Utalii Kusini mwa Tanzania unaojulikana kama *REGROW.* Pia kulikuwa na na taarifa kuhusu maendeleo ya Mradi wa Kuongeza idadi ya Faru katika Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi na kulikuwa na taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Maliasili kwa mwaka 2017/2018 na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka 2018/2019 na kuwasilisha Bungeni.

Mheshimimiwa Spika, pia tulipata taarifa kuhusu changamoto ya viumbe wageni vamizi katika maeneo yaliyohifadhiwa na hata ndani ya jamii. Tumejifunza kwamba *Invasive and Allien Species* ni pamoja na wanyama, wadudu, ndege, samaki na mimea ambayo imestawi na kujiimarisha katika sehemu ambazo siyo asili yake na kudhoofisha au kusababisha kutoweka kwa viumbe vya asili katika maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, pia kulikuwa na taarifa kuhusu utendaji wa Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori cha Mweka ambapo tumebaini kuwa bajeti inayotengwa ni ndogo; kuna upungufu mkubwa wa watumishi; uchakavu wa miundombinu na kupungua kwa wanafunzi wa kigeni wanasoma katika chuo hicho. Kamati imeitaka Serikali kufanya kila liwezekanalo kuongeza bajeti ya chuo hiki ili kiendeleee kujiendesha kwa ufanisi. Kwa maana takwimu inaonyesha kwamba 90% ya wataalam wabobezi katika masuala ya wanyamapori wamepitia katika chuo hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende moja kwa moja kwenye eneo la mapendekezo ya Kamati. Katika Sehemu ya Tatu ya ripoti yetu kuna maoni na mapendekezo ya Kamati, kama ifuatavyo:-

(i) Kuhusiana na suala la utengaji na upelekaji wa fedha za bajeti, Kamati inaishauri Bunge kuitaka Serikali kuandaa mkakati maalum wa kutenga fedha za kutosha

kwenye bajeti itakayowezesha uendeshaji na ukamilishaji wa miradi ya upimaji, upangaji na urasimishaji wa ardhi nchi.

(ii) Kuhusu tishio la kukauka kwa Mto wa Ruaha Mkuu, Kamati inalishauri Bunge kuitaka Serikali kuchukua hatua za haraka kuunusuru Mto wa Ruaha Mkuu usikauke kwa manufaa mapana ya Taifa.

(iii) Kuhusu utitiri wa ukubwa wa tozo katika huduma za kitalii nchini, Kamati inalishauri Bunge kuitaka Serikali kuangalia upya utitiri wa tozo na hata ukubwa wake kwenye huduma za utalii nchini ili kuifanya sekta hii kuwa na tija zaidi.

(iv) Kuhusu usimamizi wa rasilimali za misitu nchini, Kamati inalishauri Bunge kuitaka Serikali kuipandisha hadhi Wakala wa Misitu Tanzania kuwa Mamlaka ya Misitu Tanzania ili kuipa nguvu ya kisheria ya kusimamia na kudhibiti matumizi ya rasilimali ya misitu nchini. *(Makofi)*

(v) Kuhusu kusimama kwa baadhi ya miradi ya Shirika la Nyumba la Taifa *(NHC),* Kamati inalishauri Bunge kuitaka Serikali kukamilisha taratibu zitakazoliwezesha Shirika kupata fedha ili kumalizia miradi iliyosimama iweze kuletea tija. *(Makofi)*

(vi) Kuhusu Mradi wa Kuendeleza Ukanda wa Kusini Kiutalii *(REGROW),* Kamati inalishauri Bunge kuitaka Serikali kukamilisha mazungumzo na *World Bank* mapema ili mradi uweze kuanza kutekelezwa.

(vii) Kuhusu barabara ya lami inayopita katikati ya Hifadhi ya Mikumi, Kamati inalishauri Bunge kuitaka Serikali kujenga barabara ya mchepuko ili magari yapite nje ya Hifadhi. Hali hii itawanusuru wanyama wetu ambao kwa siku wanauliwa walau mnyama mmoja na itaongeza mapato kwa watalii ambao baada ya barabara ya mchepuko kujengwa, wakiamua kupita ndani ya *park* wataweza kutozwa tofauti na ilivyo sasa hivi.

(viii) Kuhusu mkakati wa kupambana na viumbe wageni vamizi, Kamati inalishauri Bunge kuitaka Serikali kuweka mkakati wa kitaifa wa kukabiliana na athari za viumbe wageni vamizi kuliko ilivyo sasa kila taasisi inapambana peke yake.

Mheshimiwa Spika, hitimisho. Kwanza nikushukuru wewe na niseme mafanikio ya Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii ambapo tumeweza kutekeleza majukumu yetu kwa mwaka 2018 yametokana na ushirikiano wa dhati kati ya Mawaziri wa Wizara zote mbili na Naibu wao na watendaji wa Wizara hizo.

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Stephen Kagaigai pamoja na Sekretarieti ya Kamati hii Ndugu Athumani Hussein, Ndugu Dickson Bisile, Ndugu Gerald Magili, Ndugu Haika Mtui na Ndugu Mwimbe John kwa kuratibu shughuli zote za Kamati kwa kipindi chote cha mwaka 2018.

Mheshimiwa Spika, kipekee pia napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati hii, majina yao yote sitaweza kusoma lakini nilishaomba yaingizwe kwenye Hansard. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuelezea shughuli zilizotekelezwa, uchambuzi na matokeo ya utekelezwaji wa shughuli za Kamati, maoni na mapendekezo, sasa naomba kutoa hoja kwamba Bunge lipokee na kuikubali Taarifa ya Kamati ya Bunge Ardhi, Maliasili na Utalii kwa mwaka 2018 pamoja na maoni na mapendekezo yaliyomo katika taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

# TAARIFA YA SHUGHULI ZA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI MALIASILI NA UTALII KWA MWAKA 2018 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

---

[*Imetolewa Chini ya Kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016]*

## SEHEMU YA KWANZA

## MAELEZO YA JUMLA

## 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Kamati kwa kipindi cha kuanzia Januari 2018 hadi Januari 2019, ili iweze kujadiliwa na kuridhiwa na Bunge.

Taarifa hii ina Sehemu Kuu Nne. Sehemu ya **Kwanza** inaelezea Utangulizi, Sehemu ya **Pili** inaelezea utekelezaji wa majukumu ya Kamati, kwa kipindi cha Mwaka 2018/2019 na matokeo yaliyobainishwa. Sehemu ya **Tatu** inaelezea maoni na mapendekezo ya Kamati, na Sehemu ya **Nne** ni hitimisho.

### 1.1 Majukumu ya Kamati

**Mheshimiwa Spika,** majukumu ya Kamati yameainishwa katika Nyongeza ya Nane chini ya kanuni ya 118, kifungu cha 6 (6) cha Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo 2016, kuwa:-

*"...Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii itasimamia shughuli za Wizara mbili nazo ni*

*(a)Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; na*

*(b) Wizara ya Maliasili na Utalii".*

**SEHEMU YA PILI**

## 2.0 UCHAMBUZI WA MAJUKUMU YALIYOTEKELEZWA NA KAMATI

### 2.1 ZIARA

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifanya ziara katika maeneo mbali mbali kwa lengo la kujiridhisha na hali halisi ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo na utendaji wa baadhi ya Taasisi zilizo chini ya Wizara inazozisimamia.

#### 2.1.1 Ziara Katika Mapori ya Akiba ya Biharamulo,Burigi na Kimisi

**Mheshimiwa Spika,** kati ya Tarehe 15 hadi 23 Machi,2018 Kamati ilifanya ziiara katika Mapori ya Akiba ya Biharamulo, Burigi na Kimisi kukagua utekelezaji wa miradi ya kuyajengea uwezo Mapori ya Akiba katika kupambana na ujangili. Kamati ilibaini kuwepo changamoto kadhaa ikiwemo miundombinu mibovu ya barabara katika mapori yote hali inayosababisha hali ya ulinzi na shughuli za utalii kuwa ngumu kwa vile maeneo mengi hayafikiki kwa urahisi.

Kwa mfano, katika pori la Akiba la Kimisi ambalo linapakana na nchi ya Rwanda hakuna barabara eneo la mpakani hali inayowapa majangili kutoka nchi jirani urahisi wa kuvamia pori hilo kwa ajili ya kuchunga mifugo na ujangili wa wanyamapori. Aidha, vivutio hivi vya utalii havijaendelezwa vya kutosha kwa kukosa sehemu nyingi za malazi ya kufikia watalii. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuyapandisha hadhi Mapori haya kuwa hifadhi za Taifa. Aidha Kamati inaipongeza Serikali kwa kuunda kamati ya Kitaifa ya kupambana na ujangili jambo ambalo limechangia sana kupunguza ujangili nchini. Ni imani ya Kamati kwamba sasa Serikali itawavutia wawekezaji hususan wa Mahoteli kujenga mahoteli katika hifadhi hizi sambamba na kuimarisha miundombinu ya bara bara ili kufanya sehemu za mapori haya zifikike kwa urahisi na hivyo kuvutia watalii wengi zaidi.

Tunatoa wito kwa Bodi ya Taifa ya Utalii kuzitangaza hifadhi hizi ili zijulikane duniani na zitoe fursa ya kufungua utalii katika kanda ya Ziwa.

### 2.1.2 Ziara Katika Hifadhi ya Taifa ya Serengeti

**Mheshimiwa Spika,** Tarehe 17 Desemba, 2018 Kamati ilialikwa na Waziri wa Maliasili na Utalii kuhudhuria sherehe za uzinduzi wa Jeshi Usu kwa Hifadhi za Taifa, Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania pamoja na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania uliofanyika katika hifadhi ya Taifa ya Serengeti ambapo mgeni Rasmi alikuwa Makamu wa Rais Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan.Kamati inaipongeza Serikali kwa kuanza kutumia mfumo wa Jeshi Usu katika kulinda raslimali za Taifa. Ni matumaini ya Kamati kwamba matukio ya ujangili huenda yakawa yamepata muarobaini wake.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kupitia Shirika la Utangazaji la Taifa kwa kuanzisha ***" Channel"*** ya Tanzania Safari inayotangaza vivutio vya Utalii vya nchi yetu. Pamoja na pongezi hizo Kamati inashauri matangazo hayo yawekwe kwenye ving'amuzi vya Kimataifa kama DSTV ili matangazo yawafikie watazamaji wengi. Aidha matangazo hayo yaangalie vivutio vyote badala ya kutangaza zaidi mbuga za wanayamapori tu.

### 2.1.3 Ziara katika Hifadhi ya Taifa ya Mikumi

**Mheshimiwa Spika,** Tarehe 16 Januari, 2019 Kamati ilifanya ziara ya kikazi na kupokea Taarifa ya utendaji pamoja na utekelezaji wa Programu ya kukuza Utalii Kusini mwa Tanzania katika Hifadhi ya Taifa ya Mikumi. Kamati inaipongeza menejimenti ya Hifadhi ya Taifa ya Mikumi kwa kufanikiwa kumaliza migogoro yote ya mipaka kati yake na vijiji inavyopakana navyo. Ni vyema Hifadhi nyingine zote ambazo bado zina migogoro ya mipaka zikaiga mfano wa hifadhi ya Taifa ya Mikumi kumaliza migogoro yake. Aidha Kamati ilielezwa kuwepo kwa changamoto ambazo zinahitaji hatua za haraka kukabiliana nazo. Miongoni mwa

changamoto hizo ni kugongwa kwa wanyamapori kutokana na barabara kuu kupita kati kati ya hifadhi hiyo**.** Aidha Kamati ilielezwa kuwepo kwa changamoto ya upungufu wa sehemu za malazi kwa ajili ya watalii. Imeelezwa kukosekana kwa sehemu za malazi kumesababisha idadi ya wageni kupungua na hivyo kuikosesha hifadhi mapato.

### 2.1.4 **Ziara katika Hifadhi ya Taifa ya Ruaha**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifanya ziara katika Hifadhi ya Taifa ya Ruaha tarehe 22 Januari,2019 kwa lengo la kukagua utendaji wa hifadhi hiyo na utekelezaji wa programu ya kukuza Utalii Kusini mwa Tanzania inayotekelezwa katika hifadhi hiyo. Kamati imebaini kwamba hifadhi hii inakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

- Tishio la kukauka kwa mto Ruaha Mkuu ambao ndiyo tegemeo kubwa la maji kwa ajili ya wanyamapori;

- Migogoro ya Mipaka kati ya hifadhi na vijiji inavyopakana navyo;

- Ubovu wa miundombinu hususan barabara pamoja na;

- Uhaba wa sehemu za malazi ya watalii.

Kamati inashauri Serikali ifanye kila liwezekanalo kuunusuru mto Ruaha Mkuu usikauke. Taarifa zilizopo ni kwamba kuanzia mwaka 1993 mto ulikuwa unakauka kwa wiki mbili kwa sasa mto Ruaha Mkuu unakauka kwa takriban miezi minne mfano mzuri ni mwaka 2017 mto ulikauka kuanzia mwezi Agosti na kuanza kutiririka tena mwezi Februari 2018 hali inayosababisha wanyamapori kutoka nje ya hifadhi kwenda kutafuta maji na kuchangia kuongezeka kwa matukio ya wanyamapori kushambulia mashamba na binadamu. Aidha ubovu wa miundombinu ya barabara husababisha eneo la hifadhi kutofikika wakati wa masika na hivyo kusababisha kusitishwa kwa shughuli za utalii jambo ambalo husababisha mahoteli kufungwa kwa kipindi chote

hicho kwa kukosa watalii na hivyo kuikosesha Serikali mapato.

### 2.1.5 Ziara katika Shamba la miti la SAO HILL

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipata fursa ya kutembelea na kujionea shughuli mbali mbali zinazofanywa na shamba la miti la SAO HILL. Kamati inapongeza jitihada za Serikali katika kuhakikisha kuwa rasilimali za Misitu zinatunzwa na kuendelezwa. Hata hivyo zipo changamoto kadhaa zinazohitaji kufanyiwa kazi ikiwemo kasi ndogo ya upandaji miti pamoja na matukio ya moto kuunguza misitu yetu. Kamati inaishauri Serikali kuongeza kasi ya upandaji miti kwa kufungua mashamba ya miti sehemu nyingine nchini. Aidha kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inajenga mahusiano mazuri na jamii inayozunguuka mashamba ya miti ili kuwa na ulinzi shirikishi na kupunguza matukio ya wananchi kuchoma moto misitu ya Serikali kutokana na sababu mbali mbali.

### 2.1.6 Ziara katika makumbusho ya Taifa kituo cha Kalenga

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipata fursa ya kutembelea makumbusho ya Taifa kituo cha Kalenga na kupokea taarifa ya Serikali kuhusu utendaji wa kituo hicho. Kamati inampongeza Mkuu wa kituo hicho Bwana Eric Jordan kwa umahiri wake wa kuelezea historia ya Kabila la Wahehe na ushujaa wa Chifu Mkwawa aliyewasambaratisha wajerumani walipojaribu kuwateka Wahehe kwa mara ya kwanza. Kamati inaishauri Serikali kuimarisha mipaka ya eneo hili kwa kuweka alama madhubuti. Aidha kamati inaishauri Serikali kuwekeza zaidi katika eneo hili kwa kuweka vivutio vingine vya utalii ili kuvutia watalii wengi zaidi.Vile vile Kamati inahimiza wananchi kutembelea makumbusho hii ya Chifu Mkwawa ili kujifunza historia ya utawala wa Machifu wetu. Aidha Kamati inaishauri Serikali kuwajengea uwezo waongoza watalii ili waweze kuelezea historia ya nchi yetu

kwa umahiri na weledi hali ambayo itavutia watalii wengi kujifunza historia ya nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Kamati ilifanya ziara katika maeneo yafuatayo**:**

#### 2.1.7 **Ziara katika Mpaka wa Tanzania na Uganda**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipata fursa ya kutembelea mpaka wa Tanzania na Uganda katika eneo la Mutukula na kubaini kuwepo kwa changamoto kadhaa zinazowakabili walinzi wa mipaka yetu. Changamoto kubwa ni kutokuwepo kwa bara bara mpakani hali inayofanya shughuli za ulinzi kuwa ngumu. Aidha kutokuwepo kwa alama madhubuti mipakani kunasababisha wananchi wa nchi jirani kuvamia maeneo ya nchi yetu. Kamati inaishauri Serikali kuimarisha mipaka ya nchi yetu kwa kuweka alama madhubuti.

#### 2.1.8 **Ziara katika Miradi ya Shirika la Nyumba la Taifa (NHC)**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitembelea miradi ya ujenzi wa nyumba za biashara kwa ajili ya kupangisha pamoja na nyumba za makazi kwa ajili ya kuuza zinazotekelezwa na Shirika la Nyumba la Taifa katika maeneo ya Morroco Square na Victoria. Kamati inapongeza jitihada za Shirika kwani fedha zinazopatikana kutokana na miradi hii ndiyo hutumika kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za gharama nafuu katika maeneo mbali mbali nchini. Hata hivyo Kamati ilifahamishwa kuwa Serikali ililiondolea Shirika idhini ya kukopa fedha katika Mabenki ili kutekeleza miradi yake na hivyo kulifanya Shirika lishindwe kumalizia miradi inayoendelea. Taarifa zilizopo ni kwamba miradi mingi ya Shirika imesimama kwa kukosa fedha.

#### 2.1.9 **Ziara katika Mradi wa Mfumo unganishi wa Taarifa za Ardhi (Intergrated Land Management Information System-ILMIS)**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipata fursa ya kukagua maendeleo ya mradi wa kujenga mfumo unganishi wa Taarifa za ardhi unaotekelezwa na Ofisi ya Waziri Mkuu na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa majaribio katika wilaya za Kinondoni na Ubungo. Kamati inaridhishwa na hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa mradi huo. Hata hivyo Kamati hairidhishwi na utaratibu wa Serikali kutenga bajeti ndogo ya fedha za ndani kwa ajili ya kutekeleza miradi ya kimkakati kama huu na badala yake inategemea zaidi fedha za wafadhili hali inayoashiria kuwa wafadhili wakiondoka miradi mingi haitaendelezwa kama ilivyokusudiwa. Ni imani ya Kamati kwamba Serikali itawajengea uwezo wataalam wa kitanzania ili baada ya wafadhili kuondoka mradi uwe endelevu na uweze kusambazwa katika maeneo mengine.

### 2.1.10 Ziara katika Programmu ya urasimishaji makazi holela katika Mkoa wa Dar Es Salaam

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitembelea Mradi wa Urasimishaji makazi holela unaotekelezwa katika jiji la Dar Es Salaam.Kamati hairidhishwi na namna mradi ule unavyotekelezwa. Yapo malalamiko mengi kutoka kwa wananchi hali inayoashiria kwamba Serikali haikuwa imejipanga. Ni imani ya kamati kwamba Serikali itawashirikisha wananchi kwa kuwapa elimu ya kutosha juu ya manufaaa yatakayopatikana kutokana na zoezi hilo pamoja na wajibu wao katika kuchangia gharama za urasmishaji.

### 2.1.11 Ziara katika Programmu ya upimaji na umilikishaji ardhi katika wilaya za Kilombero, Malinyi na Ulanga

**Mheshimiwa SPika**, Kamati ilifanya ziara Mkoani Morogoro katika Wilaya za Kilombero, Malinyi na Ulanga ambako kunatekelezwa mradi wa kuwezesha upimaji na umilikishaji wa ardhi. Mradi huu unatekelezwa kwa majaribio katika Wilaya nilizozitaja na ulipangwa kutelezwa kwa miaka mitatu kuanzia Januari, 2016 hadi Juni 2019.Fedha zilizotengwa kwa ajili ya mradi ni shilingi bilioni **28,000,000,000** fedha za nje

na shilingi bilioni saba **7,000,000,000** fedha za ndani. Hadi wakati Kamati inafanya ziara jumla ya shilingi billion **25,127,902,152** fedha za nje sawa na asilimia 90% na shilingi Milioni **710,000,000** fedha za ndani sawa na asilimia 10% zilikuwa zimetolewa. Kwa kunagalia mwenendo wa utoaji wa fedha za ndani ni dhahiri kuwa Serikali haiwezi kufikia malengo ya kupima kila kipande cha ardhi ya nchi yetu hasa baada ya wafadhili kuondoka.

**Mheshimiwa Spika**, Programu hii ina manufaa mengi kwani siyo tu imechangia kupunguza migogoro ya ardhi bali pia inawawezesha wananchi kiuchumi kwani hati za haki miliki za kimila wanazopewa zinaweza kutumika kama dhamana ya kukopa benki. Ni matarajio ya Kamati kwamba Serikali itaweka mkakati maalum utakaowezesha kupima na kumilikisha ardhi yote ya nchi yetu. Hali hiyo itaiongezea serikali mapato hasa katika ardhi za mijini kwani itakuwa rahisi kukusanya kodi ya pango la ardhi.

## 2.2 MIKUTANO

### 2.2.1 Mikutano na Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi

Kamati ilikutana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa nyakati tofauti, kupokea na kujadili taarifa mbalimbali zilioletwa mbele ya Kamati kama ifuatavyo;-

**1. Taarifa kuhusu Migogoro ya Ardhi nchini**

**Mheshimiwa Spika,** kumekuwepo na ongezeko kubwa la migogoro ya ardhi inayotokana na sehemu kubwa ya ardhi ya nchi yetu kutokupimwa na kupangiwa matumizi na hivyo kusababisha mgongano baina ya watumiaji mbalimbali wa ardhi. Aidha mashamba makubwa yaliyotelekezwa yamekuwa kichocheo cha migogoro kwa

sababu wakulima na wafugaji wasio na ardhi wamekuwa wakiyavamia na kuyatumia bila kuwa na kibali maalum.

Ni vyema Serikali ikaweka mkakati wa kitaifa ili kuhakikisha kuwa ardhi yote inapimwa na kupangiwa matumizi hali ambayo itachangia kupunguza migogoro ya ardhi nchini. Kipekee Kamati inampongeza Rais Dkt. John Joseph Magufuli kwa tamko lake la hivvi karibuni la kuwataka Mawaziri wa Sekta husika kuhakikisha wanamaliza migogoro katika muda aliowapangia. Kamati inaamini kuwa hii ni hatua muhimu ya kumaliza migogoro ya ardhi hapa nchini. **Kamati inashauri zoezi hili liratibiwe vizuri ili kupata matokeo yaliyotarajiwa.**

**2. Taarifa ya Utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka 2016/ 2017 pamoja na mapendekezo ya Mapato na Matumizi ya wizara hiyo kwa Mwaka 2017/2018**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa Fedha 2017/18, pamoja na mapendekezo ya mapato na matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka 2018/19 na kuiwasilisha Bungeni.

2.2.2 **Mikutano na Wizara ya Maliasili na Utalii**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipata fursa ya kukutana na Wizara ya maliasili na Utalii na kupokea na kujadili Taarifa mbali mbali zilizowasilishwa na Wizara. Katika mikutano hiyo, taarifa zifuatazo zilijadiliwa:-

(1) **Taarifa kuhusu Utekelezaji wa mradi wa kuendeleza Utalii kusini mwa Tanzania (REGROW)**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya Serikali kuhusu programu ya kuendeleza Utalii kusini mwa Tanzania itakayotekelezwa kwa fedha za mkopo kiasi cha Dola za Kimarekani miliioni mia moja na hamsini (USD 150,000,000**) sawa na Shilingi za Kitanzania biliioni miatatu**

**na ushei** kutoka Benki ya Dunia.Mradi huu una malengo yafuatayo:-

(a) Kuboresha miundo mbinu ya bara bara na viwanja vya ndege katika hifadhi zetu zilizoko kusini hususan Hifadhi za Taifa za Mikumi, Udzungwa, Ruaha pamoja na Pori la Akiba la Selous.

(b) Kuongeza mtiririko wa maji katika mto Ruaha Mkuu ambao ni roho ya hifadhi ya Taifa ya Ruaha pamoja na mabwawa ya kufua umeme ya Mtera, Kidatu na Stieglers Gorge. Inakadiriwa kuwa Mto Ruaha Mkuu unachangia asilimia 25% katika mradi wa kufua umeme wa Stieglers baada ya Kidatu na Mtera. Hata hivyo kutokana na shughuli za kilimo cha mpunga katika bonde la Ihefu na Usangu kumesababisha mto Ruaha Mkuu kukauka kwa takriban miezi minne kwa mwaka hali inayotishia uhai wa wanyamapori katika hifadhi ya Taifa ya Ruaha pamoja na mabwawa ya kufua umeme ya Mtera, Kidatu na hatimaye mradi wa Stieglers.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuwa utekelezaji wa mradi huu unasuasua kutokana na Serikali kukiuka baadhi ya makubaliano ya awali na Benki ya Dunia**.**

(2) **Taarifa kuhusu Maendeleo ya mradi wa kuongeza idadi ya Faru katika Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Maliasili na Utalii kuhusu mradi wa kuongeza idadi ya Faru Weusi katika hifadhi ya Taifa ya Mkomazi. Kamati inapongeza juhudi za Serikali za kuongeza idadi ya Faru na Mbwa mwitu wanyamapori ambao wako katika hatari ya kutoweka. Hata hivyo Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto kadhaa ikiwemo ukosefu wa miundo mbinu ya maji ambayo inaongeza gharama za kuwatunza wanyama hao, kodi nyingi zinazotozwa kwa wanyamapori hao pamoja na vifaa vinavyotolewa kama msaada na wahisani hali inayowakatisha tamaa wahisani kuendelea kutoa misaada, na hivyo kuathiri uendelevu wa mradi baada

ya wahisani kuondoka kwani bajeti inayotengwa na Serikali ni ndogo.

Kamati inaishauri Serikali kutenga bajeti ya ndani ya kutosha kwa ajili ya kutekeleza mradi, kuchimba visima vya maji ili kupunguza gharama ya kutoa maji mbali, kuondoa kodi kwa wanyama na vifaa vinavyotolewa na wahisani kama msaada.

(3) **Taarifa ya Utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka 2017/2018 pamoja na makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa Mwaka 2018/2019**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya utekelezaji wa bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2017/18, pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2018/19 na kuiwasilisha Bungeni.

(4) **Taarifa kuhusu uendelezaji wa Raslimali za Misitu Nchini**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea taarifa kuhusu maendeleo ya rasilimali ya Misitu na Nyuki nchini.Katika taarifa hiyo Kamati ilibaini kuwepo kwa changamoto inayotokana na mfumo wa usimamizi na mgawanyo wa raslimali za misitu ambao kwa kiasi kikubwa unaleta mgongano na mwingiliano katika kusimamia raslimali hizo. Mfano:-

- Serikali kuu kupitia Wakala wa Misitu inamiliki na kusimamia misitu yenye hekta 15.84 millioni sawa na asilimia 35
- Serikali za vijiji hekta 21.6 millioni sawa na asilimia 45
- Serikali za Mitaa hekta 3.36 millioni sawa na asilimia 7
- Sekta binafsi hekta 3.36 sawa na asilimia 7
- Ardhi ya jumla hekta 2.4 millioni sawa na asilimia 5 na,

· Ardhi za miliki nyingine hekta 480.000 sawa na asilimia 1

Takwimu zinaonyesha kuwa Serikali za vijiji na Serikali za mitaa kwa pamoja zinamiliki asilimia 52 wakati Serikali kuu inamiliki na kusimamia asilimia 35 tu. Aidha uharibifu mkubwa wa misitu unatokea katika misitu ya Serikali za vijiji na ile ya Serikali za mitaaa.

Kamati inashauri kuwa ili kukabiliana na changamoto hii ni **vema usimamizi wa raslimali za misitu zisimamiwe na Mamlaka moja yenye nguvu lakini umiliki wa misitu hiyo ubaki kwa wahusika.**

(5) **Taarifa Kuhusu Changamoto ya viumbe wageni vamizi katika maeneo yaliyohifadhiwa**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Maliasili na Utalii kuhusu atahari za viumbe wageni vamizi katika maeneo yaliyohifadhiwa. Ilielezwa kwamba viumbe wageni vamizi (***Invasive and Allien Species***) ni wanyama, wadudu, ndege, samaki au mimea ambayo imestawi na kujiimarisha katika sehemu ambazo siyo asili yake na kudhoofisha au kusababisha kutoweka kwa viumbe vya asili katika maeneo husika.

Mifano iliyotolewa ni magugu maua ambayo yamestawi sana katika Ranchi ya kongwa na kuchukua eneo kubwa la malisho ya mifugo,magugu ambayo yamestawi sana katika hifadhi zetu za wanyamapori hasa katika Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro ambapo magugu yameenea sehemu kubwa ya hifadhi na kupunguza eneo la malisho ya wanyamapori hivyo kusababisha wanyama wengi kurundikana katika eneo dogo, miti ambayo imevamia hifadhi zetu za misitu ya asili na kutishia kutoweka kwa baadhi ya miti ya asili, kunguru weusi wa Zanzibar,ambao wanakula mayai na makinda ya ndege wengine na kutishia kutoweka kwa aina nyingine za ndege hususan katika visiwa vya Zanzibar, Samaki sangara katika ziwa victoria ambaye amesababisha aina ya samaki zaidi ya mia mbili kutoweka

katika ziwa Victoia, viwavi jeshi vinavyoshambulia nafaka hasa mahindi na vingine vingi.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuangalia athari zinazoletwa na viumbe wageni vamizi utagundua kuwa hili ni janga la kitaifa na kimataifa ambalo linahitaji mkakakti maalum wa kukabiliana nalo. **Kamati inaipongeza Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kuanza kuchukua hatua kwa kuunda Kamati ya wataalam kushughulikia jambo hili.**

(6) **Taarifa kuhusu utendaji wa Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori cha Mweka**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Maliasili na Utalii kuhusu utendaji wa Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapri cha Mweka.Kamati ilibaini kuwepo kwa changamoto kadhaa zikiwemo bajeti ndogo inayotengwa kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za chuo, upungufu wa watumishi, uchakavu wa miundombinu kwani majengo yake ni ya zamani sana, upungufu wa vyumba vya madarasa, na kushuka kwa idadi ya wanafunzi kutoka nje ya nchi ikilinganishwa na miaka ya nyuma. Kutokana na changamoto hizi Kamati inaitaka Wizara ya maliasili na Utalii kuongeza bajeti ya chuo hiki ili kiweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Takwimu zinaonyesha zaidi ya asilimia 90% ya wataalam wabobezi katika masuala ya wanyamapori wamepita katika chuo hiki. Hivyo ni vyema Serikali ikakienzi chuo hiki kwa kuhakikisha kinakuwa na miundombinu bora ili kirejeshe hadhi yake inayoelekea kupotea. Kuhusu kupungua kwa idadi ya wanafunzi kutoka nje, Kamati inaitaka Wizara ya Maliasili na Utalii kukaaa pamoja na Wizara ya Elimu kuona jinsi gani ya kuongeza udahili wa wanafunzi wa nje kwa kuweka vigezo rafiki vitakavyowawezesha wanafunzi kutoka nje ya nchi kudahiliwa bila kuwekewa vikwazo. Ilielezwa kwamba baadhi ya sifa za kitaaluma walizonazo wanafunzi kutoka nje hazitambuliwi na Tume ya vyuo vikuu. Mfano wanafunzi kutoka Rwanda katika mitaala yao wanasoma somo la Utalii katika kidato cha tano na sita

lakini somo hilo halitambuliwi na Tume yetu ya Vyuo vikuu na hivyo kuwakosesha udahili baadhi ya wanafunzi kutoka nje.

### 2.2.3 Mkutano na Wadau wa Utalii nchini

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipata fursa ya kukutana na wadau wa utalii nchini na kupokea maoni yao kuhusu changamoto mbali mbali zinazoikabili sekta ya utalii nchini. Changamoto zilizoibuliwa na wadau ni hizi zifuatazo:-

(1) Utozaji wa kodi ya ongezeko la thamani (VAT) katika huduma mbalimbali za Utalii, zinaifanya "Destination Tanzania" kuwa ghali sana ikilinganishwa na washindani wake hususan Kenya, Zambia, Zimbabwe na Msumbiji.Ukiachia suala la kutoza VAT ,kutokuwa na safari za ndege za moja kwa moja kutoka nje hadi hapa nchini pia kunachangia kuwaongezea watalii gharama za safari. Hivyo kuna haja ya Serikali kuliangalia suala hili kwa makini ili kuongeza mchango wa utalii katika pato la Taifa. Serikali iweke utaratibu mzuri na uratibu katika kupanga tozo mbalimbali katika huduma za utalii. Aidha wakati umefika kwa Shirika letu la Ndege ( ATCL ) kutumia ndege zake kupanga safari ambazo zitawaleta watalii moja kwa moja nchini kwetu kuliko ilivyo sasa watalii wengi hutua nchi jirani kabla ya kufika Tanzania.

(2) Utalii wa Kitamaduni (*Cultural Tourism)* ni eneo ambalo likiwekewa mikakati thabiti linaweza kuliingizia Taifa mapato mengi. Kwa sasa Sekta hii haifanyi vizuri kutokana na kuwa ni ngeni na hiatambuliki na wengi. Serikali inatakiwa kurasimisha na kuiwekea Sheria, Kanuni na Taratibu zitakazowezesha kusajili wahusika na kurahisisha ukusanyaji wa mapato yatokanayo na Utalii wa Kiutamaduni;

(3) Utaratibu wa kuingia hifadhini kwa mfumo wa "Single Entry" uangaliwe kwa mapana yake ili uweze kuinufaisha Serikali kwa upande mmoja na Wadau wengine kwa upande mwingine. Utaratibu huu umeelezwa kuzikosesha Jumuiya za hifadhi za wanyamapori (WMA's)

mapato kwa vile watalii wanapotoka hifadhini kwenda sehemu nyingine kama vile kwenye maeneo yenye Utalii wa kitamadunii ndani ya masaa 12 hutakiwa kulipia tena ada ya kuingilia hifadhini. Hali hii imechangia kutovutia Wawekezaji kuwekeza katika WMA's na hivyo kuzoofisha WMA'S nyingi kwa kukosa mapato. **Kamati inaishauri Serikali kutumia mfumo wa " Biometric" kwa watalii wanaoingia hifadhini ili hata wakitoka na kurudi waweze kutambulika kwa urahisi.**

(4) Kupunguzwa kwa muda wa Umiliki vitalu kutoka miaka mitano hadi miwili (2) kumesababisha vitalu vingi kurudishwa na mapato yameshuka sana kutoka USD milioni 27 mwaka 2008 hadi USD milioni 8 mwaka 2018. Hali hii imesababisha shughuli za uhifadhi kuzorota na kutishia kuongezeka kwa ujangili wa wanyamapori, misitu, uvamizi wa mifugo na shughuli za kilimo. Kamati inaitaka Serikali kuchukua hatua za haraka kuinusuru Sekta hii kwa kuwaruhusu Wamiliki waliokwishahuishiwa leseni zao kumiliki vitalu kwa miaka mitano yaani 2018 hadi 2022 au kuwalipa fidia wale waliofanya Uwekezaji kabla ya kuvitwaa na kuvigawa kwa njia ya mnada. Aidha ilielezwa ada za Uwindaji ziko juu ikilinganishwa na nchi jirani hali iliyosababisha kushuka kwa idadi ya wawindaji wa kitalii kutoka 1500 hadi kufikia 475;

(5) Serikali haina mitaala maalum kwa ajili ya kufundishia waongoza Watalii (Tour Guides) na Wapagazi (Porters) watu ambao hukaa muda mrefu na Watalii. Hili ndio kundi linalotoa taswira ya nchi yetu kwa Wageni hivyo wasipoandaliwa vizuri watachangia kupungua kwa Utalii nchini;

(6) Imebainika kwamba baadhi ya Makampuni hayawapi mikataba maalum Waongoza Watalii na wapagazi hali inayofanya wawe na mazingira magumu ya kazi. Aidha ilielezwa kuwa Wanahitaji kukatiwa bima ya afya na bima ya mazingira magumu ya kazi. **Kamati inaitaka Serikali kuweka Sheria na Kanuni zitakazowabana Waajiri**

**kuwapa mazingira mazuri ya kazi Waongoza Watalii na Wapagazi;**

(7) Dhana ya Uhifadhi Shirikishi wa Wanyamapori kupitia Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori (WMA's) haijapewa uzito unaostahili usimamizi mbovu wa WMA umeshindwa kuwanufaisha Wananchi. Aidha, ilielezwa mgawanyo wa mapato na urejeshwaji wa Fedha kutoka Serikali kwenda kwa WMA's siyo rafiki. **Kamati inaishauri Serikali kuboresha Usimamizi wa WMA's kwa kubadili mfumo wa uendeshaji wake ili uendane na wakati uliopo.**

2.2.4 **Mkutano na Wadau wa Misitu Mufindi**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipata fursa ya kukutana na wadau wa misitu wilayani Mufindi na kupokea maoni yao kuhusiana na changamoto mbali mbali katika sekta ya misitu kama ifuatavyo:-

(1) Sharti la kusafirisha mazao ya misitu hasa mbao wakati wa mchana tu na kuzuiliwa kusafirisha wakati wa usiku linawaongezea gharama za usafirishaji na kuwapunguzia ushindani katika soko kwani bidhaa hazifiki kwa wakati muafaka. **Serikali iangalie uwezekano wa kubadili utaratibu huu kama ilivyofanya katika usafirishaji wa nguzo.**

(2) Utozwaji wa kodi ya ushuru wa mazao kusikokuwa na uwiano kunawanyima wafanyabiashara nguvu ya ushindani katika soko. Mfano ilielezwa katika Halmashauri nyingine ushuru wa mazao (CES) hutozwa kati ya asilimia 2-3 wakati katika Halmashauri ya Mufindi na Mji wa Mafinga hutozwa kwa asilimia 5%. Hivyo wafanyabiashara kutoka Kilimanjaro na wale wa kutoka mufindi wakikutana katika soko moja wale wa asilimia 5 mbao zao zinakuwa ghari ikilinganishwa na wale wa asilimia 2-3%. **Kamati inashauri Serikali kuweka uwiano sawa wa tozo ya ushuru wa mazao katika Halmashauri zote.**

(3) Utitiri wa kodi kwa maana ya kodi nyingi na ukubwa wa kodi yaani kiasi kinachotozwa kwa

wafanyabiashara zinachangia ongezeko la bei za bidhaa kwani mfanyabiashara lazima azijumlishe gharama zake zote hivyo kumuumiza mlaji wa mwisho. Inashauriwa Serikali iziangalie upya kodi hizi ili zile zilizopitwa na wakati izifute na zile ambazo ni kubwa zipunguzwe pia uwekwe utaratibu wa kulipa kodi zote katika kituo kimoja badala ya utaratibu wa sasa ambapo kodi zinalipwa katika maeneo tofauti totauti.

(4) Mikataba ya mwaka mmoja mmoja kwa vibali vya kuvuna miti kunawanyima wafanyabiashara hasa wadogo fursa ya kuendelea kwani anakuwa hana uhakika kama mwakani atapata. **Ni vyema mikataba ikawa ya miaka mitatu hadi mitano ili kuwawezesha wafanyabiahara kukopa benki na kuwa na fursa ya kurejesha mikopo yao**.

(5) Kuwe na uwazi katika ukusanyaji na matumizi ya Kodi ya kusaidia kuendeleza mashamba ya miti (LMDA). Kwa utaratibu wa sasa wadau hawajui imekusanywa kiasi gani na imetumikaje.

2.2.5 **SEMINA**

**Mheshimiwa Spika,** katika nyakati tofauti**,** Kamati ilipewa Semina mbali mbali na Wizara ya Maliasili na Utalii katika mada zifuatazo:-

(a) Kodi ya ongezeko la thamani katika huduma za utalii
(b) Changamoto za uvamizi wa mifugo na kilimo katika maeneo ya hifadhi
(c) Hali halisi ya maeneo ya Jumuiya za hifadhi za wanyamapori
(d) Hali ya uwindaji wa nyara
(e) Mfumo wa ukusanyaji mapato kwa njia ya Kielektroniki
(f) Kanuni za udhibiti wa wafanyakazi katika Tasnia ya Utalii; na
(g) Uanzishwaji wa Studio ya utangazaji utalii kimtandao (E_Marketing Studio)

Aidha Kamati kupitia ufadhili wa mradi wa kuwajengea uwezo wabunge LSP II ilipatiwa semina kupitia chama cha Wabunge marafiki wa Mazingira (TAPAFE) kuhusu umuhimu wa maeneo yaliyohifadhiwa pamoja na misitu asilia katika kuhifadhi bioanuwai.

Kutokana na mafunzo ambayo Kamati imeyapata katika Semina hizo, Kamati inaishauri Serikali mambo yafuatayo:-

(a) Serikali ifanye utafiti wa kutosha kuhusu kutoza kodi ya ongezeko la thamani (VAT) katika huduma za utalii kama haiathiri idadi ya watalii wanaokuja nchini kwani inadaiwa kodi hiyo inafanya Tanzania kuwa "expensive Destination "ikilinganishwa na nchi nyingine.

(b) Serikali iwatengee wafugaji maeneo yao maalum pamoja na kuwajengea miundombinu muhimu ili wasiendelee kuvamia maeneo ya hifadhi na kusababisha uharibifu mkubwa wa mazingira.

(c) Serikali ibadili mfumo wa uendeshaji wa Jumuiya za Hifadhi za wanyamapori ili ziwe na ufanisi.

(d) Serikali itoe elimu kwa wananchi juu ya umuhimu wa maeneo yaliyohifadhiwa ili waweze kuyatunza na kuyalinda kwa manufaa makubwa ya taifa na kwa faida ya vizazi vya sasa na vijavyo.

(e) Serikali iweke utaratibu wa kuwapatia mafunzo watumishi katika Tasnia ya utalii hususan waongoza watalii ili kuwajengea weledi na umahiri kisha kuwasajili ili kujihakikishia kwamba watu wanaongoza watalii ni mahiri kwani wamebeba dhamana kubwa ya kuitangaza nchi yetu.

(f) Serikali iweke mkazo wa kuvitangaza vivutio vya utalii vya nchi yetu kwa njia ya mtandao na kwa kutumia lugha mbali mbali za kimataifa ikiwemo lugha yetu ya Kiswahili.

(g) Serikali ifanye jitihada za makusudi kuiimarisha Tasnia ya uwindaji wa kitalii ambayo kwa sasa imeonekana kutetereka.

**SEHEMU YA TATU**

**3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kufanya uchambuzi wa shughuli zilizotekelezwa, Kamati ina maoni na mapendekezo yafuatayo:-

**3.1 UTENGAJI NA UPELEKAJI WA FEDHA ZA BAJETI**

Kwa kuwa kumekuwa na changamoto kubwa ya utengaji wa fedha za kutosha kwenye miradi ya maendeleo na pia hata fedha zinazotengwa zimekuwa hazitolewi kwa wakati na zikipelekwa ni kwa kiwango kisichoridhisha hasa kwenye miradi ya kimkakati iliyo chini ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Miradi hiyo ni ile inayohusisha upimaji, upangaji na umilikishaji wa ardhi nchini. Na kwa kuwa kwa sasa miradi hii imekuwa ikiendeshwa kwa asilimia kubwa kwa fedha za kutoka nje, fedha ambazo sio za kudumu wala za muda wote. Na kwa kuwa miradi hii pamoja na kulenga kumaliza kabisa tatizo la la migogoro ya ardhi nchini, ikikamilika inaweza kuwa chanzo kizuri na cha uhakika cha mapato ya Serikali**. Kwa hiyo basi, Kamati inalishauri Bunge kuitaka Serikali kuandaa mkakati maalum na kutenga fadha za kutosha kwenye bajeti itakayowezesha uendelezaji na ukamilisha wa miradi ya upimaji,upangaji na umilikishwaji wa ardhi nchini.**

**3.2 TISHIO LA KUKAUKA KWA MTO RUAHA MKUU**

Kwa kuwa uhai wa Hifadhi ya Taifa ya Ruaha ambayo ndiyo hifadhi kubwa kuliko zote nchini inategemea uwepo wa Mto Ruaha Mkuu, na mchango wa maji ya Mto Ruaha Mkuu kwa mabwawa ya kufua umeme ya Mtera, Kidatu na hata bwawa la kufua umeme la mto Rufiji ( Stieglers ) ni zaidi ya asilimia ishirini na Tano ( 25%), na Kwa kuwa kwa sasa hali ya Mto Ruaha Mkuu ni mbaya sana kiasi cha kufikia kutotiririka kabisa kwa zaidi ya wiki 19 ( zaidi ya miezi minne)

hali hii inachangiwa kwa kiasi kikubwa na kuendelea kwa shughuli za binadamu kwenye bonde la Ihefu na Usangu ambayo ni chanzo kikubwa cha Mto ruaha Mkuu. **Kwa hiyo basi, Kamati inalishauri Bunge kuitaka Serikali kuchukua hatua za haraka kuunusuru Mto Ruaha Mkuu usikauke kwa manufaa mapana ya Taifa.**

### 3.3 UTITIRI NA UKUBWA WA TOZO KATIKA HUDUMA ZA KITALII NCHINI

Kwa kuwa huduma mbali mbali kwenye Sekta ya Utalii ni kigezo muhimu katika kuhakikisha Sekta ya Utalii inakua na hivyo kuendelea kuchangia kwenye mapato ya nchi yetu hasa fedha za kigeni. Na kwa kuwa kumekuwa na mabadiliko ya Tozo kila mara kwa kuongezeka kwa idadi na ukubwa, jambo ambalo linayumbisha Sekta ya Utalii nchini. **Kwa hiyo basi, Kamati inalishauri Bunge kuitaka Serikali kuangalia upya utitiri wa Tozo na hata ukubwa wake kwenye huduma za utalii nchini ili kuifanya sekta hii kuwa na tija zaidi.**

### 3.4 USIMAMIZI WA RASLIMALI ZA MISITU NCHINI

Kwa kuwa nchi yetu imebarikiwa kuwa na raslimali nyingi ya misitu ambayo imekuwa ikisimamiwa na Mamlaka tofauti nchini. Na kwa kuwa Wakala wa huduma za misitu nchini ( TFS ) wamekuwa wakifanya kazi nzuri ya udhibiti wa matumizi ya misitu ya Serikali , Na kwa kuwa bado kuna changamoto ya udhibiti wa matumizi ya misitu isiyo ya serikali, hali ambayo pamoja na kuleta mgongano kwenye matumizi ya misitu yetu inatishia pia uendelevu ( Sustainability) wa misitu yetu**. Kwa hiyo basi, Kamati inalishauri Bunge kuitaka Serikali kuipandisha hadhi wakala wa Misitu Tanzania kuwa Mamlaka ya Misitu Tanzania ili kuipa nguvu ya kisheria ya kusimamia na kudhibiti matumizi ya raslimali ya misitu nchini.**

### 3.5 KUSIMAMA KWA BAADHI YA MIRADI YA SHIRIKA LA NYUMBA LA TAIFA (NHC)

Kwa kuwa kwa muda sasa baadhi ya miradi ya maendeleo ya Shirika la Nyumba la Taifa iliyoanza utekelezaji

wake ambayo mingi ya miradi hiyo ilianza kutekelezwa kwa fedha za mkopo imesimama, na kwa kuwa kutokamilika kwa wakati kwa miradi hii siyo tu kwamba kunaweza kuliyumbisha Shirika bali kulitia hasara Taifa. Na kwa kuwa kwa mujibu wa Taarifa za Shirika la Nyumba la taifa miradi hii imesimama baada ya kukosa fedha baada ya kusitishwa kwa kibali cha shirika kukopa fedha kwa miradi husika. **Kwa hiyo basi Kamati inalishauri Bunge kuitaka Serikali kukamilisha taratibu zitakaloliwezesha shirika kupata fedha za kumalizia miradi iliyosimama ili ilete tija.**

### 3.6 MRADI WA KUENDELEZA UKANDA WA KUSINI KIUTALII-REGROW

Kwa kuwa nchi yetu imebarikiwa kwa kuwa na fursa kadhaa za kiutalii katika ukanda wa Nyanda za juu Kusini. Na kwa kuwa mradi wa REGROW ungesaidia sana kufanya ukanda huu kutoa matokeo yanayokusudiwa, na kwa kuwa mazungumzo kati ya Serikali na mtoa mkopo yaani Benki ya Dunia yamechukua muda mrefu**. Kwa hiyo basi, Kamati inalishauri Bunge kuitaka Serikali kukamilisha mazungumzo mapema ili mradi uanzwe kutekelezwa.**

### 3.7 CHANGAMOTO YA BARA BARA KUPITA KATI KATI YA HIFADHI YA TAIFA YA MIKUMI

Kwa kuwa bara bara kuu itokayo Dar Es Salaam kwenda Nyanda za juu kusini inapita kati kati ya Hifadhi ya Taifa ya Mikumi, Na kwa kuwa kumekuwa na matukio mengi ya kugongwa kwa wanyamapori kwa wastani wa mnyama mmoja kila siku hali inayotishia uhai wa hifadhi hiy**o,Kwa hiyo basi Kamati inalishauri Bunge kuitaka Serikali kujenga bara bara ya mchepuko ili magari yapite nje ya hifadhi . Hali hii itawanusuru wanyamapori wetu na kuchangia kuongezeka kwa mapato kwani watalii watakaotumia barabara inayopita kati kati ya hifadhi watalipa ushuru wa utalii kuliko ilivyo sasa ambapo magari yanayopita hayatozwi ushuru na hivyo kufanya utalii wa bure na hivyo kuikosesha hifadhi yetu mapato.**

### 3.8 MKAKATI WA KUPAMBANA NA VIUMBE WAGENI VAMIZI

Kwa kuwa viumbe wageni vamizi wameenea katika sehemu nyingi nchini, na kwa kuwa uwepo wao umeleta athari nyingi zikiwemo kupungua kwa eneo la malisho na kutoweka kwa baadhi ya viumbe vya asili, na kwa kuwa Taasisi nyingi zimekuwa zikikabiliana bila kushirikiana, **kwa hiyo basi Kamati inalishauri Bunge kuitaka Serikali kuweka Mkakati wa Kitaifa wa kukabiliana na athari za viumbe wageni vamizi kuliko ilivyo sasa kila Taasisi inapambana kivyake**

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 HITIMISHO

### 4.1 Shukurani

**Mheshimiwa Spika,** mafanikio ya Kamati ya Ardhi Maliasili na Utalii katika kutekeleza shughuli zake kwa Mwaka 2018, yametokana na ushirikiano wa karibu sana wa Mhe William Lukuvi ( Mb), Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, na Mhe Dkt Angeline Mabula (Mb) Naibu Waziri, Mhe Dkt Hamisi Kigwangalla (Mb), Waziri wa Maliasili na Utalii na Mhe Constantine Kanyasu (Mb) Naibu Waziri,Makatibu wakuu na watendaji wengine wa Taasisi na Mashirika yaliyo chini ya Wizara hizi, Mashirika ya Kitaifa na Kimataifa pamoja na wadau wetu wote, napenda kuwashukuru wote kwa ujumla kwa ushirikiano mliotupa.

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee napenda kukushukuru kwa ushirikiano tulioupata kwa mwaka mzima wakati Kamati inatekeleza majukumu yake. Aidha, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge ndugu Stephen Kagaigai pamoja na sekretarieti ya Kamati hii Ndugu Athuman Hussein, Dickson Bisile,Gerald Magili, Haika Mtui na Mwimbe John kwa kuratibu shughuli zote za Kamati kwa kipindi chote cha Mwaka 2018.

**Mheshimiwa Spika,** Kipekee niwashukuru waheshimiwa wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya

Ardhi, Maliasili na Utalii kwa kutoa maoni, ushauri pamoja na ushirikiano wao kwenye Kamati, hali iliyowezesha kufanikisha kazi zote za Kamati yetu. Naomba niwatambue kama ifuatavyo.

1. Mhe. Nape Moses Nnauye, Mb - Mwenyekiti
2. Mhe. Kemirembe Rose Julius Lwota, Mb - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Boniface Mwita Getere, Mb
4. Mhe. Grace Sindato Kiwelu, Mb
5. Mhe. Magdalena Hamis Sakaya, Mb
6. Mhe. Joshua Samwel Nassari, Mb
7. Mhe. Halima Abdallah Bulembo, Mb
8. Mhe. Khalifa Salum Suleiman, Mb
9. Mhe. Lucy Fidelis Owenya, Mb
10. Mhe. Hussein Nassor Amar, Mb
11. Mhe. Shabani Omari Shekilindi, Mb
12. Mhe. Neema William Mgaya
13. Mhe. Mch. Peter Simon Msigwa, Mb
14. Mhe. Flatei Gregory Massay, Mb
15. Mhe. Risala Saidi Kabongo, Mb
16. Mhe. Dkt. Jasmine Tiisekwa Bunga, Mb
17. Mhe. Dkt. Stephen Lemomo Kiruswa, Mb
18. Mhe. Yussuf Haji Khamis, Mb
19. Mhe. Yussuf Salim Hussein, Mb
20. Mhe. Zainab Nuhu Mwamwindi, Mb
21. Mhe. Mbarouk Salim Ali, Mb
22. Mhe. Salim Hassan Turky, Mb
23. Mhe. Lucy Thomas Mayenga, Mb
24. Mhe. Timotheo Paul Mnzava
25. Mhe. Pauline Philip Gekul, Mb

### 4.2 Hoja

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kueleza Shughuli zilizotekelezwa, Uchambuzi wa matokeo ya utekelezaji wa shughuli za Kamati, maoni na Mapendekezo sasa naomba kutoa hoja kwamba Bunge sasa liipokee na kuikubali Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Ardhi Maliasili na Utalii kwa Mwaka 2018, pamoja na maoni na mapendekezo yaliyomo katika Taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

Mhe. Kemilembe J. Lwota, Mb
**MAKAMU MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI,**
**MALIASILI NA UTALII**
9 Februari, 2019

**SPIKA:** Ahsante sana. Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Kiruswa kwa kuisoma hotuba yako vizuri kwa niaba ya wanakamati wenzako. *(Makofi)*

Sasa nimuite Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji, tafadhali. Mheshimiwa Mgimwa dakika 15. *(Makofi)*

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kumshukuru sana Mungu, aliyenipa fursa na uwezo wa kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu. Naomba nichukue fursa hii kukushukuru wewe mwenyewe kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha ripoti hii. Kwa namna ya kipekee naomba nichukue fursa hii kumpongeza sana Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli, kwa kazi nzuri ya kizalendo anayoifanya ya kuwatumikia Watanzania. Pia nawashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri ambao wako kwenye Kamati hii, Mheshimiwa Hasunga, Mheshimiwa Profesa Mbarawa na Mheshimiwa Mpina kwa ushirikiano walioipa Kamati yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, taarifa yangu imegawanyika katika sehemu kuu tatu: maelezo ya ujumla; uchambuzi wa matokeo ya utekelezaji wa majukumu; na maoni na mapendekezo ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, naomba *Hansard* ichukue kwa rekodi taarifa ya Kamati kama ilivyo kwenye vitabu vyetu.

Mheshimwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni 117(150, Toleo la Januari 2016, naomba kuwasiisha taarifa ya shughuli

zinazotekelezwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kwa kipindi cha Januari, 2018 hadi Januari 2019 ili iweze kujadiliwa na kutolewa maamuzi na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, majukumu ya Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji yameainishwa katika Kanuni za Kudumu za Bunge kuwa ni kusimamia shughuli za Wizara ya Kilimo na Umwagiliaji; Wizara ya Maji; Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Ili kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, Kamati ilitumia mbinu mbalimbali kama ilivyoainishwa kwenye ukurasa wa 2 - 3 kwenye taarifa mliyopewa. Katika kipindi cha kuanzia Januari 2018 hadi 2019, Kamati imeweza kutekeleza shughuli mbalimbali zilizoainishwa kwenye ukurasa wa 2 -3 katika taarifa ya Kamati mliyopewa.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Pili ya taarifa inahusu uchambuzi na matokeo ya utekelezaji wa majukumu ya Kamati. Uchambuzi huu unahusu masuala 19 ambayo yalitokana na Kamati kutekeleza majukumu ya kimsingi yaliyoainishwa kikanuni kupitia vikao, ziara na ufuatiliaji wa ziara na taasisi inazozisimamia kisha kutoa maoni na ushauri na mapendekezo. Maelezo ya uchambuzi wa taarifa ya Kamati yamechambuliwa kwa kina kuanzia ukurasa wa 3 - 58 kama inavyoonekana kwenye vitabu tulivyovigawa kwa Waheshimiwa wabunge.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tatu, maoni na mapendekezo. Sehemu hii imegawanyika katika sehemu mbili. Sehemu ya kwanza inahusu maoni ya ujumla na sehemu ya pili inahusu maoni maalum kwa kila kazi iliyotekelezwa na Kamati.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapenda kutoa ushauri kwa ujumla wenye nia ya kuitaka Serikali kutekeleza ipasavyo ushauri unaotolewa na Bunge. Yapo masuala yanayoshughulikiwa mara kwa mara lakini hayatekelezwi. Mfano wa masuala hayo ni:-

(a) Ucheleweshaji katika kutoa fedha za miradi ya maendeleo kama ilivyoainishwa na Bunge kwa sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi na maji.

(b) Serikali kuendelea kutenga bajeti ndogo isiyokidhi mahitaji ya kuendeleza sekta ya kilimo, mifugo na maji na hivyo kukwamisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara zinazosimamiwa katika sekta hii.

(c) Serikali kuanzisha miradi mipya ya kilimo mifugo na uvuvi na maji kabla ya kukamilisha kwa miradi ya zamani.

(d) Serikali kutokutekeleza Mkataba wa Maputo na Malabo wa mwaka 2014 ambapo Tanzania imeridhia kutenga na kuhakikisha bajeti ya Wizara ya Kilimo inakuwa zaidi ya asilimia 10 ya bajeti yote na inatolewa kwa wakati ili ikatekeleze programu mbalimbali za kilimo.

(e) Kuongeza tozo ya shilingi 50 kwa kila lita ya mafuta ya diesel na petrol kama chanzo cha Mfuko wa Taifa wa Maji.

(f) Serikali kushindwa kutenga asilimia 1 ya *GDP* ya Taifa kwa ajili ya utafiti.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, naomba sasa niwasilishe maoni na mapendekezo 19 ya Kamati yanayotokana na shughuli zilizotekelezwa na Kamati kwa kipindi cha mwaka mmoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Tume ya Maendeleo ya Ushirika. Tume hii inakabiliwa na upungufu wa watumishi 1,272 na kupelekea kushindwa kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Kamati inapendekeza kwamba Serikali iipatie Tume ya Ushirika watumishi wanaohitajika ili iweze kusimamia utendaji wa Vyama vya Ushirika vya Kilimo na Masoko.

Mheshimiwa Spika, umuhimu kwa kuongeza mnyororo wa thamani wa mazao yenye fursa katika

kuchangia malighafi ya viwanda. Azma ya Serikali ni kujenga uchumi wa viwanda kwa kufungamanisha na shughuli za kilimo, ufugaji na uvuvi ili kuchochea mageuzi ya kiuchumi na maendeleo ya watu. Sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi ni moja ya sekta zinazotoa malighafi nyingi kwa ajili ya viwanda huku wananchi wanaojishughulisha na sekta hizo wakikabiliwa na changamoto ya ukosefu wa rasilimali fedha. Kamati inapendekeza Bunge lako Tukufu liazimie kwamba Serikali iweke mazingira wezeshi yatakayozitaka taasisi za fedha kuwakopesha wakulima, wafugaji na wavuvi mikopo ambayo ina riba nafuu ili wakulima, wafugaji na wavuvi waweze kuendesha shughuli zao kwa kutumia zana bora na za kisasa.

Mheshimiwa Spika, Mfumo wa Ununuzi wa Mbolea ya Pamoja *(Bulk Procurement)*. Serikali imefanikiwa kudhibiti bei ya mbolea kupitia utaratibu wa bei elekezi na kusambaza kwa mawakala elekezi na kusababisha mawakala wanaosambaza mbolea kupungua hivyo kupelekea mbolea nyingi kuishia mijini na kutokwenda vijijini. Kamati inapendekeza Bunge liazimie kwamba Serikali isitoe leseni kwa wasambazaji wakubwa ambao hawana matawi ya usambazaji kwa kila kanda. Aidha, watakiwe kufungua ofisi vijijini ili kuwezesha upatikanaji wa mbolea kwa wakati kulingana na misimu tofauti ya kilimo na kulingana na eneo husika.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa viwanda vya mbolea nchini. Mbolea nyingi inayotumika nchini huagizwa kutoka nje ya nchi kwa utaratibu wa Ununuzi wa Mbolea ya Pamoja *(Bulk Procurement)*, utaratibu huu siyo suluhisho la kudumu la kukidhi mahitaji ya mbolea. Kamati inapendekeza Bunge liazimie Serikali ikamilishe mapema iwezekanavyo mazungumzo yanayoendelea ya ujenzi wa viwanda vya mbolea kati ya Kampuni ya Mbolea ya *OCP* ya Morocco, Kampuni ya Mbolea kutoka Misri na muunganiko wa makampuni ya Ferostaal, Haldo topsoe na Fauji ili waweze kuanzisha ujenzi wa viwanda vya mbolea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, changamoto la zao la korosho. Serikali ilianza operesheni ya korosho kwa ajili ya kubangua na kununua korosho kwa wakulima kwa bei yenye tija ili kuwasaidia wakulima wa korosho kunufaika na jasho lao baada ya bei hiyo ya minadani kushuka na hivyo kuwanusuru kwa hasara ambayo wangeipata kwa msimu huu. Operesheni korosho inakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo kuchelewa kwa malipo ya wakulima; uwezo mdogo wa viwanda vya ndani kubangua korosho iliyovunwa; uwezo mdogo wa ghala kuu kuhifadhi korosho; kuchelewa kulipwa kwa malipo ya Halmashauri; kuchelewa kufanyika kwa malipo ya vyama vya msingi; kushuka kwa mapato ya fedha za kigeni na kukosekana kwa Bodi ya Korosho ya Tanzania na hivyo kupelekea ugumu wa utekelezaji wa operasheni nzima. Kamati inapendekeza Bunge liazimie Serikali itekeleze yafuatayo:-

(a) Bodi ya Korosho iteuliwe mapema iwezekanavyo ili itekeleze majukumu yake badala ya majukumu hayo kutekelezwa na Bodi ya Nafaka ya Mazao Mchanganyiko ambayo ina majukumu mengi kimsingi.

(b) Ili kudhibiti mazingira ya rushwa kutokana na kuchelewa kwa zoezi la uhakiki kwa malipo ya wakulima ni vyema uhakiki ukamilike mapema iwezekanavyo.

(c) Ulipaji wa fedha za korosho kwa wakulima uende sambamba na malipo ya ushuru wa Halmashauri ili kuziongezea Halmashauri uwezo wa mapato ya ndani kwa ajili ya kuendesha shughuli za kila siku ambazo sasa hivi zimesimama.

(d) Kwenye mipango ya muda mfupi na muda mrefu Serikali ihamasishe ujenzi wa viwanda vya kubagua korosho pamoja na kujenga maghala ya kutosha kuhifadhi korosho.

(e) Kwa misimu ijayo minada ya korosho ifunguliwe mapema kwenye maeneo ambayo korosho

inawahi kukomaa ili kudhibiti walanguzi wa korosho, maarufu kama kangomba.

(f) Zoezi la uhakiki lifanyike kwa uwazi na kushirikisha wakulima na wawakilishi kutoka vyama vyao.

(g) Serikali iandae mkakati wa muda mrefu wa kushughulikia changamoto za korosho.

Mheshimiwa Spika, changamoto za upanuzi wa viwanda vya sukari. Serikali ilikuwa na nia njema kulinda uzalishaji wa ndani wa sukari na kuamua vibali vya uagizaji wa sukari vipewe wenye viwanda ili kufidia naksi ya sukari *(gap)* wanayoizalisha. Kamati inapendekeza yafuatayo:-

(a) Serikali kwa kutumia wataalamu wake ifanye tathmini ifanye tathmini ya mwenendo wa kuagiza sukari nje ya nchi ili kupitia kwenye viwanda vya kuzalisha sukari ibaini namna bora zaidi ya kuagiza sukari nje ya nchi wakati mipango ya upanuzi wa viwanda vya kuzalisha sukari ikifanyika haraka.

(b) Wakati mipango wa upanuzi wa viwanda vya sukari ikiendelea, Kamati inapendekeza Serikali iangalie uwezekano wa kutumia mfumo wa *bulk procurement.*

Mheshimiwa Spika, umuhimu wa utafiti katika maendeleo ya kilimo cha miwa. Kwa kuwa matokeo ya tafiti ni muhimu katika kuboresha uzalishaji wa miwa, hivyo kuhakikisha upatikanaji wa malighafi ya viwanda vya sukari. Kamati inapendekeza kuwa Bunge liazimie na kuitaka Serikali kuwasilisha taarifa Bungeni itakayoeleza matumizi ya fedha kiasi cha shilingi bilioni 4.6 zilizotolewa na wazalishaji wa sukari kwa kipindi cha miaka 5 kwa ajili ya utafiti wa miwa.

Mheshimiwa Spika, changamoto za zao la pareto. Kamati inapendekeza Bunge liazimie Serikali iandae mkakati wa makusudi kuwezesha kilimo cha pareto kufanyika.

Mheshimiwa Spika, changamoto ya Tume ya Umwagiliaji. Kamati inapendekeza Bunge liazimie kuitaka Serikali kufanya uchambuzi wa kina ili kubaini ubadhirifu wa fedha za miradi ya kilimo na umwagiliaji na endapo itabainika kuna matumizi mabaya fedha za miradi hatua za kisheria zichukuliwe dhidi ya watendaji.

Mheshimwa Spika, changamoto zinazoyakabiii mashamba ya malisho. Kamati inapendekeza Bunge liazimie kuitaka Serikali kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya kujenga na kuendesha miundombinu ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, changamoto ya Kampuni ya Ranchi za Taifa. Kamati inapendekeza Serikali ibadilishe mapema iwezekanavyo umiliki wa hisa kutoka kwa wamiliki wa watu binafsi na kwenda kwenye umiliki wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, changamoto zinazoikabili tasnia ya maziwa. Kamati inapendekeza maziwa na bidhaa zinazotokana na maziwa viondolewe VAT; na kuwepo upendeleo maalum wa viwango vya kodi ili kuhamasisha na kuvutia uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, changamoto zinazoikabili Mamlaka za Maji Mijini. Sera ya Maji inaelekeza kujenga, kukarabati na kupanua miundombinu ya maji safi na usafi wa maji taka ili kuweza kutoa huduma endelevu kwa wakazi waishio mijini na pembezoni mwa mijini. Kamati inapendekeza Bunge liazimie na kuitaka Serikali kuwa na mpango wa nchi nzima utakaowezesha kuwa na mfumo wa maji taka.

Mheshimiwa Spika, maendeleo ya maji kwa Miji 28. Kwa kuwa fedha za mradi wa maji katika miji 28 imeshapatikana, Kamati inashauri Serikali kuhakikisha wakandarasi wanaopatikana wawe wenye sifa stahiki na waweze kukamilisha miradi hiyo kwa wakati na hatimaye huduma ya maji safi iwafikie wananchi wa maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lipokee, lijadili na liazimie Serikali itekeleze maoni na mapendekezo yaliyowasilishwa kwenye taarifa yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

## TAARIFA YA SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA NA KAMATI KWA KIPINDI CHA KUANZIA JANUARI 2018 HADI JANUARI 2019 KAMA ILIVYOWASILISHWA BUNGENI

*(Imetolewa chini ya Kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016)*

**SEHEMU YA KWANZA**
**MAELEZO YA JUMLA**

### 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa Kanuni ya 117(15), Toleo la Januari 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya shughuli zilizotekelezwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kwa kipindi cha Junuari 2018 hadi Januari 2019, ili iweze kujadiliwa na kutolewa maamuzi na Bunge lako.

### 1.1 *Majukumu ya Kamati*

**Mheshimiwa Spika,** Majukumu ya Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji yameainishwa katika Kanuni za Kudumu za Bunge kuwa ni kusimamia shughuli za Wizara ya Kilimo, Wizara ya Maji na Umwagiliaji, na Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Aidha, kifungu cha 7 (1) cha Kanuni za Kudumu za Bunge kinafafanua majukumu ya Kamati za Kudumu za Sekta ambapo Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji ni miongoni mwa Kamati hizo na ina majukumu yafuatayo:-

(a) Kushughulikia Bajeti za Wizara ya Kilimo, Wizara ya Maji na Umwagiliaji na Wizara ya Mifugo na Uvuvi;

(b) Kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara inazozisimamia;

(c) kushughulikia Taarifa za Utendaji za kila Mwaka za Wizara inazozisimamia na

(d) Kufuatilia Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara hizo.

### 1.2 *Njia / Mbinu zilizotumika kutekeleza Majukumu ya Kamati*

**Mheshimiwa Spika**, ili kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi Kamati ilitumia mbinu zifuatazo:-

1.2.1 Kufanya vikao vya kupitia, kujadili na kuchambua taarifa mbalimbali kuhusu utendaji wa sekta za Kilimo, Maji, Mifugo na Uvuvi;

1.2.2 Kufanya ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo ili kujiridhisha thamani ya fedha (*value for money*) zilizotumika kugharamia miradi hiyo;

1.2.3 Kukutana na wadau mbalimbali na kupokea maoni yaliyotumika kuboresha Muswada wa Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira; na

1.2.4 Kupata mafunzo na semina mbalimbali zilizoandaliwa na wadau wa sekta za Kilimo, Maji, Mifugo na Uvuvi.

### 1.3 *Shughuli zilizotekelezwa na Kamati*

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha kuanzia Januari 2018 hadi Januari 2019 Kamati imeweza kutekeleza shughuli mbalimbali zifuatazo:-

1.3.1 Uchaguzi wa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Kamati.

1.3.2 Kuhudhuria mafunzo kuhusu uendeshaji wa shughuli za Bunge na Kamati zake;

a) Muundo na Majukumu ya Bunge na Kamati zake;

b) Muundo na Majukumu ya Wizara za Kilimo, Mifugo na Uvuvi na Wizara ya Maji na Umwagiliaji;

c) Mafunzo kuhusu baadhi ya Sera na Sheria zinazohusiana kwa namna moja au nyingine kupitia sekta za Kilimo, Mifugo, Uvuvi na Maji; na

d) Mambo muhimu ya kuzingatia wakati wa ukaguzi wa miradi ya maendeleo, uchambuzi wa miswada na uchambuzi wa bajeti.

1.3.3 Kuchambua Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti za Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi na Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

1.3.4 Kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara za Kilimo, Mifugo na Uvuvi na Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

1.3.5 Kushughulikia Taarifa za Utendaji za Wizara za Kilimo, Mifugo na Uvuvi na Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

1.3.6 Kufuatilia Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara za Kilimo, Mifugo na Uvuvi na Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

1.3.7 Kukagua utekelezaji wa baadhi ya miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018; na

1.3.8 Kuchambua Muswada wa Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira wa Mwaka 2018 [*The Water Supply and Sanitation Bill, 2018*].

**SEHEMU YA PILI**

## 2.0 UCHAMBUZI WA MATOKEO YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU

### 2.1 *Maelezo ya Jumla*

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Pili ya Taarifa inahusu uchambuzi wa matokeo ya utekelezaji wa majukumu ya Kamati. Uchambuzi huu unahusu masuala ishirini ambayo yalitokana na Kamati kutekeleza majukumu ya msingi yaliyoainishwa Kikanuni kupitia vikao, ziara na ufuatiliaji wa Wizara na Taasisi inazozisimamia kisha kutoa maoni, ushauri na mapendekezo.

**Mheshimiwa Spika,** ufuatao ni uchambuzi wa shughuli zilizotekelezwa na Kamati kwa kipindi cha mwaka mmoja kuanzia Mwaka 2018 - 2019. Aidha, uchambuzi unaowasilishwa utafafanua shughuli zilizotekelezwa kwa kila sekta/ Wizara kama ifuatavyo

### 2.2 Sekta ya Kilimo

**Mheshimiwa Spika,** kuanzia kipindi cha Januari 2018 – Januari 2019 kwa upande wa Wizara ya Kilimo. Kamati imepokea na kujadili Taarifa za Wizara kwenye maeneo yafuatayo:-

#### 2.2.1 Tume ya Maendeleo ya Ushirika

**Mheshimiwa Spika,** ushirika wa mazao ni aina ya ushirika unaoundwa na kumilikiwa na wanachama ambao ni watekelezaji wa shughuli za kilimo kwa lengo la kuongeza uzalishaji na kipato kwa mwanachama mmoja mmoja na kuimarisha huduma za kilimo.

**Mheshimiwa Spika,** tofauti ya ushirika na mfumo wa biashara nyingine za kawaida ni kwamba mfumo wa ushirika katika kilimo

- Unamuwezesha mkulima kupata stahiki zake zote kwa wakati baada ya masoko kukamilika;
- Kupitia mfumo wa ushirika wakulima huunganishwa na kuwezeshwa kuwa na nguvu katika ushindani wa masoko;
- Mfumo wa ushirika urahisisha taratibu za usambazaji wa pembejeo kwa wakulima;
- Mfumo wa ushirika uwawezesha wakulima kuunganisha nguvu ya pamoja ili kukabiliana na changamoto ya mtaji;
- Faida itokanayo na Ushirika ni faida ya wanachama ambao ndiyo wamiliki wa ushirika
- Umiliki na uthibiti wake ni wa kidemokrasia na
- Ushirika hutizama malengo ya kijamii, kimazingira pamoja na mahitaji ya wanachama wake kwa usawa.

**Mheshimiwa Spika,** Tume ya Maendeleo ya Ushirika ina mikakati mizuri ya kuboresha mfumo wa ununuzi wa mazao ya wakulima yakiwemo mazao makuu matano ya kimkakati ambayo ni Chai, Pamba, Kahawa, Tumbaku na Korosho ikiwemo mkakati wa kuanzisha, kufufua na kuviunganisha Vyama vya Ushirika vya Kilimo na Masoko (AMCOS) katika ngazi za Mikoa inayojishughulisha na kilimo cha mazao hayo. Aidha, Tume pia ina mkakati wa kuendelea na uboreshaji wa mfumo wa usimamizi na udhibiti wa uendeshwaji wa shughuli za Vyama vya Ushirika.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na nia nzuri ya Serikali ya kufufua ushirika wa kilimo na masoka kwa lengo la kuongeza uzalishaji wa kipato kwa mwanachama mmoja mmoja na kuimarisha kilimo. Sekta ya Ushirika inakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo upungufu wa rasilimali watu, kwa sasa Tume ina Watumishi 256 katika ngazi ya Taifa, Mikoa na Wilaya kati ya **1,528** wanaohitajika ikiwa ni sawa na upungufu wa watumishi **1,272**.

**Mheshimiwa Spika**, upungufu wa Watumishi hao unakwamisha Tume kutekeleza majukumu yake ya msingi na hivyo kushindwa kufuatilia na kusimamia udhaifu kwa baadhi ya Vyama vya Ushirika na kufanya tathimini ya madeni makubwa yalioko kwenye vyama vya ushirika**.**

### 2.2.2 Mpango Mkakati wa kuongeza mnyororo wa thamani kwa mazao yenye fursa katika kuchangia malighafi ya viwanda

**Mheshimiwa Spika,** Mpango mkakati wa Serikali wa kuongeza mnyororo wa thamani wa mazao ya kilimo umelenga kuimarisha upatikanaji na utumiaji wa pembejeo hususan mbegu bora na mbolea, kuendelea kuimarisha huduma za udhibiti wa visumbufu vya mazao ya kilimo, kuimarisha huduma za utafiti, mafunzo na kuimarisha huduma za ugani pamoja na kuimarisha uratibu katika utekelezaji wa mikakati ya maendeleo ya mazao na kuimarisha stadi za kazi zinazohusu Kanuni Bora za Kilimo.

**Mheshimiwa Spika,** Mpango Mkakati wa kuongeza mnyororo wa thamani kwa mazao ya kilimo unalenga kupunguza upotevu wa mazao, kuimarisha Miundombinu ya Hifadhi ya Mazao, Kuimarisha usindikaji wa mazao ya kilimo, kufanya utafiti na kusambaza teknolojia za kilimo, na kuwaunganisha wakulima na masoko kupitia Vyama vya Ushirika katika mnyororo wa thamani ili kuongeza uzalishaji wenye tija kwa usalama wa chakula, kuchangia kuendeleza viwanda na kukuza uchumi.

**Mheshimiwa Spika,** licha ya mipango mizuri ya Serikali iliyoainishwa, bado mkakati wa kuongeza mnyororo wa thamani katika mazao unakabiliwa na changamoto zifuatazo;-

· Wakulima wengi wanakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa fedha kwa ajili ya kununua mashine za kilimo kama mashine za kuvuna na kupukuchua na hivyo kuendelea kutumia mbinu duni ambazo husababisha upotevu wa mazao na mazao kukosa ubora;

· Kuwepo kwa visumbufu vya mazao ambavyo husababisha upotevu mkubwa wa mazao na hivyo kupunguza ubora na usalama wa mazao kwa ajili ya malighafi za viwanda.

· Ukosefu na ubovu wa miundombinu ya kusafirisha mazao kutoka mashambani hadi kwenye masoko na hivyo kusababisha mazao kuoza na kuharibika wakati wa kusafirishwa;

· Uhaba wa pembejeo na upatikanaji na bei kubwa ya pembejeo na hivyo wakulima wengi kushindwa kumudu matumizi ya mbembejeo.

· Ufinyu wa Rasilimali fedha za kuwezesha utekelezaji wa mpango mkakati wa kuongeza mnyororo wa thamani.

### 2.2.3 Mfumo wa Ununuzi wa Mbolea kwa Pamoja kwa Msimu wa Mwaka 2018/2019

**Mheshimiwa Spika,** Mfumo wa Ununuzi wa Mbolea kwa Pamoja ni mfumo mpya kutumika hapa nchini na ulianzishwa kwa lengo la kuhakikisha mbolea inapatikana kwa wakati na kwa bei inayoweza kudhibitiwa na Serikali ili kuongeza matumizi ya mbolea nchini.

**Mheshimiwa Spika,** matumizi ya mbolea nchini ni wastani wa **kilo 19 kwa hekta** ikilinganishwa na lengo la **kilo 50 kwa hekta** ambalo ni Azimio la Maputo kwa nchi za SADC. Kiwango hicho ni sawa na **asilimia 38** ya lengo hilo. Katika msimu wa 2018/2019, mahitaji ya mbolea yanafikia **tani 514,138** na upatikanaji wa mbolea hadi kufikia Januari 2019 ni **tani 460, 369.2** sawa na **asilimia 90** ya mahitaji kwa msimu wa 20118/2019.

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya Tathimini ya Mfumo wa Ununuzi kwa Pamoja imeoyesha kuwa Serikali imefanikiwa kudhibiti bei ya mbolea kupitia bei elekezi ambapo upandishaji holela wa bei ya mbolea uliokuwa unafanywa

na baadhi ya wafanyabiashara wasio waaminifu umedhibitiwa. Mfumo wa Ununuzi wa Mbolea kwa pamoja umeweza kushusha bei ya mbolea kwa asilimia kati ya 11 na 40 kutegemea jiografia ya eneo husika.

**Mheshimiwa Spika,** licha ya mafanikio hayo yaliyofikiwa Mfumo wa Ununuzi wa Mbolea kwa Pamoja, Kamati imebaini mfumo huu unakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

**(a)** Bei elekezi ya mbolea kwa msimu wa 2017/ 2018 ni tofauti na bei elekezi ya msimu wa 2018/2019 kutokana na bei elekezi kuwa ndogo kuliko uhalisia wa gharama za usafirishaji kwa baadhi ya maeneo ya vijijini.

**(b)** Mbolea kutowafikia wakulima kwa wakati kutokana na ukweli kwamba mbolea iliyoagizwa iko mijini na haifiki vijijini kwa sababu ya mitaji kidogo iliyosababishwa na Serikali kutowalipa madeni yao baadhi ya Mawakala waliouza mbolea kwa msimu uliomalizika.

**(c)** Kupungua kwa idadi ya wasambazaji wa mbolea hapa nchini kutokana na kukosa faida walizokuwa wanapata kabla ya kuanzishwa kwa mfumo huu.

**(d)** Uwezo mdogo wa wakulima kununua mbolea kutokana na mauzo madogo waliyopata kutokana na bei ndogo ya mauzo za bidhaa zao.

**(e)** Wakulima wengi walizoea kupata mbolea kupitia utaratibu wa ruzuku iliyotolewa kupitia utaratibu wa vocha ambapo Serikali ilikuwa inachangia nusu ya gharama na mkulima alikuwa akichangia nusu gharama iliyobaki tofauti na utaratibu wa sasa ambapo mbolea hupatikana kwa mkulima kulipa pesa yake taslimu kutokana na bei elekezi iliyopangwa na serikali.

### 2.2.4 Mkakati wa Ujenzi wa Viwanda vya Mbolea Nchini

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilihitaji kupata Taarifa ya Utekelezaji wa Mkakati wa Ujenzi wa Viwanda vya Mbolea kutokana na ukweli kwamba mahitaji ya mbolea kwa sasa ni **tani 485,000** kati ya hizi zaidi ya **asilimia 95** ya mbolea inayotumika nchini inaagizwa kutoka nje ya nchi na **asilimia 1-2** hutengenezwa hapa nchini na kiwanda cha Minjingu kilichopo mkoani Manyara na hivyo kutokidhi mahitaji halisi ya mbolea.

**Mheshimiwa Spika,** aidha, Kamati ilitaka kufahamu mkakati wa ujenzi wa viwanda vya mbolea kwa kuwa mbolea inayoagizwa kupitia Mfumo wa Ununuzi wa Pamoja hauwezi kuwa suluhisho la kudumu la changamoto za mbolea, lakini pia uzalishaji wa mbolea hapa nchini utasaidia kupata mbolea zenye ubora unaohitajika kulingana na aina ya udongo tulionao lakini pia bei ya mbolea itakuwa nafuu ikilinganishwa na ile inayoagizwa kutoka nje ya nchi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitaka kujua hatua iliyofikiwa na Wizara ya Kilimo katika kutekeleza Mpango wa Serikali ya Awamu ya Tano wa kufungamanisha shughuli za kilimo kupitia Uchumi wa Viwanda na hasa ikizingatiwa kuwa kilimo ni moja ya sekta zinazozalisha malighafi ya viwanda zinazopatikana nchini hivyo uwepo wa viwanda vya mbolea nchini kutaongeza upatikanaji wa mbolea ambayo ni pembejeo ya msingi katika kuleta tija na uzalishaji wa mazao.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifahamishwa kuwa Serikali kupitia SUMA JKT imeanza mazungumzo ya makubaliano na kampuni ya kutoka nchini Misri kwa ajili ya kutengeneza mbolea hapa nchini. Aidha, Serikali pia imeanza mazungumzo na mwekezaji wa kujenga kiwanda cha mbolea ya kukuzia (Urea) katika mkoa wa Lindi wilayani Kilwa. Uzalishaji wa mbolea hii unatarajiwa kuanza **mwaka 2020** na inatarajiwa kiwanda kitakuwa na uwezo wa kuzalisha **tani 1.38** ambazo sehemu ya mbolea hiyo **(10%)** itatumika

hapa nchini na kiasi kingine cha mbolea **(90%)** kitauzwa nje ya nchi.

### 2.2.5 Hali ya Uzalishaji na Masoko kwa Mazao ya Korosho, Sukari na Pareto

#### (a) Zao la korosho

**Mheshimiwa Spika,** mfumo wa stakabadhi mazao ghalani ni mfumo mpya kwa zao la korosho ambapo minada hufanyika kwa uwazi. Msimu wa korosho ghafi kwa mwaka 2018/2019 ulifunguliwa rasmi tarehe 01/10/2018 na minada ya mauzo ilianza rasmi tarehe 22/10/2018 kwa Vyama Vikuu vya Ushirika kuanza kuuza korosho za wakulima kwa kutumia mfumo huu.

**Mheshimiwa Spika,** matumizi ya mfumo wa stakabadhi ghalani yalifikiwa na kukubalika kwenye Mkutano wa Wadau wa Korosho ambapo mfumo ulipoanza tarehe 22/10/2018 bei ya juu iliyofikiwa na wanunuzi wa korosho kwenye minada ilikuwa **shilingi 2,700** bei ambayo haikuwaridhisha wakulima na hivyo kukataa kuuza korosho zao.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na wakulima wa korosho kukataa kuuza korosho zao kulipelekea mwenendo usioridhisha wa masoko na mauzo ya korosho ndipo tarehe 26/10/2018 Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Kassimu Majaliwa Majaliwa (Mb) pamoja na hatua zingine alisitisha mfumo mpya wa mnada wa uwazi na kurudisha mfumo wa zamani ambao ulifanyika kwa zabuni za siri ambazo zilikuwa zinafungwa siku moja kabla ya mnada.

**Mheshimiwa Spika,** tarehe 28/10/2018 kilifanyika kikao cha majadiliano kati ya Serikali na wafanyabiashara / wanunuzi wa korosho ghafi nchini ambapo Serikali ilielekeza bei ya kilo moja ya korosho ghafi katika mnada isiwe chini ya **shilingi 3,000** kwa kilo kwa msimu wa mwaka 2018/2019. Kutokana na maelekezo hayo, wanunuzi wa korosho

waliweka mgomo baridi na kusuasua kununua korosho kwa bei iliyokubalika.

**Mheshimiwa Spika,** hali hiyo ilipelekea tarehe 12/ 11/ 2018 Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli kuagiza korosho zote za msimu wa mwaka 2018/2019 zitabanguliwa na kununuliwa na Serikali kupitia Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara, Ofisi za Wakuu wa Mikoa inayolima korosho, Benki ya Maendeleo ya Kilimo, Bodi ya Korosho Tanzania, Tume ya Maendeleo ya Ushirika, Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara, Soko la Bidhaa Tanzania, Bodi ya Usimamizi ya Stakabadhi za Ghala na Jeshi la Wananchi – Tanzania.

**Mheshimiwa Spika,** Serikali iliunda Kamati ya Operesheni Korosho 2018 ambayo ina wajibu wa kuratibu, kusimamia na kutekeleza majukumu mbalimbali katika mikoa yote inayolima korosho nchini. Majukumu ya Kamati hiyo ni pamoja na kufanya uhakiki wa malipo ya wakulima wa korosho kwa msimu wa mwaka 2018/2019, kufuatilia na kusimamia zoezi la ukusanyaji na usafirishaji wa korosho ghafi iliyonunuliwa na Serikali, uhifadhi wa korosho kwenye ghala lililoteuliwa, ubanguaji pamoja na kutafuta masoko.

**Mheshimiwa Spika,** licha ya mafanikio yaliyopatikana, Operesheni Korosho kwa msimu wa mwaka 2018/2019 inakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

i. Kuchelewa kwa malipo ya wakulima kutokana na zoezi la uhakiki linalolenga kudhibiti walanguzi (kagomba) kunufaika kupitia jasho la wakulima. Kuendelea kwa muda mrefu kwa zoezi la kuhakiki kumepelekea viashiria vya rushwa kutoka kwa wahakiki ili kuwezesha wafanyabiashara wakubwa kulipwa mapema pesa zao.

ii. Uwezo mdogo wa Viwanda vya kubangua korosho kutokana na kuwa na teknolojia duni. Uwezo wa viwanda vya ndani kubangua korosho ni tani

15,000 tu kwa mwaka kati ya tani 240,000 zilizozalishwa kwa msimu wa mwaka 2018/2019.

iii. Uwezo mdogo wa ghala kuu la kuhifadhi korosho lililopelekea ghala kuu kujaa kutokana na ucheleweshaji wa malipo ya wakulima na hivyo kushindwa kuendelea kupokea korosho kutoka AMCOS. Hatua hii imepelekea kuharibika kwa korosho zilizoko maghalani kwa kunyeshewa na mvua na hasa kwa korosho zilizoko mikononi mwa wakulima na hivyo kupoteza ubora wake ambao kwa muda mrefu ndio sifa kuu ya korosho za Tanzania.

iv. Kuchelewa kutolewa kwa malipo ya ushuru wa Halmashauri ambao kwa msimu wa mwaka huu yanakadiriwa kuwa shilingi **23,760,000,000** zitakazopatikana kutoka katika **asilimia 3** ya bei ya sokoni ya tani **240,000** na hivyo kusimama kwa shughuli nyingi za Halmashauri. Hali hii imepelekea Halmashauri kushindwa kujiendesha kwa sababu uendeshaji wa Halmashauri unategemea mapato yatokanayo na mazao ikiwemo korosho.

v. Kuchelewa kufanyika kwa malipo ya Vyama vya Msingi vya Ushirika (AMCOS) ambazo zinakadiriwa kuwa shilingi **8,840,000,000** zinazotokana na makisio ya uzalishaji wa korosho tani **240,000** kwa msimu wa mwaka 2018/2019.

**Mheshimiwa Spika,** malipo ya Vyama vya Msingi vya Ushirika yanahusisha gharama za usafirishaji kutoka kwa mkulima kwenda ghala kuu, ulinzi, malipo ya wapagazi, Makarani na malipo ya madaftari ya kumbukumbu za wakulima. Kuchelewa kufanyika kwa malipo haya kumekwamisha kipato cha wakulima na hivyo wakulima wengi wameshindwa kuendesha maisha yao ya kila siku kama ada za shule, matibabu na chakula kwa ajili ya familia zao.

vi. Kukosekana kwa takwimu sahihi kuhusu bei halisi ya korosho ghafi, Serikali imenunua kilo moja ya korosho kwa **shilingi 3,300** wakati bei halisi inayojumuisha

malipo ya moja kwa moja kwa mkulima, usafirishaji, ulinzi, uhifadhi, gharama za vyama vya ushirika na kodi za msingi za Halmashauri inafikia wastani wa **shilingi 3,850** kwa kilo.

vii. Kukosekana kwa Bodi ya korosho kumepelekea ugumu katika uratibu na usimamizi wa zao la korosho na utekelezaji wa operesheni korosho 2018/2019 na hii ni kutokana na kweli kwamba Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko ambayo imekasimiwa kwa muda jukumu la kusimamia operesheni korosho haina uzoefu wa kuendesha biashara ya korosho na hivyo watumishi wake badala ya kutekeleza kazi walioyotumwa wameanza kujifunza namna ya uendeshaji biashara ya korosho.

**Mheshimiwa Spika,** Bodi inayo majukumu yake ya msingi ya kisheria hivyo kupelekea hitaji zaidi la Watumishi. Kwa sasa Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko inakabiliwa na upungufu wa **watumishi 23** wanaofanya kazi ya uhakiki, ununuzi, malipo na upokeaji wa korosho ghafi katika ghala na hifadhi za Bodi.

**Mheshimiwa Spika,** umaalumu wa operesheni hii unahitaji uzoefu wa kutosha kwenye tasnia ya korosho, katika mazingira haya inakuwa ni vigumu kwa Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko kutekeleza majukumu iliyokabidhiwa kwa ufanisi.

viii. Kushuka kwa mapato ya fedha za kigeni na hivyo kuathiri uchumi wa nchi, hii ni kutokana na ukweli kwamba korosho ndio zao linaloingiza fedha nyingi za kigeni kuliko zao lingine lolote kutokana na soko lake kuwa la uhakika.

### (b) Uzalishaji na mahitaji ya Sukari nchini

**Mheshimiwa Spika,** Sukari ni bidhaa muhimu katika maisha ya binadamu na hutumika majumbani na viwandani kwa matumizi mbalimbali na kwa hiyo wakulima wa miwa zao ambalo ndilo sukari hutokana nalo, wafanya biashara,

wenye viwanda na Serikali kwa upande wake hunufaika na kodi na tozo mbalimbali.

**Mheshimiwa Spika,** Tanzania inazo fursa nyingi za uzalishaji wa sukari, miongoni mwa fursa zilizopo ni pamoja na kuwepo kwa ardhi inayofaa kwa kilimo cha miwa, kuwepo kwa vyanzo vya maji vingi na vya kutosha kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji, uwepo wa soko la sukari, nchi za jirani zisizojitosheleza kwa mahitaji ya sukari.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na fursa hizi zilizopo uzoefu umeonyesha kwamba bado uzalishaji wa ndani wa bidhaa ya sukari hautoshelezi na kwa nyakati mbalimbali kumekuwepo na mfumuko wa bei katika bidhaa ya sukari kunakoambatana na uhaba wa sukari hivyo kuathiri uchumi wa taifa na walaji.

**Mheshimiwa Spika,** uzalishaji wa sukari nchini hufanywa na viwanda vikubwa vitano vinavyomilikiwa na makampuni manne ya Kilombero *Sugar Company Ltd* (K1&K2), Mtibwa *Sugar Estates Ltd*, Kagera *Sugar Ltd, TPC Ltd*. Aidha, kipo kiwanda kimoja kidogo cha sukari cha Manyara *Sugar Co. Ltd*. Viwanda vyote hivi vina uwezo wa kuchangia uwezo wa kuzalisha wastani wa tani 300,000 kwa mwaka.

**Mheshimiwa Spika,** mahitaji ya sukari nchini kwa mwaka 2018/2019 ni wastani wa **tani 670,000** ambapo kati ya hizo **tani 515,000** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na tani **155,000** kwa matumizi ya viwandani. Uzalishaji wa sukari kwa viwanda vya ndani kwa mwaka 2018/2019 unakadiriwa kuwa **tani 353,900** ambazo zote ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kwa msingi huu, uzalishaji wetu wa ndani hauwezi kutosheleza mahitaji na hivyo nakisi (*gap sugar*) kwa matumizi ya kawaida huagizwa kutoka nje ili kufidia pengo la uzalishaji.

**Mheshimiwa Spika,** ili kulinda wazalishaji wa ndani na soko la sukari kwa ujumla uagizwaji wa sukari kutoka nje ya nchi huagizwa na wazalishaji wa sukari na kusambazwa na waagizaji wenyewe mara baada ya kupata kibali cha

kuagiza sukari kupitia leseni ya kuingiza sukari nchini inayotolewa na Bodi ya Sukari Tanzania.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na uzalishaji na uagizwaji wa sukari kutoka nje ya nchi kwa kipindi cha miaka kumi mfululizo sekta ya sukari imekuwa ikikabiliwa na changamoto mbalimbali zifuatazo:-

i. Uingizaji holela wa sukari inayozidi mahitaji ya soko na hivyo kuvuruga mfumo wa uzalishaji na biashara ya sukari nchini.

ii. Kukosekana kwa takwimu sahihi kuhusu gharama za uzalishaji wa sukari na mara nyingi wazalishaji huonyesha gharama za uzalishaji kuwa kubwa kuliko hali halisi.

iii. Sukari kutoka nje inayozalishwa kwa ruzuku kutotozwa kodi stahiki kwa mujibu wa sheria.

iv. Kupotea kwa imani kwa taasisi za fedha kutokana na uingizaji holela wa sukari na hivyo kutokopesha miradi ya sukari.

v. Miradi ya uzalishaji wa sukari kuhitaji mitaji mikubwa yenye masharti nafuu, kama riba na urejeshwaji wa muda mrefu, ambavyo havipatikani nchini.

vi. Huduma za utafiti, mafunzo na ugani zisizotosheleza mahitaji ya sekta.

vii. Hali isiyotabirika ya masoko na biashara ya sukari katika ukanda huu.

viii. Mabadiliko ya tabia nchi (hali ya hewa) pamoja na kutokuwepo kwa miundombinu.

**Mheshimiwa Spika,** ili nchi iweze kujitosheleza na sukari inahitajika mitaji mikubwa ya uwekezaji kwenye mashamba ya miwa, ujenzi wa viwanda, miundombinu ya barabara, teknolojia ya umwagiliaji n.k. Kwa kutambua ugumu uliopo

na kwa kuzingatia umuhimu wa bidhaa ya sukari tofauti na bidhaa zingine, sukari imewekewa utaratibu maalum wa kibiashara na kiudhibiti ili kulinda wazalishaji wa ndani na soko la sukari kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mantiki hii, kila nchi ambayo haijitoshelezi kwa sukari duniani huweka utaratibu maalum wa uagizaji wa sukari ambao unazingatia kulinda soko la sukari la ndani, kuchochea ongezeko la uzalishaji kwa viwanda, kuhamasisha uwekezaji mpya kwenye sekta ya sukari na kuhakikisha ajira kwenye tasnia hiyo zinalindwa.

**Mheshimiwa Spika,** umuhimu na unyeti wa bidhaa hiyo umefanya yawepo makubaliano maalum hata kwenye kanda mbalimbali za mashirikiano kama SADC, EAC na COMESA. Aidha, Jumuiya ya Ulaya imeweka Sera maalum ya Sukari (*EU-Sugar Policy*) kutokana na unyeti wa bidhaa hiyo.

### 2.2.6 Umuhimu wa Utafiti katika kukuza Uzalishaji wa Miwa

**Mheshimiwa Spika,** uzalishaji wa sukari hapa nchini unategemea upatikanaji wa miwa. Kwa sasa wakulima wa miwa wa nje (*Outgrowers*) wanachangia asilimia 30 ya miwa inayosagwa kwa uzalishaji sukari. Ili kuongeza uzalishaji wa miwa, na kwa kutambua umuhimu wa miwa kama malighafi ya viwanda vya sukari, wenye viwanda vya miwa kwa kushirikiana na Serikali walikubaliana kuchangia kiasi cha mapato yao kwa ajili ya tafiti za miwa ili kuendeleza ukulima wa miwa wenye tija**.**

**Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia 2014/2015 hadi 2018/2019 wazalishaji wa miwa wamechanga kiasi cha **shilingi 4,688,885,111.36** kama inavyoonekana kwenye **Jedwali Na. 1** kwenye Taasisi ya Utafiti Sukari (*Sugar Research Institute*), Taasisi ya Taifa ya Sukari (*National Sugar Institute*) na Jumuiya ya Sukari Tanzania (*Tanzania Society of Sugar*) na Teknologia ya Miwa (*Cane Technologists*).

**Mheshimiwa Spika,** ilitazamiwa fedha hizi zikasaidia utafiti utakaowezesha ukulima wa miwa kuwa wenye tija kwa ajili ya kuchangia malighafi ya viwanda vya miwa, hata hivyo hakuna mafanikio yoyote yaliyopatikana kwani kilimo cha miwa bado kinafanyika kwa kutumia teknolojia za kizamani zisizo na tija.

### 2.2.7 Kiwanda cha Sukari Zanzibar

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipata nafasi ya kupokea taarifa ya utekelezaji wa Kiwanda cha Sukari Zanzibar. Kiwanda hiki kilianzishwa mwaka 1974 chini ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Jamhuri ya watu wa China.

**Mheshimiwa Spika,** mwaka 2005 kiwanda kilikabidhiwa chini ya muwekezaji ambae alishindwa kukiendesha na mwaka 2013 kuchukuliwa na muwekezaji wa sasa *Shanta Sugar Holdings*, ambae alikifufua kiwanda na mashamba kwa kufunga mashine mpya za kisasa na kufanikiwa kuanza uzalishaji rasmi mwaka 2015.

**Mheshimiwa Spika,** kwa sasa kiwanda kina uwezo wa kuzalisha sukari **tani 30,000** kwa mwaka, hata hivyo kiasi kinachozalishwa kwa sasa ni **tani 8,000** na kimeajiri wafanyakazi 200 wa kudumu na wafanyakazi 200 wa ajira ya msimu. Aidha, kiwanda kinazalisha umeme kiasi cha 1.6 MW ambao wote hutumika kuendeshea kiwanda.

**Mheshimiwa Spika,** kiwanda cha sukari Zanzibar kinakabiliwa na changamoto ya soko la sukari na bei ndogo ya sukari inayouzwa Zanzibar kutokana na kipato na uwezo wa walaji kununua sukari na hivyo kupelekea hasara ya **shilingi 29,860** kwa kila **kilo 50** za sukari. Kutokana na hasara hiyo, ili kunusuru kiwanda, kulinda ajira na uchumi soko la Tanzania bara ambalo ni la uhakika linaweza kusaidia kiwanda hiki kuendelea kuzalisha.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kwa muda mrefu sasa kumekuwepo na mkanganyiko kwa sukari inayozalishwa Zanzibar kuuzwa Tanzania bara wakati hakuna

sheria ya ushuru wa forodha, sheria ya kodi au sheria ya Bodi ya Sukari inayozuia bidhaa iliyozalishwa Zanzibar kuingia Tanzania Bara.

### (c) Zao la Pareto

**Mheshimiwa Spika,** zao la pareto liliingia nchini kwa mara ya kwanza miaka ya 1930 na kuanza kulimwa kwa majaribio katika kituo cha uchunguzi maeneo ya Ihemi na baadaye kusambaa maeneo mengi ya mkoa wa Iringa. Kwenye miaka ya 1938 zao hili lilianza kulimwa kwa wingi na wakulima wa kigeni na baada ya uhuru zao hili lilianza kulimwa na wazawa.

**Mheshimiwa Spika,** kiwanda cha kwanza cha kusindika pareto kilifunguliwa miaka ya 1962 mkoani Arusha kilijulikana kwa jina la *Mitchell Cotts Ltd* na kilimilikiwa na kampuni ya Kingereza. Aidha, mwaka 1982 Serikali ililenga kuongeza uzalishaji wa pareto na kujenga kiwanda kingine mkoani Iringa eneo la Mafinga.

**Mheshimiwa Spika,** kiwanda cha Serikali cha Mafinga-Iringa hakikufanya vizuri ndipo mwaka 1998 kiwanda hiki kilipata muwekezaji kutoka Afrika chini ya kampuni ya *International Chemicals Producers*.

**Mheshimiwa Spika,** kuanzia mwaka 2000/2001 hadi 2003/2004 kampuni hii ilipata changamoto kubwa ya soko la bidhaa zake kutokana na ukweli kwamba muwekezaji huyu hakuwa na soko la uhakika ndani na nje ya nchi hali hii ilipelekea wakulima wa pareto kushindwa kulipwa madeni ya maua waliyokuwa wameuza ndipo Serikali iliingilia kati na kulipa fedha kiasi cha **shilingi bilioni 1.4**.

**Mheshimiwa Spika,** ukosefu wa soko la uhakika wa bidhaa za pareto ulipelekea uzalishaji wa pareto nchini kushuka kwa kiwango kikubwa na hivyo kuwakatisha tamaa wakulima wa pareto. Ili kukabiliana na changamoto ya soko la bidhaa za pareto, mwaka 2005/2006 kampuni ya TPPMCL /ICP iliuzwa kwa kampuni ya *Pyrethrum Company of Tanzania*

– kampuni ambayo hadi sasa ndio kampuni iliyowekeza kwa kiwango kikubwa katika tasnia ya pareto nchini.

**Mheshimiwa Spika,** kimataifa zao la pareto linalimwa kwa wingi katika nchi za Austaralia, Tanzania, Papua Guinea, Kenya na Rwanda. Tanzania ni nchi ya kwanza Afrika kwa uzalishaji wa pareto na nchi ya pili duniani baada ya Australia.

**Mheshimiwa Spika,** nchini Tanzania zao la pareto hustawi vizuri kwenye maeneo ya ukanda wa juu ambayo mara nyingi hupata mvua za kutosha. Maeneo hayo yanajumuisha Kanda za Nyanda za Juu Kusini katika mikoa ya Mbeya (Mbeya Vijijini na Rungwe), Songwe (Ileje), Njombe (takribani Halmashauri zote za mkoa wa Njombe) na Iringa (Mufindi, Kilolo, na Iringa vijijini) na Kanda za Kaskazini mikoa ya Arusha (Arusha DC na Meru), Manyara (Babati, Mbulu Mji, Halmashauri ya Mbulu na Halmashauri ya Hanang' ambayo ipo katika hatua za awali za kuanza uzalishaji) na mkoa wa Kilimnjaro, katika wilaya ya Siha.

**Mheshimiwa Spika,** licha ya kuwa Tanzania ni nchi ya pili duniani kwa uzalishaji wa pareto, zao hili hulimwa na wakulima wadogo wengi wao wanalima eneo la kuanzia nusu ekari hadi ekari moja ambao huzalisha takribani **tani 600** kwa mwaka ikilinganishwa na uwezo wa nchi wa kuzalisha zaidi ya **tani 5,000** kwa mwaka. Aidha, Tanzania kuna viwanda viwili tu vya pareto ambavyo ni kiwanda cha Kampuni ya Pareto Tanzania (*Pyrethrum Company of Tanzania)* Kilichopo Mafinga – Iringa na kiwanda cha kampuni ya *TANEXTRACT Co Ltd* kilichoko Inyala – Mbeya.

**Mheshimiwa Spika,** inakadiriwa mahitaji ya pareto duniani ni kati ya **tani 15,000 hadi 16,000** kwa mwaka. Aidha, bei ya pareto ulimwenguni imeendelea kupanda kila msimu; kwa mfano kwa msimu wa mwaka **2015/2016** ilikuwa kati ya shilingi **1,500/= na 2,700/=** kwa kilo kutegemeana na ubora wa maua, bei ya msimu wa mwaka **2016/2017** ilikuwa **shilingi 2,000/= na 3,000/=** kwa kilo. Wakati bei ya msimu wa mwaka **21017/2018** ilikuwa kati ya **shilingi 2,300/= na 3,300/=** kwa kilo ya maua kutegemeana na ubora wa maua yaliyouzwa na

kwa msimu wa mwaka **2018/2019** bei ya maua ni kati ya **shilingi 2,300/= hadi 2,400/=** na **3,400/= na 2,400/= hadi 4,000/=** kwa kilo kulingana na ubora wa maua.

**Mheshimiwa Spika,** kuongezeka kwa bei ya kilo ya maua ya pareto kwa kila msimu, uwepo wa ardhi inayofaa kwa kilimo pamoja na upatikanaji wa hali ya hewa nzuri kwa kanda za Nyanda za Juu kusini na Kanda ya Kaskazini, kuongezeka kwa matumizi ya bidhaa zitokanazo na pareto duniani na taswira nzuri kimataifa kuwa Tanzania ni nchi ya pili duniani kwa uzalishaji wa pareto, hii ni fursa nzuri kwa nchi yetu kukazania kilimo cha kuzalisha pareto ili iweze kuzalishwa kwa wingi zaidi.

**Mheshimiwa Spika,** licha ya fursa nzuri ya kilimo cha pareto iliyopo nchini na kimataifa, zao la pareto linakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

i. Ukosefu wa kiwanda cha kuongeza thamani zao la pareto kabla ya kuuzwa nje ya nchi.

ii. Kukosekana kwa kiwanda cha mtambo (*refinery)* kwa ajili ya kutengeneza viuatilifu mbalimbali na hivyo kusababisha upatikanaji wake kuwa mgumu na vikipatikana huuzwa kwa gharama kubwa.

iii. Kukosekana kwa maabara huru kwa ajili ya kupima ubora wa maua.

iv. Uhaba wa watumishi na upungufu wa wataalamu wa kada mbalimbali kwenye Bodi ya Pareto.

v. Wawekezaji wanakabiliwa na changamoto ya upatikanaji wa haraka wa vibali vya kazi kwa wafanyakazi wa kigeni.

vi. Wawekezaji na ushindani usio wa haki kutokana na baadhi ya wafanyabiashara kutofuata vigezo, masharti, kanuni na taratibu za uwekezaji kwenye sekta ya pareto kutokana na vyombo vya Serikali vinavyosimamia pareto kukosa udhibiti.

### 2.2.8 Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko

**Mheshimiwa Spika,** Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko ilianzishwa Mwaka 2009 ili kutatua changamoto ya ukosefu wa masoko ya uhakika kwa mazao ya wakulima hususan mazao ya Nafaka na mazao mchanganyiko. Hivyo Bodi hii ni taasisi ya Serikali inayojiendesha kibiashara na jukumu lake la msingi ni kuwapatia wakulima fursa ya kupata bei ya ushindani na soko la uhakika. Yafuatayo ni baadhi ya majukumu ya Bodi:-

- Kununua na kuuza nafaka na mazao mchanganyiko kwa bei ya soko la ushindani;

- Kuuza nafaka na mazao mchanganyiko kwenda nje ya nchi;

- Kufanya shughuli nyingine za kibiashara zitakazosaidia uongezaji wa thamani na uendelezaji wa biashara ya nafaka na mazao mchanganyiko.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na majukumu muhimu Bodi iliyonayo, Bodi hii inakabiliwa na changamoto mbalimbali zifuatazo:-

- **Kutopatikana fedha ya kutosha ya ununuzi wa mazao na au fedha kupatikana kwa kuchelewa**

Bodi imekuwa haipati fedha za ununuzi wa mazo kwa wakati, mara nyingi fedha zimekuwa zikitolewa wakati msimu wa mavuno umemalizika na hivyo kulazimika kununua mazao kwa bei ghali na kupelekea gharama za bidhaa zinazozalishwa kuwa juu.

- **Uhaba wa Watumishi**

Bodi inakabiliwa na uhaba wa Watumishi na kupelekea baadhi ya nafasi muhimu kukosa watumishi na hivyo kuathiri utekelezaji wa shughuli za Taasisi. Kwa mfano; Bodi hii inaendesha shughuli zake kibiashara wakati nafasi ya Mkurugenzi wa Biashara iko wazi. Aidha, Bodi imepewa dhamana na Serikali ya kusimamia, zoezi la ununuzi, malipo

na ubanguaji na uuzaji wa korosho katika msimu wa 2018/2019 kufuatia shughuli hii watumishi wote wa Bodi wamehamia Mtwara na kuacha kutekeleza majukumu ya msingi ya kuanzishwa kwa Bodi.

· **Kukosekana kwa magari ya kusambazia bidhaa** Kukosekana kwa magari kumepelekea bidhaa kuwafikia walaji kwa kasi ndogo, hivi sasa Bodi inatumia usafiri wa baiskel kupeleka bidhaa zake sehemu mbalimbali.

· **Uchakavu wa miundombinu ya Usindikaji na Uhifadhi**

Mitambo ya usindikaji ni chakavu hivyo imepelekea kupunguza ufanisi na baadhi haifanyi kazi kabisa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati pia imebaini kwamba kwa muda mrefu Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko imekuwa ikishughulika kwa kiasi kikubwa na mazao ya mahindi na alizeti pekee na kuacha mazao kama mbaazi, ngano, mchele, mtama, mihogo, ngano n.k na kuacha wakulima wa mazao hayo wakihangaika kujitafutia masoko wao wenyewe.

### 2.2.9 Tume ya Taifa ya Umwagiliaji

**Mheshimiwa Spika,** kwa muda mrefu kilimo cha nchi yetu kimekuwa kikitegemea mvua kwa kiwango kikubwa, hata hivyo mabadiliko ya tabianchi yamepelekea ukosefu wa mvua ya uhakika kumepelekea kilimo kisicho na tija na hivyo mara nyingi kumekuwepo na hofu ya upungufu wa mazao ya chakula na biashara.

**Mheshimiwa Spika,** ili kuleta mapinduzi katika kilimo na kuongeza tija na uzalishaji wa mazao kwa lengo la kulihakikishia Taifa usalama wa chakula na kuwaongezea wakulima kipato na Serikali kwa ujumla kilimo cha umwagiliaji ni suluhisho la kilimo cha kutegemea mvua.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kutambua umuhimu wa umwagiliaji katika kilimo Serikali imeihamishia Tume ya Umwagiliaji Wizara ya Kilimo ili kuwezesha mipango ya kilimo

kwenda sambamba na mipango ya umwagiliaji hivyo kuongeza uzalishaji wa tija wa mazao ya kilimo, uamuzi huu ni utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kutekeleza ushauri huu wa Kamati. Pamoja na pongezi hizo, Kamati inatambua changamoto ya utekelezaji na usimamizi wa miradi ya umwagiliaji iliyoanza kutekelezwa miaka mingi na bado haijakamilika kutokana na uzembe uliofanywa na watendaji wa Tume na kuisababaibishia Serikali hasara pamoja na Tume kutengewa fedha zisizotosheleza mahitaji na kutolewa zikiwa zimechelewa.

### 2.3 *Sekta ya Mifugo*

**Mheshimiwa Spika,** Tanzania ni Nchi ya Tatu kwa wingi wa mifugo barani Afrika baada ya nchi ya Sudan na Ethiopia. Mifugo hiyo ni pamoja na **ng'ombe milioni 30.5**, **mbuzi milioni 18.8**, **kondoo milioni 5.3**, **kuku wa asili milioni 38.2**, **kuku wa kisasa milioni 36.6, nguruwe milioni 1.9** na **punda 595,160**. **Asilimia 97** ya mifugo hii hufugwa kwa mfumo wa asili na kaya **milioni 5** sawa na **asilimia 50** ya kaya zote vijijini zinajishughulisha na mifugo.

**Mheshimiwa Spika,** ili mifugo hii iweze kufungwa kwa ufanisi panahitajika uwepo wa eneo la malisho linalotosheleza mahitaji ya mifugo iliyoko nchini. Tanzania ina takriban **hekta milioni 50** zinazofaa kwa malisho, kati ya hekta hizo ni **hekta milioni 10.5** ndio zinatumiwa na mifugo kwa ajili ya malisho, sehemu iliyobaki inatumika kwa matumizi mengine ya kiuchumi na kijamii.

**Mheshimiwa Spika,** maeneo ya malisho yameendelea kupungua kutokana na kuongezeka kwa mahitaji ya ardhi, ongezeko la watu, mifugo na shughuli za kiuchumi na kijamii. Ongezeko la watu limesababisha gawio la ardhi lipungue kutoka **hekta 5.2 (mwaka 1978)** hadi **hekta 2.0 (2012)** na kwa upande wa mifugo gawio limeshuka kutoka **hekta 3.7 (mwaka 1984)** hadi **hekta 1.8 (2017).** Hali hii imepelekea ubora wa malisho kupungua kutokana na kuwa na mifugo mingi

katika eneo dogo na kutumika mfululizo na hivyo kuathiri uzalishaji wa mifugo na kusababisha kuwepo kwa upungufu katika uzalishaji wa mazao ya mifugo ikiwemo nyama, maziwa na ngozi. Aidha, muunganiko wa wadau katika mnyororo wa thamani ya mazao ya mifugo unakosa mfumo sahihi wa kuunganisha mazao haya na viwanda, hivyo kukosa hamasa ya uzalishaji toshelevu wa mazao ya mifugo viwandani.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kutambua changamoto hiyo, Serikali ilianzisha mashamba ya mifugo ambayo yamegawanyika maeneo mawili ambayo ni Mashamba ya kuzalisha Mifugo na Mashamba ya kuzalisha Mbegu za malisho ya Mifugo kwa madhumuni ya kuzalisha mifugo bora hasa ng'ombe chotara wa maziwa na kuwasambaza kwa wananchi kwa bei ya ruzuku, lengo likiwa kuzalisha **ng'ombe 5000** kutoka katika **mashamba 5**.

**Mheshimiwa Spika**, licha ya kuanzishwa kwa mashamba hayo ya Mifugo kampuni ya NARCO imekuwa ikijiendesha kwa hasara kwani Takwimu zinaonyesha kuwa namba ya mifugo imekuwa ikipungua mwaka hadi mwaka na kufika **ng'ombe 12,650** ilipofika Desemba, 2017 ambapo Juni 2016 walikuwa **ng'ombe 13,343** kutokana na ukweli kwamba bado hakuna uwekezaji wa kutosha kwenye ranchi za Taifa licha ya kuwa na vyanzo vingi vya mapato.

**Mheshimiwa Spika, mashamba** ya mifugo yanasaidia uzalishaji wa wingi wa mazao ya mifugo, pamoja na umuhimu huo mashamba ya Serikali ya malisho yanakabiliwa na:-

- Upungufu wa miundombinu ya maji itakayowezesha kilimo cha umwagiliaji wa malisho, kwa sasa mashamba haya yanazalisha malisho kwa kutegemea mvua;

- Upungufu wa rasilimali fedha za kuwekeza na kuendesha mashamba kwani uzalishaji mbegu za malisho uhitaji mitambo yenye gharama kubwa;

· Upungufu wa elimu na teknolojia ya uzalishaji na uhifadhi wa malisho na mbegu za malisho; na

· Kukosekana kwa mfumo rasmi wa kusambaza malisho na mbeguu.

### 2.3.1 *Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO)*

**Mheshimiwa Spika,** Kampuni ya Ranchi za Taifa ilianzishwa kama NACO mwaka 1968 na kusajiliwa kama Kampuni tanzu ya kibiashara chini ya Sheria ya Makampuni (Sura 212) ikiwa na lengo la kuendeleza na kueneza ufugaji bora hususan ufugaji wa ng'ombe bora wa nyama (Boran) kwa ajili ya soko la ndani na nje ya nchi kwa kutumia mbinu za kisasa. Hivi sasa Kampuni inamilikiwa na Serikali kwa **asilimia mia moja (100%)** licha ya kwamba Hati ya Makubaliano (*Memorandum and Articles of Association* - MEMARTS) za NARCO zinaonyesha kuwa wanahisa wa Kampuni ya Ranchi za Taifa ni Clement George Kahama na Hippolitus Pamfili Njau ambao walisani kwa vyeo vyao walipokuwa Meneja Mkuu na Katibu wa Shirika la Maendeleo la Taifa NDC wakati NARCO ilipoanzishwa mwaka 1968.

**Mheshimiwa Spika,** kwa maantiki hii umiliki wa NARCO ni wa watu binafsi licha ya sheria ya Makampuni sura 212 kurekebishwa na kuruhusu kusajili kampuni ikiwa na mwanahisa mmoja MEMARTS hizi zimeendelea kusomeka hivyo mpaka sasa ingawa upo uwezekano wa kubadilisha wanahisa wa NARCO na kuwa mwanahisa mmoja ambae ni Msajili wa Hazina.

**Mheshimiwa Spika,** Kampuni ya Ranchi za Taifa ina ranchi nane (8) zenye jumla ya hekta **230,384,** ranchi hizo ni Kalambo (Rukwa), Kikulula Complea (Kagera), Kongwa (Dodoma), Misenyi (Kagera), Mkata (Morogoro), Mzeri (Tanga), Ruvu (Pwani) na West Kilimanjaro (Kilimanharo). Ranchi hizi zina uwezo wa kuweka ng'ombe kati ya **80,000-90,000** hata hivyo kwa sasa inakadiriwa ranchi zote zina ng'ombe **12,681**.

**Mheshimiwa Spika,** idadi ndogo ya ng'ombe walioko kwenye Ranchi za Taifa ukilinganisha na uwezo wa rachi hizo inadhihirisha kwamba hakuna uwekezaji wa kutosha kwenye Ranchi za Taifa kutokana na ukosefu wa fedha, mikataba mibovu na isiyo na tija iliyofungwa baina ya kampuni na wawekezaji wa vitalu.

**Mheshimiwa Spika,** vitalu vilivyokodishwa kwa wawekezaji vinakabiliwa na changamoto mbalimbali, baadhi ya changamoto hizo ni pamoja na:-

- Mikataba yote iliyofungwa baina ya NARCO na wawekezaji katika vitalu ilikuwa ya aina moja (*Standard Contract)* bila kuzingatia uwezo wa kimtaji wa kiundeshaji wa kila mwekezaji;

- Baadhi ya vitalu havijaendelezwa kabisa, na vingine vimekodishwa na kubadilshwa matumizi, mfano : Kitalu Na. 645/6 – Mzeri;

- Baadhi ya vitalu vimeendelezwa kwa kuongezewa aina nyingine za ufugaji tofauti na makubaliano; Kitalu Na. 645/1 Stage Farm kinafuga samaki na 417 Mkata anafuga samaki na nyuki;

- Baadhi ya vitalu vimevamiwa na wavamizi wanaolima, kuchunga, na kuweka makazi ndani ya vitalu. Aidha baadhi ya vitalu vimemegwa maeneo yake na kupewa watu na vijiji; na

- Wawekezaji wengi katika vitalu wameshindwa kuwekeza kulingana na makubaliano ya kimkataba na ufugaji unaofanywa katika vitalu vingi ni kama ufugaji wa asili na hivyo kutokuwa na tija iliyotarajiwa ya kufuga ng'ombe wa maziwa.

**Mheshimiwa Spika,** changamoto zilizoainishwa hapo juu zimesababishwa kwa kiasi kikubwa na uzembe wa watendaji wa Wizara kwa kutokufanya ufuatiliaji makini wa utekelezaji wa mikataba na matokeo yake ni kuwa

japokuwa baadhi ya wakodishaji wa vitalu hawajatimiza masharti ya mikataba, bado mikataba yao haijavunjwa. Aidha, wawekezaji kwenye vitalu hawafanyiwi tathimini kila mwaka ili kujiridhisha utekelezaji wa masharti ya mikataba waliyopewa.

### 2.3.2 *Tasnia ya Maziwa*

**Mheshimiwa Spika,** tasnia ya maziwa ni mojawapo ya muhimili muhimu katika sekta ya mifugo ambayo inachangia katika kuhakikisha usalama wa chakula, kipato, ajira na maendeleo ya viwanda hapa nchini. Maziwa huchangia theluthi moja ya mapato ya sekta ya mifugo ambayo kwa ujumla wake inachangia 3.8% ya pato la taifa. Tasnia ya maziwa pia ina mchango mkubwa katika kuongeza lishe bora, kuongeza kipato na kumwondolea umaskini mwananchi hususan katika maeneo ya vijijini.

**Mheshimiwa Spika,** ni muhimu kwa Serikali kuimarisha sekta ndogo ya maziwa kwa kuwa maziwa ni:-

· Chakula kamili, yana virutubisho vyote vinavyohitajika mwilini.

· Ni tasnia ambayo huchukua fedha toka kwenye miji na kuzirejesha vijijini kwa mkulima.

· Maziwa ni zao pekee linaloweza kuzalishwa kila siku na kumpa mtu fedha kila siku kwa mwaka mzima.

· Sekta ya maziwa inaweza kutengeneza ajira nyingi kupitia mnyororo wa thamani. Inakadiriwa kwamba kila **lita 100** za maziwa hutengeneza ajira kwa **watu 3**.

· Sekta ya mifugo inachangia pato la ndani la Taifa kwa **3.8% (GDP)** ambapo Sekta ndogo ya Maziwa inachangia **30%** ya pato litokanalo na mifugo.

**Mheshimiwa Spika,** maziwa ni zao pekee linaloweza kumpatia mfugaji pato la uhakika katika kipindi chote cha mwaka tofauti na mazao ya msimu hivyo kumuwezesha kukidhi mahitaji ya kila siku. Hivyo nidhahiri zao la maziwa linaweza kuongeza ajira na kupunguza umasikini kwa kiwango kikubwa kwa wananchi vijijini na kutimiza azma ya Serikali kupitia Mipango ya ujenzi wa viwanda na

kuchangia Taifa kufikia malengo ya kuwa nchi yenye kipato cha kati unaotegemea viwanda vinavyojiendesha kwa kutegemea malighafi za ndani.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na umuhimu huo wa tasnia ya maziwa, maziwa yanayozalishwa kwa ng'ombe wa asili na ng'ombe wa kisasa kwa kiwango kikubwa yanatokana na wafugaji wadogo kwenye mashamba machache ambapo uzalishaji wa maziwa umefikia takribani lita **bilioni 2.4** mwaka 2017/2018 ambapo **asilimia 70** ya maziwa yanazalishwa na ng'ombe wa asili na **asilimia 30** ya ng'ombe wa maziwa wa kisasa.

**Mheshimiwa Spika**, maziwa yanayozalishwa kwa kiasi kikubwa yanatumika katika maeneo ya uzalishaji yani vijijini na kiasi kidogo **asilimia 10** ndiyo yanaingia kwenye mfumo rasmi, ambapo **asilimia 3** ndiyo yanayosindikwa. Hali hii pamoja na mambo mengine inasababishwa na mfumo wa uzalishaji na mtawanyiko wa wafugaji, hivyo kuwa vigumu kuyakusanya maziwa yanayozalishwa na kuyafikisha sokoni.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande mwingine maziwa yanakusanywa na kufikishwa viwandani kupitia vyama vya ushirika yanakusanywa na wakusaji wadogo waliojiajiri kwa kazi hii na kuyafikisha kwenye vituo vya kukusanyia maziwa ambavyo ndio sehemu muafaka kwa ajili ya kukagua na kudhibiti ubora. Hivi sasa vipo **vituo 184** vya kukusanyia maziwa ambavyo uwezo wa ufanyaji kazi wake ni **asilimia 32.9** tu, hali hii husababishwa na kukosekana kwa vifaa vya kupooza maziwa, kukosekana kwa umeme wa uhakika, uchakavu na kukosekana kwa maziwa wakati wa kiangazi.

**Mheshimiwa Spika,** maziwa yanayokusanywa kupitia vituo vya ukusanyaji maziwa husindikwa viwandani. Hivi sasa kuna **viwanda 82** vya kusindika maziwa vyenye uwezo wa kusindika takribani **lita 757,550** kwa siku, kati ya hivyo ni **viwanda 76** ndivyo vinavyofanya kazi. Hivi sasa usindikaji ni **lita 154,100** kwa siku sawa na **asilimia 20.34** ya uwezo wa usindikaji wa viwanda vilivyopo. Hali hii imepelekea uagizwaji wa maziwa kutoka nje ya nchi ili kujaza pengo la

uzalishaji wa ndani ambao hautoshelezi hususan kipindi cha kiangazi. Hivi sasa nchi huagiza takriban **kg LME milioni 20.9** yenye thamani zaidi ya shilingi **30.3bilioni**.

**Mheshimiwa Spika,** maziwa ya unga na maziwa ya muda mrefu (UHT) ndiyo yanayoagizwa kwa wingi kutokana na ukweli kwamba ni viwanda viwili tu vya *Milk Com* – Dar es salaam na Tanga *Fresh* ndio vinazalisha maziwa ya UHT. Aidha, kiwanda cha Azam *Dairies* kilichopo Zanzibar kinazalisha maziwa ya UHT kutokana na maziwa ya unga yanayoagizwa kutoka nje ya nchi.

**Mheshimiwa Spika,** uchache huu wa viwanda vinavyozalisha maziwa ya muda mrefu umetokana na Gharama kubwa za uendeshaji zikiwemo gharama za usindikaji zilizotokana uamuzi wa Serikali kutoza VAT kwenye maziwa na bidhaa zake zilizosindikwa kwa kiwango cha asilimia 18% na kupelekea **viwanda 15** kufunga. **Jedwwali Na. 2** linaonyesha viwanda vya maziwa vilivyofungwa **toka** 2000 hadi Aprili 2018.

**Mheshimiwa Spika,** kufutwa kwa msamaha huo wa VAT sifuri kuanzia mwezi July, 2015 kufuatia marekebisho kwenye Sheria ya VAT 2014 kumekatisha tamaa wawekezaji wa ndani na nje walioonesha nia ya kuwekeza zaidi kwenye sekta ya maziwa hasa katika usindikaji kwani gharama za uendeshaji zimeongezeka na zinahusisha pia Input -Tax zinazotozwa kwenye umeme, maji, usafirishaji (*fuel*), vifungashio na vipuri vya mashine za kusindika maziwa. Hapa nchini Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT), hutozwa kwa bidhaa za maziwa yaliyosindikwa (*processed milk*) kama *yogurt*, *cheese*, *ghee*, *buter* n.k.

**Mheshimiwa Spika,** maziwa yasiyosindikwa (*unprocessed milk*) kama Fresh milk na Cream yamesamehewa kodi (*VAT Exempt)* lakini wakati yanasindikwa (andaliwa) yanatumia gharama mbalimbali kama umeme, usafirishaji, maji, vifungashio ambavyo vina VAT tayari. Hivi vyote huingia kwenye gharama za uzalishaji na hivyo kufanya maziwa yawe ghali na msindikaji hawezi

kudai kurejeshwa Input Tax iliyotumika kutokana na mfumo wa kodi unaotumika sasa ya *VAT Exempt* kutomruhusu.

**Mheshimiwa Spika,** usindikaji ni kitu muhimu katika mnyororo wa thamani wa maziwa. Hapa nchini usindikaji unakabiliwa na gharama kubwa za usindikaji zinazochangiwa na uwepo wa tozo na mamlaka nyingi zinazosimia sekta ya maziwa (*multiple regulations and levies*) kama inavyoonyeshwa kwenye **Jedwali Na.3.** Tozo hizo hutozwa pamoja na zile za VAT kwenye vifungashio, umeme, maji n.k. Tozo hizi kwa pamoja zimefanya gharama za usindikaji kuwa kubwa hivyo kusababisha viwanda kushindwa kufanya kazi kwa uwezo wake.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na gharama kubwa za uzalishaji na usindikaji maziwa zimepelekea nchi yetu kushindwa kushindana katika ushindani wa soko la Afrika Mashariki kutokana na nchi za Afrika Mashariki kuzalishwamaziwa kwa gharama ndogo na hivyo Tanzania kulazimika kuagiza kutoka nje ya nchi, ambapo bidhaa za maziwa chini ya HS 0401, ambayo ni UHT, zaidi ya asilimia 98 ya maziwa yanayoingizwa nchini yanatokea Kenya.

**Mheshimiwa Spika, Jedwali Na. 4** linaonyesha ufanisi wa uzalishaji na usindikaji wa maziwa baina ya Tanzania, Uganda na Kenya. Katika jedwali hili inaonekana kuwa, maziwa yanayozalishwa Tanzania yanazalishwa na kusindikwa kwa gharama kubwa na hivyo kushindwa kushindana katika soko.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na changamoto hizo zilizoainishwa hapo juu, tasnia ya maziwa inakabiliwa pia na changamoto mbalimbali zifuatazo:-

· Uhamasishaji mdogo wa kutumia bidhaa zitokanazo na maziwa inayopelekea unywaji wa maziwa kuwa chini takribani lita 47 kwa mwaka chini ya kiwango cha lita 200 kwa mwaka kinachopendekezwa na FAO.

· Matumizi ya Maziwa ya unga na UHT toka nje kwenye ofisi na taasisi za Serikali kwa nyakati kadhaa imekuwa ikitoa msisitizo wa kutokutumia maziwa yanayozalishwa ndani katika taasisi na ofisi za Serikali na mashirika ya umma.

· Kutokuwepo kwa vituo vya kukusanya maziwa (*Milk collection center*) kwenye maeneo yenye wafugaji wa maziwa.

· Uhaba wa maziwa unaotokana na uzalishaji mdogo wa maziwa kutokana na uhaba wa malisho ya mifugo wakati wa kiangazi.

· Idadi ndogo ya ng'ombe wa maziwa.

· Ufugaji wa ng'ombe usio na tija.

· Upungufu wa wataalam wa usindikaji.

**2.3.3 *Tasnia ya ngozi***

**Mheshimiwa Spika,** ngozi ni moja ya mazao muhimu ya mifugo na imekuwa ikiingizia Taifa fedha za kigeni kwa kuuzwa nje ya nchi. Zao la ngozi limeendelea kuchangiakatika kipato cha wananchi wanaojihusisha na zao hili katika mnyororo mzima wa thamani, wafugaji, wafanyabiashara wasindikaji na watengenezaji wa bidhaa za ngozi.

**Mheshimiwa Spika,** idadi ya mifugo iliyopo nchini inategemewa kuzalisha vipande **milioni 3.1** vya ngozi ya **ng'ombe**, **milioni 4.7** vya ngozi za **mbuz**i, na **milioni 1.3** ya ngozi za **kondoo** ambavyo vingeweza kusindikwa kulingana na idadi ya viwanda vilivyopo nchini. Utengenezaji wa bidhaa za ngozi kwa kiasi kikubwa bado uko katika kiwango cha chini kwani kuna viwanda vikubwa vichache vya kutengeneza viatu na bidhaa za ngozi nchini. Aidha, wapo watengenezaji wadogo wadogo wanaotengeneza jozi chache za viatu vya ngozi ambazo haziwezi kukidhi mahitaji ya viatu nchini.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na kwamba Tanzania inao uwezo mkubwa wa kuzalisha ngozi, kutokana na uwepo wa idadi kubwa ya mifugo, kiuhalisia ngozi zinazokusanywa ni nusu tu ya zile ambazo zingetakiwa kuzalishwa. Hali hii inatokana na changamoto mbalimbali zinazoikabili sekta ya ngozi katika mnyororo mzima wa thamani. Changamoto zilizopo zinaanzia kwa wafugaji, waboreshaji wa ngozi, wasindikaji, wafanyabiashara wa nje na ndani ya nchi, na watengenezaji wa bidhaa za ngozi. Changamoto hizo zimegawanyika katika maeneo matatu ya uzalishaji ngozi, usindikaji ngozi na utengenezaji wa viatu na bidhaa za ngozi.

**Mheshimiwa Spika,** katika eneo la uzalishaji kuna changamoto zifuatazo:-

- Ufugaji duni unaosababisha uharibifu wa ngozi- mfano magonjwa ya ngozi;

- Ubora hafifu wa ngozi kutokana na upigaji ovyo chapa;

- Uchunaji mbovu; na ukaushaji na uhifadhi duni wa ngozi na hivyo kuwepo kwa makusanyo madogo ya ngozi zinazofaa katika usindikaji.

**Mheshimiwa Spika,** katika hatua ya usindikaji wa ngozi kuna changamoto mbalimbali zinazosababisha sekta ya ngozi kutokuwa kwa kiwango kinachotarajiwa, changamoto hizo ni pamoja na:-

- Ubora hafifu wa ngozi unaosababishwa na ufugaji wa kienyeji, uchinjaji na uchunaji mbovu, uhifadhi duni na ulaji hafifu wa nyama ndani ya nchi na kukosa soko la kutosha kuuza nyama nje ya nchi;
- Utoroshwaji wa ngozi mipakani;
- Machinjio yasiyokidhi viwango;
- Ukosefu wa wataalamu waliobobea kwenye sekta ndogo ya ngozi;
- Upatikanaji mgumu wa kemikali za ngozai;

- Uwezao wa viwanda kusindika ngozi katika hatua ya awali hali inayosababisha watengeneza bidhaa za ngozi kukosa maligahafi ya kutengenezea bidhaa za ngozi;
- Upatikanaji mgumu wa mikopo kwa wawekezaji wa sekta ndogo ya ngozi;
- Kukosekana kwa umeme wa uhakika; na
- Ucheleweshwaji wa bandarini na forodha.

**Mheshimiwa Spika,** eneo la utengenezaji wa vitu na bidhaa za ngozi unakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

(i) Ubora duni na upatikanaji wa ngozi zilizosindikwa hadi hatua ya umaliziaji;

(ii) Gharama kubwa ya malighafi zinazoagizwa kutoka nje ya nchi;

(iii) Ushindani usio sawia unaosababishwa na uangizaji wa bidhaa duni na za mitumba ambazo huuzwa kwa gharama nafuu;

(iv) Kukosekana kwa ubunifu na utaalamu wa utengenezaji wa bidhaa za ngozi;

(v) Mbinu duni za utafutaji wa masoko na

(vi) Kukosekana kwa uwekezaji.

**Mheshimiwa Spika,** changamoto zote hizo zimesababisha uhaba wa upatikanaji wa malighafi ya ngozi ukilinganisha na kiwango kikubwa cha mifugo iliyopo nchini na hivyo kushindwa kutumia fursa iliyopo nchini ya mahitaji ya bidhaa za ngozi kwani viatu pekee huitajika **jozi milioni 54** ambapo viatu **jozi miliuoni 40** huagizwa kutoka nje kila mwaka wakati mahitaji ya viatu vya shule ni wastani wa **jozi milioni 12** kwa mwaka. Mahitaji mengine ni pamoja na mabegi, mikoba, mikanda na makoti.

**Mheshimiwa Spika,** endapo sekta ya ngozi itawekewa mikakati madhubuti katika kufundisha wafugaji na maamfisa ugani kuhusu ufugaji bora wa awanyama na upigaji chapa unaofaa bila kuharibu ngozi, kukamilisha mapema iwezekanvyo upanuzi wa kiwanda cha ngozi cha Karanga na kuhamasisha sekta binafsi kufungua viwanda vya ndozi nchini ,kuhamasisha matumizi ya bidhaa za ngozi

zinazozalishwa na viwanda vya ndani kama viatu vya shule na majeshi pamoja na kuweka ushuru wa uagizaji wa viatu vinavyotoka nje ya nchi kutasaidia kuimarisha sekta ya ngozi na kulinda viwanda vya ndani.

### 2.4 *Sekta ya Uvuvi*

**Mheshimiwa Spika,** Tanzania imejaliwa kuwa na maeneo mengi ya maji baridi na maji bahari ambapo kuna rasilimali nyingi za uvuvi. Eneo la maji ya ndani lenye ukubwa wa takriban **kilomita za mraba 62,000** ambazo ni **asilimia 6.5** ya eneo lote la ardhi. **Ziwa Victoria** lina **kilomita za mraba 35,088**; **Ziwa Tanganyika** lina **kilomita za mraba 13,489**; **Ziwa Nyasa** lina **kilomita za mraba 5,760**; **Ziwa Rukwa** lina **kilomita za mraba 3,000**; **Ziwa Eyasi** lina **kilomita za mraba 1,000**; na maeneo madogo ya maji (maziwa madogo,mito na mabwawa) yenye jumla ya kilomita za mraba 1,000.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa maji ya bahari, nchi yetu ina eneo la **kilomita za mraba 64,000** na ukanda wa pwani wenye urefu wa **kilomita 1,424** kutoka mpaka wa kaskkazini na Kenya mpaka wa kusini na Msumbiji. Ukanda wa uchumi wa Bahari Kuu una ukubwa wa maili za majini zipatazo 200 sawa na **kilomita za mraba 223,000**, eneo hili lina ipa nchi eneo la ziada la bahari na rasilimali za uvuvi. Maeneo haya yakitumiwa ipasavyo yataiwezesha sekta ya uvuvi kuwa na mchango mkubwa katika kuwapatia wananchi ajira, lishe bora, kipato na kuchangia katika pato la Taifa.

**Mheshimiwa Spika,** zaidi ya wananchi **milioni 4.0** wameendelea kutegemea shughuli za uvuvi ikiwemo biashara ya samaki, uchakataji wa mazao ya uvuvi, utengenezaji wa zana na vyombo vya uvuvi na biashara zingine zitokanazo na mazao ya uvuvi. Katika kipindi cha mwaka 2016/2017 sekta ya uvuvi ilikuwa kwa **asilimia 4.2** na kuchangia **asilimia 2.0** katika pato la Taifa.

**Mheshimiwa Spika,** sekta ya uvuvi inachangia takribani asilimia 30 ya protini inayopatikana na wanyama.

Hivi sasa wastani wa ulaji wa samaki kwa mtanzania unakadiriwa kuwa **kilo 8** kwa mtu kwa mwaka ikilingnishwa na **kilo 18** kwa mtu kwa mwaka ambazo zinapendekezwa na Shirika la Kilimo na Chakula la Umoja wa Mataifa (FAO).

**Mheshimiwa Spika,** kiwango cha rasilimali za uvuvi kinachoweza kuvuliwa bila kuathiri uwepo wa rasilimali ya uvuvi ni **tani za kimetriki 750,000**. Wastani wa uvunaji wa samaki kwa mwaka ni **tani 350,000** wakati mahitaji ya samaki kwa mwaka yanakadiriwa kuwa **tani 378,352**.

**Mheshimiwa Spika,** kufuatia maelezo hayo, inadhihirisha kuwa Tanzania hatujaweza kutumia fursa za sekta hii kwa kiwango kikubwa kwa kuzingatia mnyororo mzima wa kuongeza thamani unaohusisha usindikaji wa samaki.

### 2.4.1 Ukuzaji viumbe kwenye maji

**Mheshimiwa Spika,** nchini Tanzania kuna uwezekano mkubwa wa kuendeleza ukuzaji viumbe kwenye maji kwa kuwa nchi ina rasilimali kubwa za maji ambayo yanajumuisha Bahari ya Hindi, maziwa, mito na mabwawa yaliyoenea nchini kote.

**Mheshimiwa Spika,** licha ya uwepo wa rasilimali nyingi zenye kuhitaji kuwezesha ukuaji viumbe kwenye maji, maendeleo ya tasnia hii yamekuwa yakikua kwa kasi ndogo ikilinganishwa na rasilimali zilizopo. Kasi ndogo ya ukuzaji viumbe kwenye maji imechangiwa na ukosefu wa rasilimali watu, mbegu bora, chakula bora, teknolojia sahihi na huduma za ugani.

**Mheshimiwa Spika,** ukuzaji viumbe kwenye maji ili uwe na tija unapaswa kuchukuliwa kama shughuli muhimu ya kibiashara na yenye uwezo wa kuzalisha samaki bora kwa ajili ya soko la ndani na la nje ya nchi, kuboresha hali ya maisha ya jamii kwa kutengeneza ajira, kuhakikisha usalama wa chakula na kuongeza kipato.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia kuwa uvuvi katika maji ya asili unazidi kupungua wakati mahitaji ya samaki duniani yanazidi kuongezeka kutokana na kuongezeka kwa idadi ya watu na umuhimu wa samaki na mafuta yake kwenye mwili wa binadamu, hivyo ukuzaji viumbe kwenye maji unapaswa kuziba pengo la upatikanaji wa samaki na mazao yake kwa kuzalisha samaki kwa njia endelevu. Ili tasnia hii iweze kufanikiwa Serikali inapaswa kuboresha mifumo ya ufugaji samaki ambao kwa muda mrefu umechukuliwa kama shughuli ya kujikimu katika ngazi ya familia.

**Mheshimiwa Spika,** tasnia ya ukuzaji viumbe kwenye maji ni moja kati ya sekta za kilimo zinazokua kwa kasi duniani kwani takwimu za FAO kwa mwaka 2018 zinaonyesha takriban **asilimia 53** ya mazao yanayovunwa kutokana na rasilimali za kwenye maji inatokana na ukuzaji viumbe kwenye maji.

**Mheshimiwa Spika,** fursa za kuendeleza ukuzaji viumbe kwenye maji zipo nyingi na endapo zitatumika vizuri tasnia hii itakuza biashara ya mazao na bidhaa zinazotokana na viumbe wakuzwao kwenye maji na kuongeza kipato kwa wazalishaji binafsi na Taifa kwa ujumla. Baadhi ya fursa zilizopo ni pamaoja na:-

i. Taifa lina bandari na viwanja vya ndege kwa ajili ya kuwezesha urahisi wa kuingiza pembejeo za ukuzaji viumbe kwenye maji na kusafirisha mazao yatokanayo na viumbe waliokuzwa kwenye maji nje ya nchi;

ii. Kuna taasisi zinazotoa mafunzo yanayohusiana na ukuzaji viumbe kwenye maji. Taasisi hizo ni pamoja na Wakala wa Mafunzo ya Uvuvi Tanzania (FETA), Vyuo Vikuu kama Chuo Kikuu cha Dar es salaam, Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine na Chuo Kikuu cha Dodoma pamoja na Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanznia (TAFIRI);

iii. Rasilimami maji ya kustosha;

iv. Uwepo wa Ardhi ya kutosha;

v. Fursa ya kuzalisha mbegu / vifaranga vya samaki;

vi. Fursa ya kuongeza thamani mazao yatokanayo na viumbe wakuzwao kwenye maji;

vii. Fursa ya kuwekeza kwenye park za samaki wa burudani.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na fursa zilizoainishwa hapo juu na uwepo wa rasilimali za kutosha zinazohitajika kwa maendeleo ya uzalishaji wa mazao ya ukuzaji viumbe kwenye maji bado ni mdogo. Baadhi ya changamoto hizo ni pamoja na:-

- Ukosefu wa mbegu/vifaranga bora vya samaki;
- Ukosefu wa vyakula bora kwa samaki wakubwa na vifaranga;
- Ukosefu wa mitaji na mikopo kwa ajili ya uwekezaji wa ukuzaji viumbe kwenye maji;
- Ukosefu wa zana, vifaa na pembejeo zinazotumika kukuza viumbe kwenye maji n.k

### 2.4.2 Shirika la uvuvi Tanzania- TAFICO

**Mheshimiwa Spika,** Ukanda wa Uchumi wa Bahari Kuu (EEZ) una kina kikubwa cha samaki ambacho huitaji meli kubwa na za kisasa ili kuweza kuwafikia samaki walioko majini. Kwa sababu hiyo meli za kigeni ndio zimekuwa zikifika katika eneo la bahari kuu sehemu ya Tanzania na kuvua samaki huku watanzania wakiwa hawanufaiki na rasilimali hiyo muhimu.

**Mheshimiwa Spika,** ili kuiwezesha nchi kunufaika na rasilimali za uvuvi wa bahari kuu katika kufikia Uchumi wa Viwanda katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari Kuu, Serikali imedhamiria kufufua Shirika la Uvuvi Tanzania ambalo litawezesha Serikali kuwa na Meli za Kitaifa (*National Fleets*) zitakazovua kibiashara kwenye eneo la bahari kuu.

**Mheshimiwa Spika,** Mpango wa Muda Mrefu unahusisha kununua meli mbili aina za *Purse Seiner* (kwa kadirio la **Shilingi Bilioni 19.8**) na *Long Liner* (kwa kadirio la **Shilingi Bilioni 13.4**) ifikapo Desemba, 2019. Aidha, Mpango

wa Muda Mfupi unalenga uvuvi katika maji ya kitaifa (*Territorial Waters*) unahusisha kununua meli ndogo za uvuvi ifikapo Desemba, 2019 kwa kadirio la **Shilingi Bilioni 2**.

**Mheshimiwa Spika,** mipango hii ni mikubwa na inahitaji fedha nyingi kwa muda mfupi hivyo utekelezaji wake unatakiwa kufanyika mapema iwezekanavyo. Hata hivyo, tangu kikao cha Baraza la Mawaziri kilichokaa tarehe 05 Februari, 2015 na kuiagiza Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kufufua Shirika la Uvuvi, hadi sasa hatua iliyofikiwa ya kufufuliwa kwa shirika hili ni kuanzishwa kwa Manejimenti ya TAFICO ambayo ina wafanyakazi wanne tu ambao ni Kaimu Meneja Mkuu, Kaimu Meneja Uzalishaji na Operesheni, Katibu Muhtasi na Dreva.

**Mheshimiwa Spika,** Menejimenti hii ina wajibu wa kuratibu ufufuaji wa shirika na katika kutekeleza wajibu huo, Menejimenti imetekeleza kazi mbalimbali zifuatazo:-

- Kutambua, kuainisha na kuhakiki mali za TAFICO;
- Kuandaa Dhana kuhusu Mradi wa kufufua TAFICO;
- Kuandaa Mpango wa Biashara; na
- Kuandaa Mikutano mbalimbali na wadau wa maendeleo kwa ajili ya kuijengea TAFICO uwezo.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia upotevu mkubwa wa mapato ya mazao ya samaki wanaopatikana kwenye Ukanda wa Uchumi wa Bahari kuu kwa muda mrefu, mchakato wa kufufua shirika hili ulitakiwa ufanyike kwa haraka ili kulinusuru Taifa kuendelea kupata hasara.

### 2.4.3 Operesheni Sangara 2018

**Mheshimiwa Spika,** Sera ya Taifa ya Uvuvi ya Mwaka 2015 imeeleza umuhimu wa sekta ya Uvuvi ili kuchangia kikamilifu kufikia malengo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2025 ambapo lengo kuu la sekta ya uvuvi ni kuendeleza, kuhifadhi, kusimamia na kuvuna kwa uendelevu rasilimali za uvuvi kwa manufaa ya kizazi cha sasa na vizazi vijavyo.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia lengo la sekta ya uvuvi, Wizara ya Mifugo na Uvuvi iliendesha Operesheni Sangara 2018 kutokana na kukithiri kwa Uvuvi haramu uliokuwa ukifanyika bila kufuata Sheria na Kanuni zinazosimamia rasilimali za uvuvi na hivyo kupelekea kuendelea kupungua kwa idadi ya samaki sangara ambao hawaruhusiwi kuvuliwa kisheria **(chini ya sm 50)** na ukweli kwamba samaki aina ya sangara waliko wengi ziwani ni wachanga kutokana na uvuvi haramu na endapo watadhibitiwa ili wakue itasaidia kuongeza uzalishaji wa samaki.

**Mheshimiwa Spika,** kabla ya kuanza kwa Operesheni Sangara, 2018 ilibainika kuwa zaidi ya **asilimia 75** ya wavuvi wote wa Ziwa Victoria walikuwa wanavua kwa kutumia nyavu haramu, maduka yote ya vifaa vya uvuvi yalikuwa yanauza nyavu haramu, viwanda vya kutengeneza nyavu vilikuwa vinatengeneza nyavu haramu, Watendaji na viongozi wa vikundi vya Usimamizi wa Rasilimali za uvuvi (BMUs) walikuwa wanajishughulisha an uvuvi haramu.

**Mheshimiwa Spika,** unaweza kumtambua mvuvi aneyejishughulisha na uvuvi haramu ikiwa mvuvi huyo anatekeleza shughuli zake za uvuvi bila kuwa na leseni, kuvua katika maeneo yasiyoruhusiwa, kutumia chombo kisichosajiliwa, matumizi ya mabomu na sumu wakati wa kuvua, kutumia nyavu za utali/ timba, na kuvua kwa kokoro/ juya/ kavogo na nyavu zenye macho madogo chini ya inchi tatu kwa nyavu za makila na chini ya nchi nane kwa nyavu za dagaa. Mara nyingi wavuvi hutumia njia na mbinu haramu za uvuvi ili kujipatia utajiri wa haraka

**Mheshimiwa Spika,** Operesheni Sangara 2018 ililenga kudhibiti usafirishaji na uchakataji wa biashara ya samaki wachanga, kuongeza maduhuli ya Serikali, kudhibiti uharibifu wa maliasili na mazingira, kuwatambua wamiliki wa vyombo vya uvuvi haramu na wanaofanya biashara ya uvuvi haramu na kuwachukulia hatua za kisheria, kudhibiti zana za uvuvi haramu zilizopo madukani, viwandani na mipakani.

Aidha, malengo mengine ya Operesheni Sangara 2018 yalikuwa kubaini na kuvichukulia hatau viwanda vinavyotengeneza nyavu haramu, kufanya ukaguzi maalumu katika viwanda, *cold storage facilities*, *deep freezers* ili kubaini samaki wachanga na wakubwa kama ilivyoelekezwa na Sheria na kujifunza na kupata uzoefu namna bora ya kulinda na kuendeleza rasilimali za uvuvi na kutoa mapendekezo kwa Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Operesheni Sangara 2018 imewezesha kuongezeka kwa makusanyo ya maduhuli ya Serikali Kuu yaliongezeka kutoka shilingi **8,521,301,826.26** kabla ya operesheni (**Julai- Desemba, 2017**) hadi shilingi **17,731,902,460.74** (**Januari- Juni 2018**), kuongezeka kwa mapato ya soko la Kirumba Mwaloni kutoka **shilingi milioni 30** hadi **shilingi milioni 190** kwa mwezi, kuongezeka kwa kiwango cha utii wa sheria na kanuni za uvuvi kutoka kwa wafanyabiashara, upatikanaji wa samaki wanaokubalika kisheria umeongezeka bila hata ya wavuvi kwenda umbali mrefu kuvua na hivyo kuwapunguzia wavuvi gharama za uendeshaji na kuongezeka kwa ukubwa wa samaki wanaochakatwa viwandani n.k.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio yaliyopatikana, Serikali imetambua kuwa Sheria ya Uvuvi ya Mwaka 2003 na Kanuni zake za Mwaka 2009 hazikidhi usimamizi wa rasilimali nyingi za uvuvi zilizopo nchini, kutofanyika kwa doria za mara kwa mara kunapelekea wananchi kuwa huru na kuvua watakavyo na upo upungufu mkubwa katika utoaji wa vibali vya kusafirisha mazao na zana za uvuvi hivyo kukaribisha mazingira ya rushwa.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio yaliyopatikana Opereshion Sangara, 2018 ilikabiliwa na malalamiko kutoka kwa wananchi na wadau wa uvuvi kuwa operesheni hii iliendeshwa kwa namna ya kukiuka misingi ya haki za binadamu kwani utekelezaji wake uligubikwa na vitisho, ubabe na rushwa.

### 2.4.4 Dawati la Sekta Binafsi na Umuhimu wake katika kukuza Uchumi

**Mheshimiwa Spika,** Sekta binafsi ni mdau muhimu na inajihusisha katika kuendeleza biashara kwa kuwekeza kwenye shughuli za uzalishaji, usindikaji na masoko ili kuendeleza sekta ya Mifugo na Uvuvi. Kwa kutambua fursa kubwa ya uwekezaji iliyopo kwenye mazao ya mifugo ambayo ni nyama, ng'ombe, kuku, maziwa, mayai na ngozi na kwa upande wa uvuvi ni uvuvi wa samaki kwenye mito na maziwa, uvuvi wa kando kando ya bahari na kwenye kina kirefu na ufugaji wa samaki kwenye mabwawa na vizimba vilivyoengwa kwa ajili hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kutambua fursa hizo, Wizara imeanzisha Dawati la Sekta Binafsi kwa kuwezesha sekta binafsi kuongeza uwekezaji wenye tija katika mazao ya mifugo na uvuvi ili kuongeza uchangiaji wa kukuza sekta hizi na hatimae kuongeza ajira na pato la Taifa.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mambo mengine, Dawati la Sekta binafsi lina wajibu wa kuamsha na kuvutia wawekezaji katika taasis za uwekezaji za mifugo na uvuvi na kuziunganisha na taasisi za kifedha ndani nan je ya nchi kwa ajili ya kupata mitaji. Aidha, Dawati la sekta binafsi linashirikiana na wadau mbalimbali kutangaza fursa za sekta za mifugo na uvuvi na kufanya kazi kwa karibu na wawekezaji wanaoendelea kuwekeza.

**Mheshimiwa Spika,** tangu kuanzishwa kwake mwezi Oktoba, 2018 Dawati hili limewezesha:-

- Kuunganisha makampuni yanayotoa huduma za pembejeo za mifugo na uvuvi na wawekezaji mbalimbali;
- Kutatua changamoto zinazowakabili wawekezaji kwenye sekta za mifugo na uvuvi;
- Kuwa na vikao vya kila mwezi vinavyokutanisha watendaji wakuu wa wizara na wawekezaji kwa ajili ya kujadili changamoto zinazowakabili wawekezaji na kutafuta ufumbuzi wa haraka wa changamoto zilizobainika na kujenga mahusiano mazuri nay a karibu na wawekezaji.

· Kuwaunganisha wawekezaji na kufuatilia upatikanaji wa mikopo yenye riba nafuu kutoka Benki ya Maendeleo ya Kilimo pamoja na taasisi zingine za fedha, ikiwa ni pamoja na kuhamasisha uanzishwaji wa vyama vya ushirika ili kupata mikopo;

· Kuwezesha makubaliano ya MOU yatakayo pelekea ongezeko la uchakataji wa Maziwa katika viwanda vinne vya kimkakati vya (ASAS LTD – IRINGA, TANGA FRESH LTD-TANGA, MILK COM LTD – DAR ES SALAAM na AZAM DAIRY PRODUCTS – ZANZIBAR) kwa **asilimia 84** kutoka **lita 154,100 kwa siku** hadi **lita 284,500** sawa na ongezeko la **lita 130,500** kufikia Desemba, 2019 na

· Kuongeza ushirikiano na wadau wa maendeleo kama vile WORLD BANK, DALBERG, ANSAF, ASPIRE, TADB, PASS na SAGCOT.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imefurahishwa na ubunifu huu uliofanywa na watendaji wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi na inatoa pongezi kwa uongozi wa wizarana kuzitaka wizara zingine kwenda kujifunza namna dawati la sekta binafsi linavyofanya kazi kwa nia ya kujenga uchumi wa nchi yetu.

### 2.5 *Sekta ya Maji*

**Mheshimiwa Spika,** Sera ya Taifa ya Maji ya mwaka 2002 inaelekeza kuwapatia wananchi waishio vijijini maji safi na salama katika umbali usiozidi **mita 400** kutoka kwenye makazi yao. Ili kufikia azma hiyo, Serikali imeendelea kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji kwa wananchi waishio vijijini kwa kujenga, kupanua na ukarabati miradi ya maji kwa lengo la kufikia **asilimia 85** ya wananchi wanaopata huduma ya maji safi na salama katika maeneo ya vijijini ifikapo mwaka **2020**.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa mijini, ili kuhakikisha wakazi waishio mijini wanapata huduma bora ya maji safi na usafi wa mazingira, Sera ya Maji inaelekeza kujenga, kukarabati na kupanua miundombinu ya maji safi na usafi wa maji takaili kuweza kutoa huduma endelevu kwa

wakazi waishio mijini na pembezoni mwa miji. Ili kufikia malengo hayo, katika mwaka 2017/2018, Wizara imeendelea kutekeleza miradi yamaji katika jiji la Dar es Salaam, Miji Mikuu ya Mikoa, Miji Mikuu ya Wilaya, Miji Midogo pamoja na miji na vijiji vinavyohudumiwa na Miradi ya Maji ya Kitaifa.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia maelezo hayo, wakati wa utekelezaji wa majukumu yake Kamati ilipata taarifa kuhusu:-

**i.** Hali ya upatikanaji wa huduma ya maji safi na uondoshaji majitaka katika miji mikuu ya mikoa ya Shinyanga, Bukoba, Mwanza, Geita, Manyara, Dodoma, Arusha, Dar es salaam, Kilimnjaro.

**ii.** Hali ya upatikanaji wa huduma ya maji safi na uondoshaji majitaka katika Miji Mikuu ya Wilaya za Same – Mwanga- Korogwe, Kigoma Ujiji.

### 2.5.1 *Utekelezaji wa Miradi Mbalimbali ya Maji Katika Mkoa wa Arusha*

**Mheshimiwa Spika,** huduma za maji katika moa wa Arusha zinasimamiwa na Mamlaka ya Maji katika jiji la Arusha na Mamlaka za Maji katika miji midogo ya Karatu, Loliondo, Monduli na Usa River kwa upande wa maji mijini; na halimashauri za wilaya kwa upande wa maji vijijini.

**Mheshimiwa Spika,** hali ya upatikanaji wa huduma za maji hadikufikia mwezi Agosti, 2018 imefikia wastani wa **asilimia 52.2** kwa upande wa mijini na **asilimia 65.61** kwa upande wa vijijini ikilinganishwa na lengo la Taifa la kuongeza huduma ya upatikanaji wa maji safi na salama, kufikia **asilimia 85** vijijini, na **asilimia 90** miji mikuu ya Wilaya na **asilimia 95** miji mikuu ya mikoa ifikapo mwaka 2020.

**Mheshimiwa Spika,** changamoto kubwa katika mkoa wa Arusha ni upatikanaji wa vyanzo vya uhakika vya maji hasa katika miji ya Longido, Loliondo/ Ngorongoro na Karatu kutokana nahali ya kijiografia na hali ya hewa ya ukame katika maeneo hayo.

**Mheshimiwa Spika,** katika kuboresha upatikanaji wa huduma ya maji katika mkoa wa Arusha, Serikali inatekeleza miradi mbalimbali ikiwa ni sehemu ya Utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji Awamu ya Pili.

**Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa miradi hiyo unakabiliwa na changamoto mbalimbali kama vile upatikanaji wa fedha za miradi usiokuwa na uhakika, uhaba wa vyanzo vya maji, migogoro ya kimkataba kati ya Halmashauri na Wataalamu Washauri/ Wakandarasi, uhaba wa wataalam katika halmashauri na miradi kutokuwa endelevu kutokana na kukosa matengenezo ya mara kwa mara.

### 2.5.2 *Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Shinyanga (SHUWASA)*

**Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Shinyanga (SHUWASA) ina vyanzo viwili vya maji ambavyoni Bwawa la Ningh'wa linalokidhi **asilimia 20** ya kiasi cha maji yanayotumika na mradi wa maji wa Ziwa Victoria unaokidhi **asilimia 80**.

**Mheshimiwa Spika,** matumizi ya mji kwa Mji wa Shinyanga kwa sasa kwa eneo ambalo lina mtanadao wa maji ni mita za ujazo 12,000 kwa siku wakati makadirio ya maji mahitaji kwa eneo lote linalohudumiwa na Mamlaka ni ita za ujazo 20,000 kwa siku. Sababu ya matumizi ya maji kuwa kidogo kuliko mahitaji ni ufinyu wa mtanado, ambapo wananchi wengi wa Manispaa ya Shinyanga hawajafikiwa na mtandao wa maji.

**Mheshimiwa Spika,** hali hii imesababishwa na usanifu waujenzi wa mradi wa Ziwa Victoria, uwezo wa bomba linalofikisha maji ktika mji wa Shinyanga ni lita 40 kwa siku, hivyo changamoto ya mji wa Shinyanga ni ufinyu wa mtanadao wa usambazaji.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa huduma ya uondoaji Maji Taka Manispaa ya Shinyanga haina

miundombinu ya mfumo wa uondoaji majitaka. Kwa sasa, huduma ya kuondoa maji taka Mjini Shinyanga inaendeshwa na Halimashauri ya Maniaspaa na watu binafsi kwa kutumia magari ya kunyonya maji taka na kuyamwaga katika eneo mahsusi kwa kazi hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya SHUWASA inakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

· Ufinyu wa mtandao wa usambazaji majji safi hivyo wananchi wengi kutofikiwa na huduma hiyo;

· Kukosekana kwa miundombinu ya mfumo wa huduma ya uondoaji wa maji taka katika Manispaa ya Shinyanga;

· Uvamizi wa wananchi na kufanya shughuli mbalimbali za kibinadamu ikijumusha kilimo, uvuvi na mifugo kwenye chanzo cha maji cha bwawa la Ning'huwa na

· Madeni makubwa ya Taasisi za Serikali zinazochangia kwa kiasi kikubwa kuzorotesha ufanisi wa SHUWASA kwenye uendeshaji wake.

### 2.5.3 Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Bukoba (BUWASA)

**Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Bukoba (BUWASA) inahudumia wakazi wa Manispaa ya Bukoba wapatao takribani **169,000**, kati ya hao wakazi walio ndani ya mtandao wa usambazaji maji ni **149,318** ambao wanapata huduma ya maji safi na salama sawa na **asilimia 88.4** ya wakazi wote waishio kwenye eneo hilo.

**Mheshimiwa Spika**, chanzo kikubwa cha Maji kwa sasa ni chanzo kipya cha BUNENA aidha, vyanzo vya maji vya dharura ni pamoja na Custom, Kagemu Nyakanyasi, Kisindi Mafumbo na G/ Gallary ambavyo hutumika endapo chanzo kikuu cha BUNENA kitasimama kwa matengenezo.

**Mheshimiwa Spika,** mahitaji ya maji kwa wakazi wa Manispaa ya Bukoba ni yanakadiriwa kuwa mita za ujazo **13,000** kwa siku kwa kata 14, kwa sasa uwezo wa uzalishaji

maji kwa siku ni mita za ujazo **8,500** ambazo zinahudumia kata 12. Kata mbili zilizobaki zinatafutiwa fedha kwa ajili ya kuweka miundombinu ya maji.

**Mheshimiwa Spika,** licha ya kwamba Mamlaka ya Maji Bukoba imefanikiwa kutoa huduma ya maji kwa kiwango kikubwa kwa wakazi wa Manispaa, BUWASA inakabiliwa na changamotao ya uchafuzi wa mazingira kwenye vyanzo vya maji kutokana na shughuli za binadamu kama kilimo, mifugo na uvuvi, upotevu wa maji kwa **asilimia 42** unaotokana na uchakavu wa miundombinu na wizi wa maji, ukosefu wa huduma ya maji taka na ucheleweshaji wa kulipa ankara za maji.

**2.5.4 Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Dodoma (DUWASA)**

**Mheshimiwa Spika,** utafiti nastadi za juu ya mahitaji ya maji kwa wakazi wa Jiji la Dododma ulifanywa mwaka 2002/2003 ambapo ulibaini mahitaji ya maji mjini ni wastani wa mita za ujzao 46,000 kwa siku, kiasi hiki kinajumuisha mahitaji ya Chuo Kikuu Dodoma yanayofikia wastani wa mita za ujazo 3,000 kwa siku.

**Mheshimiwa Spika,** chanzo pekee cha uzalishaji maji kwa matumizi ya wakazi wa Jiji la Dododma ni visima virefu vilivyochimbwa katika Bonde la Makutupora ambavyo uwezo wa visima hivi kusafirisha maji ni mita za ujazo 61,500 kwa siku.

**Mheshimiwa Spika,** uwezo huu wa uzalishaji maji uliongezeka mwaka 2015 baada ya uwekezaji mkubwa wa mradi wa kuboresha huduma ya upatikanaji maji safi kwa wakazi wa Dodoma kutoka chanzo cha Mzakwe kutoka wastani wa mita za ujazo 32,000 kwa siku hadi kufikia mita za ujazo 61,500 kwa siku.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na kwamba mahitaji yankadiriwa kuwa mita za ujazo 46,000 kwa siku, hivi sasa DUWASA inazalisha, kusafirisha na kusambaza wastani wa

mita za ujazo 44,000 kwa siku. Hali hii imesababishwa na ufinyu wa mabomba ya kusambazia maji, hata hivyo matarajio ni kufikisha mita za ujazo 61,000 kwa siku ili kukidhi mahitaji ya idadi ya watu waliongezeka kutokana na Serikali kuhamia Dodoma. Kwa sasa asilimia 80 ya wakazi wa Mjini Dododma wanapata maji yanayosambazwa na DUWASA.

**Mheshimiwa Spika,** mtandao wa majitaka uliopo ni kilomita 86 wakati mahitaji ni kilomita 250, na hivyo kupelekea huduma ya maji taka DUWASA kuhudumia **asilimia 20** tu ya wakazi wa Mji wa Dodoma mjini na hii pia ni kutokana na ukosefu wa mitambo midogo ya mabomba ya kukusanyia maji taka.

**Mheshimiwa Spika,** mitambo ya kukusanyia maji taka imeenea kikamilifu kwenye maeneo matatu ya mji ambayo ni Mlimwa *West* (*Area* C), Mlimwa *East* (*Area* D) na *Central Business Area*, kwa maeneo ambayo mtandao wa maji taka haujafika, wananchi wamekuwa wakitumia magali maalumu ya kunyonya maji taka ambapo huduma hiyo hutolewa na DUWASA, Manispaa na watu binafsi.

**Mheshimiwa Spika,** mfumo wa kukusanya na kutibu maji taka unaotumika mjini Dodoma ni wa mabwawa yaliyopo kilomita 60 kutoka mjini na una jumla ya mabwawa ma nne (4) yenye ukubwa mita 200x 200 na yanauwezo wa kuhudumia watu 68,000 tu. Kwa sasa mabwawa haya yamezidiwa kutokana na kuhudumia watu wanaozidi usanifu wake, DUWASA ina mpango wa kujenga mabwawa mengine ya kudumu katika eneo la Nzunguni na ipo katika hatua za kutafuta fedha za ujenzi wa mabwawa hayo.

**Mheshimiwa Spika,** DUWASA inakabiliwa na changamoto mbalimbali zifuatazo:-

- Taasisi za Serikali kutolipa ankara zake kwa wakati;
- Ufinyu wa mtandao wa kusambaza maji safi, ambapo zaidi ya kilomita 400 zinahitajika;
- Ufinyu wa mtandao wa kusambaza maji taka, ambapo zaidi ya kilomita 164 zinahitajika;

· Upotevu wa Maji unaofikia wastani wa asilimia 29;

· Kuziba mara kwa mara kwa mfumo wa maji taka kwa maeneo ya Area C na D kutokana na kuchakaa kwa mitambo ya maji taka iliyojengwa kwa zege miaka mingi iliyopita;

· Gharama kubwa za umeme wa kuzalisha, kusafirisha na kusambaza maji ambazo zinafikia wastani wa Shs. 485 milioni kwa mwezi;

· Kukatika kwa umeme mara kwa mara katika mitambo ya uzalishaji maji na hivyo kusababisha uzalishaji wa maji kupungua na

· Wizi wa maji unaofanywa na baadhi ya wateja wasio waaminifu hali inayosababisha upotevu wa maji.

**2.5.5 Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mwanza (MWAUWASA)**

**Mheshimiwa Spika,** huduma ya maji katika jiji la Mwanza (Ilemela na Nyamagana) pamoja na sehemu ya Mji wa Kisesa Wilayani Magu inatolewa na Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira jijini Mwanza (MWAUWASA).

**Mheshimiwa Spika,** chanzo cha maji yanayozalishwa ni Ziwa Victoria na mitandao ya uzalishaji maji ina uwezo wa kuzalisha mita za ujazo **108,000** sawa na **lita 108 milioni** kwa siku, kwa sasa Mamlaka inazalisha wastani wa **lita 85** milioni kwa siku ambayo huhudumia **asilimia 90** ya maeoneo yote ya mjini kati. Aidha, maeneo ya mjini yakichanganywa nay a pempezoni huduma ya maji inawafikia wananchi kwa **asilimia 70**. MWAUWASA ina ina jumla ya wateja 68,760 inayowahudumia na wote wamefungiwa dira za maji.

**Mheshimiwa Spika,** huduma ya uondoaji maji taka hufanyika kwa kutumia mtandao wa mabomba yenye jumla ya urefu wa kilomita 102, pamoja na mabwawa 13 ya kutibu majitaka yaliyoko Ilemela katika eneo la Bujuta. Jumla ya kaya 4,024 zimeunganishwa katika mfumo wa uondoaji maji taka. Aidha, kutokana na jiografia ya Jiji la Mwanza kuwa

na miinuko maji taka husafirishwa kwa kusukumwa kwa pampu ambazo zipo katika vituo vitatu vya Makongoro, Mwaloni – Kirumba na Mwanza South (Igogo).

**Mheshimiwa Spika,** mbali na mafanikio yaliyofikiwa, MWAUWASA inakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

- Gharama kubwa za umeme wa kuzalisha na kusambaza maji ambazo kwa sasa zimefikia Shilingi Milioni 560 kwa mwezi;
- Ukuaji wa Mji kwa kasi zaidi ya uwezo wa Mamlaka kujenga miradi ya maji katika maeneo ambayo yanaendelea kujengwa;
- Baadhi ya sehemu za jiji la Mwanza ni za miinuko hivyo wakazi waliojenga nyumba zao katika maeneo ya miinuko ya usawa wa mantenki ya maji huwa vigumu kwa wao kupata huduma;
- Kukosekana kwa mfumo wa uondoshaji maji taka katika maeneo ya mlimani na hivyo kusababisha baadhi ya wakazi wanaoishi maeneo hayo kuchimba vyoo vyenye vina vifupi na hivyo kuwa chanzo cha uchafuzi wa mazingira na Ziwa Victoria;
- Ufinyu wa mtandao wa maji taka ambao unahudumia asilimia 15 tu ya maeneo ya Jiji la Mwanza na
- Baadhi ya Taasisi za Serikali kutolopa madeni ya ankara za maji ambayo yamefikia zaidi ya shilingi bilioni 1.5.

### 2.5.6 Mradi wa Maji katika Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma Ujiji

**Mheshimiwa Spika,** Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma Ujiji ilipanga kutekeleza miradi mitatu ya Mradi wa Maji Kibirizi, Mradi wa Maji Kagera na Mradi wa Maji Mgumile chini ya programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini.

**Mheshimiwa Spika,** mradi wa maji wa Kagera haujaanza kutoa huduma kwa sababu bado haujaunganishwa na mtandao wa maji wa Mamlaka ya Maji safi na Usafi wa Mazingira Kigoma Ujiji (KUWASA) kutokana na Mamlaka kukosa fedha za kukamilisha ujenzi wa njia kuu

ya maji kwenda tenki ya Kagera yenye urefu wa kilomita 8.28 kutoka eneo la Mwanga. Matokeo ya mradi kutoanza kutoa huduma ni kuharibika kwa miundombinu iliyokamilika ujenzi kwa kuwa haitoi huduma kwa muda mrefu.

**Mheshimiwa Spika,** mradi wa maji wa Kibirizi ulianza ujenzi tarehe 28/01/2013 na ilipofika tarehe 28/11/2013 mkataba ulisitishwa na mradi kukabidhiwa Mamlaka ya Maji safi na Usafi wa Mazingira Kigoma Ujiji (KUWASA) hivyo kufanya mradi kutokamilika hadi leo kutokana na Mamlaka kukosa fedha za kuukamilisha.

**Mheshimiwa Spika,** mradi wa Maji Mgumile ulisainiwa mkataba na mkandarasi wa ujenzi tangu mwezi April, 2014 na kukubalika kuanza ujenzi tarehe 01/02/2017 na ulitegemewa kumalizika tarehe 30/07/2017 mara baada ya ujenzi kuanza ilibainika kuwepo kwa dosari katika usanifu na kulazimika kusimamisha kazi ili mapitio ya usanifu yafanyike upya na hivyo mradi kuchelewa kukamilika.

**Mheshimiwa Spika,** kufanyika upya kwa mradi kulipelekea kuongezeka kwa gharama za mradi ambazo zilihusisha fidia na ujenzi wa miundombinu. Aidha, wanufaika wa mradi kukataa chanzo cha maji kuwa kisima kirefu na badala yake walitaka chanzo cha maji kiwe Ziwa Tanganyika.

### 2.5.7 Mradi wa Maji Same-Mwanga – Korogwe

**Mheshimiwa Spika,** mradi wa maji Same- Mwanga-Korogwe ni miongoni mwa miradi mikubwa inayotekelezwa na Serikali kwa lengo la kuondoa kero za maji kwa wakazi wa Same, Mwanga, na Korogwe pamoja na vijiji 38 vilivyoko katika eneo la mradi. Mradi unatarajiwa kunufaisha jumla ya wananchi wapatao 438,931 katika Wilaya za Same (246,763), Mwanga (177,085) na Korogwe (15,053) na unatarajiwa kugharimu Dola za Marekani Milioni 300.

**Mheshimiwa Spika,** ujenzi wa mradi ulianza tarehe 1/06/2017 baada ya kufanyika kwa malipo ya awali, hata

hivyo kuchelewa kwa malipo kumesababisha ongezeko la gharama inayolipwa na Serikali kutokana na riba inayotozwa na wakandarasi kwa kucheleweshewa malipo yao pamoja na kuongezeka kwa gharama ya usimamizi wa mradi kutokana na ongezeko la muda wa ujenzi unaotolewa kufidia muda uliopotea kulingana na mkataba.

**Mheshimiwa Spika,** vilevile mradi unakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa fedha za utekelezaji wa kipande cha pili cha ujenzi wa miundombinu ya usambazaji wa maji katika vijiji 9 vya awamu ya kwanza na usambazaji wa maji kwenye vijiji 29 vilivyo kando kando ya bomba kuu na hivyo kupelekea kuchelewa kuanza kwa utekelezaji wa kipande cha tatu ambacho ni kiungo muhimu kati ya uzalishaji na usambazaji wa maji. Kuchelewa kuanza kwa kipande hiki kutaathiri muda wa majaribio ya mradi kwa kipande cha kwanza na cha nne vitakapokamilika, na hivyo kushindwa kutoa huduma ya maji kwa wakati unaotarajiwa na wnanchi.

### 2.5.8 Umuhimu wa Kuuwezesha Kifedha Mfuko wa Taifa wa Maji

**Mheshimiwa Spika,** Sheria ya fedha ya mwaka 2015 ilianzisha tozo ya shilingi hamsini (50) kwa kila lita ya mafuta ya diseli na petroli kama chanzo cha mapato ya Mfuko wa Taifa wa Maji. Kwa kufanya hivi kumewezesha upatikanaji wa fedha zaidi kwa ajili ya kugharamia miradi ya maji.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kutambua mchango wa Mfuko wa Taifa kutokana na maendeleo yaliyopatikana kwenye miradi ya maji, ili kufikia azma ya kuwapatia wananchi wengi zaidi maji safi na salama ifikapo mwaka 2021, Kamati iliona upo umuhimu wa kuuongezea uwezo Mfuko wa Taifa wa Maji, ndipo katika taarifa ya utekelezaji wa shughuli zake kwa mwaka 2016/2017 Kamati ilipendekeza na Bunge likaazimia marekebisho yafanyike wakati wa utungaji wa Sheria ya fedha ya mwaka 2017 kwa kuongeza tozo ya shilingi hamsini (50) kwa kila lita ya petrol na diseli

hadi kufikia shilingi mia moja (100) ili kutununisha Mfuko wa Taifa wa Maji.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inashangazwa na hatua ya Serikali kutotekeleza azimio hili la Bunge ambalo liliamuliwa na kukubaliwa na Wabunge ambao kimsingi ndio wawakilishi wa wananchi. Kamati inataka kufahamu sababu zinazopelekea Serikali kushindwa kutekeleza maamuzi ya Bunge.

**2.5.9 Muswada wa Sheria ya Huduma ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira wa Mwaka 2018.**

**Mheshimiwa Spika,** Muswada wa Sheria ya Huduma za Maji Safi na Usafi wa Mazingira wa Mwaka 2018 ulileta na Serikali Bungeni kwa nia ya Bunge kutunga sheria mpya ya Huduma za Maji Safi na Usafi wa Mazingira ya Mwaka 2019 ambayo itasimamia utoaji wa huduma za maji safi na usafi wa mazingira nchini kwa lengo la kuwa na Sheria moja itakayosimamia kikamilifu shughuli zote za utoaji wa huduma za maji safi na usafi wa mazingira katika ngazi mbalimbali nchini.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifanya kazi hiyo kwa umakini mkubwa na kushirikiana na wadau mbalimbali na hivyo kuliwezesha Bunge kutekeleza wajibu wake wa kutunga sheria ambapo tarehe 31/01/2019 Bunge lilikamilisha kazi ya utungaji wa sheria hii. Hatua inayosubiriwa ni ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Pombe Joseph Magufuli kusaini sheria hiyo ili ianze kutumika.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kutunga sheria hii kwani kwa kufanya hivyo kumedhihirisha dhamira ya Serikali ya kuharakisha upatikanaji wa huduma bora za maji safi na maji taka kwa wananchi wote.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mambo mengi ya msingi yalioainishwa katika sheria hii, Kamati inaitaka Serikali mara baada ya sheria hii kusainiwa kuharkisha kuanzishwa

kwa Wakala wa Maji Vijijini (*Rural Water Agency-RUWA*) ambao utasimamia miradi na utoaji na huduma za maji vijijini ikiwemo uchimbaji visima na ujenzi wa mabwawa na kutambuliwa na kuanzishwa kwa Mfuko wa Taifa wa Maji (*The National Water Fund*) ambao utakuwa na wajibu wa kutafuta fedha kwa ajili ya kusaidia uwekezaji katika miradi ya maji.

### 2.5.10 Maendeleo ya Utekelezaji wa Miradi ya Maji katika Miji 28 kwa fedha za mkopo wa masharti nafuu kutoka Serikali ya India

**Mheshimiwa Spika,** mradi wa kuboresha upatikanaji wa maji safi katika miji 28 ya Muheza, HTM- Korogwe, Makonde (Mtwara), Pangani, Ifakara, Kilwa Masoko, Wanging'ombe, Makambako, Nanyumbu, Njombe, Songea, Chunya, Rujewa, Mafinga, Manyoni, Sikonge, Singida, Kiomboi, Mpanda, Chamwino, Chemba, Urambo/ Kaliua, Mugumu (Serengeti), Geita, Kayanga, Tarime, Chato na Kasulu. Fedha hizi pia zinahusisha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambao wana mji mmoja na mchakato wa kumpata wa kupata wataalam washauri na wakandarasiunafanywa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yenyewe.

**Mheshimiwa Spika,** miji hii ilichaguliwa kutokana na changamoto kubwa ya maji inayoyakabili maeneo hayo na hakuna miradi mikubwa ya maji inayoendelea katika maeneo hayo. Hata hivyo miji mingine itaendelea kufikiwa kwa kadri ya upatikanaji wa fedha na hatimae kufikia miji yote nchini.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

**Mheshimiwa Spika,** sehemu hii inahusu maoni na mapendekezo ya Kamati na imegawanyika katika sehemu mbili. Sehemu ya kwanza inahusu maoni ya jumla na sehemu ya pili inahusu maoni maalum kwa kila kazi iliyotekelezwa na Kamati.

### 3.1 *Maoni ya Jumla*

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inapenda kutoa ushauri wa jumla wenye nia ya kuitaka Serikali kutekeleza ipasavyo ushauri unaotolewa Bungeni. Yapo maswala yanayoshauriwa mara kwa mara lakini hayatekelezwi. Mfano wa maswala hayo ni:-

(a) Ucheleweshaji katika kutoa fedha za miradi ya maendeleo kama zilivyoidhinishwa na Bunge kwa sekta za Kilimo, Mifugo, Uvuvi na Maji.

(b) Serikali kuendelea kutenga bajeti ndogo na isiyokidhi mahitaji ya kuendeleza sekta za Kilimo, Mifugo, Uvuvi na Maji na hivyo kukwamisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara zinazosimamia sekta hizi.

(c) Serikali kuanisha miradi mipya ya Kilimo, Mifugo, Uvuvi na Maji kabla ya kukamilika kwa miradi ya zamani.

(d) Serikali kutotekeleza mkataba wa Maputo na Malabo 2014 ambao Tanzania imeridhia kwa kutenga na kuhakikisha bajeti ya Wizara ya Kilimo inakuwa zaidi ya 10% ya bajeti yote na inatolewa kwa wakati ili ikatekeleze program mbalimbali za kilimo na

(e) Kuongeza tozo ya shilingi 50 kwa kila lita ya mafuta ya diseli na petrol kama chanzo cha Mfuko wa Taifa wa Maji.

(f) Serikali kushindwa kutenga asilimia 1% ya GDP ya Taifa kwa ajili ya utafiti.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo, naomba sasa niwasilishe maoni na mapendekezo kumi na tisa ya Kamati yaliyotokana na shughuli zilizotekelezwa na Kamati kwa kipindi cha mwaka mmoja, kama ifuatavyo:-

#### 3.1.1 Tume ya Maendeleo ya Ushirika

**Kwa kuwa** Tume ya Maendeleo ya Ushirika ina wajibu wa kuvijengea uwezo na kuvisimamia vyama vya ushirika

vya kilimo na masoko ili viweze kujiendesha kwa ufanisi na kuwasaidia wakulima kuongeza kipato na kuimarisha kilimo,

**Na kwa kuwa**, Tume ya Maendeleo ya Ushirika inakabiliwa na upungufu wa Watumishi **1,272** na kupelekea Tume kushindwa kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

**Hivyo basi**, Kamati inapendekeza kwamba, Serikali iipatie Tume ya Ushirika watumishi wanaohitajika ili Tume iweze kusimamia utendaji wa vyama vya ushirika vya kilimo na masoko.

### 3.1.2 Umuhimu wa kuongeza mnyororo wa thamani kwa mazao yenye fursa katika kuchangia malighafi ya Viwanda

**Kwa kuwa** azma ya Serikali ni kujenga uchumi wa viwanda kwa kufungamanisha shughuli za kilimo, ufugaji na uvuvi ili kuchochea mageuzi ya kiuchumi na maendeleo ya watu,

**Na kwa kuwa** sekta za kilimo, mifugo na uvuvi ni moja ya sekta zinazotoa malighafi nyingi kwa ajili ya viwanda huku wananchi wanaojishughulisha na sekta hizo wanakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa rasilimali fedha.

**Hivyo Basi,** Kamati inapendekeza Bunge liazimie kwamba, Serikali iweke mazingira wezeshi yatakayozitaka Taasisi za Fedha kuwakopesha Wakulima, Wafugaji na Wavuvi mikopo yenye riba nafuu ili wakulima, wafugaji na wavuvi waweze kuendesha shughuli zao kwa kutumia zana bora na za kisasa.

### 3.1.3 Mfumo wa Ununuzi wa Mbolea kwa Pamoja

**Kwa kuwa,** Mfumo wa Ununuzi wa Mbolea kwa Pamoja ulianzishwa kwa lengo la kuhakikisha matumizi ya mbolea yanaongezeka, mbolea inapatikana kwa wakati na kwa bei nafuu,

**Na kwa kuwa** Serikali imefanikiwa kudhibiti bei ya mbolea kupitia utaratibu wa bei elekezi na kusababisha mawakala wa kusambaza mbolea kupungua na hivyo kupelekea mbolea nyingi kuishia mijini na kutofika vijijini kwa wakati.

**Hivyo basi,** Kamati inapendekeza Bunge liazimie kwamba, Serikali isitoe leseni kwa wasambazaji wakubwa ambao hawana matawi ya usambazaji kwa kila kanda. Aidha, watakiwe kufungua ofisi vijijini ili kuwezesha upatikanaji wa mbolea kwa wakati kulingana na misimu tofauti ya kilimo na kulingana na eneo husika.

### 3.1.4 Ujenzi wa viwanda vya mbolea nchini

**Kwa kuwa** mbolea nyingi inayotumika nchini huagizwa kutoka nje ya nchi kwa utaratibu wa ununuzi wa mbolea kwa pamoja. Utaratibu huu sio suluhisho la kudumu la kukidhi mahitaji ya mbolea nchini.

**Na kwa kuwa** Tanzania ina kiwanda kimoja tu cha Minjingu kinachotengeneza mbolea za kupandia na kukuzia na hakijaweza kukidhi mahitaji halisi ya mbolea hapa nchini.

**Hivyo basi,** Kamati inapendekeza Bunge liazimie Serikali ikamilishe mapema iwezekanavyo mazungumzo yanayoendelea ya ujenzi wa viwanda vya mbolea kati ya kampuni ya mbolea ya OCP- Morocco, kampuni ya mbolea kutoka Misri na muunganiko wa kampuni za Ferostaal, Haldo topsoe na Fauji ili kuwezesha kuanza kwa ujenzi wa viwanda vya mbolea.

### 3.1.5 Changamoto za zao la korosho

**Kwa kuwa** Serikali ilianzisha operesheni korosho kwa ajili ya kubangua na kununua korosho za wakulima kwa bei yenye tija ili kuwasaidia wakulima wa korosho kunufaika na jasho lao baada ya bei ya minadani kushuka hivyo kuwanusuru kwa hasara ambayo wangeipata kwa msimu huu,

**Na kwa kuwa,** operesheni korosho inakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo kuchelewa kwa malipo ya wakulima, uwezo mdogo wa viwanda vya ndani kubangua korosho iliyovunwa, uwezo mdogo wa ghala kuu la kuhifadhi korosho, kuchelewa kulipwa kwa malipo ya Halmashauri, kuchelewa kufanyika kwa malipo ya vyama vya msingi, kushuka kwa mapato ya fedha za kigeni na kukosekana kwa Bodi ya Korosha Tanzania na hivyo kupelekea ugumu wa utekelezaji wa operesheni nzima.

**Hivyo basi,** Kamati inapendekeza Bunge liazimie Selikali itekeleze yafuatayo:-

**Moja,** Bodi ya Korosho iteuliwe mapema iwezekanavyo ili itekeleze majukumu yake badala ya majukumu hayo kutekelezwa na Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko ambayo ina majukumu yake ya msingi.

**Mbili,** Ili kudhibiti mazingira ya rushwa kutokana na kuchelewa kwa zoezi la uhakiki kwa malipo ya wakulima ni vyema uhakiki ukakamilika mapema iwezekanavyo.

**Tatu,** Ulipaji wa fedha za korosho kwa wakulima uende sambamba na malipo ya ushuru wa Halmashauri ili kuziongezea Halmashauri uwezo wa mapato ya ndani kwa ajili ya kuendesha shughuli zao za kila siku zilizosimama.

**Nne,** Kwa mipango ya muda mfupi na muda mrefu Serikali ihamasishe ujenzi wa viwanda vya kubangua korosho pamoja na kujenga maghala ya kutosha kuhifadhia korosho.

**Tano,** Kwa misimu ijayo ya korosho minada ya korosho ifunguliwe mapema kwenye maeneo ambayo korosho inawahi kukomaa ili kudhibiti walanguzi wa korosho maarufu kama kangomba.

**Sita,** zoezi la uhakiki lifanyike kwa uwazi kwa kushirikisha wakulima wenyewe au wawakilishi kutoka kwenye vyama vyao vya ushirika wa masoko na

**Saba,** Serikali iandae mkakati wa muda mrefu utakaoshughulikia changamoto za masoko kwa mazao yote.

### 3.1.6 Changamoto ya Upanuzi wa Viwanda vya Sukari

**Kwa kuwa** Serikali ilikuwa na nia njema ya kulinda wazalishaji wa ndani wa sukari na kuamua vibali vya uagizaji wa sukari vitolewe kwa wenye viwanda vya sukari ili kufidia naksi ya sukari (*gap sugar*) wanayozalisha,

**Na kwa kuwa,** wazalishaji wa sukari ni wafanya biashara na lengo la biashara yoyote ni kupata faida na kwa vile uagizaji wa sukari kutoka nje ya nchi unafaida kubwa kuliko uzalishaji wa sukari unaofanywa na wazalishaji na hivyo kuzoretesha juhudi za kupanua viwanda kutokana na gharama kubwa za uwekezaji.

**Hivyo basi,** Kamati inapendekeza Serikali ifanye yafuatayo:-

**Moja,** Serikali kwa wataalamu wake ifanye tathimini ya mwenendo wa kuagiza sukari nje ya nchi kupitia wenye viwanda vya kuzalisha sukari ili kubaini namna bora zaidi ya kuagiza sukari nje ya nchi wakati mipango ya upanuzi wa viwanda vya kuzalisha sukari ikifanyika kwa haraka.

**Mbili,** wakati mipango ya upanuzi wa viwanda vya sukari ikiendelea, Kamati inapendekeza Serikali iangalie uwezekano wa kutumi mfumo wa ununuzi wa sukari kwa pamoja (*Bulk Procurement*).

### 3.1.7 Umuhimu wa Utafiti katika Maendeleo ya Kilimo cha Miwa

**Kwa kuwa** matokeo ya tafiti ni muhimu katika kuboresha uzalishaji wa miwa na hivyo kuhakikisha upatikanaji wa malighafi ya viwanda vya sukari.

**Na kwa kuwa** wazalishaji wa miwa wanatambua umuhimu wa utafiti na wamekuwa wakichangia kila mwaka gharama za utafiti kwa kuzipatia fedha nyingi taasisi za Serikali zinazofanya utafiti wa miwa ili kuwezesha tafiti za miwa na sukari zifanyike kwa lengo la kuboresha upatikanaji wa mallighafi za viwanda vya sukari nchini. Hata hivyo, hakuna maelezo ya kuridhisha kuhusu matumizi ya pesa zilizotolewa kwa ajili ya utafiti wa miwa unafanyika.

**Hivyo basi,** Kamati inapendekeza Bunge liazimie na kuitaka Selikali kutekeleza yafuatayo:-

**Moja,** kuwasilisha Taarifa Bungeni inayoelezea matumizi ya fedha kiasi cha shilingi **bilioni 4,688,885,111.36** zilizotolewa na wazalishaji wa sukari kwa kipindi cha miaka mitano kwa ajili ya utafiti wa miwa na sukari.

**Mbili,** kama Taasisi za Serikali zinazopewa pesa kwa ajili ya kufanya utafiti wa miwa na sukari zimeshindwa kufanya kazi hiyo kwa ufanisi, basi ziache wazalishaji wa miwa wafanye wenyewe utafiti kwa ajili ya maendeleo ya viwanda vyao.

### 3.1.8 Changamoto za zao la pareto

**Kwa kuwa** Tanzania ni nchi ya pili kwa ulimaji wa zao la pareto ulimwenguni na ina ardhi nzuri na upatikanaji wa hali ya hewa nzuri inayofaa kwa kilimo.

**Na kwa kuwa** mahitaji ya pareto duniani yanongezeka na kufanya bei ya pareto kupanda kila msimu na hivyo kunufaisha wakulima wa pareto na kuongeza mapato ya Serikali.

**Hivyo basi,** Kamati inapendekeza Bunge liazimie Serikali iandae mkakati wa makusudi wa kuwezesha kilimo cha pareto kufanyika kwa ufanisi ikiwa ni pamoja na kuweka mazingira wezeshi ya kusaidia wazalishaji wa pareto na kuhamasisha sekta binafsi kushiriki kikamilifu kwenye zao la pareto.

### 3.1.9 Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko

**Kwa kuwa,** Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko ilianzishwa ili kutatua changamoto ya ukosefu wa masoko ya uhakika kwa mazao ya wakulima hususan mazao ya nafaka na mazao mchanganyiko ambayo jumla yake yako mazao 32,

**Na kwa kuwa,** Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko ndio mteja mkubwa wa wakulima kwa mazao ya nafaka na mazao mchanganyiko, hivyo Bodi inahitaji kuwa na pesa za kununua mazao wakati wa kipindi cha msimu wa mavuno ili kuwahakikisha wakulima soko la uhakika, hata hivyo Bodi hii imekuwa inapata pesa kidogo zisizokidhi mahitaji tena kwa kuchelewa.

**Hivyo basi,** Kamati inapendekeza kwamba Selikali

**Moja,** Kuipelekea pesa za kutosha na kwa wakati Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko.

**Mbili,** Kuisaidia Bodi ya Nafaka na Mazao mchanganyiko kupata mikopo yenye riba na masharti nafuu.

**Tatu,** Bodi inunue mazao ya aina zote na kutafuta masoko kama ilivyoainishwa kwenye sheria iliyoanzisha Bodi hii na

**Nne,** Serikali iipatie Bodi Watumishi wa kutosha na vifaa vya kufanyia kazi ili Bodi iweze kutekeleza malengo yake kwa ufanisi.

### 3.1.10 Changamoto za Tume ya Taifa ya Umwagiliaji

**Kwa kuwa** Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imehamia Wizara ya Kilimo kwa lengo la kutekeleza vyema kilimo cha umwagiliaji na miradi iliyoshindwa kukamilika kwa muda mrefu wakati Tume hii ilipokuwa Wizara ya Maji**,**

**Na kwa kuwa** wapo watendaji wa Tume ya Umwagiliaji waliokwamisha utekelezaji wa miradi hii.

**Hivyo basi, Kamati** inapendekeza Bunge liazimie kuitaka Selikali

**Moja,** kufanya uchunguzi wa kina ili kubaini ubadhirifu wa fedha za miradi ya kilimo cha umwagiliaji na endapo itabainika kuna matumizi mabaya ya fedha za miradi hatua za kisheria zichukuliwe dhidi ya watendaji waliohusika.

**Mbili,** kuharakisha ukamirishaji wa ujenzi wa miradi ya maendeleo ambayo haijakamilika kabla ya kuanza miradi mipya na

**Tatu,** ihakikishe inawashirikisha wakulima katika skimu za umwagiliaji pamoja na kuimarisha vyama vya wamwagiliaji (*Irrigators Associations*) ili kuwezesha miradi ya umwagiliaji kuwa endelevu.

### 3.1.11 Changamoto zinazoyakabili mashamba ya malisho

**Kwa kuwa** mabadiliko ya tabianchi yana athari kwa mazingira na kupelekea uhaba wa malisho na hivyo upungufu katika uzalishaji wa mazao ya mifugo ikiwemo nyama, maziwa na ngozi na kusababisha mazao ya mifugo kukosa mfumo sahihi wa kuunganisha mazao haya na viwanda.

**Na kwa kuwa** Serikali ilianzisha mashamba ya kuzalisha mbegu za malisho ya mifugo kwa madhumuni ya kuzalisha mbegu bora hata hivyo mashamba ya malisho yanakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo miundombinu ya maji kwa ajili ya kuwezesha kilimo cha umwagiliaji badala ya kutegemea mvua zilizoathiriwa na mabadiliko ya tabianchi kwa ajili ya kuzalisha malisho.

**Hivyo basi,** Kamati inapendekeza Bunge liazimie kuitaka Serikali kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya kujenga na kuendesha miundombinu ya umwagiliaji.

**3.1.12 Changamoto zinazoikabili Kampuni ya Ranchi za Taifa**

**Kwa kuwa** Kampuni ya Ranchi za Taifa ilianzishwa kwa lengo la kuendeleza na kueneza ufugaji bora kwa kutumia mbinu za kisasa kwa ajili ya soko la ndani na nje ya nchi.

**Na kwa kuwa,** kampuni hii ina rachi nane zenye uwezo wa kuweka na kuendeleza ng'ombe kati ya **80,000-90,000**, hata hivyo inakadiriwa ranchi zote zina ng'ombe 12,681 tu ambayo ni sawa na **asilimia 15**. Idadi ndogo ya ng'ombe walioko kwenye Ranchi za Taifa ukilinganisha na uwezo wa ranchi hizo. Hali hii inadhihirisha kuwa hakuna uwekezaji wa kutosha kutokana na ukosefu wa fedha na mikataba mibovu iliyofungwa baina ya kampuni na wawekezaji wa vitalu.

**Hivyo basi,** Kamati inapendekeza Bunge liazimie Selikali itekeleze yafuatayo:-

**Moja,** Ibadilishe mapema iwezekanavyo umiliki wa hisa kutoka umiliki wa watu binafsi na kwenda kwenye umiliki wa Serikali kisheria.

**Mbili,** Kupitia upya mikataba yote iliyofungwa baina ya NARCO na wawekezaji wa vitalu ili kuwa na mikataba yenye tija kwa kampuni.

**Tatu,** Wizara iweke utaratibu wa kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa mikataba ya vitalu na ikibainika wamiliki wa vitalu waliovunja makubaliano kwa mujibu wa mikataba mikataba yao ivunjwe na

**Nne,** Serikali itenga fedha za kutosha kwa ajili ya kuendeleza uendeshaji wa Rachi za Taifa.

### 3.1.13 Changamoto zinazoikabili Tasnia ya Maziwa

**Kwa kuwa** mwaka 2012 Serikali iliondoa kodi ya VAT kwenye bidhaa za maziwa na bidhaa zitokanazo na maziwa yanayopatikana hapa nchini ikiwa ni juhudi za kutengeneza mazingira mazuri ya uwekezaji wa ndani kwenye eneo la uzalishaji na usindikaji na hivyo kuvutia wawekezaji na kuongezeka kwa viwanda vipya vya kusindika maziwa nchini na hivyo kuongezeka kwa usindikaji wa maziwa kutoka lita 112,500 mwaka 2012 hadi 167,070 mwaka 2015.

**Na kwa kuwa,** mwaka 2014 Serikali ilifanya marekebisho kwenye Sheria ya VAT na kufuta msamaha wa VAT sifuri. Uamuzi ambao ulianza kutekelezwa Julai 2015 umeathiri tasnia ya maziwa kutokana na ukweli kwamba gharama za undeshaji zimeongezeka na kukatisha tamaa wawekezaji wa ndani na nje walioonyesha nia ya kuwekeza zaidi.

**Hivyo basi,** Kamati inapendekeza Bunge liazimie Serikali itekeleze yafuatayo:-

**Moja,** Maziwa na bidhaa zitokanazo na maziwa ziondolewe VAT na ziwe *Zero Rated* ili kumuwezesha msindikaji wa maziwa kuongeza usindikaji, kukua na kuongeza ajira pamoja na kuongeza Pato la Taifa na kuweza kuhimili ushindani wa bidhaa za kutoka nje ambazo zinaongezeka kila mwaka na hasa kutoka nchi za Afrika Mashariki ambazo hupata ruzuku kutoka Serikalini.

**Mbili,** kuweka upendeleo maalum wa viwango vya kodi ili kuhamasisha na kuvutia wawekezaji.

**Tatu,** Serikali ifanye tathimini na kupitia upya gharama kubwa za usindikaji zinazochangiwa na uwepo wa tozo nyingi za Mamlaka zinazosimamia sekta ya maziwa na

**Nne,** Serikali kupitia taasisi zake ihakikishe inaweka mazingira ya kulinda soko la ndani dhidi ya bidhaa toka nje

zisizokuwa na ubora, zisizosajiliwa na zisizolipiwa kodi na tozo stahiki ili kuleta ushindani wenye usawa (*Fair competition*).

### 3.1.14 Changamoto zinazoikabili tasnia ya ngozi

**Kwa kuwa** Tanzania ina uwezo mkubwa wa kuzalisha ngozi kutokana na uwepo wa idadi kubwa ya mifugo.

**Na kwa kuwa** ngozi zinazokusanywa ni nusu tu ya ngozi zilizotakiwa kuzalishwa kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo ufugaji duni, machinjio yasiyokidhi viwango, kukosekana kwa wataalamu wabobezi kwenye sekta ya ngozi, utoroswaji ngozi na kukosekana kwa wawekezaji kwa ajili ya viwanda vya kusindika ngozi.

**Hivyo basi,** Kamati inapendekeza Bunge liazimie Selikali itekeleze yafuatayo:-

**Moja,** kushirikiana na sekta binafsi kukamilisha mapema iwezekanavyo upanuzi wa kiwanda cha ngozi cha Karanga.

**Mbili,** kuhamasisha vyombo vya ulinzi na usalama, shule na taasisi zingine za aina hiyo kutumia viatu vitokanavyo na ngozi zinazozalishwa nchini.

**Tatu,** kusomesha wataalamu watakaobobea kwenye sekta ya ngozi ili kuwa na wabunifu watakaotengeneza bidhaa za ngozi.

**Nne,** kuboresha machinjio ili yawe ya kisasa na hivyo kuwezesha uchunaji ngozi kisasa unaotoa ngozi bora na

**Tano,** Serikali iimarishe ulinzi mipakani ili kudhibiti mianya ya utoroshaji ngozi.

### 3.1.15 Changamoto za Ukuzaji Viumbe kwenye Maji

**Kwa kuwa** mahitaji ya samaki duniani yanaongezeka kutokana na umuhimu wa samaki na mafuta yake katika

mwili wa binadamu huku uvuvi katika maji ya asili unazidi kupungua siku hadi siku,

**Na kwa kuwa** ukuzaji viumbe kwenye maji ndio njia mbadala ya kuziba pengo la mahitaji makubwa ya samaki na mazao yake na hivyo kuzalisha samaki kwa njia endelevu na hivyo kuongeza kipato na ajira kwa wazalishaji binafsi na Taifa kwa ujumla. Umuhimu huu ulipeleka Serikali kuongeza kodi kwa waagizaji wa samaki kutoka nje ili kuongeza ufugaji wa samaki kwenye mabwawa na vizimba. Hata hivyo, uamuzi huu wa kuongeza kodi ya uagizaji samaki (*Import Loyality*) umewavunja moyo wafanyabiashara waagizaji samaki na hivyo kuikosesha Serikali mapato.

**Hivyo basi,** Kamati inapendekeza Bunge liazimie Selikali itekeleze yafuatayo:-

**Moja,** kupunguza kodi ya ushuru iliyopandishwa zaidi ya mara tatu kwa waagizaji samaki kutoka nje ili kuvutia wafanyabiashara kuendelea kuagiza samaki.

**Mbili,** kuanzisha Mfuko wa maendeleo wa ukuzaji viumbe kwenye maji ili mapato ya kodi yatakayopatikana kutokana na kuagiza samaki kutoka nje yaingizwe kwenye mfuko huu kwa ajili ya kusaidia kukuza tasnia ya ukuzaji viumbe kwenye maji na

**Tatu,** kuhamasisha wananchi kwa kutoa elimu kuhusu umuhimu wa ukuzaji viumbe kwenye maji pamoja na kuandaa mazingira wezeshi kwa wafugaji kukopesheka na upatikanaji wa vifaa, zana na bembejeo zinazotumika kufuga viumbe kwenye maji.

### 3.1.16 Shirika la Uvuvi Tanzania na Umuhimu wake katika Uvuvi wa Bahari Kuu

**Kwa kuwa** nchi yetu imekuwa hainufaiki ipasavyo na mazao ya samaki kutoka kwenye Ukanda wa Uchumi wa Bahari katika eneo la Tanzania kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo kukosekana kwa Shirika la Uvuvi Tanzania.

**Na kwa kuwa** Serikali imedhamiria kufufua Shirika la Uvuvi Tanzania ambalo pamoja na majukumu mengine litawezesha Serikali kuna na meli zake yenyewe kwa ajili ya kuvua kibiashara kwenye eneo la Bahari Kuu.

**Hivyo basi,** Kamati inapendekeza Bunge liazimie na kuitaka Serikali kurahakisha zoezi la ufufuaji wa Shirika hili ili malengo ya Serikali kunufaika na rasilimali za Bahari Kuu yaweze kufikiwa kwa wakati.

### 3.1.17 Changamoto za utekelezaji wa Operesheni Sangara, 2018

**Kwa kuwa** Operesheni Sangara 2018 ilifanikiwa kudhibiti usafirishaji na uchakataji wa biashara ya samaki wachanga, kuongeza maduhuli ya Serikali, kudhibiti zana za uvuvi haramu zilizoko madukani na kuwatambua wamiliki wa viwanda vinavozalisha zana haramu za uvuvi.

**Na kwa kuwa** operesheni hii ni miongoni mwa operesheni za Serikali zilizopata malalamiko mengi kutoka kwenye jamii.

**Hivyo basi,** Kamati inapendekeza Bunge liazimie na kuitaka Serikali kutekeleza yafuatayo:-

**Moja,** kubainisha na kujifunza kasoro zilizojitokeza wakati wa kutekeleza Operesheni Sangara 2018 ili dosari zilizobainika zisitokee tena.

**Mbili,** kuharakisha mapitio ya Sheria ya Uvuvi ya mwaka 2003 na Kanuni zake za mwaka 2009 ili kubaini mapungufu ya kisheria yanakwamisha ufanisi wa sekta ya uvuvi.

**Tatu,** Kufanya doria za mara kwa mara kwenye viwanda vya kuzalisha zana za uvuvi na kwenye mialo ya uvuvi ili kubaini watengenezaji na watumiaji wa zana za uvuvi haramu na kuwafikisha kwenye vyombo vya kisheria na

**Tano,** kujiridhisha na taratibu zote za kisheria na kikanuni kabla ya kutoa vibali vya kusafirisha mazao na zana za uvuvi.

### 3.1.18 Changamoto zinazozikabili Mamlaka za Maji Mijini

**Kwa kuwa** Sera ya maji inaelekeza kujenga, kukarabati na kupanua miundombinu ya maji safi na usafi wa maji taka ili kuweza kutoa huduma endelevu kwa wakazi waishio mijini na pembezoni mwa miji,

**Na kwa kuwa** Mamlaka mbalimbali za maji zimeonyesha ufanisi na uwezo wa kujiendesha na kuwapatia wananchi huduma bora za maji safi, hata hivyo Mamlaka karibu zote zinakabiliwa na changamoto zinazofana.

**Hivyo basi,** Kamati inapendekeza Bunge liazimie na kuitaka Serikali itekeleze yafuatayo:-

**Moja,** kuwa na Mpango wa nchi nzima utakaowezesha kuwa na mfumo wa maji taka.

**Mbili,** Serikali na Taasisi zake kulipa madeni makubwa ya ankara za maji inazodaiwa na Mamlaka za maji ili Mamlaka hizi ziweze kujiendesha kwa ufanisi na kuwapatia wananchi huduma bora za maji safi na maji taka.

**Tatu,** kulinda vyanzo vya maji na uvamizi wa wananchi wanaofanya shughuli mbalimbali za kijamii na hivyo kuhatarisha vyanzo vya maji vilivyopo.

**Nne,** kushughulikia changamoto ya gharama kubwa za umeme wa kuzalisha, kusafirisha na kusambaza maji ambazo zinaongeza mzigo kwa wananchi na

**Tano,** kudhibiti mianya yote inayopelekea upotevu wa maji.

### 3.1.19 Maendeleo ya Mradi wa Maji katika Miji 28

**Kwa kuwa** fedha za mradi wa maji katika Miji 28 imeshapatikana,

**Na kwa kuwa** mradi huu ni wa fedha nyingi na sasa hatua iliyofikiwa ni mchakato wa kupata wataalamu washauri na badae wakandarasi.

**Hivyo basi,** Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha wakandarasi wanaopatikana wawe na sifa stahiki ili waweza kukamilisha miradi hiyo kwa wakati na hatimae huduma ya maji safi iweze kuwafikia wananchi wa maeneo hayo na kumaliza tatizo la upatikanaji wa maji safi na salama kama inavyotarajiwa na Serikali.

## 4.0 HITIMISHO

### 4.1 Shukrani

**Mheshimiwa Spika,** napenda kutumia fursa hii kukushukuru wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge, kwa uongozi wenu uliotukuka. Kupitia uongozi wenu na maelekezo ya mara kwa mara mnayoyatoa yamewezesha utekelezaji wa shughuli za Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** kwa umuhimu mkubwa napenda kuishukuru Serikali na kutambua mchango mkubwa uliotolewa na Watendaji wa Wizara zinazosimamiwa na Kamati, utaalamu na ushirikiano wao umeiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

**Mheshimiwa Spika**, napenda pia kuwashukuru wadau wote wa sekta za Kilimo, Mifugo, Uvuvi na Maji ambao kwa namna moja au nyingine walishirikiana na Kamati wakati wa uchambuzi wa Muswada, kutoa semina

na mafunzo kwa lengo la kuongeza uelewa na hata wa uchambuzi wa Bajeti.

Mheshimiwa Spika, **k**wa dhati kabisa napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano na michango yao waliyoitoa wakati wa utekelezaji wa majukumu ya Kamati. Aidha, nawapongeza kwa kushiriki kikamilifu katika kuboresha mijadala, maoni na mapendekezo ya Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii. Naomba kuwatambua kwa kuwataja majina yao kama ifuatavyo:-

| | |
|---|---|
| 1. Mhe. Mahmoud Hassan Mgimwa , Mb | Mwenyekiti |
| 2. Mhe. Dkt. Christine G.Ishengoma, Mb | M/Mwenyekiti |
| 3. Mhe. Emmanuel Papian John, Mb | Mjumbe |
| 4. Mhe.Eng. Edwin A. Ngonyani , Mb | Mjumbe |
| 5. Mhe. Justine Joseph Monko, Mb | Mjumbe |
| 6. Mhe. Deo Kasenyenda Sanga , Mb | Mjumbe |
| 7. Mhe. Katani Ahmad Katani, Mb | Mjumbe |
| 8. Mhe. Khadija Hassan Aboud, Mb | Mjumbe |
| 9. Mhe. Kunti Yusuph Majala, Mb | Mjumbe |
| 10. Mhe. Haroon Mullah Pirmohamed, Mb | Mjumbe |
| 11. Mhe. Ritta Enespher Kabati, Mb | Mjumbe |
| 12. Mhe. Lucy Saimon Magereli , Mb | Mjumbe |
| 13. Mhe. Prof. Sospeter M. Muhongo, Mb | Mjumbe |
| 14. Mhe. Dkt. Mary Michael Nagu, Mb | Mjumbe |
| 15. Mhe. Omar Abdallah Kigoda, Mb | Mjumbe |
| 16. Mhe. Anna Richard Lupembe, Mb | Mjumbe |
| 17. Mhe. Devotha Mathew Minja, Mb | Mjumbe |
| 18. Mhe. Pascal Yohana Haonga, Mb | Mjumbe |
| 19. Mhe. Haji Khatibu Khai, Mb | Mjumbe |
| 20. Mhe. Sikudhani Yasin Chikambo, Mb | Mjumbe |
| 21. Mhe. Mbaraka Salim Bawazir, Mb | Mjumbe |
| 22. Mhe. Juma Ali Juma, Mb | Mjumbe |
| 23. Mhe. Anthony Calist Komu, Mb | Mjumbe |
| 24. Mhe. Haji Ameir Haji, Mb | Mjumbe |
| 25. Mhe. Mattar Alli Salum, Mb | Mjumbe |
| 26. Mhe. Jitu Vrajial Soni, Mb | Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika,** mwisho napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Stephen Kagaigai kwa ushirikiano wake na kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Aidha, naishukuru Idara ya Kamati za Bunge chini ya uongozi wa Mkurugenzi wa Kamati za Bunge Ndugu Athuman Hussein akisaidiana na Ndugu Msigwe D. Bisile.

**Mheshimiwa Spika,** kipekee napenda kuishukuru Sekreterieti ya Kamati ambao ni Ndugu Rachel Nyega, Ndugu Martha Chassama, Ndugu Virgil Mtui na Ndugu Mwimbe John kwa kuihudumia Kamati pamoja na kukamilisha taarifa hii kwa wakati. Mwisho lakini sio kwa umuhimu nawashukuru watumishi wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuliwezesha Bunge kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

### 4.2 Hoja

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lipokee, lijadili na liadhimie Serikali ikatekeleze maoni na mapendekezo yaliyowasilishwa kwenye taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

Mahmoud Hassan Mgimwa, (Mb)
**MWENYEKITI,**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO,**
**MIFUGO NA MAJI**
5 FEBRUARI, 2019

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji, umetoa hoja na imeungwa mkono. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaanza uchangiaji, mchangiaji wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Selemani Bungara kwa dakika tano.

**MHE. SULEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Spika, dakika tano ni kidogo sana. Kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi hii, nitaongelea mambo mawili tu kuhusu uvuvi na kilimo.

Mheshimwa Spika, Wilaya ya Kilwa ni wavuvi wakubwa wa daga, hususan dagaa mchele na dagaa lumbunga. Kwa kipindi kifupi tumepata mtafaruku mkubwa tulipoingiliwa na operesheni, ikiongozwa na Wanajeshi na kuambiwa kwamba uvuvi tunaotumia ni uvuvi haramu na nyavu tunazotumia ni nyavu ambazo hazitakiwi kuvulia.

Mheshimiwa Spika, wavuvi hao walikuwa na leseni na nyavu zao zilikuwa zinakaguliwa tangu mwaka 2009 mpaka leo. Cha kusikitisha sana nyavu hizo zimeambiwa zisivue. Katika ukurasa wa 37 wa kitabu hiki, wanasema unaweza kumtambua mvuvi anayeshughulika na uvuvi haramu ikiwa mvuvi huyo atatekeleza shughuli zake za uvuvi bila kuwa na leseni. Kwa hiyo, mvuvi haramu ni yule ambaye anavua bila kuwa na leseni lakini wavuvi wetu waliokamatwa waliokuwa na leseni wanaambiwa wavuvi haramu.

Mheshimiwa Spika, naomba jambo hili liangaliwe upya na wale wavuvi waruhusiwe kuvua na nyavu zile kwa sababu leseni wanazo na nyavu zao zilikaguliwa. Hata kama sheria zinasema zile nyavu ni haramu, lakini wananchi walinunua zile nyavu wakapewa leseni. Siyo chini ya wavuvi 3,000 katika Wilaya yangu ya Kilwa wameambia wasivue kuanzia sasa wakati leseni wanazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana kwamba pengine zile nyavu ni haramu, lakini leseni wanazo na waliotoa ni Serikali. Naiomba Serikali itumie hekima ili wale wavuvi waendelee kuvua kwa nyavu zile mpaka hiyo sheria itakaporekebishwa. Kwa sababu sisi wengine Waislamu tunasema, nguruwe haramu lakini dharura ikitokea ni halali kula kidogo ili mambo yaendelee. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimwa Spika, naomba Serikali sikivu ya ...

**SPIKA:** Mheshimiwa Bungara aya ya ngapi hiyo?

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Aya ya 150 Surat Maida. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimwa Spika, kwa hiyo, kwa heshima na taadhima, kwa kuwa Serikali hii sikivu na wale wananchi wavuvi watakuwa hawana kazi, hali zao za kimaisha zitakuwa mbaya, nakuomba Mheshimiwa Mpina uongee na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Rais wa wanyonge na hakuna wanyonge nchi hii kama wavuvi, waruhusiwe kuvua ili waende na maisha yao. Hilo moja. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimwa Spika, pili, nguruwe haramu lakini katika dharura unakula. Basi na nyavu hizo haramu lakini wapewe wavue.

Mheshimiwa Spika, nakuja katika korosho. Sisi tunaishukuru sana Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ikiongozwa na Mheshimiwa Magufuli kwa kutuambia mtanunua korosho kwa shilingi 3,300; wakulima waliandamana wakafurahi, lakini kilichotokea hali ni mbaya sana. Mpaka leo wakulima bado hawajalipwa.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Dakika zako zimeisha Mheshimiwa.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** *Allah!! (Kicheko)*

**SPIKA:** Zimeisha kaka.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Namalizia tu. Ninachoomba watu wa Kangomba nao walipwe kwa sababu na wao walipeleka korosho *AMCOS* zikapokelewa na Serikali wanazo. Kwa kuwa wanazo korosho, za Kangomba walipwe, ndio hoja. Kwa sababu muda wangu umeisha, nilitaka nifafanuliwe sana hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya ahsante sana. Mheshimiwa Pauline Gekul, dakika 10. Hizi dakika jamani sipangi mimi, mmeshajigawia wenyewe. Mtu asije akawa anahisia tofauti. Ni mgawanyo mlioufanya wenyewe huko, mimi natamka tu hapa. Mheshimiwa Pauline, dakika 10.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Awali ya yote nikitakie heri Chama cha Mapinduzi katika siku yake ya kuzaliwa, miaka 42 siyo mchezo. Naamini tutaendelea kuwaongoza Watanzania ili wafikie ndoto zao za maendeleo. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, niweze kutoka moyoni kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kauli ambayo ameitoa hivi karibuni kwa wananchi wetu ambao wanaishi katika hifadhi mbalimbali katika vijiji vyao, ambao walikuwa wakipata matatizo makubwa na hifadhi zetu, lakini pia wakulima mbalimbali ambao walikuwa wanatumia maeneo ya vijiji lakini walikuwa na migogoro na hifadhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili halidhihirishwi tu na Wabunge tunaotokana na maeneo hayo, lakini limedhihirishwa na wananchi wetu ambao kwa namna moja au nyingine wamejitokeza hadharani kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kauli yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilichogundua ni kwamba kwa kauli hii, anayevaa kiatu ndiye anayefahamu ni wapi mwiba unamchoma. Kuna miongoni mwetu ambao wanabeza kauli ya Mheshimiwa Rais, lakini kwa wale ambao miaka yote tumekuwa tukiomba Serikali iangalie hili, kwa kweli tumepokea kwa moyo wa faraja na wa pongezi kwa Serikali na kwa Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, miaka mitano iliyopita, nilikuwa nikiongelea vijiji vya Gedhamaru, Gijedabung, Ayamango na maeneo mengine katika Mkoa wetu wa Manyara. Tumeona sasa wale wafugaji na wakulima jinsi ambavyo wameguswa na kauli ya Mheshimiwa Rais. Naomba nimtie moyo aendelee kutumikia Watanzania bila kuchoka, kwa sababu maamuzi anayofanya yanawagusa na yanagusa maisha ya wanyonge. Tunamshukuru sana. Ombi langu kwa Serikali, watusaidie mapema. Wizara husika waweze ku-*identify* hayo maeneo mapema ili wale wananchi sasa watulie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maana kauli ya Mheshimiwa Rais ni jambo moja lakini pia utekelezaji ni jambo lingine. Nina imani na Serikali yangu na ninaamini kabisa kwamba hili litafanyika mapema na hatutamwangusha Mheshimiwa Rais kwa kauli nzuri aliyotoa kwa Watanzania ambao kwa kweli wamepokea kwa moyo wa shukrani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie kwa ufupi changamoto ambazo tumeziona kwenye hifadhi zetu. Mimi ni Mjumbe wa Kamati hiyo, tunafahamu hifadhi zetu ambazo zinapatikana Kusini mwa Tanzania ukiachilia mbali za Kaskazini mwa Tanzania, zimekuwa na mchango kidogo kwenye Bajeti yetu ya Kitaifa lakini kwenye pato la Taifa ni kwa sababu ya changamoto ambazo wamekuwa wakikutana nazo.

Mheshimiwa Spika, kwenye kitabu chetu cha Kamati, wamezungumzia au tumezungumzia changamoto za Hifadhi ya Mikumi, jinsi ambavyo ile barabara kuu wanyama wamekuwa wakigongwa zaidi ya wanyama 100, kwa

mwaka tunapoteza wanyama hao. Pia hifadhi hizi au hii ya Mikumi imekuwa ikipata kuchafuliwa kwa sababu wanapopita panakuwa hapana doria ya kutosha na hata zile doria hazitoshelezi na wanaopita barabarani wanakuwa watupa uchafu na vitu kama hivyo.

Mheshimiwa Spika, Hifadhi ya Ruaha inahitaji kuangaliwa kwa karibu. Nafahamu kwamba hifadhi zetu zinachangia zaidi ya asilimia 17 katika bajeti yetu na katika pato letu la Taifa, lakini kama hifadhi hizi za Kusini zisipopewa kipaumbele na zikasaidiwa kwa karibu kwa kuondoa zile changamoto wanaweza wakawa wanaendelea kurudi nyuma katika mapato ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa Hifadhi ya Ruaha, naiomba Serikali yangu na ninaamini ni Serikali sikivu, hii barabara kutoka Iringa mpaka hifadhini zaidi ya kilometa 100 ni ombi la muda mrefu kwamba sasa iweze kuwekewa lami. Naamini katika mpango mzima uliopo wa *REGRO* ambao unalenga kukuza utalii na kusaidia hifadhi zetu kwa upande wa Kusini, unaoendeleza ungeweza kusaidia. Naiomba pia Serikali waweze kuharakisha kusaini mkataba huo wa *REGRO* ili isaidie katika kuondoa changamoto ambazo ziko kwenye hifadhi zetu.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara husika isaidie pia kuharakisha mfano miundombinu katika hifadhi zetu, Kwa Hifadhi ya Ruaha pamoja na Mikumi na hifadhi nyingine wanatamani sana ndege zitue katika hifadhi zetu ili watalii wale ambao wanatamani kufikia kule waweze kufikia.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu siyo watalii wote ni vijana ambao wanaweza wakastahimili kutembea katika barabara zetu. Kuna watalii ambao ni wazee, wao wanahitaji kutua moja kwa moja katika hifadhi zetu. Kwa hiyo, naomba pia Serikali iangalie kwa karibu sana ili waone pia tunakuwa na viwanja vya ndege katika hizo hifadhi.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, pia naiomba Serikali, sisi tuna hifadhi yetu ya Tarangire katika Mkoa wetu

wa Manyara ambako geti la Babati – Tarangire kupitia Babati Mjini pale, sisi tumesharidhia na geti limeshafunguliwa. zaidi ya kilometa 20 ni za *rough road*. Naiomba Serikali na asubuhi pia mlinijibu swali la *bypass*, mmeahidi kushughulikia. Tukipeleka lami pale, tutasaidia watalii wetu waweze kufikia hizo hifadhi.

Mheshimiwa Spika, naamini changamoto ni nyingi katika hifadhi zetu, lakini Serikali yetu ni sikivu na inaweza ikafanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ambalo nilitaka niipongeze Serikali kwa moyo wa dhati na ninampongeza Mheshimiwa Waziri pia, ni suala la mradi huu wa kurasimisha vijiji na upimaji ambao unafanyika kwa majaribio katika Mkoa wetu wa Morogoro na katika Wilaya za Malinyi, Ulanga na Kirombero, kwa kweli ni mradi uliosimamiwa vizuri.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa moyo wa dhati, huu mradi umesaidia wananchi kumilikishwa maeneo yao na wamepata Hati. Tumefika *site*, tumeona ni kwa kiasi gani hata akina mama wamepatiwa Hati, siyo wanaume tu. Tumeona ni kiasi gani wale wananchi wameshirikishwa.

Mheshimiwa Spika, nisipoipongeza Serikali kwa mradi huu, nitakuwa sijitendei haki. Nami naomba Serikali itusaidie, kuna fedha za ndani zaidi ya shilingi bilioni saba, lakini ni shilingi milioni 710 ndiyo zimetolewa. Mheshimiwa Waziri, pamoja na kazi nzuri, zikitolewa zile shilingi bilioni saba ambazo ni fedha za ndani, zitatusaidia kukamilisha ule mradi. Huo mradi sasa Mheshimiwa Waziri uweze kupelekwa kwa nchi nzima. Naamini nia ya Serikali ni njema sana, lakini tatizo lako ni bajeti.

Mheshimiwa Spika, nawaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu, tunapoelekea kwenye Bunge la Bajeti, Wizara hii tuipatie fedha kwa sababu wanapowapimia wananchi wakapata haki zao migogoro ya ardhi itakuwa imeisha katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nashukuru, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Gekul. Tunaendelea na Mheshimiwa Dkt. Sware.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi. Hoja yangu itajikita katika ukurasa wa 25 wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii ambayo imeelezea kuhusu kusimamia miradi ya Shirika la Taifa *(NHC).*

Mheshimiwa Spika, kwa kifupi naungana na maoni ya Kamati kwamba *National Housing Corporation* imesitisha miradi yake ya ujenzi kwa maendeleo ilhali kwamba iko katika mikopo. Sasa mikopo hii inazidi kukusanya riba inakuwa ni hasara katika uchumi wa nchi. Kwa hiyo, naomba Serikali ijitathmini kwa upya ili kuwezesha shirika hili likaendeleza kazi yake.

Mheshimiwa Spika, suala la pili katika maoni ya Kamati, ukurasa wa 23 inaongelea tishio la kukauka kwa Mto Ruaha Mkuu. Sasa naomba nijikite zaidi katika kulichanganua hili.

Mheshimiwa Spika, mto huu wa Ruaha Mkuu, ni moja ya mito ambayo ni muhimu sana katika nchi yetu. Kwanza, inasaidia katika Sekta nzima ya Utalii ambayo ina-*link* na sekta nyingine za kiuchumi kwa ujumla wake. Katika hali ya sasa, Sekta ya Utalii ina-*contribute 17%* ya tunachokipata kama *forest contribution* takribani sawasawa na Dola bilioni 2.1 kwa mwaka. Kwa hiyo, ni sekta ambayo ikilelewa au ikiangaliwa kwa jicho la ziada inaweza ikatutoa katika hii hali ya umasikini na kwenda kwenye uchumi wa kati.

Mheshimiwa Spika, ni kwa sababu gani inaweza ikatutoa hapa tulipo? Sekta ya Utalii inagusa sekta nyingine mbalimbali. Ni mambo ya hoteli, mambo ya usafirishaji, mambo ya vyakula, mambo ya *exchange rate,* ina-*influence* hapo. Kwa hiyo, tuiangalie kwa jicho la ziada kwa sababu

mto huu Ruaha ndio unaobeba, kama Kamati walivyoeleza vizuri, ni roho ya *Ruaha National Park.* Sasa hii *National Park* ndiyo kubwa zaidi hapa nchini na inaongoza kwa idadi kubwa ya tembo na simba.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tusiiache tu juu juu jinsi ambavyo inaweza ikatutoa hapa tulipo ilhali sasa hivi huu Mto Ruaha unakaribia kufa. Kwa sababu Mto huu *resource* yake ni maji, maji haya sasa hivi yamepungua, sasa hivi kunakuwa kuna misimu mirefu ya kuwa hakuna maji. Karibu asilimia 77 ya chanzo cha Mto Ruaha kwenye Bonde la Ihefu na Usangu yameharibiwa. Kwa hiyo mto ule unaenda kufa.

Ya pili, inaenda kuua vyanzo vyetu vya umeme. Tanzania sasa hivi tunategemea takribani asilimia 70 ya umeme kutoka kwenye vyanzo vya maji, ikiwepo Kidatu, Mtera na sasa hivi tuna-*propose* mradi mpya wa *Stiegler's Gorge.* Sasa nini kina-*feed* katika mabwawa makubwa ni huu Mto Ruaha Mkuu. Mtera karibia asilimia 56, Kidatu karibia asilimia 25 na kwenda *Stiegler's Gorge* kinacho-*contribute* yale maji ni asilimia 25 ya huu mto ambao tayari unakufa.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nataka pia tutafakari jinsi huu mto ambavyo unaenda kuharibu. Tumejikita kwenye Sekta ya Umeme tunategemea maji. Hivi karibuni tumepitisha mradi wa *Stiegler's Gorge* ambao ulikuwa unaleta sintofahamu na nilisimama kwenye Bunge lililopita.

Mheshimiwa Spika, wenzetu wa Kenya jirani, asilimia 65 ya chanzo cha umeme wao ni kutoka kwenye jotoardhi (*Geothermal)* na sisi Tanzania tuna hiyo *potential* ya ku-*top* umeme wetu ambao tuna uhakika nao kutoka kwenye *Geothermal.* Nafikiri Mkoa wa Songwe au Mbeya wana uwezo huo. Tuna *Rift Valley* ambayo ni *source* ya hiyo *Geothermal.*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, *investment* ambayo tunaweza tukaiweka katika kutafuta umeme katika nchi hii ambao unaweza uka-*boost* sekta zote *including* utalii ni umeme wa uhakika. Kwa hali ilivyo sasa mtakumbuka kwa

wale wahenga wenzangu, mwaka 2006 Mtera ilikauka. Tulikosa umeme kwa muda gani? Kwa hiyo, mabadiliko ya tabia nchi, uharibifu wa mazingira, mito yetu iko katika hali mbaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Makamba atani-*support* kwenye hilo, yaani hapa naomba tusifanye ubishani wala tusifanye siasa. Nchi yetu ina hali mbaya katika Mito yetu, mmojawapo ni Mto Ruaha, Mto Ruaha ndiyo huo umebeba utalii, ndiyo umebeba sekta ambayo inaenda kukuza huo utalii *including* umeme.

Kwa hiyo, naomba tutafakari kwa upya. Hata kama sasa tumeamua kuendelea hivyo hivyo na tumelazimishia kufanya *Stiegler's Gorge,* basi Wizara sekta husika iangalie jinsi ya kufufua hii mito iweze kutiririsha maji. Kama ikiwa *too late,* basi turudi nyuma tena tujitathmini. Kama kweli tunahitaji kutumia *Stiegler's Gorge* kama chanzo chetu cha maji wakati kinaenda kuharibu utalii Ruaha, kinaenda kuharibu utalii *Selous Game Reserve.* Yaani kunakuwa na sintofahamu iliyopitiliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba kwa hali ya pekee bila kuleta ushabiki, naomba tujitafakari kwa upya kama kweli tunataka kukuza sekta yetu ya utalii ambayo tuna uhakika katika kuimarisha uchumi wetu. Sisi wenyewe pia tujitafakari kama kweli ile *engine* ya kuleta maendelea ambayo ni umeme, basi tuangalie vyanzo vingine vya umeme tusitegemee *Hydroelectric Power.*

**MHE. DKT. JASMINE T. BUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Basi kama hatutaki kutoka hapo, tuangalie *means* mbalimbali za kuweza kuimarisha upatikanaji wa maji katika mito yetu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Sware.

**TAARIFA**

**MHE. DKT. JASMINE T. BUNGA:** Mheshimiwa Spika, naomba nimtaarifu Mheshimiwa Dkt. Sware kwamba hata hivi vyanzo vingine ambavyo vinaambiwa *geothermal*, *solar*, upepo na kadhalika, kutokana na hii *climate change* hakuna kitu ambacho kitabaki kama kilivyo. Kuna sehemu ambazo kuna *hot springs,* lakini zilikuwa labda 20, sasa hivi unaweza ukakuta ni mbili tu. Kwa hiyo, kuwa na vyanzo vingi vya umeme itasaidia nchi hii. Uharibifu wa mazingira, hata ukienda kule *Europe* kwa mfano, ukienda Ujerumani kule *industrial pollution* wameharibu *biodiversity* kiasi gani? Wamefanya *land reclamation* kwenye bahari, wameharibu *biodiversity* kiasi gani?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nafikiri labda tuangalie tu changamoto labda hii ya maji tuangalie namna ya kutunza vyanzo vyetu vya maji, lakini siyo ku-*discourage.* Kwa sababu kama utalii, Tanzania tuna Mbuga nyingi, lakini tunahitaji Selous kuendelea kwa matumizi ya uhakika ya umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Sware unapokea hiyo shule?

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Spika, sielewi anani-*support point* yangu au alikuwa anakinzana na *point* yangu, sijaweza kupata *conclusion*. Naomba niichukulie *positive* kwamba tusitegemee chanzo kimoja cha umeme maji ambacho kina sintofahamu kubwa kwa sababu ya uharibifu wa mazingira, kwa sababu ya shughuli za kiuchumi. Nimetoa mfano kwamba chanzo cha maji cha huu Mto Ruaha ni katika Bonde la Ihefa, si ndiyo!

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, bonde hili limeharibiwa kwa asilimia 77 kwa sababu ya shughuli za kiuchumi, kilimo cha *rice farming,* kwa hiyo lazima tu-*balance* kwani ukiwa na *diversity* kubwa ya vyanzo vya umeme una uhakika na upatikanaji wa umeme, lakini tusitegemee 70

*percent* ya umeme wetu iwe chanzo chake ni maji, ambacho kina sintofahamu.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa niende kwenye Kamati ya Kilimo, Mifugo, Maji na Uvuvi, naomba nijikite katika ukurasa wa 64, nakubaliana na maoni ya Kamati ambayo tunasema lazima tufufue Shirika letu la Uvuvi Tanzania na nataka nisisitize kwamba sio tu kulifufua Shirika hili, bali tutengeneze na miundombinu rafiki ya kufanya hili shirika liweze kufanya kazi. Tununue meli za uvuvi, tujenge bandari ya uvuvi na iweze pia kuziwezesha zile taasisi ambazo zitakuwa zinategemeana na Shirika hili ikiwa ni pamoja na *Tanzania Fisheries Research Institute.* Tunaita ni Taasisi ya kufanya *Research* lakini Taasisi hii, haijawezeshwa kufanya kazi kwa kukosa rasilimali fedha, Wataalam tunao lakini hatuna rasilimali fedha katika taasisi hii ili kuweza kukuza sekta ya uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa ....

**SPIKA:** Ahsante. Muda wako umekamilika.

Mheshimiwa Julius Kalanga, atafuatiwa na Mheshimiwa Zitto Kabwe. Dakika kumi Mheshimiwa Julius Kalanga.

**MHE. JULIUS K. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Napenda kutumia nafasi hii, kipekee kabisa kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa John Pombe Magufuli kwa kauli yake ya kusaidia wananchi wanaoishi katika maeneo ya hifadhi kwa muda mrefu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Kalanga, nataka kuwaarifu Wabunge kwa Mamlaka niliyonayo, naongeza nusu saa, tutamaliza saa saba na nusu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Kalanga endelea.

**MHE. JULIUS K. LAIZER**: Mheshimiwa Spika, kwa sababu wewe ni mzoefu katika nchi hii, Bunge hili limejadili mara nyingi operesheni mbalimbali zilizofanyika katika hifadhi ambazo ziliwaumiza wafugaji wa nchi hii kwa kiwango kikubwa sana, ni mtu tu asiye na akili timamu atakayeacha kumpongeza Mheshimiwa Rais Magufuli kwa jambo hili jema na la kiutu alilofanya katika kusaidia wafugaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wako watu ambao hawataki kuona jema analofanya Mheshimiwa Rais katika kipindi hiki cha miaka mitatu, lakini hao hao ndio wanaoomba viwanja vya ndege katika maeneo yao viboreshwe lakini wakati huo huo wakipinga uagizaji wa ndege katika nchi yetu. Hao hao ndiyo wanaosema tupunguze deni la Taifa lakini wanachukua Rais akinunua ndege kwa *cash* ya fedha ya walipa Kodi wa Watanzania hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipindi hiki cha Mheshimiwa Rais Magufuli cha miaka mitatu tumeshuhudia vituo 360 vya Afya vikijengwa katika nchi hii, ambayo ni historia, haijawahi kuitokea. Ndiyo maana wengine tunasema lazima tupongeze na kutambua kazi kubwa ambayo Rais huyu amefanya, katika muda mfupi ambao amekuwa katika madaraka haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunazo Hospitali 60 zinajengwa kwenye nchi hii, nani ambaye haioni katika utawala huu wa Rais Magufuli. Nataka tuyaseme haya kwa sababu Watanzania wengi wanatambua na wako wengi wanaopambana kufifisha ndoto ya Rais, lakini nataka tumtie moyo kwamba hata wakati ule Yesu alivyokuwa amepingana na matendo yake, akawaambia hata kama hamniamini aminini kazi ninazozifanya. Kwa kazi hizi ambazo Rais anafanya tunazitambua na kumpongeza na kumtia moyo, asonge mbele Watanzania wako nyuma yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hili la kumpongeza Rais, kwa dhati kabisa, naomba niipongeze Wizara ya Mifugo kwa mara ya kwanza wamesimama na wafugaji wa nchi hii na kutambua kwamba na sisi ni Watanzania walio huru katika

Taifa hili na kutetea maslahi ya Wafugaji. Pamoja na changamoto zingine lakini katika hili tuko pamoja na Mheshimiwa Waziri, asonge mbele, tutamsaidia katika kusimamia Wizara ya Mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumekuwa tukijiuliza maswali mengi kwa nini katika nchi hii, hatujawahi kuona oparesheni ya wakulima katika maeneo ya hifadhi isipokuwa operesheni ya wafugaji. Ni kwa sababu wafugaji mara nyingi wana *cash* mkononi kwa sababu wana ng'ombe, kwa hiyo viashiria vinafanyika wakati mwingine sio halali, ni operesheni za kutafuta rushwa na kunyang'anya wafugaji wetu mali zao. Katika hili ndio maana nasema tunampongeza Rais na Wizara kwamba angalau sasa ile mianya ambayo watu wachache waliitumia kuwaumiza wafugaji imefungwa na ndio maana wengine wanapiga kelele, lakini sisi tuko nyuma ya Rais kwa kazi kubwa ambayo ameifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka niseme mambo machache, nataka niombe Serikali watusaidie, wanazuia wafugaji wetu wasipeleke ng'ombe Kenya wanafanya operesheni ambayo sio halisia katika mipaka ya nchi yetu, lakini nataka niwauze Wizara ya Mifugo, Viwanda vyetu 82 vya maziwa nyakati za Nyerere mpaka kipindi cha Mwinyi kidogo, viko wapi? Viwanda vya nyama vilivyokuwa vinafanya kazi katika nchi hii, viko wapi? Kama ndani ya nchi yetu hakuna soko la uhakika kwa nini watuzuie sisi kwenda kutafuta soko huko linakopatikana na kama wanafikiri kuweka kodi kubwa kwa mifugo ni kuzuia mifugo isiende nje ya nchi, tunataka Wizara watuambie masoko ya kupeleka bidhaa yetu yako wapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni aibu, ni aibu kwenye Taifa linalozalisha ng'ombe nchi ya tatu Afrika, mali zetu za ng'ombe zinaenda nje bila kuongezwa thamani, tunapeleka kwato, maziwa, ngozi na nyama, halafu tunasema ipo Wizara inayojali mifugo, tunataka Serikali ituambie iko wapi mikakati ya Wizara ya kuhakikisha rasilimali hii ya Taifa ambayo ni neema kwa nchi yetu, inabaki kwa maslahi mapana ya Taifa letu na kuongeza pato la Taifa. Ni aibu kwa nchi

ambayo ni ya tatu kwamba pato la Taifa halilingani na mifugo tuliyonayo na wakati mwingine tunasema mifugo yetu inaharibu mazingira, tunataka Serikali itupe mikakati ambayo Waziri wa Viwanda jana alituambia, kwamba wamepanga kuhakikisha kwamba tunachakata mazao ya mifugo, tunataka *frame time,* ni lini viwanda vya kuchakata mazao ya mifugo kwenye nchi vitasimamiwa na kuonekana kwamba vinakidhi matakwa ya wafugaji wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka Serikali kwa kweli katika hili ituambie, tunaridhika na pato la Taifa linalochangiwa na mifugo yetu, tunaridhika na upekaji wa ng'ombe zetu Kenya bila kuongeza thamani. Hivi Wakenya wanatuzidi nini? Tunaridhika na uamuzi wa Afrika Mashariki wa kuweka vikwazo vya ngozi na nchi kama Rwanda na Burundi ambayo hawazalishi ng'ombe lakini wanatuletea ngozi, wakati tulikuwa tukizalisha ngozi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ipo Mikataba tunaingia na nchi, lakini kwa kweli haina manufaa kwa nchi yetu, nchi zile zingine hazizalishi ng'ombe, hazina ng'ombe, lakini wanaamua, wao ukipeleka ngozi Uganda, Rwanda inaenda kama *reject* kwa hiyo, sisi tunakosa mapato na ngozi zetu zinakuwa *useless. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara ituambie kuwepo kwa Wizara hii, ni kutafsiri ndoto ya Rais ya Tanzania ya viwanda ambayo kila mwananchi ataona umuhimu wa kuwepo kwenye Taifa lake na umuhimu wa kuwa na rasilimali katika nchi yetu. Haiwezekani tukasema tuna viwanda kadhaa, lakini kama viwanda hivyo havibadilishi maisha na uchumi wa nchi yetu viwanda hivyo havitakuwa na maana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo naomba kabisa, wakati Waziri wa Mifugo anakuja kuchangia baadaye atusaidie ni kwa namna gani nchi yetu inaondokana na hili tatizo la kupeleka rasilimali na bidhaa ambayo haijachakatwa katika nchi zingine za wenzetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho, tunalo tatizo pale Namanga, mfugaji akitaka kuvusha ng'ombe zake kwenda Kenya analipa si chini ya elfu 70 kwa kichwa cha ng'ombe, ipo Sh.30,000 wanaita ni fedha za ushuru wa Wizara, lakini ipo Sh.2,500 ya *movement permit* na kodi zingine za Halmashauri, hivi kwa nini ng'ombe peke yake tuyaangalie na mazao mengine tunayozalisha, wanakuwa na kodi kubwa kuliko mazao mengine yoyote kwenye nchi yetu? Tunaomba Waziri atuambie wakati wa bajeti hii ni kwa namna gani Serikali itapunguza kodi ambazo zimewekwa kwenye mifugo ya nchi yetu kwa sababu kuzuia tu isiende nje kwa kuweka kodi kubwa wakati huku ndani hakuna viwanda vya kuchakata, ni uonevu kwa wafugaji. Kwa hiyo naomba kwa kweli, kodi hizi zipunguzwe kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Spika, suala la ardhi, ni kweli tumesikia ushauri wa Kamati, lakini nami nampongeza Rais na nimpongeze Waziri wa Ardhi kwa dhati ya moyo wangu kabisa. Moja ya Wizara zinazofanya kazi na zinafanya vizuri katika nchi yetu, ni Wizara ya Ardhi na faida yake ni kwamba, wamekataa rushwa, sio kwamba hakukuwahi kuwepo Wizara katika nchi hii, lakini Wizara hii ina mchakato mkubwa sana wa rushwa. Sisi tunaamini hawa wamekataa rushwa ndio maana migogoro ya ardhi imepungua katika nchi yetu. Kwa hiyo tunawatia moyo, msikate tamaa, tunahitaji ardhi yetu kwa sababu imekaa muda mrefu haitumiki na sisi tunaihitaji.

Mheshimiwa Spika, tunajua wako wachache watakaotumiwa na watu wenye ardhi hiyo, lakini sisi tuko tayari kuungana na nguvu na shughuli za Wizara katika kurejesha rasilimali ardhi kwa nchi yetu na kwa Watanzania wanyonge ili waweze kutumia katika kuzalisha. Haiwezekani tukawa na ardhi lakini Watanzania walioko maeneo hayo hawana uhalali wa kutumia ardhi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeenda Misenyi wakati wa Kamati, ardhi kubwa iliyoko kule, Watanzania wamenyimwa kutumia, lakini Waganda wanaingiza mifugo, wanatoa jioni lakini ukienda Tanzania wanakwambia ni hifadhi. Hii si sawa,

lazima ardhi yetu itumike kwa maslahi ya Watanzania ambayo Mungu ametupa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara songeni mbele, lakini tunaomba mtuletee *modality* ya mchakato mzima wa kutatua migogoro ya ardhi katika nchi.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Julius Kalanga. Mheshimiwa Peter Msigwa atafuatiwa na Mheshimiwa Hawa Ghasia.

**MHE. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi.....

**SPIKA:** Dakika kumi.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia kwenye mjadala ulio mbele yetu. Kabla sijasahau, Mheshimiwa Sware amezungumza sana kuhusiana na Ruaha mto mkuu kukauka, lakini nataka tukumbushane kama Wabunge kuna mwandishi wa kitabu anasema: "*The Politicians don't care about economics, and the economists don't understand politics*."

Mheshimiwa Spika, ni kweli watu wamepongeza nia njema ya Rais ya kutaka wale watu walionyanyaswa kwenye maeneo mbalimbali jinsi ambavyo wametendewa vibaya, lakini vilevile kama viongozi ambao tunalitakia mema Taifa hili tusije tukaziacha faida za kiuchumi ambazo zinatokana na kutunza mazingira. Kwa hiyo, natamani wote kwa pamoja kama Wabunge hayo tuyaangalie, tusipige kelele tu watu wanapovamia maeneo ya utunzaji, hatuwezi kusahau eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, takwimu za mwaka 2009 katika sekta ya utalii zinaonesha mapato duniani, yaliyotokana na shughuli za utalii yalikuwa dola za

Kimarekani bilioni 852, watalii waliosafiri duniani kote walikuwa zaidi ya milioni 800 na sekta hii ilitoa ajira zaidi ya milioni 255 duniani kote, hii ilikuwa ni asilimia 11 ya ajira duniani.Hii inaonesha jinsi gani sekta hii ilivyo na umuhimu na inaajiri watu wengi na inazalisha shughuli mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kumbuka wakati huo Serikali ilijaribu kupanua wigo, lakini kama dunia nzima toka wakati huo, miaka kumi sasa imepita watu walikuwa milioni 800 wanaotalii, wakati huo nchi yetu ilikuwa na uwezo wa kuvutia watalii laki nane na kitu, Mahiga atanisaidia, alikuwa Waziri wakati huo.

Mheshimiwa Spika, lakini mpaka leo, pamoja na fursa nzuri tulizonazo katika nchi yetu, hatujaweza kufikisha watalii 1500, tunahangaika hangaika kwa sababu hatuna mipango endelevu, milioni moja na nusu hatujafikisha, tunahangaika kwa sababu hatuna mipango endelevu. Hatuna mipango endelevu kwa sababu hatu-*plan* kama Taifa.

Mheshimiwa Spika, katika Wizara hii, Waziri aliyekaa muda mrefu katika historia ya nchi hii ni Mheshimiwa Zakhia Meghji na huyu Waziri inasemekana alikaa muda mrefu katika Wizara hii kwa sababu alikuwa anawasikiliza wataalam. Nchi yetu ni miongoni mwa nchi ambazo zina vivutio vingi sana, tungeweza kuwa-*attract* kwa sababu hawa watalii tunanyang'anyana na nchi zingine, lakini kwa bahati mbaya Wizara hii imekuwa ikibadilishwa Mawaziri ambao wanaenda wanakuwa kama ni wajuaji kuliko uhalisia.

Mheshimiwa Spika, tuna fukwe nyingi, katika nchi yetu hatuja-*utilize,* tuna maeneo mbalimbali hatujaya-*utilize,* wakati ule takwimu hizi zinatokea wataalamu walikuwa wamejua kwamba na *World Bank* ilikuwa imesema kwamba kwa sababu sekta hii inaajiri watu karibu laki tano kama tukikuza utalii, upande wa kusini tutakuwa mara mbili, kwa sababu kaskazini ndio iko zaidi. Kwa hiyo tukikuza kusini itakuwa mara mbili.

Mheshimiwa Spika, nazungumza kwamba Wizara hii, tumekuwa hatuko *consistency* watu wanaoingia, kwa sababu tumeenda kwa pamoja mradi wa *REGROW* alikuja Makamu wa Rais alikuja Iringa, akauzindua lakini kwa taarifa nilizonazo kama Mbunge na Mjumbe wa Kamati, huu mradi wa *REGROW* unaonekana unasua sua na kuna dalili kwamba *World Bank* wame-*pull off* hata hiyo hela tena, haipo tena. Kwa hiyo ile mipango yote mizuri, ambayo tulitakiwa tukuze Mikumi, tukuze Ruaha tuuokoe mto Mkuu Ruaha mipango hii yote inakufa tena.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tunaanza kulalamika katika suala la Utalii kwa sababu mipango tunayopanga inakuwa sio endelevu, kila anayeingia kwenye Wizara ni kama yeye ndio anaanza anaacha mipango mizuri ambayo wengine wameanza. Mfano mzuri rafiki yangu Mheshimiwa Kigwangalla amekuwa na matamko mengi ambayo ni matamko ambayo yanaleta madhara, *Twitter* zake zinaleta madhara. Juzi ameenda kwenye *TTB* amevunja Bodi, tumesikia tena hiyo Bodi haijavunjika bado ipo. Kwa hiyo masuala haya wanafanya mambo ambayo hawafanyi utafiti, yana-*disturb industry.*

Mheshimiwa Spika, *industry* hii ni *very delicate,* hawa watalii waliokuzwa kutoka laki nane mpaka tulipofika imefanyika kazi kubwa sana ya kutangaza utalii huu. Sasa tunapokuwa hatuko *consistency,* hatufanyi kama ambavyo tume-*plan,* tunasababisha *industry* iyumbe na inaingiza uchumi mkubwa sana katika nchi yetu. Kwa hiyo niiombe Wizara itafakari kwa makini, ni namna gani inaweza kuiendeleza sekta hii.

Mheshimiwa Spika, tuna matatizo ya *hospitality* tunapozungumza masuala ya *hospitality* ina-*involve* mambo ya *customer care,* ina-*involve* mambo ya *customer service, ina-involve* hoteli zetu nyingi ziko *sub-standard* watalii hawaendi tu kwa sababu ya kwenda hotelini na kwao kuna hoteli nzuri, hoteli ziko *sub-standard,* watu hatujawa-*train,* watu wakifika hapa wanapata shida. Sasa hao watalii wataongezekaje? Watalii wakija hapa kwetu watakwenda

kulala wapi, watakaa wapi, kama hiyo *competition* hatulingani na watu wengine duniani. Hilo nilitaka nizungumze kwa mapana.

Mheshimiwa Spika, takwimu ambazo zimetolewa na Wizara yenyewe, tatizo lingine kubwa ambalo limesababisha watalii Tanzania isionekane ni nzuri zaidi mambo ya usafi, *hygine* kunaonekana kuna uchafu, watalii wanalalamika, ni takwimu za Wizara yenyewe, kuna mambo ya usalama, kuna mambo ya *infrastructure,* haya mambo yote wanayolalamika yanasababisha utalii uwe wa hovyo.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine nataka kuzungumza ambalo kwa masikitiko makubwa niseme katika Kamati tulipokuwa tuna-*windup* jana tulilipanga nalo lingeweza kuzungumzwa katika Kamati hii, kwa bahati mbaya halijazungumzwa, ambalo katika Kamati yetu tulipata malalamiko kuhusu unyang'anywaji wa mashamba makubwa. Hatuna tatizo na mashamba makubwa kunyang'anywa kwa mujibu wa sheria, lakini kuna mashamba makubwa katika Wizara ya Ardhi, pamoja na sifa nyingi ambazo Mheshimiwa Lukuvi hata mimi nimeshiriki kumpa, lakini suala hili la mashamba makubwa lina harufu fulani ya ukakasi, lazima tuelezane ukweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mashamba makubwa haya, kwa mfano Mheshimiwa Sumaye...

**MHE. JAMES K. MILLYA:** Taarifa.

**SPIKA**: Haya hiyo taarifa

**MHE. JAMES K. MILLYA:** Mheshimiwa Spika, mimi natoka Jimbo la Simanjiro, ambalo Mheshimiwa Waziri Lukuvi alipita mwezi mmoja uliopita, alifuta takribani mashamba ishirini na nne, nina hakika mashamba haya yote yalikuwa hayajafuata *procedure* katika kupata *title deed* yake na hakuna harufu yoyote ya rushwa naweza nikadiriki kusema. Kwa hiyo, asimchamchafue Mheshimiwa Waziri kwa sababu inawezekana yeye maisha yake hayajaguswa na mwendelezo

mzuri wa Mheshimiwa Waziri ndio maana anamchafua. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Msigwa.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Spika, sasa mimi nimemchafuaje hapa anavyosema? Nadhani anaenda haraka, kwani nimesemaje sasa, anasema nimemchafua, wapi? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nimezungumza kwamba sina tatizo kabisa na mashamba makubwa kunyang'anywa kwa mujibu wa Sheria na taratibu kwa kufuata *procedure*. Nimetoa mfano mmoja, mimi sijagusa mashamba ya Jimboni kwake, nimetoa mfano kwamba Mheshimiwa Sumaye, alikuwa na shamba lake, alilipata kihalali, ameliendeleza mpaka wana-*revoke* lile shamba lake alikuwa na ng'ombe 200 kwenye shamba, alikuwa na kondoo 350, nyumba kubwa ya umwagiliaji, visima, *go-down*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ameambiwa hajaendeleza, nasema unyang'anyaji huu, Rais kubadilisha hati ana mamlaka hayo, Rais anaweza akabadilisha sio tatizo, lakini ninachosema...

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Ninachozungumzia...

**SPIKA:** Aaah, muda umekwisha Mheshimiwa, dakika kumi zimekwisha.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Spika, dakika nane mpaka sasa hivi nikisoma hapa, ziko dakika nane....

**SPIKA:** Malizia sentensi yako basi.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Spika, mpaka sasa hizi ukiangalia jinsi ambavyo mashamba hayo yamechukuliwa, akina MO, wameendeleza mashamba lakini wamenyang'anywa, ndio maana sisi, lazima, bila ubaguzi…….

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walizomea)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Lazima bila ubaguzi, tulitaka Kamati ya Uchunguzi iundwe, kwa nini mnakataa kuunda Kamati ya Uchunguzi? Lazima Kamati ya Uchunguzi iundwe ili tuone uhalali wa mashamba hayo kunyang'anywa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa. Nilikuwa nimesema atakayefuata ni Mheshimiwa Hawa Ghasia, Mheshimiwa Hawa Ghasia dakika kumi tafadhali.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nami napenda niungane na wajumbe wenzangu kuwapongeza Wenyeviti wa Kamati ambao wamewasilisha taarifa zao katika Bunge letu asubuhi ya leo. Kwa kuwa muda wangu ni mfupi, napenda nijielekeze moja kwa moja katika masuala ambayo nimejipanga kuyachangia.

Mheshimiwa Spika, eneo la kwanza ni uvuvi. Eneo la uvuvi kwa kweli Serikali haijawekeza ipasavyo. Mara nyingi tumekuwa tukijielekeza kwenye operesheni zaidi kuliko kuwawezesha wavuvi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leseni za uvuvi zinafuata kalenda ya mwaka yaani Januari – Desemba. Januari ilivyoanza tu hata tarehe 15 bado operesheni za kuwasaka wasiokuwa na leseni zimeanza na kuwatoza faini kubwa zaidi ya shilingi milioni 1 kwa mvuvi mmoja wakati faini inaanza kutolewa baada ya mwezi Machi, kuanzia Januari, Februari mpaka Machi wanatakiwa wavuvi wakate leseni lakini mwaka huu

kabla hata ya Februari operesheni imeanza, wavuvi wangu wa Naumbu, Msanga Mkuu, Mkubiru na Msimbati wamepigwa faini mpaka shilingi milioni 4, hali kwa kweli kule ni mbaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri pamoja na kwamba tumezungumza naye, walikuja wavuvi pamoja na Waheshimiwa Madiwani kutoka Kilwa, ameahidi kwenda Kilwa siku ya Jumapili. Nimuombe Mheshimiwa Waziri asiishie Kilwa Kivinje na Kilwa Masoko, katika ziara yake aende mpaka Mtwara, Msanga Mkuu, Mkubiru, Msimbati, Naumbu na Mgau kwa sababu kero hiyo kwa kweli ipo kwa wavuvi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutoa ushauri kwa Serikali, naomba wafanye utafiti wajue ni nyavu zipi zinazoweza kuvua dagaa na baada ya kuzijua Serikali yenyewe iingie mkataba na viwanda wanunue hizo nyavu, waweke mawakala wa kuuza hizo nyavu Kilwa, Mafia na Mtwara ili wavuvi wetu ikiwezekana wakopeshwe na wanaoweza wanunue ili kuondoa hii sintofahamu ya kila siku tunawaelekeza nyavu za kununua halafu baada ya siku mbili tunaenda kuzikamata hizo hizo tunazichoma moto. Kwa hiyo, niiombe Serikali yenyewe kama inavyofanya kwa pembejeo za kilimo na katika maeneo mengine na huku kwenye uvuvi yenyewe itafute mawakala wa kusambaza zana za uvuvi ambazo wao wamezipitia na kuzithibitisha na kuziona kwamba baada ya utafiti wao zinafaa kuvua dagaa, pweza na kamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huo ndiyo ulikuwa mchango wangu wa kwanza kwa kweli wavuvi wetu hawana amani lakini ni eneo ambalo kwa kweli kama Serikali hatuwawezeshi. Ukiacha mradi wa *MANCEP* ambao ulipita kipindi hicho, hakuna mradi mwingine wa uhakika ambao umekuja wa kuwawezesha wavuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nililetewa na Naibu Mheshimiwa Waziri injini ambazo kama Wizara iliona wangeweza kuzitoa kwa ruzuku kwa wavuvi. Nilivyoenda kuwatangazia wavuvi

wangu waliniambia hizo mashine ni ndogo sana kwa kwenda nazo baharini. Sasa sijui wakati Wizara wananunua waliwashirikisha vipi wavuvi wetu.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ambalo nilitaka nilichangie ni ununuzi wa korosho. Tulifurahi sana Serikali ilivyoamua kununua korosho kutoka kwa wakulima wetu na bei ambayo iliitoa lakini muda ambao tunauchukua katika mchakato mzima wa kununua korosho kwa kweli ni mrefu mno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kawaida ununuzi wa korosho unaanza mwezi Oktoba ikifika Desemba wale wanunuzi wanavyokwenda Chrismas inakuwa ni kama ununuzi umeishia, wanavyorudi sikukuu za mwaka mpya labda minada ikiendelea ni mitatu, minne na ununuzi unakuwa umeisha. Sasa hivi mpaka mwezi Februari hata asilimia 60 ya ununuzi haijafikiwa. Wamehakiki zaidi ya tani 200,000 lakini waliolipwa hawajafika hata tani 150,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, cha kushangaza katika takwimu zetu tunaambiwa katika vyama 605, wameshalipa vyama 600 lakini ukiangalia tani zilizouzwa hazijafika hata tani 150,000. Sasa sijui hizo takwimu zimekaaje, watatuambia wanaokuja kutujibia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine, Halmashauri zetu zote za Kusini ushuru wa korosho ndiyo chanzo chetu kikubwa cha mapato. Mpaka sasa hivi tunavyozungumza mwaka wa fedha 2018/2019 bado miezi mitano tumalize na hatujapata ushuru na hatuna uhakika kama tutapata na hatujui kama tutapata tunaupata lini. Niiombe Serikali suala la ushuru kama ambavyo wadau wengine wamelipwa na kwa kawaida ileile Sh.3,300 ambayo Serikali ilisema itanunua kutoka kwa wakulima, wadau wote wangepata pesa zao kutoka kwenye pesa zilezile bila hata kuhitaji bajeti nyingine.

Mheshimiwa Spika, niiombe Serikali ijitahidi kuhakikisha wadau wote wanaohusika katika ununuzi wa korosho na wakulima wetu hasa wakubwa maana yake

wakulima wakubwa mpaka sasa hivi hawajaanza kulipwa. Imekuwa kama ni adhabu sasa kuwa mkulima mkubwa wa korosho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Hawa Ghasia, Mheshimiwa Mwita Getere tafadhali.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuongea. Ni dakika ngapi Mheshimiwa?

**SPIKA:** Dakika kumi.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa hizo dakika kumi.

Mheshimiwa Spika, nchi zetu za Afrika zilikuwa zinatawaliwa na wakoloni kwa miaka mingi tu ikiwemo Tanzania nayo ilitawaliwa na Waingereza lakini kwa sasa wakoloni hawawezi kutawala nchi za Kiafrika, kilichobaki ni kuwatawala katika fikra zao yaani fikra za Waafrika wengi viongozi wengi na hasa wasio kwenye chama tawala wamekuwa *colonized* na Wazungu. Ndiyo maana utawakuta wapo maeneo mbalimbali wanazungumza mambo mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa sababu gani? Nilikuwa naangalia hapa kwenye takwimu mbalimbali wanasema *top ten best performing President in Africa,* Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli yumo. Ana miaka mitatu tu toka ametawala nchi hii lakini ameingia ni wa nane, amemzidi mpaka wa Rwanda miaka mingapi ametawala? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa natazama mtu anazungumza mambo ya *Stiergler's Gorge* namshangaa. Nataka ni-*declare interest* kwamba mimi nimesoma *diploma, certificate* na *degree* ya mazingira. Sheria ya Mazingira

inasema hivi utawale mazingira na mazingira yakutawale. Ukiangalia nchi zote duniani zilizoendelea zina mabwawa ya *hydroelectric power;* Marekani, China, Uingereza zote wanayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitoe mfano mmoja tu, China sasa ina mahali panaitwa *Gorges Dam capacity* yake ni MW 22,500. China imechukua mito kama mitatu imekusanya yote, ina watu bilioni sijui 3 leo tunazungumza Tanzania MW 2,400 watu ng'e, ng'e, ng'e, hivi wamekuwaje? *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, Marekani wana bwawa linaitwa *Grand Coulee Dam, capacity* yake ni 6,809. Sasa Marekani wametengeneza mto unaitwa Colombia, ule China unaitwa *Yangtze*, leo wale waliokuwa-*colonized* kwenye akili *they are talking about* mambo ya wazungu, sasa akili gani hizi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitoe tu angalizo, nampenda sana rafiki yangu Msigwa na tupo Kamati moja, mimi Mungu alinisaidia kuwa mkweli, ni vizuri tuwe wakweli. Kwanza amezungumza kwamba kwenye Kamati yetu hakuna taarifa lakini taarifa hiyo imo. Kamati imempongeza Rais kwa kutatua migogoro mbalimbali ya ardhi nchini. Wewe ulitaka tuseme kwamba wamenyang'anya mashamba ya Sumaye? Rais anapofanya kazi nzuri ni kumpongeza. Naishukuru Kamati yangu ya Ardhi imefanya kazi nzuri sana. Kwa hiyo, tumempongeza Rais kwa kufanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini Rais hanyang'anyi watu mashamba na Rais yeye hafuti umiliki. Nataka nitoe mfano, Bunge lako ndiyo linatunga sheria, leo mwanafunzi wa darasa la kwanza, la pili au la tano akiulizwa nani anatunga sheria za Tanzania watasema Bunge la Tanzania lakini hizo sheria haziwezi kwenda kufanya kazi bila Rais kupitisha. Kwa hiyo, Rais akipitisha ndiyo inakuwa sheria. *(Makofi)*

## T A A R I F A

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Ndiyo taarifa.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Napenda kumpa taarifa Mjumbe anayeendelea kuzungumza kwamba Kamati ingekuwa inafanya kazi vizuri Mwenyekiti wake asingeweza kujiuzulu jana kwa mashinikizo na ndiyo maana leo unaona Mwenyekiti, Mheshimiwa Nape Nnauye hayupo hapa. Kwa hiyo, inawezekana kuna matatizo kwenye Kamati ndiyo maana Mwenyekiti kajiuzulu.

**WABUNGE FULANI:** Ooooooo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Haonga, unaweza ukathibitisha hayo unayoyasema?

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Spika, jana Mwenyekiti wa Kamati ya Maliasili amejiuzulu sasa leo wajumbe hatujatangaziwa, hatuna taarifa humu na Kamati haijasema.

**SPIKA:** Umesema kwamba amejiuzulu kwa mashinikizo, nakuuliza unaweza ukathibitisha hayo mashinikizo? *(Makofi)*

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Spika, hapa labda neno mashinikizo niliondoe lakini hatuna taarifa kama Bunge.

**WABUNGE FULANI:** Aaaaaa.

**SPIKA:** Basi huna unachokiongea, Mheshimiwa Mwita Getere endelea.

**MBUNGE FULANI:** Nguchiro.

**MBUNGE FULANI:** Huo ni umbea. *(Kicheko)*

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, matatizo ya hawa jamaa ndiyo hayo hayo, yaani wao ni kukuza maneno, Mwenyekiti wetu sisi anafanya kazi nzuri, kama amejiuzulu, amejiuzulu kwa utaratibu wa kawaida wa watu kujiuzulu. Mimi nampongeza Mwenyekiti kama amejiuzulu kwa utaratibu wa kawaida basi sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niendelee, hakuna siku kwenye Kamati yetu na Mwenyekiti wangu yupo hapa tumewahi kuita watu wenye mashamba walionyang'anywa wakalalamika, tumeita watu wa porini, *tourism* na watu wa kila mahali, Kamati tuna majina.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. BONIFACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, tuna orodha ya mashamba mengi nchi hii yanayotegemea kufutwa na mengine yamefutwa...

## TAARIFA

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. BONIFACE M. GETERE:** Na sheria iko wazi...

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwita kuna taarifa.

**MBUNGE FULANI:** Ataje Kanisa lake.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Spika, anayezungumza ni mjumbe mwenzangu kwenye Kamati yetu. Kamati ya Ardhi ya Mheshimiwa Lukuvi ilikuja na kuna barua za malalamiko ya watu walionyang'anywa mashamba. Kamati ilivyokuja tuliitimua ikajiandae vizuri kwamba tuje tujadiliane vizuri. Akisema hatujawahi kufanya anasema uongo, tusifiche uongo hapa kama kuna jambo tulitibu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Getere.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nadhani huyu ana jambo analo kichwani ndiyo linalomsumbua, kwa hiyo, tuendelee na utaratibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuja na orodha ya mashamba yanayopendekezwa kunyang'anywa au kufuta miliki siyo kuleta wadau waliolalamika. Ni kweli kwamba Kamati ilikuja na mashamba mengi tu ya wakulima wadogo na wakulima wakubwa. Sheria ya Ardhi iko wazi inakutaka ukipewa uwekezaji miaka mitatu uwe umeendeleza.

**MBUNGE FULANI:** Ndiyo.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Sheria hiyo inasema tukitaka kunyang'anya shamba tutakupa siku 90 za kujitetea. Nani aliwahi kuleta hiyo barua wewe ukaiona? *(Makofi)*

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, niombe nchi yetu tufanye kazi moja kuwaelimisha Watanzania waelewe nini maana ya kuwa mzalendo.

**T A A R I F A**

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Getere, kuna taarifa ya Mheshimiwa Mlinga.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nataka nimpe taarifa Mheshimiwa Mbunge anayezungumza kuwa hapo linalopigiwa kelele ni shamba la Sumaye ambalo taarifa zake ni hizi. Mheshimiwa Sumaye alikuwa na shamba la hekari 326 amekaa nalo miaka 15, ameendeleza heka sita (6), amejenga kibanda kimoja (1) kina

watu watatu (3), lilikuwa na miembe mitatu (3), miche ya mahindi sabini na sita (76), mnazi mmoja (1), ng'ombe watatu (3), mbuzi kumi na moja (11), bata sita (6) na kuku tisa (9). Ahsante sana. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Engineer Mlinga soma hiyoo ngapi huko?

**SPIKA:** Hiyo haijawahi kutokea, Mheshimiwa Msigwa yupo *flat* kabisa hawezi kusimama tena. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, niwakumbushe suala la shamba la Mheshimiwa Sumaye nadhani lipo mahakamani. Kama hivyo ndivyo tuliache jambo hilo tusije tukatuhumiwa kuingilia kwenye mhimili mwingine.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Mama Margareth Sitta anawatangazia Wabunge wanawake *(TWPG)* kuwa leo baada tu ya kuahirisha shughuli hapa kuna mafunzo maalum ya malezi *(mentorship program)* yatakayofanyika katika Ukumbi wa Msekwa mara tu baada ya kumaliza shughuli za hapa. Mafunzo haya ni muhimu sana na tutakuja kuyazindua au kuyafungua. Tunaomba Wabunge akina mama wote muhudhurie yameandaliwa vizuri kabisa. *(Makofi)*

Pia Wabunge Wakristo mnaombwa baada ya hapa wale ambao huwa wanashughulika na masuala ya maombi, Mwenyekiti wenu wa ibada Mheshimiwa Anna Lupembe anaomba mkutane pale pale ambapo huwa mnafanya ibada.

Kipekee nimeambiwa Baba Askofu Chilongani yupo, karibu sana. Kwa wale ambao hamumfahamu Baba Askofu Dickson Chilongani ndiye Askofu wa Dayosisi ya *Central Tanganyika* ambayo makao makuu ni hapa Dodoma. Karibu sana Baba Askofu pamoja na wageni uliofuatana nao, tunafarijika sana kwa wewe kuwa miongoni mwetu kwa siku ya leo. *(Makofi)*

Vilevile, tuna Makatibu Wakuu wa Mifugo na Uvuvi, Prof. Elisante Ole Gabriel na Dkt. Rashid ambao wapo miongoni mwetu, karibuni sana. Kama kuna viongozi wengine wa Kiserikali ambao mpo karibuni sana na wageni wetu wote ambao mmefika karibuni sana; muda haupo upande wetu, naomba niwashukuru sana kwa kuja kwenu. *(Makofi)*

Tutaendelea na shughuli zetu saa kumi kamili jioni, kuendelea kujadili mambo haya yanayoendelea na mchangiaji wa kwanza atakuwa ni Mheshimiwa Zitto Kabwe, atafuatiwa na Mheshimiwa Jitu Soni.

Waheshimiwa Wabunge, sasa naomba nisitishe shughuli za Bunge hadi saa kumi kamili jioni ya leo.

*(Saa 7.34 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 10.00 Jioni)*

*(Saa 10.00 Jioni Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Majadiliano yanaendelea na kama nilivyoahidi asubuhi, tutaanza na Mheshimiwa Zitto Kabwe na atafuatiwa na Mheshimiwa Jitu Soni. Mheshimiwa Zitto Kabwe, dakika kumi.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuchangia Kamati zetu hizi mbili; Kamati ya Maliasili na Utalii na Kamati ya Kilimo ambazo zinabeba Wizara muhimu sana. Kamati ya Kilimo peke yake mchango wake kutoka kwenye idara ambazo inazisimamia katika Pato la Taifa ni takribani asilimia 33 na tunaambiwa sekta ya utalii peke yake inachangia asilimia 17 katika pato la Taifa. Kwa hiyo, tuna hoja nyeti sana ambazo naamini kwamba Wabunge tunazitendea haki pia.

Mheshimiwa Spika, nitaanza na jambo la uelewa kidogo, jana na juzi tumekuwa na mjadala hapa kuhusiana na masuala ya biashara ya korosho na kulikuwa na ubishani kidogo kuhusu masuala ya kangomba na kadhalika. Kuna jambo ambalo naomba Waheshimiwa Wabunge tulitazame,

leo hii sisi tumeweka nguvu kubwa Kagera kuzuia kahawa yetu isiende Uganda. Kahawa yetu ikishakatiza tu mpaka wa Uganda, kule Uganda hawana shida yoyote. Ndiyo maana leo ukitazama mauzo ya kahawa nje, pamoja na kwamba Uganda eneo lake la kahawa ni dogo lakini wanauza tani 306,000 za kahawa kwenye soko la dunia wakati sisi tunasuasua kati ya tani 100,000 na 137,000, sina uhakika sasa hivi tumeuza kiasi gani, lakini Uganda mara zote wanauza nje mara mbili. Uganda sasa hivi ni namba nane duniani na namba moja Afrika kwa kuuza kahawa nje. Kahawa ile ambayo Waganda wanauza, sehemu yake inatoka Tanzania, Burundi, Rwanda na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi leo anaweza akasimama Mkuu wa Wilaya akaita na vyombo vya habari kutangaza kwamba eti amezuia korosho kutoka Msumbiji kuja Tanzania. Nadhani ifike wakati viongozi wetu ngazi za chini na naomba radhi, nitatumia neno tuache ushamba. *Re-export* ni biashara kubwa duniani, sisi tunapaswa kuweka *incentives* kama kuna watu wana bidhaa zao ambazo zinauzwa wakazileta tukaziuza sisi zita-*appear* kwenye *balace of payment* yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana leo *United Arab Emirates* wanauza nje bidhaa za thamani ya Dola za Kimarekani bilioni 295. Katika hizo *re-export* ni Dola za Kimarekani bilioni 137 yaani ni bidhaa za nchi zingine zikifika pale Dubai au Abu Dhabi na kadhalika, wanazifanyia *repackaging* wanauza nje, inaitwa *re-export.* Kwa hiyo, naiomba Serikali izungumze na hawa Wakuu wetu wa Wilaya wa mipakani huko waachane na hayo mambo, waache tabia za kishamba, kama mali inakuja kwetu acha iingie tutaiuza sisi dola zitaingia kwetu. Kwa hiyo, naomba hili jambo tulitazame vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pili na naomba hili nimu-*address* Waziri wetu wa Kilimo, rasimisha kangomba, ndiyo njia pekee ya kuhakikisha kwamba tunaondoa ulanguzi. Vyama vyetu vya Ushirika havina *incentive* ya kuwawezesha wakulima wetu wapate mikopo midogomidogo ya kuweza

kushughulika na kero zao ndogondogo. Ndiyo maana ukienda Kagera kule na rafiki yangu Naibu Waziri wa Kilimo anajua kuna Obutura, ndiyo kangomba hiyo ni majina tu tofautitofauti, rasimisheni haya mambo, wapeni leseni. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Wapeni mizani, wataacha kufanya kazi ya ulanguzi na itatusaidia korosho, kahawa au pamba nyingi kukusanywa na tutakuwa hatuna mambo haya.

Mheshimiwa Spika, haiwezekani leo mtu ambaye anafanya *brokerage Dar es Salaam Stock Exchange* anaonekana ni mtaalam kwelikweli, halafu unakwenda unamdhalilisha kangomba unamuita mlanguzi, unamuita nini, haya mambo yamepitwa na wakati. Rasimisheni, wapeni leseni na mizani tuweze kufanya kazi vizuri, matatizo mengine yatakuwa yamekwisha bila shida yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ninalotaka kulizungumzia, sasa hivi tuna wakati mgumu sana, ni kweli tuna miradi mikubwa inafanyika, ni kweli kabisa lakini wachumi wenzangu hapa watanisaidia. Duniani kote pale ambapo hali ya uchumi ni mbaya, kuna *recession* (mdororo), Serikali hutekeleza miradi mikubwa ili watu wapate fedha kuongeza *aggregate demand* ili uzalishaji uweze kurudi. Sisi hapa kwetu tuna miradi mikubwa kwelikweli lakini *aggregate demand* haionekani, haiongezeki ni kwa nini? Kwa sababu katika hali ya kawaida ilitakiwa leo Watanzania wawe na furaha kwelikweli kwa sababu tuna miradi inayoingiza fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni kwa sababu miradi yetu inatoa fedha kupeleka nje, miradi yetu ni *outflows* siyo *inflows* ndiyo maana kuna shida, ndiyo maana *liquidity* ni *problem* katika nchi yetu. Ndiyo maana tunazungumzia sijui *inflation* kwamba imeshuka na nini, ni *inflation* ambayo inatokana

na watu kutokuwa na fedha za kununua bidhaa, ndiyo maana *inflation* iko *very low. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana ndani ya miaka mitatu, kwa mujibu wa taarifa ya *World Bank* na jana Mheshimiwa Komu amezungumza hapa, Watanzania milioni mbili wameingia kwenye *poverty.* Kwa sababu mifumo na maamuzi yetu ya kiuchumi sio ambayo yanakwenda kuwasaidia wale wadogo. *Fine,* tuna miradi mikubwa tutashangilia lakini hii miradi mikubwa haitengenezwi kwa namna ambayo itamfanya mpaka mtu wa chini aweze kupata hali nzuri ya uchumi.

Mheshimiwa Spika, suala lingine naomba nipate maelezo ya Serikali, tunaambiwa kwamba *Tanzania Agricultural Development Bank* imepata mkopo kutoka *African Development Bank* ndiyo fedha ambazo zinatumika kwa ajili ya kununua korosho. Sisi ni watu wazima humu ndani, leo hii nenda kwenye *website* ya *African Development Bank* angalia kama kuna *credit* inayokwenda *Tanzania Agricultural Development Bank,* hutaona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo hii dakika chache kabla sijaanza kuongea nimetazama na nimekuta mara ya mwihso ni *credit* ya tarehe 24 Januari, 2019. Serikali itueleze hizi bilioni 900 zimetoka wapi? Mmekwenda Benki Kuu kuondoa kwenye *deposits* za Mashirika ya Umma kwa ajili ya kupeleka *Agricultural Development Bank* na kwenye Bodi ya Mazao Mchanganyiko kwa ajili ya kununua korosho? Haitakuwa mbaya lakini mtuambie badala ya kudanganya.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu mlituambia tutanunua korosho, tutazibangua, tutauza nje, tunauza korosho ghafi kama vile walivyokuwa wanafanya watu wengine. Naomba sasa hivi tuondokane na hiki kitu cha kudanganyana na kutoelezana ukweli. Naomba Serikali itueleze leo fedha zile zimetoka wapi kwa sababu fedha za *African Development Bank* pale hazipo, sasa mtueleze Benki Kuu mmezichukua kutoka kwa nani, kutoka kwenye akaunti zipi na taratibu zipi ambazo zitatengenezwa kwa ajili ya

kuzirejesha fedha hizo, kwa sababu tunajua Benki yetu hii ya Kilimo haina mtaji huo wala hizo *deposits* za kuweza kununua hizo fedha ambazo zinatakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho ambalo ninapenda kulichangia ni hili suala la *TFS.* Kamati ya Utalii imezungumzia kuifanya *TFS* iwe Mamlaka kutoka kuwa Wakala, naunga mkono ukurasa wa 13 wa Kamati hiyo kwa sababu wanashughulikia misitu mingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yale matatizo ambayo yalitokea Iringa juzi ya miti ile ya watu wa *REA* na makampuni yanayotutengezea umeme kuzuiwa kwa ajili ya ushuru wa Halmshauri na kadhalika, ile ni *double payment* kwa sababu *TFS already* imeshalipa zile *cess* lakini pili, Mkuu wa Mkoa akaagiza tena kwamba Halmashauri zilipwe tena, matokeo yake ni nini, sisi ndiyo ambayo tunaathirika tunakosa nguzo kwa ajili ya umeme. Tukiipa *TFS* mamlaka ya kutosha ikawa mamlaka inaweza ikasaidia kuondokana na hizi kero nyingine ambazo zimetokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, nakubaliana na mapendekezo ya Kamati zote mbili ambazo zimeleta taarifa zake hapa na naamini kabisa kwamba zitaweza kufanyiwa kazi na Serikali italeta taratibu za utekelezaji wake. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Jitu Soni, dakika kumi.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza kabisa, naomba nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu siku ya leo kunipa fursa ya kuchangia hapa.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kwa niaba ya Wabunge wote ambao wanatokana na maeneo ya ufugaji lakini pia wafugaji Tanzania nzima kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa maamuzi ya busara na makubwa aliyofanya hivi karibuni. Katika maeneo mbalimbali nchini, ni furaha kubwa sasa watu wamekuwa na matumaini

makubwa na tunaamini kabisa kwamba suala hili sasa litafika mwisho na hii migogoro baina ya hifadhi mbalimbali, baina ya wakulima, wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi yote sasa itafika kilele. Tunampongeza Mheshimiwa Rais na tunaomba sasa watendaji wote ambao watafuatilia wafanye kazi kwa umakini ili patokee matokeo mazuri na pande zote ziwe na mafanikio makubwa. *(Makofi)*

Mhesheshimiwa Spika, naomba pia nikumbushe kuwa haya maeneo mengi ambapo wafugaji wapo watu wengi sasa hivi hata humu ndani baadhi ya Wabunge wamechangia kwamba ni waharibifu wa mazingira, kama sio wafugaji wa asili hizi hifadhi zote zisingekuwepo. Kwa mfanom Kanda ya Kaskazini kama siyo wafugaji wale wametunza hayo mazingira na yamekaa vizuri na wanyamapori, hizo hifadhi zote zisingekuwepo.

Mheshimiwa Spika, tunapongeza na tunajua kabisa sasa katika maeneo ya Ayamango, Gedamag, Gidejebong ambayo tumeyasemea kwa muda mrefu lakini pia kwa maeneo ya *WMA* ya Burunge katika Wilaya ya Babati, changamoto zote hizi sasa zitapata ufumbuzi. Nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Ulega, kwa kufika pale, alitolea ufafanuzi mzuri na kila upande ulifurahi na sasa wanasubiri utekelezaji lakini naamini kwamba na wengine wote watafuata nyayo za Mheshimiwa Ulega. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikijikita kwa upande wa kilimo, nipongeze Kamati zote kwa kazi na ripoti nzuri na nikiwa mmojawapo katika Kamati ya Kilimo. Nimpongeze Waziri wa Kilimo na Naibu wake wote wawili, Waziri wa Maliasili na Utalii lakini pia Waziri wa Ardhi kwa kazi kubwa na nzuri wanayofanya, changamoto zitaendelea kuwepo, ni kawaida lakini naona mafanikio ni mengi ziadi kuliko changamoto. Kwa hiyo, tuendelee kushirikiana, tuendelee kufanya kazi ili changamoto zote ziishe.

Mheshimiwa Spika, ombi langu kubwa kwa upande wa kilimo, ili tuwe na usalama wa chakula ambao tunaimba kila siku, jambo la kwanza kabisa naomba tuwe tunazalisha

mbegu zetu. Asilimia 75 ya mbegu zetu zinatoka nje ya nchi hasa mbegu ambayo ni ya chakula chetu kikubwa yaani mahindi lakini pia mbegu za mbogamboga zote asilimia zaidi ya 90 zinatoka nje ya nchi. Nashauri tuiwezeshe *ASA* ambao ni Wakala wa Mbegu nchini pamoja na mashamba yao waweze kuzalisha mbegu ya msingi *(foundation seed)* ili tuwe na uhakika wa mbegu ndani ya nchi ambazo zitakuwa zinafanya vizuri badala ya kuagiza mbegu kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, tunaagiza bidhaa kutoka nje ambazo zinaweza kuzalishwa hapa nchini kwa mfano sukari, mafuta ya kula, mchele, ngano, mbogamboga, matunda, maziwa pia nyama na samaki. Hizi zote tuziwekee muda kwamba ndani ya muda fulani, ndani ya miaka mitatu au mitano itakuwa hatuagizi tena kutoka nje badala yake tutakuwa tunazalisha ndani ya nchi, fursa zipo na tuwekeze katika hayo maeneo ili tuweze kuzalisha vya kutosha lakini pia ziada tuwe tunatuma nje na uwezo huo upo kabisa.

Mheshimiwa Spika, lingine naomba tuwekeze kwenye utafiti hasa katika masuala ya bioteknolojia na vituo hivi 17 vya utafiti hapa nchini. *TARI* ambayo inafanya kazi kubwa isipowezeshwa, haya mambo ya mbegu lakini pia utafiti mbalimbali wa udongo na mambo mbalimbali, hatutaweza kufikia malengo ambayo tunatarajia. Jambo la muhimu ni kwamba ile bajeti ambayo tumetenga kwenda kule *TARI* iende. Lengo ilikuwa tutenge asilimia 1 ya bajeti yetu nzima iweze kwenda katika masuala mbalimbali ya utafiti kwa ujumla, siyo kilimo peke yake.

Mheshimiwa Spika, pia kwenye kilimo, mbali na kuchanganya bajeti zile nyingine ambazo zinaingiliana ambazo ni mtambuka, bajeti ya kilimo peke yake tu kama kilimo iwe ni asilimia 10.

Mheshimiwa Spika, lingine ni uzalishaji wa mbolea, tunaagiza mbolea nyingi sana kutoka nje ya nchi. Tunacho kiwanda kimoja ambacho mbolea yake hatuitumii hapa nchini inavyotakiwa badala yake mbolea nyingi ya Kiwanda cha Minjingu inapelekwa nchi za jirani. Serikali za huko zinanunua kama Bodi ya Mazao Mchanganyiko Kenya ndiyo

wananunua tani zaidi ya 20,000. Mheshimiwa Rais alishatolea maelekezo kwamba mbolea hiyo inunuliwe katika maeneo ambayo inafaa itumike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mbolea ni sawa na binadamu, unapoumwa ndiyo unaenda unapimwa, ukipimwa ndiyo unapewa dawa, tusichukulie tu kwamba mbolea ya Minjingu kila mahali itafanya kazi. Mahali mbolea ya Minjingu isipofanya kazi hata hiyo *DAP* inayotoka nje ya nchi haitafanya kazi kwa sababu haitakiwi hiyo *DAP.* Kwa hiyo, tuendelee na utafiti na masuala ya kitaalam, kwa hiyo, tutumie viwanda vya ndani.

Mheshimiwa Spika, tuliambiwa kwamba kuna suala hili la kujenga kiwanda kule Lindi ili tuzalishe *urea* nchini. Tukiwa na *urea* na *phosphate, NPK* itapatikana hapa nchini. Baada ya hapo ni kuchanganya *ratio* kwamba unahitaji asilimia ngapi ya aina moja ya *N, P* au *K* unapata mbolea za aina mbalimbali, hakuna zaidi ya hapo, hiyo ni *baseline* nyingine zote ni *nutrients* za ziada ambazo zinatakiwa zinatokana na upimaji wa udongo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye suala la maji, nipongeze Wizara inafanya kazi nzuri sana, wamekuwa na mpango mzuri na niwapongeze kwa kupitisha sheria hii mpya juzi ambayo italeta mabadiliko makubwa kwa upande wa maji. Nikirudia kwa upande wa maji vijijini, napongeza na naomba suala hili la uanzishwaji wa *RUWASA,* uwe wa haraka lakini pia kwenye jambo hilo kanuni zake zitoke mapema.

Mheshimiwa Spika, ombi langu lilikuwa ile shilingi 50 ambayo tulikuwa tunasema iende kwenye Mfuko wa Maji, narudia tena kwamba iende kwenye *RUWASA* yaani maji vijijini. Ikienda huko ambapo kuna changamoto kubwa huu Mfuko mwingine wa Maji mkubwa utaendelea kupata kutoka kwenye vyanzo mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bado naendelea kuomba tuongeze na shilingi 50 nyingine ili iwe 100. Hata ukiangalia kwenye mtiririko, fedha nyingi ambazo zimekwenda huko

vijijini ndiyo hiyo shilingi 50 ambayo tulitenga kwenda huko na bajeti ya kawaida pesa iliyoenda ni kidogo sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia Serikali iangalie tutakapofika kwenye bajeti iendelee kuondoa kodi na tozo mbalimbali katika kuagiza mitambo ya uchimbaji maji, mitambo ambayo inaweza kutengeneza mabwawa na malambo mbalimbali ili tuwe na uvunaji wa maji. Tukivuna maji katika maeneo mbalimbali kwanza tutaondoa uharibifu unaotokea kwenye miundombinu ya barabara, reli, lakini yale maji yatatumika kwenye kunywa binadamu na mifugo, ufugaji wa samaki na kwa matumizi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kama walivyosema pia watu wa Maliasili, ni muhimu sana tuhakikishe kwamba Mto Ruaha Mkuu unaendelea kutiririka. Njia pekee sisi kwenye umwagiliaji lazima twende na mambo ya kisasa, mambo ya teknolojia mpya, tukitumia teknolojia ile ya zamani ya kumwagilia kwa kujaza ardhi yote ijae maji iwe kama bwawa ndiyo upande mpunga au mazao mengine, tuondokane na huko tutumie *drip irrigation.*

Mheshimiwa Spika, tukitumia *drip irrigation,* mahali ambapo una maji ya eka tano kwa kumwaga kwenye shamba zima kwa *drip irrigation* utamwagia eka 20. Kwa hiyo ukiwa na eka moja ya kawaida utafanya eka tano. Kwa hiyo, tunaweza kutumia maji kidogo lakini kwa kutumia teknolojia tukapata mashamba makubwa mengi zaidi ambapo kutakuwa na ufanisi mkubwa na ule mto ukiendelea kutiririka, *Stiegler's Gorge* pia itaweza kufanikiwa kwa sababu lazima tuhakikisha maji yanatembea ili *Stiegler's Gorge* iweze kupata maji ya uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mbali na hiyo, kwa upande wa utalii, naipongeza Serikali kwa kazi kubwa na naomba hizi ndege ambazo tumenunua sasa ziendelee kufanya kazi na ziweze kutangaza nchi yetu ili kuleta mafanikio. Ombi moja tuangalie *charges* mbalimbali ambazo zipo katika viwanja vyetu, kwa nini bado gharama zetu za usafirishaji, hasa kwenye mazao ya kilimo, maua zinakuwa juu na badala yake

kupelekea kupitia Kenya. Kwa hiyo, Wizara zote zikishirikiana naamini tutapata mafanikio. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ombi lingine kwa ujumla kwenye kilimo, mifugo na maji huko kote tuangalie. *Blue print* ile tuliyoileta hapa Bungeni na Serikali iliahidi itaifanyia kazi bado uzalishaji wetu gharama yetu iko juu sana; *regulatory bodies* zina-*charge* gharama nyingi sana na ndiyo maana inafanya biashara zetu zote hazikui, haswa viwanda ambavyo vinachakata mambo mbalimbali ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye utalii bado wamekuwa na changamoto kubwa, wameendelea kupigwa faini za ajabu. Mtu akikutwa na nyama ambayo haina *label* ambapo sisi tunahamasisha wafugaji wadogo wadogo wafuge kuku, samaki wakiuzwa kwenye zile *hotel* wanapigwa faini ya shilingi milioni moja, milioni tano, milioni 20, hilo jambo naomba lifike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, juzi tu, halina siku mbili jirani na Jimbo la Babati Vijijini hoteli moja imepigwa faini ya shilingi milioni moja kwa ajili ya kutoa nyama kwenye *fridge* ili iyayuke (*defrost)*. Wamekata tamaa wanauliza wawe wanaagiza kutoka sokoni au buchani mtalii akija ndiyo tuweze kuwapikia watu? Naomba tusifike huko, naamini Serikali hii itaweza kuleta mabadiliko. Juzi kwenye *briefing* tuliambiwa kwamba suala hili limesitishwa lakini naweza kuleta ushahidi kwamba bado linaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nipongeze kwamba sasa tuna Waziri wa Uwekezaji. Naamini Waziri huyu akikaa pamoja na Mawaziri wote wa Kilimo, Mifugo, Uvuvi tutaweza kufanya kazi kubwa na kuleta mabadiliko.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo naunga mkono hoja, ahsanteni sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Jitu Soni. Sasa naomba nimuite Mheshimiwa Timotheo Mnzava, Mbunge wa Korogwe Vijijini, dakika kumi.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Nitumie nafasi hii kwanza kabisa kumshukuru Mungu ambaye anatupa uzima, pia nitumie nafasi hii kuzishukuru na kuzipongeza Kamati zote mbili ile ya Kilimo pamoja na Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Spika, ningeomba kuchangia kwenye maeneo machache. Ningeomba nichangie kidogo kwenye utalii na baadaye nitaenda kuchangia kidogo kwenye eneo la ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye eneo la utalii, tulipokuwa kwenye Kamati tumepata taarifa na tumetembelea Mradi huu wa *REGROW.* Ni mradi mzuri ambao utasaidia nchi yetu kuinua utalii kwenye maeneo ya Kusini mwa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba kushauri tu, ilizungumzwa asubuhi hapa, tunapotaka kuinua watalii kwenye maeneo ya Kusini lazima twende sambamba na kuangalia namna ya kuboresha na kusimamia uhai wa hizi hifadhi zetu. Imezungumzwa kuhusu Hifadhi ya Taifa ya Mikumi kuhusu ile barabara, barabara ile ina madhara mengi. Kwa haraka haraka kuna changamoto kama nne zinazosababishwa na barabara hii. Changamoto ya kwanza inarahisisha sana shughuli za ujangili na inasababisha uwepo wa takataka ambazo nyingine ni hatari kwa maisha ya wanyama wenyewe. Taarifa tuliyopewa ni kwamba kuna wastani wa kilo 318 za takataka kwa siku ambazo zinazalishwa kutokana na kuwepo na barabara katikati ya hifadhi.

Mheshimiwa Spika, changamoto nyingine ni kugongwa kwa wanyama. Mwaka 2015/2016 wanyama 361 wamegongwa, mwaka 2016/2017 wanyama 218 na mwaka jana Julai mpaka Desemba 2018 ni wanyama 130. Ukichukua mwaka wa fedha wa 2013/2014 mpaka 2017/2018 ni wafanyama 1,062 wamepoteza maisha kwa sababu ya barabara ile. Idadi hii ni kubwa, ni lazima tufanye maamuzi mazito na magumu.

Mheshimiwa Spika, natambua kwamba barabara hii ni ya kimataifa na inawezekana kuna mikataba ya kimataifa ambayo inatuongoza kutumia barabara ile. Lazima ifike mahali Serikali au nchi tuamue na tukapokuja kuamua mambo mazito kwa ajili ya maslahi na ustawi wa nchi yetu haswa maslahi ya hifadhi zetu hatuna haja ya kuangalia sana makele yanayotoka huko nje na maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, tumeona hili kwenye *Stiegler's,* watu wamepiga kelele nyingi sana lakini tumesema kama Taifa tunahitaji kuwa na uchumi wa viwanda na ili tuwe na uchumi wa viwanda tunahitaji kuwa na umeme wa uhakika. Tumeamua hakuna namna nyingine lazima nchi kutekeleze mradi huu kwa ajili ya kupata umeme wa kutosha kwa maendeleo ya nchi yetu. Kama Mheshimiwa Rais alivyoamua chini ya Serikali yake kuendesha mradi ule, naishauri Serikali iangalie kwa jicho la haraka na la dharura juu ya barabara hii ili tuendelee kulinda maisha na uhai wa Hifadhi ya taifa ya Miukumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumze kidogo kwenye sekta ya ardhi. Nitumie nafasi kwa dhati kabisa kumpongeza sana Mheshimiwa wa Ardhi na Naibu wake, wanafanya kazi kubwa tunawaona wanavyoangaika kwenye maeneo mbalimbali ya nchi kutatua migogoro ya ardhi. Nachoomba kuwashauri kama Wizara waendelee kutengeneza utaratibu maalumu na mahsusi wa namna gani ya kuondokana na changamoto za ardhi ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kwenye jambo hili la ardhi nilisikia asubuhi watu wanazungumza hapa na ziko dhana na hisia kwamba kuna watu wanaonewa kwenye mchakato wa kufuta mashamba. Kwanza niseme, nilimshangaa sana kumsikiliza ndugu yangu mmoja akisema kwamba tulikubaliana kwenye Kamati lakini anashangaa huko haikusomwa. Mimi ni Mjumbe wa Kamati na kama ndugu yangu yule angekuwa ni Mtumishi wa Mungu kama nilivyo mimi nisingesema hapa tungeenda kuzungumza kiroho lakini kwa sababu si Mtumishi wa Mungu lazima nitumie nafasi hii

kusema, hatukukubaliana jambo la namna hiyo kwenye Kamati yetu ya Ardhi, Maliasili ya Utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia Mheshimiwa Rais hafuti tu mashamba kwa kukurupuka, mashamba yanafutwa kwa mujibu wa sheria zilizotungwa na Bunge hili. Bahati nzuri ni Mwanasheria na nimepata nafasi ya kufanya kazi kwenye Wilaya zenye migogoro mikubwa sana ya ardhi na nimewahi kuwa Wakili wa watu waliokuwa na kesi dhidi ya Serikali kwa ajili ya kufutiwa mashamba, nafahamu changamoto ilipo. Kama kuna watu wanaobebembelezwa ni watu wenye mashamba, anapewa onyo, anapewa *notice* ya siku ya 90 ili ku-*remedy breach* za *conditions* za hiyo *right of occupancy* aliyoipewa, hawafanyi. *Technique* ambayo inatumika mara nyingi unakuta mtu anakuja dakika za mwisho, siku 90 zimekwisha anaanza kwenda kugusagusa sehemu ndogo anaondoka halafu anasema nimeendeleza, si sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii niseme kwamba nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi aliyoifanya ya kufuta hati za shamba ya baadhi ya wawekezaji kwenye nchi yetu. Ukienda Korogwe leo wananchi wamemwelewa sana Mheshimiwa Rais na wamemshukuru. Bunge hili waliokuwepo muda mrefu ni mashahidi, mtangulizi wangu Profesa Maji Marefu alikuwa kila akisimama analia na mashamba yasiyoendelezwa Korogwe. Leo Mheshimiwa Rais amefuta mashamba watu wanapiga kelele kwa maslahi ya nani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi watu wa Korogwe tunamshukuru Mheshimiwa Rais na tumuombe Waziri wa Ardhi bado kuna mashamba mengine ya akina Chavda yamekaa ni mapori, mpelekeeni Mheshimiwa Rais atafutie wananchi wapate maeneo. Ukienda kule Magoma na Kwa Shemshi kuna ardhi kubwa mashamba yamekaa, hayaendelezwi yamekuwa mapori na wengine wanakodisha, mpelekeni Mheshimiwa Rais atufutie ili wananchi wapate maeneo ya kilimo na makazi. Mimi nawapenda sana wawekezaji lakini lazima tuwe na wawekezaji ambao

wanatutendea haki na wanatendea haki masharti ya umiliki waliyopewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiangalia vizuri watu wanalaumu lakini kama kuna mtu anamwelewa Rais ni mimi, ni Rais anayependa haki na ni asiyemuonea mtu. Mimi ninao ushahidi wa baadhi ya mashamba, kwa sababu michakato inaanzia kwenye Halmashauri, yako baadhi ya mashamba ambayo wenzetu kwenye Halmashauri waliwahi kutengeneza na kupeleka kwa Rais yakafutwe. Hata hivyo, yalipofika Wizarani na Mheshimiwa Rais wakaona utaratibu umekiukwa yalirudishwa na Mhesimiwa Rais, tunataka haki ya namna gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nenda Wilaya ya Arumeru, Mheshimiwa Lukuvi anafahamu liko shamba la *Karamu Coffee Estate*, Halmashauri, Mkoa kote tulipeleka lakini lilipofika juu Rais akasema utaratibu unaonekana hauko sawasawa rudisheni mkarekebishe. Achana na hilo, nenda Kilombero, yuko mtu mmoja alikuwa na nafasi kubwa sana kwenye nchi hii sitamtaja, sasa hivi ni marehemu, Halmshauri walipitisha wakataka yale yafutiwe hati wakapeleka kwa Mheshimiwa Rais akasema hapa kuna uonevu rudisheni, tunataka Rais wa namna gani, tunataka Rais afanye nini tena? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimeona hapa watu wanasema ooh watu wanaonewa, wanasumbuliwa, wameendeleza, nataka niwaambie ndugu zangu kama kuna Rais tunamshukuru watu wa Korogwe ni Mheshimiwa Rais Magufuli. Sisi watu wa Korogwe hatusimuliwi, tumeona wenyewe, mwacheni Mheshimiwa Rais afanye kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wote tunawataka wawekezaji lakini waacheni wawekezaji hao wafuate taratibu, sheria na kanuni za nchi yetu na yule ambaye atakiuka achukulie hatua kama ambavyo hatua zimeendelea kuchukulia. Mheshimiwa Lukuvi nakukumbusha tu tunakuomba Korogwe mashamba ya Chavda, Kwa Shemshi na Magoma mwende

mkampelekee Mheshimiwa Rais, tufute tuwapelekee Watanzania wakatumie ardhi ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hakuna mtu anayepewa haki bila kuwa na wajibu. Sheria ya Ardhi inayowapa watu haki ya kumiliki ardhi inawapa na masharti na mtu asipokiuka masharti nimesema anastahili zake, stahili ni pamoja na hizo. Kwenye suala la mashamba, mimi kama Mjumbe wa Kamati, kama Mwakilishi wa watu wa Jimbo la Korogwe Vijijini tuko na Mheshimiwa Rais na tunampongeza Mheshimiwa Rais kwa jambo kubwa alilolifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeuona ule Mradi wa Kurasimisha na Kumilikisha Ardhi uliokuwa unatekelezwa kwenye maeneo ya kule Malinyi, Kilombero na Ulanga, ni mradi mkubwa. Nimefarijika mradi ule, niliambiwa hata Mheshimiwa Waziri kuwa unasimamiwa na vijana, wamefanya kazi kubwa. Hatusemi kwamba wazee hawafanyi kazi kubwa lakini wale vijana kwenye mradi ule wameutendelea haki wanastahili kupewa pongezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ombi langu kwa Wizara, tuwe na utaratibu wa kuendeleza mradi huu kwenye maeneo mengine. Safari hii tumepata hela za wafadhili hatujui mbele ya safari tutakuwa na hela za wafadhili au tutazikosa. Kwa vyovyote itakavyokuwa mradi ule ni wa muhimu kutusaidia kupunguza migogoro ya ardhi ndani ya nchi.

Mheshimiwa Spika, mwisho naomba nizungumze kidogo kuhusu Hifadhi ya Taifa ya Ruaha. Hifadhi hii ni kubwa, ndiyo hifadhi ya kwanza kwa ukubwa kwenye nchi yetu na Afrika Mashariki. Ni miongoni mwa hifadhi chache ambazo hazijaathiriwa na shughuli za kibinadamu. Kamati imesema kwenye taarifa yake kwamba changamoto kubwa ni kuelekea kukakuka kwa Mto Ruaha Mkuu ambao ndiyo roho ya hifadhi ile. Niiombe Serikali kwenye jambo hili la Hifadhi ya Taifa ya Ruaha ili tunusuru hifadhi ile tunahitaji kunusuru Mto Ruaha Mkuu.

Mheshimiwa Spika, tukisema kunusuru Mto Ruaha Mkuu watu wanafikiria kwenda kuwafukuza watu wanaolima kule kwenye Bonde la Usangu na maeneo mengine. Kama alivyosema mzee wangu, Mheshimiwa Jitu, tunazo teknolojia za kisasa zitumike. Pia changamoto kubwa ukienda kule Mabarali si tu kwamba wanalima mpunga kwa kutumia yale maji, hapana, lakini watu wanashilikia maji kwa kuzua magugu na vitu vingine hata baada ya muda wa kilimo cha mpunga. Wizara ya Maliasili ishirikiane na watu wa Ardhi na watu wa Kilimo tuwe na teknolojia nzuri ili yale maji yakimaliza kufanya shughuli za kilimo basi yaachiwe yaendelee kutiririka kwenye mto ili usiendelee kukauka. Tukifanya hivyo tutakuwa tumeisaidia sana Hifadhi ya Taifa ya Ruaha na nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE.TIMOTHEO P. MNZAYA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja za Kamati zote mbili na mapendekezo yake, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Timotheo Mnzava, Mbunge wa Korogwe Vijijini. Mimi nikiwa hapa ni mchango wako wa kwanza, kwa kweli hii bunduki mpya ni hatari kabisa. *(Makofi)*

Tunaendelea na Mheshimiwa Magdalena Sakaya, atafuatiwa na Mheshimiwa Ryoba Chacha. *(Makofi)*

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, nami nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia kwenye taarifa mbili za Kamati. Nazipongeza taarifa zote mbili ile ya Kilimo na ile ya Maliasili ambayo mimi ni Mjumbe wake.

**SPIKA:** Mheshimiwa Sakaya, nilikuwa nakukumbusha una dakika tano tu, endelea.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais ameona kilio cha wakulima na wafugaji ambapo wamenyanyaswa sana hasa wafugaji na wameonewa kwa miaka mingi na ametoa tamko na ameagiza Mawaziri walishughulikie suala hili kwa haraka. Tamko hili linaweza kuchukuliwa tofauti na likichukua muda bila kufanyiwa kazi watu wataingia ndani ya hifadhi na kuharibu uhifadhi wakisema kwamba walikuwepo miaka mingi. Kwa hiyo, tunaomba Mawaziri waliopewa jukumu hili wachukue hatua za haraka kuhakikisha kwamba tamko hili la Mheshimiwa Rais linafanyiwa kazi kwa haraka ili kuokoa uhifadhi.

Mheshimiwa Spika, tunapoongea yapo maeneo ambapo watu walikuwa wametoka miaka mingi kwa mfano Bonde la Kilombero lakini baada ya lile tamko tunaona wanarudi kule kwenda kulima kwa matreka usiku na mchana. Kwa hiyo, hili litakuwa ni tatizo kama hatua za haraka hazitachukuliwa, tutakuwa tunakwenda kuharibu uhifadhi. Naomba tamko hili lifanyike kwa uhakika ili migogoro ya wakulima na wafugaji iweze kuisha na waweze kupata maeneo ya kufugia na kulima.

Mheshimiwa Spika, niende kwenye *National Housing.* Kwa miaka mingi *National Housing* imefanya kazi nzuri na baada ya kuwepo kwa Mkurugenzi Mkuu aliyeondoka, Ndugu Mchechu. *National Housing* kwa mwaka 2010 mpaka 2018 wameweza kutengeneza mtaji kutoka shilingi trilioni 4.3 na walikuwa na *projection* ya kwenda kwenye shilingi trilioni 7 mwaka 2025 lakini *National Housing* leo ni kama iko *stacked,* imetulia. Walikuwa na miradi mingi ya *strategic* kama Mradi wa Kawe na Morocco lakini miradi ile imesimama wakati wameshawekeza fedha nyingi na mingi iko zaidi ya 40% ya utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, tunaiomba Serikali kwa kuwa wamezuiliwa sasa kuchukua mikopo kuendeleza miradi ile

Serikali ione mikopo iliyowekezwa pale inazalisha riba waweze kutoa kibali waweze kuiendeleza ili kuokoa fedha ambayo imewekwa pale lakini pia *National Housing* iendelee. Tusipoangalia Shirika ambalo tumelipongeza miaka mingi litakufa kwa sababu tu ya watu ambao walikuwa wana maslahi yao.

Mheshimiwa Spika, tunajua wako watu wengi sana walitamani *National Housing,* miaka mingi lilikuwa ni shirika ambalo linamilikiwa na watu, nyumba zilikuwa hazijulikani, ni kama lilikuwa si shirika la umma, walikuwa wanamiliki watu mikononi. Baada ya kuonekana kwamba nyumba sasa zimetambuliwa ni nyumba za umma, shirika linafanya kazi, linapendezesha miji yetu mikubwa, watu walipiga vita kubwa sana na wamefanikiwa. Serikali iangalie, si kila ushauri waupokee waangalie ushauri ambao unawezesha kupiga hatua kwenda mbele. Wengine walitamani tu kwamba viongozi waliokuwa wanasimamia Shirika lile wakae pembeni ili waendelee kupiga *deal* na huu ndiyo uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumzie shamba la miti la *Sao Hill.* Tumekwenda *Sao Hill* na nashukuru *TFS* kwa kazi nzuri sana lakini zipo changamoto. Tunaiomba Serikali, kuna utitiri mkubwa wa kodi zaidi ya 32 kwa wafanyabiashara. Tunajua wafanyabiashara wa Taifa hili ni wadau wakubwa wa maendeleo na Mheshimiwa Rais kila siku anasema, tunaomba kwanza kodi zile zipungue.

Mheshimiwa Spika, lakini kingine, kuna kodi moja ambayo inaitwa kodi ya *cess.* Bungeni mwaka jana tulibadilisha sheria ya *cess* kutoka 5% kwenda 3% lakini Mkoani Iringa bado *cess* ya mazao bado ni 5%. Si hilo tu wanatoza mara mbili; mti ukiwa porini unatozwa *cess* 5% na ukitolewa mbao unatozwa *cess* 5%, Halmashauri na *Sao Hill* wote wanatoza. Wafanyabiashara wanaumizwa na hawa ndiyo wadau wa maendeleo. Tunaomba kwanza *cess* iwe moja lakini pia kodi zipungue ili waweze kuchangia vizuri maendeleo.

Mheshimiwa Spika, tumekwenda pale kwenye kiwanda tumeangalia, zaidi ya malori 20 yana nguzo za *REA* yamekaa mwezi mzima yamezuiliwa kuondoka kwa sababu *TANESCO* inatakiwa kulipa *cess* kwa mara ya pili wakati nguzo hizo zimelipiwa *cess* zikiwa kule *Sao Hill. Sao Hill* inakusanya zile *cess* inatoa *percent* inapeleka kwenye Halmashauri. Leo mbao ziko kiwandani tayari kusafirishwa Halmashauri inasema hakuna kutoa nguzo mpaka ilipwe tena *cess* nyingine, kwa nini kuwe na *double taxation?* Tunaiomba Serikali ihakikishe kunakuwa na *cess* moja lakini pia kodi ziondolewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni la *LMD*, kuna fedha ambayo wafanyabiashara wenyewe wamemua kuchanga...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sakaya, dakika tano zimeisha, pole sana, najua, ahsante sana. Nilishakutaja Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha dakika kumi.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana. Nianze kwa kunukuu kifungu cha Biblia kinasema, nchi na vyote viijazavyo ni mali ya Bwana, dunia na wote wakaao humo. Sehemu nyingine Biblia inasema Mungu ndiye anayetawala katika falme za wanadamu na yeye huamua kumpa mtu awaye yote amtakaye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge mwaka 2015 ulifanyika Uchaguzi Mkuu na kulikuwa na miamba miwili iliyokuwa inamenyana; alikuwepo Mheshimiwa Magufuli na Mheshimiwa Lowassa. Mimi nilikuwa Upinzani wakati huo; kwa kweli niwaambie Mheshimiwa Lowassa alipata umaarufu mkubwa sana hususani kwa wafugaji kwamba kwa kuwa yeye ni Mmasai anatokea Umasaini kwa wafugaji angekamata nchi hii wafugaji wangepata neema sana, lilimpa umaarufu mkubwa sana na hata huko nakotoka wafugaji walimwanini sana.

Mheshimiwa Spika, nataka niwambie kama kuna jambo ambalo Mheshimiwa Rais Magufuli amelifanya la kihistoria katika nchi hii ni jambo la kukubali kupitia upya *GN* ili wafugaji na wakulima wapate maeneo kwa ajili ya kulisha mifugo yao. Kwa wale ambao si wafugaji hawawezi kujua kwa sisi tunaotokea maeneo ya ufugaji, tunafahamu taabu ambayo wafugaji wanazipata katika nchi hii. *(Makofi)*

**TAARIFA**

**MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Haya taarifa Mheshimiwa nimekuona.

**MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA:** Mheshimiwa Spika, naomba nimweleze mtoa hoja kwamba aliyekuwa Mgombea wa Kiti cha Urais kupitia tiketi ya Chama cha CHADEMA siyo Mmasai. Ni Mmeru asilimia 100 aliyelelewa katika Wilaya ya Jamii ya Kimasai. *(Makofi)*

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Spika...

**SPIKA:** Jamani, kuna anayebisha huku hiyo taarifa? Endelea Mheshimiwa. *(Kicheko)*

Endelea Mheshimiwa.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Naipokea taarifa hiyo, nilikuwa sijui, ahsante. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati nikiwa pale ng'ambo mwaka 2018, nilitoa shilingi kwa ajili ya kusimamisha zoezi la kuweka vigingi kwenye vijiji vilivyozunguka hifadhi mbalimbali ikiwemo hifadhi ya Serengeti. Wakati ule zoezi lilikuwa likiendelea kule Tarime kwenye vijiji vya kando kando ya hifadhi vikiwemo Vijiji vya Serengeti, Merenga, Machochwe, Nyamakendo, Mbalibali, Visarara, Bonchugu, Pakinyigoti, Miseke na kadhalika. Kama kuna wananchi wamefurahi

baada ya tamko la Rais, ni Wananchi ambao wanazunguka maeneo haya.

Mheshimiwa Spika, ukikumbuka, Hifadhi za Serengeti na hifadhi nyingine zilianzishwa kwa mujibu wa Sheria na *GN* na kilichokuwa kinatokea katika maeneo haya, walikuwa wanapanua mipaka na kwa kweli kulikuwa na *confusion* kati ya TAMISEMI na Wizara ya Maliasili na Utalii, kwamba mipaka inawekwa kwenye vijiji, wananchi wanyang'anywa maeneo yao. Kwa kweli wananchi wamefarijika sana. Kwa hiyo, nina kila sababu ya kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli kwa hiki alichokifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwaambie, Tanzania tumepata neema ya kuwa na Rais ambaye pengine akiondoka madarakani ndio Watanzania watakuja wakumbuke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwaambie, wakati nikiwa ng'ambo ile, Mheshimiwa Rais, Dkt. Magufuli alikuwa anatunyima usingizi kweli kweli. Ndiyo ukweli! Kwa sababu kule ng'ambo tulikuwa tumezoea ufisadi. Yaani ikitokea *issue* ya ufisadi, tunapiga kelele kweli kweli. Sasa jamaa amekuja amekaba hakuna cha ufisadi tena; na amekaba kweli kweli. Ukijulikana umefanya ufisadi anatumbua, hana mswalie Mtume, hata wao wanajua. Kwa hiyo, niwaambie tumepata Rais...

**TAARIFA**

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Taarifa.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Spika, wakati mwingine niseme ni maombi ya Watanzania, wewe ni shahidi.

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Taarifa iko wapi?

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Taarifa huku.

**SPIKA:** Ooh, nimekuona Mheshimiwa.

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** *Yes,* nilitaka tu nimpe taarifa mwenzangu pale kwamba alisahau kwamba tulipokuwa ng'ambo ile, wiki mbili tu baada ya kuingia Bungeni tulibadilika na ikawa ajenda ni kutetea ufisadi. Ikafika mahali tukapata ugonjwa ambao haueleweki. Leo tunatetea ufisadi, leo wana-CCM fulani wakianza kugombana ndani sisi ndiyo agenda yetu, lakini imefika mahali hata wale wezi wa ardhi ndiyo ndugu zetu na ndiyo wafadhili wetu. *(Kicheko/ Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**Spika:** Mheshimiwa Marwa, unapokea hiyo taarifa?

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Spika, napokea taarifa yake, ni kweli, si tulikuwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama kuna wakati ambapo…

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Hajaongea chochote bado, ngoja aongee kidogo basi halafu ndiyo utasema taarifa.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Spika, ameshaongea tayari. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Subiri aongee basi.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Spika…

**SPIKA:** Endelea Mheshimiwa Marwa kwanza basi. *(Kicheko)*

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Spika…

**SPIKA:** Ukiongea saa hizi utakuwa unampa taarifa yule kule ambaye siyo mchangiaji. Wewe mwache kwanza. Endelea Mheshimiwa Marwa. *(Makofi)*

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Spika, naomba unilindie muda wangu. Kwa hiyo, ukweli ni hivi, 2010 Watanzania walikuwa wanaomba, yaani unajua inatakiwa tupate Rais wa kufanya maamuzi magumu.

Mheshimiwa Spika, unakumbuka ilifikia sehemu, sisi ambao tulikuwa huko duniani hatujaja humu, wananchi walikuwa wanasema, yaani tunatakiwa tupate Rais kichaa ili hii nchi inyooke. Nchi sasa hivi imenyooka. Nchi imenyooka Mura, wewe vipi? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, ngoja niwaambie, hivi kwa mfano, nani angeweza kuanzisha Bwawa kwenye *Stiegler's Gorge?* Tuseme ukweli, nani? Yaani nchi za Ulaya hazitaki, Marekani haitaki, sijui nani hataki, nani? Huyu jamaa ana maamuzi magumu, tumuunge mkono. Umeme wa *Stiegler's Gorge* ni kwa ajili ya maslahi ya Watanzania. Tutapata umeme kwa *cheap price,* wewe hutaki hiyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, unajua wanasiasa wengi wanapenda kitu kinaitwa *cheap politics*. Mheshimiwa Dkt. Magufuli hapendi *cheap politics* anafanya *hard politics*. Hakuna ambaye angeweza kujenga reli, hakuna ambaye angenunua ndege. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, unajua wanasiasa wengi, hususan wa ng'ambo ile wangependa wajenge madarasa, vitu vidogo vidogo tu, lakini mambo mazito yenye kulinufaisha Taifa kwa miaka mingi, hakuna ambaye angethubutu kufanya. Kwa hiyo, ukiona tumehamia upande huu, tumeona mbali. *(Makofi)*

*Mheshimiwa Spika, ile hoja yako ya miaka saba, ile tumpe Magufuli hata miaka saba aendelee. Hivi...*

***SPIKA:*** *Waheshimiwa Wabunge, wanaoafiki!*

**WABUNGE FULANI:** *Ndiyoooooo.*

***SPIKA:*** *Hapana, hiyo futa kwenye Hansard. Endelea Mheshimiwa. (Makofi)* **[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana, naona wamekaa kimya, wanaelewa ndiyo ukweli.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine nilitka niongelee ni jambo la *cultural tourism. Cultural tourism* kwa maeneo ya Serengeti inakuwa *affected* na *single entry.* Naomba kupendekeza kupitia Kamati ya Maliasili na Utalii, ongezeni jambo la *single entry, is a big challenge* kwa watu wetu. Watalii wanaishia hifadhini. Watalii wanatakiwa wakifika hifadhini, waende kutembea kwenye vijiji.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Marwa.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naunga mkono hoja*. (Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Haya, Waheshimiwa Wabunge sasa ni wakati wa Mheshimiwa Pascal Haonga. Una dakika 10.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mgeshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Naomba kuchangia hizi Kamati mbili, lakini nitajikita zaidi kwenye Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji. Naomba nianze kwa kusema kwamba Sekta ya Kilimo imeajiri zaidi Watanzania kwa asilimia 70, lakini pia inachangia zaidi ya asilimia 30 ya *GDP,* lakini sekta hii pia inachangia chakula kwa nchi yetu kwa zaidi ya asilimia 100, lakini pia Sekta ya Kilimo inatoa malighafi za viwandani kwa zaidi ya asilimia 65.

Mheshimiwa Spika, pamoja na umuhimu wa Sekta ya Kilimo lakini imesahauliwa na Serikali hii ya Awamu ya Tano, leo hakuna masoko ya mazao ya wakulima. Leo Serikali inakwenda kununua kwa mfano, korosho. Badala ya kutafuta masoko ya mazao, kama masoko ya korosho, mahindi, pamba, mbaazi, tumbaku na kahawa, leo Serikali inakwenda kununua mazao. Haitaweza kununua mazao yote kwa sababu nchi hii tuna mazao mengi sana ambayo kwa kweli bei yake iko chini sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niseme tu kwamba mimi naishauri Serikali ijikite kutafuta masoko ya mazao. Huu ndiyo utakuwa mwarobaini kuliko kwenda kununua mazao, haitaweza, zoezi hili ni gumu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunafahamu kwamba mahindi tuna miaka miwili sasa hali siyo nzuri, bei iko chini; tumbaku iko kwenye maghala kwa mura mrefu hainunuliwi; mbazi kutoka kilo shilingi 2,000/= tunafahamu kwamba shilingi 80/= hadi shilingi 100/= hali ni mbaya. Leo wakulima nchi nzima wanalia. Kwa hiyo, Serikali imejikita zaidi kwenda kutafuta masoko ya mazao kuliko kwenda kununua mazao kwa sababu haitaweza.

**TAARIFA**

**MHE. ALMAS A. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Pascal, kuna taarifa kwako.

**MHE. ALMAS A. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, naomba nimpe taarifa msemaji anayeongea sasa, hakuna tumbaku kwenye maghala, tumbaku yote tumeshauza. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Pascal, unapokea taarifa hiyo?

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Spika, ngoja nimwache nisimjibu, kwa sababu wakati mwingine unaacha wafu wazikane wao wenyewe. Kwa hiyo, naomba nisimjibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimekuja kuzungumzia maslahi ya Watanzania. Leo ninavyozungumza nawe kwa mfano kwenye zao la kahawa, nami nilileta hoja binafsi japokuwa haikupata kibali cha kuingia Bungeni, lakini nilileta hoja binafsi ya kuhusu zao la kahawa. Kinachoendelea kwenye kahawa, hali ni mbaya kuliko kawaida.

**KUHUSU UTARATIBU**

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Kuhusu utaratibu.

**SPIKA:** Kuhusu utaratibu

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nasimama kwa Kanuni ya 64(1)(g) kwamba *"Mbunge hatatumia lugha ya kuudhi au inayodhalilisha watu wengine."* Neno wafu wamalizane wao wenyewe, siyo lugha fasaha inayotumika hapa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Pascal neno hilo limewakera na kuwaudhi baadhi. Busara ni kwako, unasemaje?

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba kuna watu wengine hawafahamu misemo na methali na kadhalika. Kwa hiyo, naomba niendelee. Labda ni vizuri tu kwa sababu nafahamu yeye alikuwa ni Mtangazaji, nadhani vitu hivyo anavifahamu vizuri sana. Haitakiwi tupoteze muda mwingi sana kwenye hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kungumza hivyo, naomba niendelee sasa kwa ruhusa yako.

**SPIKA:** Tuvumilie.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Naomba niendelee kwa sababu alikuwa wanatupiga, sisi hatuwapigi, tumeamua kuwasemehe.

**SPIKA:** Endelea, ila kuna neno moja umesema ulileta hoja binafsi.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Spika, ndiyo.

**SPIKA:** Halafu ikakataliwa. Nikuhakikishie mezani kwangu sijawahi kuona hoja binafsi kutoka kwako.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Spika, nita…

**SPIKA:** Endelea tu kuchangia, lakini sijawahoi kuiona.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Ahsante. Nikimaliza nitakuletea zile nakala ambazo nilikuwa najibiwa kutoka kwenye Ofisi ya Katibu wa Bunge. Nitakuletea Ofisini kwako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo kwa mfano kwenye zao la kahawa, Serikali imeamua kuyakataza Makampuni yaliyokuwa yananunua kahawa yote, yamezuliwa, badala ya kuruhusu soko huria; kwa sababu tunaamini kwamba soko huria ndilo ambalo linaleta bei nzuri kwa wakulima. Tungeruhusu Makampuni yanunue, yashindane na hivyo Vyama vya Msingi vya Ushirika vilivyoanzishwa ili mwisho wa siku mkulima aweze kunufaika na bei nzuri ya kahawa.

Mheshimiwa Spika, kabla hatujawa na *AMCOS* (Vyama vya Msingi vya Ushirika) bei ya kahawa mwaka 2017 tuliuza shilingi 4,000/= na kitu, hadi shilingi 5,000/= kwa kilo moja, lakini baada ya kuanzisha, tumeuza kilo moja ya kahawa hadi shilingi 1,800/=. Kwa hiyo, nashauri, ni vizuri Serikali ikaruhusu soko huria kwenye zao la kahawa na wakati mwingine kwa sababu pembejeo ziko juu, mkulima analima kwa jasho sana, anapouza ndipo Serikali inapojitokeza inasema usipeleke kahawa yako Uganda, sijui usipeleke wapi. Nchi hii kuna matatizo makubwa sana ya kilimo. Naiomba Serikali kwa sababu tayari ndiyo inayoongoza, ijitahidi kutatua matatizo ya Watanzania. Kama haiwezi, basi iwaachie wengine ambao wako tayari kuongoza nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimia Spika, jambo lingine, ili tuweze kuondokana na bei ndogo; badala ya Serikali kwenda

kununua mazao ambayo haitaweza, ni vizuri Serikali ikatengeneza utaratibu wa kuweka ruzuku kwenye mazao ya mkakati yale ambayo yako matano. Mazao ya mkakati kuna kahawa, pamba, chai, tumbaku na mazao mengine yale matano ya mkakati, Serikali ingeweza kuweka utaratibu kwamba bei inaposhuka, Serikali iweze kuongeza kile kiasi ambacho inaamini kwamba itamparia faida mkulima na siyo kwenda kununua. Kununua, hawataweza kutoa fedha za namna hiyo, lakini kuweka ruzuku inawezekana kabisa. Baadhi ya nchi zimefanikiwa, Indonesia wamefanikiwa na maeneo mengine mbalimbali wamefanikiwa kwenye suala hili la kuweka ruzuku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kuhusu kujenga viwanda vya mbolea. Nataka kuuliza, hii ilikuwa kwenye mpango mkakati wa viwanda wa 2025, lakini pia hata kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi hili lipo. Ujenzi wa viwanda, kiwanda kile cha mbolea kule Kilwa Masoko tumefikia wapi? Pale hamna tofali hata moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashauri, Serikali ambayo tunasema kwamba Watanzania asilimia 70 wanategemea kilimo, hawa watu wanahitaji kuwa na kiwanda. Sasa mpango wa Kiwanda cha Mbolea pale Kilwa Masoko tumefikia hatua gani? Mbolea tunayoagiza nje ya nchi ni zaidi ya asilimia 95.

Mheshimiwa Spika, Kiwanda cha Minjingu ameongea Mheshimiwa Jitu Soni pale. kinazalisha asilimia tano tu. Sasa Serikali iangalie namna ya kuweza kujenga kiwanda cha mbolea na mbolea itashuka bei na baada ya hapo mwisho wa siku tutazalisha chakula cha kutosha, tutazalisha mazao ya kutosha na wakulima wetu watakuwa na hali nzuri kuliko wakati mwingine wowote ule. Kwa hali jinsi ilivyo sasa, tukiendelea kuagiza mbolea, hatutafika popote pale.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, naomba nizungumzie suala la kupeleka fedha kidogo za miradi hasa kwenye miradi ya maji. Kuna fedha zilikuwa zimetengwa, shilingi bilioni 299.9 zilitakiwa zipelekwe kwenye miradi ya maji.

Hadi sasa zimepelekwa shilingi bilioni 1.67 sawa na asilimia 0.6 kutoka Hazina kwenda kwenye miradi ya maji. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Du!

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Kutekeleza kwa asilimia 0.6 hili ni anguko kubwa sana kwa Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Niseme tu kwamba, ni vizuri Serikali iangalie yale mambo ya muhimu, ione namna ya kuweza kupeleka fedha. Kwa mfano, kulikuwa na...

**SPIKA:** Mheshimiwa Pascal huwa ni vizuri sana ukitumia *data* ukaweka na *reference* yako, yaani umezitoa wapi. Itasaidia sana. Endelea tu kuchangia, lakini huwa ni vizuri ukisema *reference* yako.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Hizi ni takwimu kutoka Kwenye Kamati ya Bajeti na zimetolewa Bungeni hapa na Wajumbe wa Kamati ya Bajeti wapo, nataka kwenye hilo nikuondolee hofu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwenye mambo ya muhimu kama haya, kama tunaweza kutenga shilingi bilioni 299.9 kulepeka shilingi bilioni 1.67 sawa na asilimia 0.6 huku ni kuwachezea Watanzania na mchezo huu wa kuwachezea Watanzania ni vizuri tukaacha. Kuna haja gani ya kuhangaika na *SGR* Watanzania hawana maji? Kuna haja gani ya kuhangaika na *Stiegler's Gorge* Watanzania hawana maji?

Mheshimiwa Spika, ni vizuri tukaanza kugusa maisha ya Watanzania moja kwa moja kwa sababu kama mtu hana maji, huyo mtu leo unamwambia apande ndege inakuwa ni vigumu sana.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Pascal, hiyo ni kengele ya pili.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie dakika moja kwa sababu nimeingiliwa sana, naomba kwa hekima yako, kwa kiti chako...

**SPIKA:** Ni kengele ya pili Mheshimiwa, muda hauko upande wako tunashukuru. *(Makofi)*

Nilitaka kusema tu kama Kamati ya Bajeti mpo, kama *data* hizi zinakuwa zina shida, ni vizuri kuzirekebisha kuliko kumwachia Waziri peke yake endapo kweli; maana zinanipa taabu kama ni kweli, sijui. Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti.

**MBUNGE FULANI:** Siyo kweli.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:** Mheshimiwa Spika, msemaji anayezungumza amejaribu tu kusema kitu ambacho hana uhakika nacho. Kwa mujibu wa takwimu zilizoletwa na Serikali mbele ya Kamati yetu ya Bajeti, fedha zilizopelekwa kwenye miradi ya maji ni shilingi bilioni 68; ni kama 69 hivi kwa ujumla wake. Ndizo fedha zilizopelekwa kwenye bajeti ya maji. Ndiyo maana Wakandarasi wanalipwa; na ndiyo maana miradi mbalimbali inaendelea hata kule Kibakwe inaendelea kutekezwa na tumelipa. Shida moja tu ni kwamba amekariri kisehemu kimoja tu, lakini hakuiangalia ile taarifa yetu na maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, hiyo ndiyo taarifa ya Kamati. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya. Mheshimiwa Haonga umeona Bwana? Unasoma taarifa kwa makengeza. Anayefuata Mheshimiwa Serukamba.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Spika, kwenye miradi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Peter Serukamba, tafadhali.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Spika, nami nawapongeza viongozi wa Kamati zote mbili walioleta *report* yao hapa ndani. Naomba nijadili zaidi kwenye kilimo. Toka tumepata uhuru...

**SPIKA:** Dakika 10.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Spika, toka tumepata uhuru kuna mazao ndiyo mazao ya kimkakati Tanzania kwa maana ya kahawa, katani, chai, korosho pamoja na pamba pamoja na *palm oil*. Nimeamua kuangalia uzalishaji wetu wa haya mazao na ili twende mbele kiuchumi lazima tuongeze uzalishaji. Uzalishaji wa kahawa Tanzania ni tani 100,000; kwa nchi 10 bora duniani Brazil wanazalisha tani 2,500,000; Vietnam tani 1,650,000; Colombia tani 800,000; Indonesia tani 600,000; Ethiopia ambayo ni ya tano duniani inazalisha tani 4,84000.

Mheshimiwa Spika, kwa nini nasema haya? Nataka sasa kama Taifa tuanze kujielekeza kwenye uzalishaji, tuache kuhangaika na kutatua matatizo ya siku, maana mwaka jana 100,000, mwaka huu 100,000, mwaka keshokutwa, hii siyo sawa. Leo hii tuna matatizo ya fedha za kigeni, tutazipataje; ni kwa ku- *export* mazao yetu haya ya biashara. Ili tuweze kuongeza uzalishaji, najua hili jambo wengi hawalipendi, lakini ni lazima tuanzishe mashamba ya biashara, lazima tuanzishe *commercial farming in* Tanzania kwa sababu ardhi tunayo, maji tunayo, lakini tusipo-*embrace commercial farming* na *commercial farming* ina faida zifuatazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza watahangaika na ubora; pili, watahangaika na *quantity;* watahangaika kutafuta soko, watatoa ajira, watatoa mafundisho, watatoa pembejeo, watatafuta za kwao, lakini watalipa kodi, lazima kama Taifa tuseme tunapoenda ndani ya miaka mitatu ijayo,

tutaondoka kwenye kahawa kutoka 100,000 kwenda 500,000 na unajua maana yake nini? Maana yake unaingiza fedha nyingi za kigeni hata bei ya dunia ikianguka kwa sababu *quantity* inakubeba bado itakusaidia kama Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitakwenda kwenye katani, katani iliyokuwa inazalishwa miaka ya 1970 leo haipo, leo katani duniani bei imepanda, lakini tunazalisha tani 50,000, lakini tuna uwezo wa kuzalisha tani 1,000,000, tufanye nini? Ni lazima tuhangaike, tuondoke kwenye 50,000 ili twende kwenye tani angalau 500,000 na tukifika tani 1,000,000 maana yake tutaingiza dola milioni 700 kwenye uchumi wa Tanzania, lakini ili tufike tuhakikishe watu wengi *household* nyingi zinalima mkonge, tuhakikishe *financing* inakaa vizuri. Lakini ili *commercial farming* ifanye kazi lazima tulete wanasema Wazungu *legal framework with clarity.*

Mheshimiwa Spika, Mfalme wa Dubai wakati anafanya mabadiliko Dubai Baktoum familia yake walimfuata wakasema wewe mzee mbona unagawa ardhi yetu ya Dubai kwa Wachina, Wahindi na Wazungu; aliwaangalia akawajibu jambo moja tu, siku ambapo Mchina na Mhindi yuko *Airport* anaondoka na ghorofa lake mniite, hata sisi akija mtu tukampa ardhi, akalima, tukiamua kumfukuza haondoki na ardhi hawezi kuibeba, kwa hiyo lazima tubadilishe *mindset* kwenye *agriculture, we can't go like this*.

Mheshimiwa Spika, nitakwenda kwenye chai, Tanzania tunazalisha tani 19,000 tu, wakati Wakenya ambao wana eneo dogo kuliko sisi wanazalisha tani 300,000 na leo Kenya ni ya tatu kwa chai duniani, maana yake ni nini; kwa sababu wame- *embrace* mashamba makubwa, wamewekeza na ukitoka tani 18,000 ukafika tani 300,000 tu, maana yake unaingiza kwenye *economy* dola nyingi sana na *GDP* ya kilimo itatoka kutoka asilimia 30 mpaka 50 kwa sababu tunayo ardhi, tuna watu na tuna mvua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitakwenda kwenye korosho, nasikiliza kelele za korosho, unajua maana yake nini, ni kelele

za kitu kidogo wanataka kupigania watu wote. Tanzania tunazalisha tani 210,000, lakini kwenye korosho Vietnam wanazalisha tani milioni 1,200,000; Nigeria tani 900,000; India tani 600,000; Cote d'Ivoire tani 600,000; maana yake ni nini? Sisi Tanzania tunayo *capacity* ya kutoka 200,000 kufika 1,000,000. Leo ukitoka hapa 200,000 ukafika 1,000,000, 200,000 unapata dola milioni 600 kwenye *economy* dola maana yake ukienda 1,000,000 unaongelea shilingi ngapi ni *six time five that is three billion dollars* kwenye *economy* yako. Tunapambana kupigania umaskini wetu, lakini ili watu wa korosho walime wengi, tutengeneze *commercial farming,* wale wenye *commercial farming,* wanatafuta soko duniani na watawachukua hawa wachache, tutakwenda mbali kama Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namalizia suala la pamba angalia pamba leo mwaka jana tumezalisha tani 200,000, lakini kama nchi tuna uwezo wa kufika hata tani 500,000. Mimi nasema lazima mawazo ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Mheshimiwa Waziri wa Fedha tubadilike sasa tu-*invest* kwenye *grove*, bila *grove* ndugu tutabakia hapa hapa, tunatafutana kwa nini hatuendi mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *palm oil* Tanzania tuna *import* asilimia 55.5 ya *edible* oil karibia dola milioni 300 zikaenda kwenye ku-*import* mafuta ya kula, lakini tuna eneo zuri la *palm oil* Kigoma pamoja na Kyela, tuna eneo mikoa yote ya katikati kulima alizeti na siyo kwamba tumejitosheleza kwenye *edible oil* lakini na Tanzania tungeanza ku- *export edible oil*. *Balance of employment*, *export* tusipo-*invest* kwenye ukuzaji na uzalishaji, bado tutabaki tunahangaika ku-*solve* matatizo ya siku inayofuata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuna suala la ng'ombe, suala la maziwa Uganda pekee yake wanazalisha lita 1,000 000 ya maziwa, sisi wenye ng'ombe wengi, wenye ardhi kubwa lita 100,000 na angalia tunachohangaika nacho, hata wale watu ambao wana vi-*ranch* badala ya kusema tuwasaidie wazalishe zaidi tunakwenda kuongeza kodi za *per square*

*meter* maana yake waondoke, maana yake wao hawana malisho, na hiyo kodi unayoitaka mwisho wa siku hutoipata, lakini ungeunganisha wale wafugaji wakazalisha maziwa mengi ukaja na viwanda, leo tungekuwa mbali sana.

Mheshimiwa Spika, juzi Uganda mtoto wa Museveni wa kike amefungua kiwanda kimoja tu anazalisha lita 100,000 za maziwa kwa siku, wala hawatuzidi ng'ombe wengi, hawatuzidi maarifa, hawatuzidi *land,* tatizo letu ni nini? Lazima tubadilike kama Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusema tatizo la maji; kama dunia itakuja kupigana vita ya tatu ya dunia italetwa na maji, lakini kwa bahati nzuri Tanzania Mungu katupa baraka ya maji, moja ya 16 ya maji yote safi ya kunywa duniani yako *Lake* Tanganyika, lakini watu wa kilometa tano kutoka *Lake* Tanganyika hawana maji, ukienda Mwandiga hakuna maji, ukinda vijiji vyote vya Simbo hakuna maji, ukienda Kalinzi, Mkiva, Nyarubanda hakuna maji lakini tunazungukwa na *Lake* Tanganyika. Niombe sana tuhangaike na suala la maji.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hotuba zote za Kamati zote. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Peter Serukamba. Sasa ni Mheshimiwa Riziki Lulida, dakika tano na Mheshimiwa Frank Mwakajoka dakika tano, watafuatiwa na Mheshimiwa Msukuma. Mheshimiwa Riziki.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru nami kwa kunipatia dakika chache ili nichangie katika hoja iliyoko mezani. Mwenyezi Mungu aliumba binadamu, aliumba ardhi, akaumba binadamu, wanyama, mito, bahari, wote hawa walikuwa wanategemeana. Nimefurahi kusikia baadhi ya mashamba yamerudishwa Serikalini ili kuwasaidia wananchi waendeleze kilimo, hii maaana yake nini? Niliwahi kuzungumza suala la baadhi ya mashamba ikiwepo mojawapo shamba la Kikwetu lilikaa kwa muda zaidi ya miaka 40 halilimwi, watu wanachukua mikopo benki,

mashamba yale wakipewa wananchi, nina imani kuwa tutasaidia wananchi kupata ardhi na kuweza kulima.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna mashamba yalikuwepo Mtwara Kabisela, mashamba yale yalikuwa yamepigwa uzio, huruhusiwi kuingia, matokeo yake kinachoendelea ndani hujui. Huu ni unyonge ndani ya nchi yako, watu wana-*monopolize* ardhi lakini haitumiki.

Mheshimiwa Spika, nitazungumzia suala la uhifadhi Tanzania; Tanzania kuliwa na *GN* ambazo zilishawekwa kwa ajili ya uhifadhi kwa asilimia 25, lakini *GN* hizo zipo katika makaratasi, ukienda kwenye uhalisia tayari wananchi wameshavamia maeneo yale. Narudia tena naomba busara itumike na busara itumike kwa nini? Mle ndani ya zile hifadhi kuna wanyama, kuna korido za wanyama ambao wanatoka katika njia zao wanaingia ndani ya mbuga za wanyama. Kwa mfano, Mheshimiwa Spika mwaka 2005 alikuwa ni mjumbe mwenzangu katika Kamati ya Maliasili na Utalii, tulikwenda Ihefu kuwatoa wafugaji ambao walishaharibu mazingira na nchi ilikuwa gizani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo tunataka kuruhusu bila kufanya utafiti, hili zoezi litakuwa gumu na litaiingiza nchi katika mazingira magumu tena. Wanyama hawa waliandaliwa na Mwenyezi Mungu kupita katika korido zao, leo tumeona *Ivory Coast* hakuna wanyama sasa hivi, tunaona Burundi hawana wanyama, tunaona Rwanda hakuna wanyama, sasa Tanzania tumevimbiwa na wanyama wachache tunawaona hawa, lakini ni uchumi bora ambao utaifanya nchi iweze kupaa kama tutaweza kuweka mazingira bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wanyama tembo, simba, chui anatoka Niassa Mozambique, anavuka Mto Ruvuma anafika Mbarang'andu wananchi wameshavamia eneo, tembo wale wanauawa, hivyo mpaka kufika Selous karibu nusu ya tembo hawarudi tena Mozambique. Tembo anatoka Namtumbo anataka kuvuka kwenda Matambwe kwenda Mikumi tayari watu wanalipa miwa, mnyama hana mahali pa kwenda. Tembo anaingia Mikumi anataka kwenda

Mkungunero tayari ameshazuiwa katika. Leo wanapotaka kutoa maamuzi ya kukurupuka, naomba tena tukae chini tuliangalie suala la wanyamapori ama la, nchi itaingia katika hali ngumu na wanyama watatoweka, utalii tunaojivuna nao utapotea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Tanzania tunajuana kwa makabila, kuna makabila wanapenda uhifadhi kama Mmasai, Mmasai hali nyamapori na hakati misitu. Kuna Wamakonde wanatunza misitu ndiyo maana misitu hiyo ilihifadhiwa mpaka leo, leo wafugaji wamekwenda Kusini, Lindi sasa hivi ni jangwa. Tunaona mikoa mingine imeshakuwa jangwa, je, hili zoezi litatusaidia au litatuwekea hali ngumu, nchi ni jangwa, ukiingia Dodoma yote ni jangwa, Singida jangwa, ukiingia Mkoa wa Arusha yote, Monduli jangwa, Shinyanga yote jangwa, tutafakari kabla hatujatoa maamuzi ambayo yataifanya nchi i-*paralyze,* kurudisha tena hii hali itakuwa ngumu.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna baadhi ya wafugaji au makabila, kula nyama pori ni kama kazi yao, kama mtu wa Serengeti kazi yake anakimbizana kuingia ndani ya mbuga kula kimoro. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Riziki kumkumbusha Mheshimiwa Marwa Ryoba habari ya Kimoro.

Mheshimiwa Frank Mwakajoka dakika tano utafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Msukuma. Mheshimiwa Mwakajoka sasa zile taarifa zako sasa zijibu, ndiyo maana sikukupa saa zile .

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia. Napenda nizungumzie sana kuhusiana na suala la kilimo hasa kilimo cha mazao ya chakula. Najua kabisa kwamba Watanzania wote wanajua kwamba mchango wa kilimo kwenye pato la Taifa ni mkubwa na mazao haya yanategemewa sana na Watanzania wote na hata leo tuko humu ndani ya Bunge

tunaonekana tuko vizuri na tunachangia ni kwa sababu tumepata chakula.

Mheshimiwa Spika, imeonekana kabisa kwamba Serikali haijatilia mkazo kabisa kuhakikisha kwamba inawasaidia wakulima hasa wakulima wa mazao ya chakula. Najua kabisa asilimia 65 ya Watanzania wanategemea kilimo, lakini huwezi kuamini pamoja na kilimo kuchangia asilimia 30 ya pato la Taifa, lakini uwekezaji kwenye kilimo umekuwa chini ya asilimia mbili. Kwa hiyo, ninachotaka kuzungumza ningeomba sana kwamba Serikali ijaribu kuangalia ni namna gani inaweza ikawekeza kwenye kilimo hasa kilimo cha nafaka.

Mheshimiwa Spika, imetokea sasa hivi kauli mbalimbali zimekuwa zikitolewa. Nakumbuka mwaka jana Mheshimiwa Rais amejaribu kuzungumzia akasema kwamba mazao ya chakula siyo biashara, lakini ukweli tu ni kwamba watu wamewekeza fedha nyingi sana, kuna watu wanavuna mpaka tani 80, wanavuna tani 200, wanavuna tani 300, kwa ajili ya mazao ya chakula lakini leo kuna kauli zinasema kwamba mazao ya chakula siyo biashara.

Mheshimiwa Spika, ukijaribu kuangalia kwenye upande wa pembejeo za kilimo mwaka jana wamesema kwamba wataagiza pembejeo kwa ajili ya kuhakikisha kwamba wakulima waweze kupata pembejeo kwa bei ndogo, lakini ukweli tu ni kwamba katika mwaka ambao tumewahi kununua pembejeo kwa bei kubwa ni mwaka huu ambapo pembejeo zimepanda kwa asilimia zaidi ya 20 kwa kipindi hiki. Kwa kweli tunaomba Serikali ijaribu kuangalia ni namna gani inaweza ikaboresha pembejeo hizi ikaweka ruzuku kama zamani ilivyokuwa inafanya. Serikali ya Chama cha Mapinduzi katika miaka iliyokuwa imepita Mheshimiwa Kikwete na Mheshimiwa Mkapa walikuwa wameweka ruzuku kwenye pembejeo za kilimo, lakini sasa ruzuku imeondolewa na biashara inafanyika holela, Serikali inachokisema ni kwamba imeamua kusimamia pembejeo hizi kwa kuweka bei elekezi.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, bei elekezi imekuwa ni kiini macho, kwa sababu bei elekezi Serikali inasema lakini haijachukua tathmini ya kutosha kuangalia ni namna gani soko la pembejeo likipanda kwenye soko la dunia, haijaangalia mafuta yakipanda ni namna gani inaweza kuwasaidia wakulima hawa ili waweze kupata pembejeo kwa bei rahisi, kwa hiyo kumekuwa na tatizo kubwa sana. Kwa mfano mwaka jana walisema pembejeo za kilimo watu watanunua kwa mfano kama *DAP* walisema watanunua kwa Sh.58,000 lakini kutokana na bei za Soko la Dunia ilipanda mpaka kufika Sh.65,000 mpaka Sh.67,000, *Urea* pia ni hivyo hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunachoomba ni kwamba, Serikali iweze kurudisha mfumo wa ruzuku kwenye pembejeo za kilimo hasa kilimo cha nafaka ili kuhakikisha kwamba wananchi wote ambao wanalima mazao haya, waweze kupata ruzuku ili kuhakikisha kwamba mazao haya wanalima kwa urahisi lakini pia wanauza mazao yao kwa urahisi. Kama haitoshi imeonekana kwamba bei ya soko la mazao ya chakula sasa hivi imekuwa ni tatizo kubwa sana na hili tatizo siyo kwamba wakulima wamesababisha, Serikali ya Chama cha Mapinduzi ndiyo imesababisha tatizo hili la bei ya chakula kuwa chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka 2017/2018, tulikuwa tumepata soko zuri kabisa Kenya, lakini Serikali ikazuia mipaka kwamba hakuna kuuza mazao nje na badala yake mazao hayakuuzwa nje, badala yake masoko haya yakahamia katika nchi zingine sasa hivi Wakenya wanakwenda kununua mahindi Zambia na Malawi, sisi tumekosa soko kwa sababu Serikali ilizuia mazao yasitoke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini mwaka huu bado mwaka huu imetokea tatizo lingine...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Muda hauko upande wako

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Spika, dakika mbili na nusu hii.

**SPIKA:** Tayari dakika tano, muda unaenda haraka kweli, ahsante sana. Mheshimiwa Joseph Musukuma atafuatiwa na Mheshimiwa Livingstone Lusinde.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia.

**SPIKA:** Mheshimiwa Musukuma dakika 10.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, sawa. Napenda nianze kwa kuzipongeza sana Kamati zote mbili, lakini nitachangia pande zote mbili nataka nianze na uvuvi. Tuliwahi kulalamika sana wakati wa operesheni lakini tukafika mahali tukakubaliana na Mheshimiwa Waziri na tukaamua kumuunga mkono na zoezi la wavuvi haramu kwa kiasi fulani limepungua.

Mheshimiwa Spika, sasa baada ya kutoka kwenye ule uvuvi ambao Mheshimiwa Waziri alikuwa anaukataa, hata huu uvuvi tulionao tena kuna tatizo kubwa. Sasa hivi kwenye ziwa Wizara imeweka masharti kwamba unavua mwisho sentimita 50 mpaka 85, lakini mitego ile ambayo Wizara ilipendekeza ukiitupa kwenye maji inavua mpaka sentimita 100 na kuendelea, sasa inaonekana tena mtu akivua sentimita 86 na lenyewe ni tatizo anatakiwa kuadhibiwa na kutozwa faini ya mamilioni. Sasa tunashindwa kuelewa, labda leo Mheshimiwa Waziri atakaposimama aniambie kwamba hiyo mitego uliyotaka tuitumie tutumie njia gani tukiitupa kule ndani isichukue zile sentimita 86 iwe inabagua zile unazozitaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama hiyo haitoshi siyo kwamba haya masharti uliyoweka watu hawavui, nataka nikwambie Waziri Mpina umeongeza magendo makubwa kwenye ziwa letu. Hii mitego unapoitupa kule kwenye maji wanapopata wale samaki wakubwa ambao wewe huwataki na wanashikwa na mitego yako, soko lake kubwa liko Uganda

na Kenya. Hata viwanda vyetu vya sasa vilivyoko huku Kanda ya Ziwa hawakubali kupokea samaki anayezidi sentimita 85, kwa hiyo, watu wanawapata wale samaki wanapeleka kwenda kuuza Uganda.

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine hata kwenye soko la kimataifa samaki wetu wamekosa soko. Wewe ni shahidi kwenye viwanda imejaa minofu haisafirishwi kwa sababu minofu yetu ni ya samaki wachanga, wale samaki wenye afya njema wako Uganda na Kenya ndiyo wamechukua soko hilo.

Mheshimiwa Spika, nimwombe Waziri, pengine una utaalam wa kuweza kuwaelewesha wavuvi wetu kwamba mitego uliyotupa wewe mwenyewe inashika sentimita kubwa hukutaka tushike sentimita ndogo, tatizo tena limekuja kwenye sentimita kubwa. Nikushauri sana Mheshimiwa Waziri utakapokuja hapa utueleze.

Mheshimiwa Spika, lakini pia Waziri umeharibu biashara ya bondo. Wewe mwenyewe unafahamu unaposhika samaki mwenye bondo kubwa na soko lake ni kubwa. Wachina ambao walikuwa wananunua mabondo ya Tanzania sasa wamehamia Uganda na Kenya, nadhani ukija hapa utatoa ufafanuzi ili tuweze kukuelewa.

Mheshimiwa Spika, lakini suala la pili niliwahi kusema hapa mpaka nikatoa machozi kuhusiana na suala la ufugaji Mheshimiwa Maghembe akiwa Waziri. Nashangaa sana mtu ambaye hatampongeza Mheshimiwa Rais, labda wale wanaokaa mijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama mnakumbuka vizuri nilisema kuna watu humu wanafuga mbwa na nyanya, hawawezi kuona thamani ya mashamba kwa sababu vitu vinakaa kwenye mazingira ya binadamu. Kwa hiyo, nataka niseme hivi kwa mtu yeyote anayetoka jamii ya wafugaji, anayetoka vijijini asipompongeza Mheshimiwa Rais kwenye hili suala la kuruhusu watu wamegewe maeneo ni mtu wa ajabu na Watanzania mnaotutizama kwenye *TV* hawa ndiyo Wabunge

wenu wanakaa kumpongeza Mheshimiwa Rais kwenye kazi nzuri aliyoifanya, lakini sisi tunaotoka vijijini tunasema Mheshimiwa Rais tunakupongeza sana na ndiyo kilikuwa kilio cha wanyonge unaowatetea na ikiwezekana endelea na maeneo na mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, linguine ni suala la wakulima. Sisi tunaotoka kwenye jamii ya wakulima yako matatizo mengi sana ya mbolea. Unaweza ukakuta sasa hivi wakati wa kupanda mbolea inakuja mwezi Juni au Novemba wakati mnavuna. Mimi najiuliza Mheshimiwa Rais mimi namhurumia wakati mwingine atapasuka hata kichwa. Wakati akipokea Taarifa ya *CAG* mwaka jana alizungumza akaielekeza Wizara msiagize mbolea ya nje chukueni Minjigu, Minjingu *godown* zimejaa mbolea hamnunui. Mbolea ya kupandia inakuja wakati wa kuvuna mbolea ya kuvuna inakuja wakati tumeshamaliza hata kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa napenda Waziri akija hapa atuambie na bahati nzuri Mheshimiwa Rais alikuwa *live* wakati akielekeza Wizara kwamba lazima mkanunue mbolea ya Minjingu kwa sababu mbolea ya Minjingu ni ninyi wenyewe mmeipima mkaiona inafaa na mkatoa *TBS.* Utaalam wenu wenyewe tena mnaona kama haifai mnaenda kuagiza mbolea ya nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini ukiangalia kwenye hii mbolea, mimi ni mkulima ndiyo maana nalalamika, ukienda Kenya, Uganda na Burundi wao hawaagizi mbolea ya nje wanaagiza mbolea ya Minjingu ambayo sisi tunaiona haifai. Sisi tunang'ang'ana kuagiza nje huku tunasema Serikali ya Viwanda. Jamani naomba Waheshimiwa Mawaziri husika mkija hapa mnipe majibu na sisi tunataka kumuunga mkono Mheshimiwa Rais kweli anachokitaka kifanyike kutengeneza viwanda vyetu vya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimesikia watu wakilalamika hapa kuhusiana na suala la mashamba. Bado nazungumza tu yaleyale, unajua watu tunapishana kuna watu wanatoka mijini, kuna ghorofa, wengine wanakaa juu, wengine

ghorofa ya tatu, sisi ambao tunakaa *plot* kwa *plot* hakuna mtu atawasikiliza na mnajipaka nuksi, watu wakiwasikia mnang'ang'ana mashamba yarudi kwa mabepari hiki kitu Watanzania hawakikubali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niseme mimi ni mwana CCM mzuri nilikuwa Mwenyekiti. Ukisoma ukurasa wa 41 kwenye Ilani ya CCM, kifungu cha 6 kuna baadhi ya watu humu, wana CCM wenzangu wanapiga midomo kwamba tutetee mashamba, wao ndiyo walikuwa viongozi na ndiyo walioanza kuisemea Ilani hii ikiielekeza kwamba tutakapochukua Serikali tuangalie mashamba makubwa tuyafute tuyapeleke kwa wananchi, leo tena wamegeuka ya kwao yaleyale wameyageuza tena.

**TAARIFA**

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Taarifa.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kumpa taarifa mzungumzaji anayeongea kwamba katika ukurasa wa 41 wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi, kifungu cha 37(6) wanasema hivi: "Katika kipindi cha miaka mitano ijayo Chama cha Mapinduzi kinaelekeza Serikali yake kuendelea kutekeleza mipango ya kuendeleza ardhi katika maeneo yafuatayo; kufanya uhakiki wa mashamba pori yasiyoendelezwa kwa kipindi kirefu na kuyagawa kwa wananchi wanaohusika nayo." *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Musukuma.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, naikubali hiyo taarifa. Tunataka Wabunge wazalendo kama hawa wanaoijua vizuri Ilani ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilichokuwa nasema ni Ilani ambayo imeelekeza haya yafanyike Serikalini. Nami nataka niwape moyo wanaosimamia hizi sheria, Waziri Lukuvi na wenzio futeni mashamba, futa, yaani hata yale mengine futa. Haiwezekani watu wanachukua hati wanaenda kukopea nje ya nchi wanapata hela wanaenda kuwekeza Dubai sisi tunaachiwa mapori huku. Naomba wale wanaosimamia Wizara hii futeni wala msiogope. Najua yatakuja maneno ya kusema mmehongwa, mmepewa rushwa, ukiwa unatekeleza sheria kuhongwa ni maneno ya kukukatisha tamaa, futa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Joseph Musukuma. Sasa anafuata mtani wako, Mheshimiwa Livingstone Lusinde. Mheshimiwa Lusinde, tafadhali dakika kumi. *(Makofi)*

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na namshukuru Mungu kupata nafasi hii ya kuzungumzia taarifa mbili za Kamati. Nitaanza kuzungumzia taarifa inayohusiana na kilimo.

Mheshimiwa Spika, mimi ni Mbunge ninayetokana na wazazi maskini kabisa kwenye Taifa hili. Ukitaja watu maskini wa nchi hii unataja wakulima. Kama kweli tumedhamiria kuwainua wakulima basi ni lazima Serikali ijielekeze walau tuwe na kiwanda hata kimoja cha zana za kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni jambo la aibu sana panga tunaagiza kutoka nje, shoka tunaagiza kutoka nje, jembe tunaagiza kutoka nje, hivi huyu mkulima ambaye tunataka kumuinua tutamsaidiaje kwa karibu kama hatuna uzalishaji wa zana hizo ndani ya nchi? Kwa hiyo, ningeshauri kwamba walau tufufue kile kiwanda cha zana za kilimo Mbeya au tujenge kingine kipya ili mradi uzalishaji wa hizi zana za kilimo upatikane ndani ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini nimekuwa nikisema mara nyingi sana kuhusu zao la zabibu. Bahati mbaya sana kila majibu yanapotolewa wanasema zabibu iko katika Bodi ya Mazao Mchanganyiko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zabibu ni zao la kipekee kwa hapa Tanzania linalimwa katika Mkoa wa Dodoma na halilimwi Dodoma yote. Unajua kuna watu hawaelewi wanafikiri Dodoma nzima ukipanda zabibu zinakubali, hapana, zabibu zinalimwa eneo kidogo la Kongwa, baadhi ya maeneo ya Dodoma Mjini, baadhi ya maeneo ya Wilaya ya Chamwino na Wilaya ya Bahi. Kwa hiyo, unaweza kuona ni muhimu sana hata kutambuliwa tu yale maeneo ambayo zao hilo linastawi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo tumekuwa Makao Makuu ya Nchi unaweza kukuta ardhi ileile inayostawi zabibu watu wakaenda kulima na wakaweka vitu vingine tukajikuta hata maeneo tunayotegemea kuzalisha zabibu yakakosekana. Kwa hiyo, kutambua tu peke yake kwamba eneo hili linaweza kustawi zao hili na eneo hili linaweza kustawi zao hili ni jambo zuri na litasababisha wakulima wetu waweze kuinuka na kuendelea kupata uchumi mzuri. *(Makofi)*

## TAARIFA

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Pokea taarifa Mheshimiwa Lusinde.

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Spika, nilitaka nimpe taarifa tu Mheshimiwa Lusinde kwamba wakulima wa Dodoma sasa hivi ni kama wamechanganyikiwa kwa sababu Bodi ya Pamba ikishirikiana na Mkuu wa Mkoa wameanza kueneza kilimo cha pamba kwa wakulima na wakiwaahidi kwamba kwa eka moja atapata shilingi milioni moja. Matokeo yake ni kwamba baada ya muda fulani mkoa huu unaweza kupata njaa kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, nilitaka nimpe taarifa hiyo kwamba wakulima tayari wameshachanganywa tena.

**SPIKA:** Mheshimiwa Lusinde.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Juma Selemani Nkamia, mdogo wangu kwa siku mbili kwa kuzaliwa. Nikimtangulia mimi kwa siku mbili zinazofuata yeye, taarifa nimeipokea.

Mheshimiwa Spika, haya ndiyo mambo ambayo tunayaelekeza. Mwanzoni kila ukanda ulikuwa una zao lake la biashara, huku wanalima pamba, huku wanalima korosho, huku wanalima kahawa, ule utaratibu ulikuwa mzuri sana kwa sababu wananchi walikuwa wanaangalia ardhi na mazao yanayostawi kwenye ardhi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lazima tukubaliane dunia nzima ina vitu vikubwa viwili, kuna nuru na kuna giza. Kama unataka kufanya vizuri lazima uvitambue sio kwa sababu humu ndani tuna upande wa Chama Tawala na upande wa Upinzani ndiyo upinge kila kitu. Hivi Mheshimiwa Rais analetewa na Wizara juu ya mchakato wa kufuta shamba fulani ambalo limemilikiwa kwa miaka mingi, watu maskini wa eneo hilo wamekosa maeneo ya kulima, Rais anafuta, leo Mbunge unasimama kutetea kwamba Rais asifute. Mimi sielewi hapa tunatoa wapi hoja hiyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wabunge wanaokataa maskini wa nchi hii wasipewe ardhi hebu wajitambulishe kwa majina yao na majimbo yao ili wananchi wapate kuwafahamu. Tunaposema Rais anatetea wanyonge tunamaanisha na Mheshimiwa Rais hizi Wizara zote zilizotajwa katika hizi taarifa ni Wizara ambazo zinaweza kumsaidia sana katika vita hii ya uchumi. Maana tunapozungumzia vita hatuzungumzii ya kuuwana moja kwa moja kuna vita ya uchumi sasa, kilimo kikifanya vizuri, viwanda vikafanya vizuri, utalii ukafanya vizuri, maisha ya Watanzania hayatategemea tena wafadhili, tutakuwa huru hata kujitungia sheria zetu wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, juzijuzi mmeona umaskini mbaya sana, tunalazimishwa tukubaliane na sheria ambazo zinakiuka hata mila na desturi yetu kwa sababu tu tunasaidiwa. Mambo mengine hata ukiyatazama kwao hao walioendelea kidemokrasia hayapo.

Mheshimiwa Spika, juzi nilikuwa na-*Google* kama Mheshimiwa Musukuma rafiki yangu kuangalia tangu Uchaguzi Mkuu wa Marekani umepita Hillary Clinton hajafanya mkutano hata mmoja wa kushukuru wananchi lakini ndiyo haohao wa kwanza kusema sisi hatuna demokrasia. Mbona Marekani walioshindwa hawazunguki kufanya mikutano ili kuwashukuru wananchi? Haya mambo unayona kwetu tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kitu kingine, Trump, Rais wa Marekani, hataki ushoga, hakuna mtu anamuuliza, hakuna mtu anampinga, watu wamenyamaza kimya, lakini sisi kwa sababu ya umaskini wetu kila kitu kibaya wanataka kutuletea. Kwa hiyo, Serikali ikijikita kuinua wakulima, kukuza sekta ya utalii tunaweza kupata pesa nyingi ambazo zitasababisha tupange maendeleo yetu wenyewe bila kufuatwafuatwa na mtu mwingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi leo hii Wabunge tunazungumzia umeme wa *Stiegler's Gorge* wakati tayari saini zimeshawekwa, huu ni utovu wa nidhamu wa hali ya juu sana. Saini zimeshawekwa, mikataba imeingiwa, halafu sisi tunataka kuonesha kwamba eti kuna tatizo, tatizo liko wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeelimishwa...

**SPIKA:** Tena Mheshimiwa Lusinde na Spika nilialikwa nikashuhudia kwa niaba yenu wote. *(Makofi)*

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Kwa niaba ya Bunge hili. Maana popote anapoalikwa Spika anaalikwa kwa niaba ya Bunge. Kwa hiyo, Bunge lilishuhudia utiaji saini na ujenzi unaanza, tunaanza kuzungumzia eti inawezekana kuna

matatizo, jamani tumetumwa au ni akili yetu sisi wenyewe? Mbona tunazungumza kama Bunge la Ujerumani hivi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana Wizara ya Maliasili na Utalii mmeboresha mazingira. Jimboni kwangu kule tembo wameongezeka mpaka juzijuzi walikunywa pombe za wananchi. Kulikuwa na mnada pale tembo wawili wakakuta wananchi wangu wanakunywa, wananchi wakakimbia tembo wakanywa pombe, ilikuwa shughuli. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa sijawahi kushuhudia tembo akilewa balaa lake ni kubwa. Kwa hiyo, tunachokiomba walau Serikali sasa kupitia *KDU* itengeneze ulinzi wa kuzuia wanyama waharibifu ili wasiwafikie wananchi na kuchukua pombe yao. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Lusinde, nakuelekeza tu wale wananchi wenye pombe zao wapeleke *invoice* zao kwa Waziri wa Maliasili na Utalii ili wapate fidia. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Nape Nnauye, dakika 10 tafadhali.

**MHE. NAPE M. NNAUYE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie kwenye hizi taarifa za Kamati mbili.

Mheshimiwa Spika, wakati ukimuagiza Mheshimiwa Lusinde apeleke *invoice* kwa Waziri wa Maliasili na mimi kwangu tembo wameingia lakini kwangu wamekula maembe. Kwa hiyo, nami nitapeleka *invoice. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimepitia ripoti ya Kamati hii inayoshughulika na kilimo na naunga mkono mapendekezo yao mengi sana. Nitaomba tufanye maboresho maeneo

machache lakini kwa kweli wamefanya kazi nzuri ya kuchambua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi yetu ina mazao mengi, yako mazao yale ya biashara lakini yako mazao mchanganyiko. Hapa nataka nizungumzie suala la Bodi ya Nafaka ya Mazao Mchanganyiko. Tunazo Bodi kwenye mazao mengine mengi lakini hii ya mazao mchanganyiko ambayo *of course* sasa hivi inafanya kazi ya kusimamia ununuaji wa zao la korosho, kwa mujibu wa sheria imeandikwa hapa kwamba hii ni taasisi ya Serikali ambayo inajiendesha kibiashara.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana na mwaka juzi sisi ambao tuna wakulima wanalima mazao mchanganyiko na hasa sisi wa mbaazi tulipata matatizo kwa sababu tunadhani hii bodi haikutimiza wajibu wake sawasawa na ni kwa sababu ya ukosefu wa fedha kwamba hawakupewa fedha za kutosha. Kazi yao moja ni pamoja na kuyanunua haya mazao mchanganyiko kwa bei ya soko lakini kuyatafutia soko na hasa nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Kamati imeonesha hapa moja ya changamoto kubwa ambayo imewapata wenzetu wa Bodi ya Mazao Mchanganyiko ni kutopewa fedha. Ushauri wangu nadhani kwa kuwa, ni Bodi ambayo inaweza kujiendesha kibiashara badala ya kuendelea kutengewa fedha na Serikali kutoka kwenye Mfuko Mkuu, kwa nini Serikali isitengeneze utaratibu wa kuwadhamini Bodi ya Mazao Mchanganyiko wapate fedha kutoka kwenye taasisi za kifedha kwa maana ya kwamba wafanye kibiashara, wakakope, wanunue, wauze, Serikali iwe ni *guarantor* tu badala ya kupeleka fedha kule. Tuwa-*guarantee,* wapewe fedha na vyombo vya fedha wakanunue haya mazao wakatafute soko, wakulima wetu wangekuwa wako sawasawa kabisa na leo tungekuwa hatuzungumzi kabisa tatizo la mbaazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, habari nilizonazo waliomba fedha hawakupata, wakaomba kwenda kukopa kwa kupewa *guarantee* na Serikali nayo wakanyimwa, matokeo yake sasa wakabaki wako tu. Sasa wamebaki wako *loose,* tumeenda

kuwachukua kuwapeleka kununua korosho, mimi nadhani siyo sawasawa. Tuwawezeshe, tuwadhamini, wakachukue fedha kwenye vyombo vya fedha kibiashara wafanye biashara kwa kuwa sheria inasema hivyo na mapendekezo ya Kamati hapa yanaonesha wakipewa fedha watafanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili ni mapendekezo juu ya korosho. Kamati imechambua vizuri sana suala zima la korosho. Nami naamini tumejifunza mengi namna korosho ilivyoenda na bila shaka mafunzo yake yatatusaidia kuboresha namna ya kuendesha mazao yetu ya kibiashara nchini. Tumevuna tulichopanda lakini sasa tujifunze badala ya kuendelea kulaumiana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna suala la utata wa takwimu ambazo zimekuwa zikitolewa na wenzetu wa Serikali. Kila mara Serikali imekuwa ikitoa takwimu mbalimbali juu ya zoezi zima la ununuzi wa korosho. Mimi nataka niwatahadharishe, takwimu nyingi mnazozisema Serikali ukienda kule chini ukweli unakataana. Mnachokisema mmelipa na hali halisi ilivyo, ukweli unapingana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sijui kama kuna sababu ya kuendelea kutoa takwimu. Takwimu hizi kila siku zinakua, nikienda Jimboni kwangu hali ya malipo bado mbaya lakini takwimu zinaonesha mambo yanakwenda, nadhani hili tulirekebishe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kuna mambo yametokea kwenye zoezi zima na hili nadhani kwa sababu ya kuchanganya. Tumei-*suspend* Bodi ya Korosho, tumeweka Bodi ya Mazao Mchanganyiko na Jeshi, kuna matendo ya dhuluma yamefanyika kwenye maeneo haya. Nashauri Serikali tufumbue macho, twende tuchunguze na tuchukue hatua, dhuluma haitakufa kama hatutachukua hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la tatu katika korosho, zoezi la uhakiki bahati mbaya sana limeanza kutumika kama kichaka cha kulinda uzembe wa kupunguza kasi ya kulipa wakulima.

Bahati mbaya limeanza muda mrefu siyo korosho tu kila mahali tukitaka kuchelewa kulipa tunasema tunafanya uhakiki ambao unachukua muda mrefu watu wanaumiaa inafika mwisho basi inapotea hewani hivi. Wasiwasi wangu uhakiki kwenye zao la korosho isipotelee hewani, uhakiki utupe matokeo, kama kuna korosho tumeamua kuitaifisha tuseme kiasi gani tumetaifisha na kwa nini tumetaifisha. Suala hili la uhakiki tukiweka wazi kila mtu atatuelewa na tutasonga mbele pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la mwisho, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mtama nataka kuchukua nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Rais na hapa nataka tujifunze kidogo kuweka akiba ya maneno hasa tunaposhutumiana bila sababu. Mheshimiwa Rais wakati wa uchaguzi sisi Jimbo la Mtama tulipeleka maombi ya kufuta baadhi ya mashamba makubwa yaliyotelekezwa. Namshukuru Rais na Waziri wa Ardhi, moja ya shamba lililofutwa ni shamba Na. 37 lipo Maumbika – Mtama, Mkoa wa Lindi. Aliyelipeleka kuomba lifutwe ni mimi Mbunge, nilimpelekea Waziri, Waziri akapeleka kwa Rais, Rais akafuta. Nataka niwaombe wenzangu kwanza kwa niaba ya wakulima nimshukuru Waziri na Rais kwa kulifuta shamba hili kwa sababu sasa tutaenda kugawana vizuri. Kwa hiyo, wakati mwingine tunapolishwa maneno tukaanza kusema, tuweke akiba ya maneno juu ya nani anapinga nini, anasema nini, itatusaidia sana kama wanasiasa tukiwaweka akiba ya maneno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Nape Nnauye. Tunaendelea na Mheshimiwa Rashid Shangazi kwa dakika tano, anafuatiwa na Mheshimiwa Casato Chumi dakika tano.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii. Kwanza naomba nichukue nafasi hii kwa dhati kabisa kuzipongeza Kamati zote mbili kwa namna ambavyo wamechambua na kuleta ripoti zao ambazo ziko mbele ya Bunge lako Tukufu. Kipekee kabisa,

nimesimama mbele ya Bunge lako Tukufu kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kupitia Waziri wa Ardhi, Mheshimiwa Lukuvi, pamoja Naibu Waziri Mheshimiwa Mabula na sisi kule Mlalo tulikuwa na shamba la *Mnazi Sisal Estate* ambalo lilikuwa linamilikiwa na Kampuni ya *Lemashi Enterprises,* wawekezaji hawa kutoka Kenya, shamba hili lilitelekezwa kwa muda mrefu sana takribani miaka 15.

Mheshimiwa Spika, wewe ni mkongwe humu kulikuwa na Mbunge wa Jimbo la Mlalo, Mheshimiwa Charles Kagonji ndiye mtu wa kwanza kupigania shamba hili kurudishwa kwa wananchi. Kwa kipindi chake chote cha Ubunge wa Jimbo la Mlalo alishindwa. Hali kadhalika akaingia Mheshimiwa Brig. Ngwilizi naye amepambana lakini Mkenya yule pamoja na mianya mbalimbali ambayo alikuwa anaitumia kupitia watumishi ambao siyo waaminifu katika Halmashauri, Mkoa na Wizara kwa wakati huo mambo hayakwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kipekee natoa pongezi hizi kwa Mheshimiwa Lukuvi, Waziri wa Ardhi, kwa kazi kubwa sana ambayo amefanya ndani ya kipindi cha mwaka mmoja na nusu tulifanikiwa kurudisha shamba lile mikononi mwa Halmashauri ya Lushoto. Hivi navyozungumza tayari tumeweka mwekezaji mwingine, sisi kwa bahati nzuri tumechukua shamba kwa mwekezaji na tukatafuta mwekezaji mwingine na tumepata mwekezaji mpya amelipa kodi zote stahiki Serikali zaidi ya shilingi bilioni 2.8 na ameshaanza kuwekeza zaidi ya trekta tano mpya ziko ndani ya shamba, ameweka *excavator* na kila aina ya mashine. Mashine zote ambazo zilikuwa zina *process* na kuchakata mkonge kwa maana ya kuanzia kukata mpaka mwishoni kutengeneza mchakato wa *brushing* amefufua mashine zote zile za Kijerumani ambazo zilikuwepo tangu miaka ya 1936. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, natoa pongezi hizi kwa sababu sasa wananchi wote wanaozungukwa na shamba lile ambalo linazunguka takribani kata tatu wamepata ajira

za kudumu zaidi ya wananchi 330 lakini ambao wapo wamepata ajira siyo za kudumu za kwenda kukata mkonge wengine kwenda kupalilia kulima na kadhalika. Kwa hiyo, unaweza ukaona kwamba ni kwa kiasi gani uchumi wa Halmashauri ya Lushoto ulikuwa umelala kwa kipindi kirefu kwa sababu tu ya kumpata mwekezaji ambaye hakuwa sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba hili nilizungumze kwa uwazi sana, mashamba ya mkonge tunapoyazungumza ni makubwa sana, kwa mfano hili Shamba la Mnazi ni takribani heka 4,100 lakini mwekezaji huyu alikuwa amewekeza katika heka 500 tu. Kwa hiyo, shamba lingine lote likageuka pori ambalo limekuwa makazi ya nyoka baadhi ya wafugaji kulitumia kwa ajili ya shughuli ya ufugaji. Hata haya mashamba tunayoyazungumza katika Mkoa wa Tanga kwa maana ya Wilaya ya Korongwe na Muheza ambapo bado kuna mashambapori mengi unakuta hawa wawekezaji wanalima katika upande wa barabara. Kwa hiyo, unapopita huku barabarani unaona kuna shughuli zinaendelea lakini kimsingi zile shughuli ni kiini macho wanaweka tu hekari za mwanzoni barabarani lakini huko pembezoni ni machaka makubwa sana ambayo yamegeuka kuwa msitu. Kwa hiyo, nitoe rai sana kwa Wizara kwamba iendelee bado tunayo mashamba zaidi ya 36 ambayo hayaendelezwi katika Mkoa wa Tanga.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Rashid Shangazi kwa kutumia muda wako vizuri. Mheshimiwa Casato Chumi dakika tano utafuatiwa na Mheshimiwa Waziri Kakunda na yeye dakika tano.

**MHE. CASATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi, nitatumia vizuri dakika tano. Awali ya yote, kwa niaba ya wananchi wa Mafinga, niseme napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, niliposimama hapa 2017 kutetea suala la vinyungu kuna baadhi ya watu hawakunielewa lakini kwa watu wa

Mafinga, Mufindi, Iringa, Kilolo, Njombe na maeneo yanayofanana kwetu vinyungu ni maisha na maisha ni vinyungu kwa sababu ndiyo uchumi wa watu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nijielekeze kwenye jambo ambalo nimekuwa nikilisema na sitaacha kulisema, suala la Serikali kufikiria na kuona umuhimu wa kuruhusu kusafirisha mazao ya misitu saa 24. Hapa ninapozungumza saa 11.00 hii umepakia mbao zako pale Mafinga huwezi kuondoka mpaka kesho saa 12.00 asubuhi, hii tunachelewesha uchumi. Naomba Serikali na hasa Wizara ya Maliasili na Utalii waliangalie jambo hili na bahati nzuri nime-*peruse* naamini sijakosea nimegundua ni kanuni siyo sheria. Kwa hiyo, bado Mheshimiwa Waziri anaweza akakaa na wadau akalifanyia kazi tukaruhusu malori yasafiri saa 24 kusafirisha mazao ya misitu ili tu *first track* uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa nina hesabu ndogo tu, ukichukua mzigo kutoka Mafinga mpaka Mwanza unatumia mafuta takribani lita 880. Kwa maana kwenda kwa sababu una mzigo utatumia 530 kurudi kwa sababu huna mzigo utatumia 350 na katika kila lita moja Serikali inapata *fuel levy* 313. Kwa wiki moja gari inaenda mara moja lakini *the same,* lori kwa wiki moja ingeweza kwenda mara tatu na ikienda mara moja Serikali inapata *fuel levy* Sh.274,400 ikienda mara tatu kwa wiki Serikali itapata *fuel levy* Sh.826,200. Maana yake ni kwamba kwa wiki moja kama Serikali itapata fedha hiyo basi kwa mwezi itapata Sh.3,304,800 na fedha hizi zinaenda kwenye *Road Fund. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maana yake ni kwamba yaani sisi wenyewe kwa kutoruhusu magari yasafiri usiku tumejipunja kama Serikali. Maana yake ni nini, gari moja Serikali badala ya kupata shilingi milioni tatu *point something* kutokana na *fuel levy* inaishia kupata milioni moja inapata *loss* ya shilingi milioni mbili. Wote tunalia na umeme wa *REA,* Sh.100 kwa kila lita inaenda kwenye *REA.* Kwa hiyo, gari zikisafiri kwa haraka na usiku maana yake Serikali nayo itapata mapato na wale wananchi uchumi wao utakuwa umezunguka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutoka Mafinga mpaka Dar es Salaam tuna *checkpoint* siyo chini ya 10 *at the same time* tuna magari ya *patrol*, hii sheria yenyewe ukii-*trace* ni ya 1959 wakati Serikali ya wakoloni haina vitendea kazi vya kutosha ndiko uliko *originate*. Kwa hiyo, naomba kama Serikali ina wawasi na mbao pori sisi ambao miti yetu tunapanda wenyewe ituruhusu tusafirishe saa 24. Haiwezekani mchana ukutane na roli, basi na gari za Wabunge, malori hata Ulaya *traditionally* yanasafiri usiku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hilo nizungumzie suala la utalii ambao unachangia fedha nyingi za kigeni. Ukienda katika utalii kuna tozo na kodi 33 yaani kama unataka kufanya kazi kwenye *industry* hii inabidi ujipange na tozo 33 na hizo 33 zenyewe leo unaenda kushoto, kesho kulia, kesho kutwa nyuma, siku nyingine mbele. Hii ni sekta inayochangia sana mapato kuwa na *One Stop Center* ili kurahisisha *facilitation* kuhakikisha kwamba utalii na hizi ndege tulizoleta unaendelea kuchangia pato la Taifa kutoka asilimia 17 kwenda zaidi ya hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Casato Chumi kwa ushauri ambao umetupatia.

Waheshimiwa Wabunge, tuna wageni kutoka TAHLISO wakiongozwa na Peter Ndiboye na viongozi wengine wote kutoka maeneo mbalimbali ambao wanaunda Umoja huo wa TAHLISO. Karibuni sana vijana wetu hapa Bungeni. *(Makofi)*

## MICHANGO YA MAANDISHI

**MHE. PETER A. LIJUALIKALI:** Mheshimiwa Spika, tamko la Mheshimiwa Rais la kuzuia wakulima na wafugaji kutobughudhiwa katika shughuli zao za kuzalisha mali na makazi linapaswa kuwekwa katika utaratibu wa kisheria. Jambo hili lisiwe la kisiasa pekee kwani wananchi wanaweza

kuwekeza katika maeneo haya lakini baadaye wakatolewa bila fidia. Hivyo basi, naitaka Serikali ilete mabadiliko ya sheria ili jambo hili liwe la kisheria.

Mheshimiwa Spika, zoezi la upimaji ardhi katika Wilaya ya Kilombero, Malinyi, Ulanga linaendelea vizuri na lina faida kwa wananchi ingawa *speed* yake ya ugawaji wa hati ni dogo sana. Wananchi wamekaa muda mrefu baada ya kupima ardhi yao bila kupatiwa hati. Nitoe wito kwa Serikali iongeze *speed* ya kutoa hati.

Mheshimiwa Spika, kuna mashamba makubwa ambayo hayajaendelezwa kabisa na hata baadhi ya wamiliki wake wanasadikiwa kuwa wamefariki ama wameshafariki. Kwa mfano, Daudi Balali anamiliki zaidi ekari 360 ambazo hazijaendelezwa katika Halmashuri ya Mji wa Ifakara.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la korosho, Mheshimiwa Rais alitoa tamko peupe kuhusu bei ya kununulia kuwa itakuwa ni Sh.3,300 na kuendelea. Hivyo, nashangaa kusikia eti kuwa korosho inanunuliwa kwa wakulima chini ya Sh.3,000. Hii ni dhuluma kabisa, ilhali Serikali yenyewe imeuza korosho hiyo kwa bei ya zaidi ya Sh.4,000, yaani Serikali imeamua kuwa *middleman* wa korosho, huu ni udalali kabisa.

**MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD:** Mheshimiwa Spika, nazipongeza Kamati kwa taarifa nzuri na nazipongeza Wizara zote kwa kazi nzuri wanazofanya kuwatumikia Watanzania.

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Serikali kwa juhudi kubwa ya kuwaletea wananchi maendeleo pia kuwasaidia wakulima, wavuvi na wafugaji nchini kwa kutatua changamoto nyingi zinazowakabili kama kuwapunguzia kodi na kuondosha tozo mbalimbali. Maoni yangu ni kama ifuatavyo:-

(i) Nakubaliana na mapendekezo ya Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji.

(ii) Napendekeza utolewe msisitizo kuhusu kulipa madeni ya ankara za maji. Nashauri taasisi za Serikali Wizara ya Fedha zikate madeni hayo moja kwa moja.

(iii) Serikali ihamasishe wananchi kuhusu suala zima la uvunaji maji ya mvua.

(iv) Nashauri uhifadhi vya vyanzo vya maji uimarishwe.

(v) Mfuko wa Maji uongezewe fedha ili kuweza kupanua huduma za maji na hasa vijijini.

(vi) Katika sekta ya uvuvi, nashauri Serikali iendelee na juhudi ya kuliimarisha shirika la uvuvi TAFICO pia kuwekeza katika uvuvi wa bahari kuu.

(viii) Nashauri bidhaa zinazozalishwa kutokana na maziwa zipunguziwe kodi na tozo mbalimbali ili kuongeza uwekezaji katika sekta hiyo ili kuongeza pato la Taifa na kuongeza ajira.

(ix) Sekta ya kilimo iongezewe fedha kwa ujumla kwenye vitengo vyake vyake utafiti na Bodi ya Mazao Mchanganyiko ili iweze kununua mazao ya wakulima kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naunga mkono hoja.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza Mwenyekiti, Makamu na Wajumbe wa Kamati zote kwa kazi nzuri na maoni yao kwa ajili ya kuishauri Serikali.

Mheshimiwa Spika, asilimia 80 ya wananchi wa Tanzania ni wakulima na kilimo ni uti wa mgongo wa uchumi wetu lakini bado Serikali haijaweza kuwa na mkakati wa kusaidia wakulima wetu ili kilimo kiweze kuisaidia nchi yetu. Tulitakiwa kutenga 1% ya pato la Taifa kwa ajili ya utafiti lakini pesa ya utafiti iliyoweza kutolewa ni 0.03.% tu.

Mheshimiwa Spika, bila kuwa na utafiti wa kutosha kunasababisha kutokuwa na mbegu bora na kushindwa kufanya utafiti wa mbolea kulingana na udongo wa sehemu mbalimbali. Pia vituo vyetu kutopatiwa pesa ya kutosha na kwa wakati kumesababisha kuwa na changamoto kubwa sana ya kutofanya utafiti wa kutosha kusaidia kilimo cha Tanzania. Nashauri Serikali itenge pesa ya kutosha ili vituo vya utafiti viweze kufanya utafiti ili kusaidia wakulima walime kilimo chenye tija ili viwanda vyetu viweze kupata malighafi kutoka kwa wakulima wetu.

Mheshimiwa Spika, tuna eneo la umwagiliaji lenye ukubwa wa ekari milioni 22 lakini tumeweza kutumia ekari laki nne tu ambapo tunapata chakula 50%. Tungeweza kutumia eneo lenye ekari milioni moja tu tungeweza kupata chakula kwa 100%, tungeondoa umaskini kwa wananchi wetu na tungeweza kusaidia hata malighafi kwa viwanda vyetu. Nashauri Serikali itenge pesa ya kutosha na kuhakikisha wataalam wake wanaitendea haki sekta hii ya miradi ya umwagiliaji ili tutumie eneo kubwa kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji kuliko kutegemea mvua ambazo mara nyingi hutokana na tabianchi, hali ya hewa haitabiriki.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Mazao Mchanganyiko. Niunge mkono maoni ya Kamati kwamba Serikali iwezeshe Bodi hii ili iweze kufanya kazi iliyokusudiwa. Serikali ihakikishe Bodi inapatiwa pesa ya kutosha ili inunue mazao kwa wakati, iwe na wafanyakazi wa kutosha na vifaa kama magari ili iweze kusaidia wakulima wetu wawe na uhakika wa masoko.

Mheshimiwa Spika, Mabalozi wetu waliopo katika nchi mbalimbali wamekuwa wakijitahidi kutafuta masoko kwa ajili ya mazao yetu lakini sijaona juhudi ya Serikali ya kuwaunganisha wakulima wetu na masoko hayo, je, tatizo ni nini? Mfano, Comoro ina soko kubwa sana kwa mazao ya chakula na wanyama lakini tatizo ni chombo cha usafiri cha uhakika. Je, nini mkakati wa Serikali kuhakikisha tunakuwa na chombo cha uhakika cha kusafirisha bidhaa zetu hadi Comoro?

Mheshimiwa Spika, upanuzi wa miji. Wakulima wetu nchini bado hawajaweza kuwa na sheria ya kuwalinda katika ardhi ya kilimo. Kunapotokea upanuzi wa miji tumeshuhudia mashamba yao yanapokonywa na kupimwa viwanja na kuzuiliwa kuendelea na kilimo. Ukienda kwenye nchi za wenzetu unakumbana na mashamba mijini kama nchi za Malaysia, Mauritius kuna mashamba ya miwa na michikichi. Mkulima shamba lake likipimwa alime wapi, anaishije?

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, tulipotembelea wakulima wa mashamba ya maparachichi katika Mkoa wa Njombe tulikumbana na mkulima ana changamoto ya kutopatiwa hati ili akaombe mkopo sababu shamba lake linatakiwa lipimwe viwanja. Je, mkulima shamba lake likipimwa alime wapi, anaishije? Tunaomba Serikali iangalie njia thabiti ya kuwasaidia wakulima.

Mheshimiwa Spika, ipo haja mkakati uwekwe kuhakikisha vivutio vyetu vinatangazwa. Naipongeza sana Serikali kwa Mradi wa *REGROW* ambao utasaidia kukuza utalii Nyanda za Juu Kusini ukiwemo Mkoa wa Iringa. Tunaiomba Serikali yetu iweze kuboresha miundombinu ya barabara kama ile ya *Ruaha National Park* Iringa, ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Nduli na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Spika, pongezi kwa Serikali ya Awamu ya Tano kwa kutatua migogoro ya ardhi kwa wakulima na wafugaji. Nina maoni yafuatayo:-

(i) Naishauri Serikali kupeleka mbolea kwa wakulima kwa wakati hasa kwenye wilaya ambazo zinalima sana mazao ya chakula mfano, mahindi, viazi, mpunga na zao la chai katika Wilaya ya Mufindi.

(ii) Kuna miradi mingi sana ya umwagiliaji lakini haifanyi kazi ingawa Serikali imepeleka fedha nyingi sana kwenye miradi hiyo. Nashauri suala hili lifuatiliwe kwa ukaribu.

(iii) Serikali iweke kipaumbele katika kutatua tatizo la maji katika wilaya, kata na vijiji. Kwa mfano, miundombinu ya maji imechakaa sana kwenye Jimbo la Mufindi Kusini, Kata za Nyololo, Igowole, Mtambula, Itandula, Idunda na Mninga. Sehemu zote hizi bado zina tatizo kubwa la maji.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Spika, kilimo ni uti wa mgongo wa Taifa letu. Kwa bahati mbaya Watanzania tunaweka kilimo katika misamiati ya Siasa ni Kilimo, Kilimo cha Kufa na Kupona na Kilimo cha Bega kwa Bega bila kusahau Kilimo Kwanza.

Mheshimiwa Spika, napenda kufahamu, leo tunapojadili mkakati wa ujenzi wa viwanda vya mbolea nchini, kile kiwanda cha mbolea kilichokuwepo Tanga *(Tanzania Fertilizer Company*) ni sababu gani zilizopelekea kufa, hali ya kuwa kila siku mbolea za aina mbalimbali zinahitajika?

Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa la wakulima wa Tanzania ni masoko ya mazao yao. Naishauri Serikali kutafuta masoko ya mazao mbalimbali kama muhogo. Katika Jimbo langu la Tanga kuna uzalishaji mkubwa sana wa zao la muhogo katika maeneo ya Kata za Kirare, Marungu, Tongoni, Pongwe, Mzizima, Mabokweni na Kiomoni lakini unaharibika mashambani. Naiomba Serikali itafute masoko ya uhakika kwa ajili ya zao hili.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeingia katika soko la zao la korosho na sasa Serikali inanunua korosho. Ni jambo jema lakini lina ukakasi mkubwa. Wakulima wa korosho wengine wanalipwa na wengine bado na viwango vya malipo vinatofautiana na kuna maeneo ya kufanya uhakiki. Naiomba Serikali iwalipe wakulima wa korosho ili waweze

kupata fedha za kusomesha watoto, kujenga nyumba bora na shughuli nyingine za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, tahadhari, wakulima wa mazao mengine nao wana haja ya mazao yao kupatiwa soko. Sasa isije kufika wakati wakulima wa mahindi, muhogo, mtama, mbaazi, kunde na nyanya nao wakailazimisha Serikali inunue mazao yao.

Mheshimiwa Spika, maji ni chanzo muhimu katika kilimo. Ili kuepuka kutumia maji ovyo na kuharibu vyanzo vya maji, Serikali iondoe kodi katika vifaa vyote vinavyotumika katika kilimo cha umwagiliaji ili bei iwe rahisi. Pia Serikali ijipange kuwatumia wataalam wa kilimo kuwasaidia wananchi.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni nchi ya tatu kwa mifugo lakini wafugaji wamesahauliwa katika kuwatafutia masoko nje ya nchi lakini Serikali inashughulikia wafugaji wakubwa. Naishauri Serikali iwatafutie wafugaji wa ngazi zote soko la uhakika la nyama, ngozi na bidhaa zote za wanyama wafugwao ili wapate kipato na kuweza kusomesha watoto na kuongeza pato la Taifa na pia kuboresha maisha yao.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata fursa ya kuchangia kwa maandishi. Naipongeza Kamati kwa kuandaa taarifa ya utekelezaji ya Kamati kipindi cha Januari, 2018 hadi Januari, 2019. Napongeza Serikali kwa juhudi inayofanya kuhakikisha inamtua ndoo mwanamke kwa kuhakikisha maji yanapatikana katika mwendo mfupi. Nina ushauri kuhusu DAWASA wazingatie umuhimu wa maji kutokana na ongezeko kubwa la watu na huduma ya majitaka.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kusambaza maji kwa asilimia 80 kwa wakazi wa Mjini Dodoma lakini tatizo kubwa ni uchakavu wa miundombinu katika maeneo mbalimbali. Uchakavu huo unasababisha miundombinu kupasuka mara kwa mara, hivyo kuleta

upotevu mkubwa wa maji na baadhi ya maeneo kukosa maji. Nashauri Serikali ione jinsi ya kukabiliana na kadhia hii.

Mheshimiwa Spika, mtandao wa kilomita 86 wa majitaka uliopo unaleta adha kubwa sana kwa wakazi wa Dodoma katika kupata huduma ya majitaka, kwani taarifa ya Kamati imebainisha mahitaji ni kilometa 250, hivyo kufanya huduma ya majitaka kuwa ya asilimia 20 tu. Ni budi Serikali ikatenga *budget* kuanzia mwaka ujao wa fedha 2019/2020 ili kuanza kutengeneza miundombinu ya majitaka.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Jiji la Dodoma linaendelea kukua ni budi Serikali ikafikiria kujenga mabwawa zaidi ya majitaka, siyo yale ya Mlimwa pekee na mpango wa DUWASA kujenga eneo la Nzuguni, ni budi Serikali ikaona umuhimu wa kutenga maeneo zaidi ya kuweka miundombinu ya majitaka kuwa kila eneo. Mfano, eneo la Nzuguni pawepo miundombinu itakayohudumia maeneo yaliyo karibu ili kuweza kuhimili huduma ya majitaka. Maeneo ya barabara ya Iringa kuwepo na mabwawa eneo hilo, pia barabara ya Bahi yawepo mabwawa ya majitaka ili kuendana na ukuaji wa Jiji la Dodoma.

Mheshimiwa Spika, suala la usindikaji wa maziwa bado lipo chini nchini kwetu. Hivyo ni budi Serikali ikaangalia jinsi ya kuhamasisha wafugaji kufuga kitaalam ili maziwa yapatikane kwa ajili ya matumizi ya wananchi na hasa watoto. Tanzania tuna kiwango cha chini cha matumizi ya maziwa kwa mwaka kwa asilimia 43. Hivyo tuna kila sababu ya kuhamasisha ufugaji wa kisasa ili wananchi wengi zaidi waweze kunywa maziwa. Kwa kuwa Dodoma ni miongoni mwa mikoa yenye mifugo mingi ikiwemo ng'ombe, Serikali ingehamasisha uanzishaji wa *collecting centers* za maziwa na hatimaye kupatikana kiwanda cha kusindika maziwa Mkoani Dodoma.

Mheshimiwa Spika, katika suala la kilimo, bado naendelea kuishauri Serikali kwamba Kituo cha Utafiti wa Zao la Zabibu Makutupora kiimarishwe ili ipatikane mbegu bora zaidi ya zabibu. Naendelea pia kuishauri Serikali kuhusu

uendelezaji wa zao la karanga katika Mkoa wa Dodoma ili tuweze kuwakwamua wananchi kiuchumi na pia kupunguza kuagiza mafuta kutoka nje ya nchi ili kuongeza pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI:** Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara ya Mifugo na Uvuvi pamoja na Kamati ya Bunge kwa kazi kubwa walizofanya kwa mwaka mzima. Naomba nizungumze mambo mawili tu:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, ni operesheni za mifugo na uvuvi. Naipongeza Serikali kwa operesheni ilizofanya katika uvuvi na mifugo kwani faida mojawapo ni kuongezeka kwa mazao hasa ya samaki. Samaki wameongezeka na viwanda vyetu vya samaki vinapata malighafi ya kutosha kuweza kuendesha shughuli zao.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, hatuwezi kuendesha Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi kwa kutegemea operesheni tu. Madamu operesheni hizi zimeweza kufanikisha ongezeko la mazao, Serikali sasa ijielekeze kwenye mipango ya muda wa kati na mrefu ili kuhakikisha sekta ya mifugo na uvuvi inatoa mchango mkubwa katika kukuza pato la Taifa badala ya kuchangia asilimia 3.8 tu.

Mheshimiwa Spika, leo ni miaka miwili Wizara hii imetimiza toka itolewe toka Wizara ya Kilimo lakini wananchi hatujaona kama kuna *long-term plans* inayolenga kuifanya sekta hii itajirishe watu wengi wanaojihusisha na mifugo na uvuvi. Miradi mikubwa kama bandari ya uvuvi, viwanda vya nyama, viwanda vya ngozi, ufugaji wa kisasa, *aquaculture* na kadhalika inaweza kusaidia sana kubadilisha namna ya ufugaji na uvuvi wa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, pili, kilimo. Kilimo chetu kinakua lakini kwa kasi ndogo sana. Mpaka Desemba, 2018 sekta ya kilimo ilikua kwa asilimia 3.6 tu. Mchango wake kwenye pato la Taifa ni asilimia 33.5, mchango ulio mkubwa zaidi ya mchango kutoka katika sekta zingine lakini mchango wake

kwenye mapato ya kodi ni chini ya asilimia mbili. Naomba Serikali iangalie ni vikwazo gani hasa vinavyozuia tusipige hatua kubwa kwenye sekta hii. Serikali iondoe mojawapo ya vikwazo vifuatavyo:-

(i) Bajeti ndogo ya maendeleo inayolengwa na hatimaye kupelekwa kwenye sekta hii.

(ii) Upungufu wa wataalam kwenye sekta.

(iii) Kutotilia maanani kilimo cha umwagiliaji.

(iv) Ukosefu wa masoko ya mazao na bei zisizotabirika.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja zote mbili zilizowasilishwa kwako, ahsante.

**MHE. SHAABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Spika, naanza kumpongeza Rais kwa maamuzi yake ya kuwapa maeneo wakulima na wafugaji wanaoishi kwenye maeneo ya hifadhi. Mwenyezi Mungu aendelee kumbariki Rais wetu.

Mheshimiwa Spika, Kamati yetu ilifanya ziara katika mapori ya BBK na kubaini mambo muhimu katika mapori yale na ndiyo maana wajumbe walio wengi waliona umuhimu wa Uwanja wa Ndege wa Chato maana uwanja ule utakuwa umeongeza thamani ya mapori yale. Sambamba na hayo, niipongeze Serikali kwa mapori yale kuyaweka ili yamilikiwe na *TANAPA.* Ushauri wangu Serikali itenge pesa ili *TANAPA* iweze kutengeneza miundombinu ya barabara ndani ya mapori hayo ili hifadhi zile za BBK ziweze kupitika kwa maeneo yote ya hifadhi. Pia, kutangaza hifadhi zetu zile kwenye vyombo mbalimbali na kuweka mazingira wezeshi ili wadau wawekeze kwa kujenga hoteli katika hifadhi zetu hizo.

Mheshimiwa Spika, tumetembelea katika hifadhi ya Mto Ruaha Mkuu, kwa kweli hali ya hifadhi hii inaweza kuwa mbaya zaidi kama juhudi za makusudi hazijachukuliwa kwani

Mto Ruaha unakauka. Tulivyouliza ni kwa nini mto ule unakauka tukaambiwa Mto Ruaha Mkuu umeanzia huko Mbarali, Mbeya na tukaambiwa kuwa kuna kilimo kikubwa kinachoendelea. Nashauri Serikali ichukue hatua ya haraka ya kuweka mipango ya kuhakikisha kilimo kinachoendelea huko Mkoani Mbeya kisiharibu maji ya Mto Mkuu wa Ruaha ili tusije tukaathiri hifadhi zetu pamoja na malengo mazuri ya Serikali ya umeme unaotaka kujengwa katika Bonde la Rufiji pamoja na kulinda urithi wetu, hasa wa hifadhi yetu ya Ruaha.

Mheshimiwa Spika, Hifadhi ya Mikumi ni muhimu sana, kwa hiyo, naomba niishauri Serikali yangu Tukufu ichukue maamuzi magumu kuhamisha barabara ile ipite pembeni ili kunusuru wanyama wetu wanaogongwa kila uchao, hatimaye wanyama wetu wataisha. Pia wasafiri wengi wanaopita maeneo yale wanafanya utalii wa bure bila kulipia lakini tukitoa barabara sehemu nyingine ile tunaifanya ni barabara ya kitalii na tutakusanya fedha na kuongeza mapato kwenye hifadhi ile.

Mheshimiwa Spika, nashauri *TFS* iwe mamlaka kamili kuliko kuendelea kuwa wakala kwani wakala huwa wanafanya vizuri. Kwa hiyo, wakipewa mamlaka kamili watafanya vizuri zaidi, hasa katika masuala ya kupanda miti maeneo yote yenye uhitaji pamoja na maeneo ambayo misitu yake imeungua kwa moto, hasa maeneo ya Wilaya ya Lushoto ambayo misitu ile iliungua miaka sita mpaka saba iliyopita, lakini mpaka sasa msitu ule haujaota tena. Kwa hiyo, niiombe Serikali yangu ikapande miti kwenye misitu ile ya Lushoto iliyoungua.

Mheshimiwa Spika, naomba niishauri Serikali yangu iruhusu mazao ya misitu yapite usiku kama ilivyokuwa nguzo za umeme kwani hii inazorotesha maendeleo ya wananchi pamoja na Serikali kukosa mapato. Niishauri Serikali yangu, tozo hizi za mazao ya misitu zipunguzwe kutoka 18 zibaki hata 9 kama mazao mengine yalivyopunguzwa tozo; kwa mfano kahawa, pamba, tumbaku pamoja na korosho.

Mheshimiwa Spika, naomba niishauri Serikali yangu Tukufu kuhusu Shirika la Nyumba la Taifa *(NHC).* Shirika hili kwa sasa linasuasua wakati shirika hili ni muhimu sana kwani limewakomboa Watanzania wengi, hasa wale ambao hawana uwezo wa kujenga nyumba. Kwa hiyo, niendelee kuishauri Serikali yangu kwamba ikamilishe taratibu zitakazoliwezesha shirika kupata fedha za kumalizia miradi iliyosimama ili iishe na kuleta tija kwa Serikali pamoja na kwa wananchi. Mungu ibariki Tanzania, Mungu mbariki Rais wetu, Mungu endelea kumpa afya na nguvu Rais wetu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaenda upande wa Serikali kusikia wanachangia nini, muda haupo upande wetu. Waheshimiwa Mawaziri nitawapa dakika kumi kumi lakini ataanza Mheshimiwa Kakunda dakika tano ili azungumzie kidogo habari ya mbolea.

Nilisikia kwenye michango jambo lile la asilimia 5 cess ya mti kule Mafinga na *cess* asilimia 5 ya Halmashauri ya mbao. Nilitaka kuisemea hii ya mti tu kidogo endapo bado sababu ni zilezile Mheshimiwa Waziri sikumbuki lakini enzi hizo nilipokuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi na Maliasili tulishauri hii cess ya mti unapokatwa iwepo na sababu yake ni kwamba ilikuwa inabakia kwa ajili ya *nurseries* kwa sababu ilikuwa miti inakatwa hela yote inaenda Hazina halafu hamna zinazorudi. Kwa hiyo, ile asilimia 5 ya *cess* ya mti ikawa inabakia kule kwa ajili ya kuwa na vitalu vingi zaidi vya kuotesha miti na bila *cess* hiyo nadhani leo Sao Hill tusingekuwa na shamba. Leo sijui kwa nini Kamati imepata tabu ya hizi *cess* mbili lakini utatufafanulia kama kuna tatizo.

Waheshimiwa Wabunge, sasa tuanze na Mheshimiwa Kakunda, atafuata Waziri Waziri wa Maji, Mheshimiwa Profesa Mbarawa, dakika tano.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Spika, nipongeze kazi ya Kamati mbili na wachangiaji wote wamefanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Spika, la kwanza, viwanda vyetu ya *Agro-Processing* ambavyo ni *priority* namba moja; viwanda vya kubangua korosho, vya kusindika alizeti, ufuta, pamba, kuzalisha mafuta ya kula, viwanda vya nguo, viwanda vya bidhaa za ngozi vinahitaji hatua madhubuti za kuvilinda dhidi ya ushindani wa aina mbili. Kwanza, ushindani wa bei ya malighafi kwenye soko unaosababisha viwanda vyetu kukosa malighafi na pili, bidhaa zinazozalishwa kwenye viwanda hivyo kushindwa kukabiliana na bidhaa za aina hiyo hiyo zinazoagizwa kutoka nje ambazo hata tukitoza kodi asilimia 35 bado bei ya bidhaa hizo sokoni inakuwa ndogo kwa sababu huko zilipotoka zilizalishwa kwa mamilioni ya tani kwa gharama ndogo ya jumla kwa ajili ya soko zima la dunia kulinganisha uzalishaji mdogo wa hapa nchini wa mia na maelfu ya tani ambayo yanalenga soko dogo la ndani ya nchi.

Mheshimiwa Spika, kwa hali hiyo, upo umuhimu mkubwa wa kuchukua hatua za lazima. Kwanza, kuhakikisha viwanda vyetu vinakuwa na uhakika wa kupata malighafi na hatua ambazo zitapendekezwa na wataalam zitatusaidia sana kupata maamuzi sahihi kwa ajili ya kulinda viwanda vyetu vya ndani. Pili, tunahitaji kutengeneza utaratibu wa makusudi wa kukabiliana na wimbi la waingizaji kutoka bidhaa kutoka nje kwa kutumia viwango maalum vya kikodi vitakavyotozwa kwa utaratibu wa kutoza kwa tani badala ya asilimia ambayo itasaidia kulinda viwanda vyetu vya ndani.

Mheshimiwa Spika, kilimo chetu kinahitaji mbolea kama kweli tunataka kuongeza uzalishaji kwenye sekta ya kilimo. Uagizaji wa mbolea kutoka Ulaya hadi mbolea imfikie mkulima umekuwa ukigharimu fedha nyingi mno kwa mkulima. Serikali imeshawakaribisha wawekezaji kujenga viwanda vya mbolea hapa Tanzania, tunachotaka sisi ni ukweli na uwazi kwenye uwekezaji. Tunajua mwekezaji anahitaji mtaji ili awekeze lakini mtaji ule sisi tuna maslahi nao tunataka tujue, mtaji ule ndiyo unaotafsiri gharama za mitambo, majengo, teknolojia, uendeshaji ikiwepo kulipa wafanyakazi na usafiri na usafirishaji hadi kwenye soko. Pia

ni lazima tujue tunamsaidiaje mwekezaji kupata malighafi anazohitaji kwenye kiwanda kutoka ndani ya nchi na kwa gharama gani?

Mheshimiwa Spika, ili tujue vizuri lazima tulinganishe *model* yake ya kifedha na ile *model* ya mfano ambayo imetengenezwa na wataalam wa Serikali ili tuweze kubaini hasa hasa je kuna udanganyifu au hakuna kwa sababu bila kufanya hivyo tutaingia kwenye machaka ambayo tuliwahi kuingia zamani. Kwa mfano, katika *model* moja ya kifedha iliyochambuliwa tulikuta gharama za wafanyakazi wote 1,000 ikiwemo wafagizi wote wamewekewa mshahara wa kila mfanyakazi dola 3,000 yaani Sh.6,430,000 jambo ambalo ni kinyume cha uhalisia kwenye ukweli na uwazi. Kwa hiyo, lazima tuwe makini mno ili kuhakikisha tunalinda maslahi ya Taifa kikamilifu, viwanda vya mbolea vinahitaji gesi asilia kwa mfano na mali ghafi nyingine lazima tujue gezi asilia ataipata kwa gharama gani na faida ya nchi itakuwa kiasi gani.

Mheshimiwa Spika, mwezi huu Februari tunaendeleza mazungumzo na wawekezaji kwenye eneo hili la viwanda vya mbolea na mwelekeo ni mzuri naamini tutafikia makubaliano mazuri. Haiwezekani tukubali kiwanda ambacho eti kitapata hasara kwa miaka zaidi ya 10 wakati ambako ile *financial model* inaonyesha kuna udanganyifu ambao utamfanya mwekezaji yeye aanze kwa kupata faida ya dola kama 600,000 kabla hata hajaanza uzalishaji halafu ile mizania yake itasoma hasara kwa zaidi ya miaka 10. Kwa hiyo, sasa hivi Serikali ya Awamu ya Tano ipo makini katika kujenga utaratibu wa *win win situation* ili tunapoingia kwenye kiwanda lazima tuhakikishe faida ya nchi inaonekana kwa wazi na uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Profesa Mbarawa, Waziri wa Maji, dakika kumi.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWANGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kuchukuwa fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele yako na kuchangia kwenye hoja hii ya Kamati iliyowasilishwa mbele yetu. Napenda kushukuru sana Kamati yetu kwa kazi nzuri wanayofanya ya kutushauri na kwa kiasi kikubwa Kamati hii imetusaidia sana na tutaendelea kushirikiana nayo kwa maslahi ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama tulivyosikia michango mingi imezungumzwa hapa kuhusu sekta ya maji kwa sababu maji ni jambo muhimu sana na sote tunafahamu maji ni uhai, maji ni afya, kama nilivyosema juzi maji kilimo, maji ni viwanda, maji ni ustaarabu, maji ni kila kitu, bila maji huwezi kufanya jambo lolote.

Mheshimiwa Spika, nitazungumzia kama mambo matano. Jambo la kwanza ambalo Kamati limezungumzia, ni kuhusu huduma ya maji mjini na vijini. Jambo la pili nitazungumzia kuhusu Mfuko wa Maji nitazungumzia na majitaka halafu mwisho nitazungumzia. Miji 25 ambayo inapata wafadhili kutoka Serikali ya India. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama tulivyoelewa kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi, imesema waziwazi itapofika mwaka 2020, wananchi wanaokaa kwenye mikoa lazima wapate maji kwa asilimia 95, wanaokaa kwenye miji ya Wilaya lazima wapate maji kwa asilimia 90 na kwenye vijiji lazima wapate maji asilimia 85.

Mheshimiwa Spika, hivi tunavyozungumza, kwa wananchi wanaokaa kwenye vijiji, wanapata maji asilimia 64.8; na hivi tunavyozungumza, miradi takriban 1,652 imekamilika na miradi 500 sasa inaendelea kutekelezwa. Miradi inayotekelezwa sasa hivi, kwa mfano, Mkoa wa Arusha tuna mradi mkubwa pale ambao unagharimu takriban shilingi bilioni 520. Longido tuna mradi mkubwa unagharimu shilingi bilioni 15.

Mheshimiwa Spika, naendelea kwa upande wa Mkoa wa Tabora, Nzega, Igunga, tuna mradi unaogharimu takriban shilingi bilioni 604. Kwa upande Magu, Misungwi na Lamadi, tuna mradi unaogharimu takribani shilingi bilioni 42.6. Mwanza kule maeneo ya milimani tuna mradi unaogharimu shilingi bilioni 39.2. Kama nilivyosema juzi, huko Bariadi tuna mradi unaogharimu takribani shilingi bilioni 491.9; na hapa Dodoma tuna mradi wa maji unaogharimu shilingi takriban bilioni 7.288.

Mheshimiwa Spika, nikitaja miradi ni mingi na sitaweza kuitaja yote, lakini kwa ufupi tu, Serikali tunatumia matrilioni ya pesa kuhakikisha kwamba tunamaliza tatizo la maji katika nchi yetu hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na *issue* ya majitaka. Kweli majitaka miaka ya nyuma ilikuwa siyo kipaumbele, lakini sasa Wizara ya Maji tumeamua kwamba lazima tupambane na tupeleke huduma ya majitaka, kwa sababu ni muhimu na kama tunavyojua majitaka yanaweza kupunguza matatizo mengi kwa mfano, maradhi na mambo mengine.

Mheshimiwa Spika, Dar es Salaam pale tunavyozungumza, tuna miradi miwili ya majitaka, mmoja unagharimu takribani shilingi bilioni 239.3 na mradi mwingine unagharimu shilingi bilioni 149.4; kule Arusha tuna mradi wa maji unagharimu takribani shilingi bilioni 116.99 ambao unaendelea; huko Musoma tuna mradi wa majitaka unagharimu takribani shilingi bilioni 30.

Mheshimiwa Spika, kwa ufupi, katika miradi yetu yote ya maji sasa hivi tunahakikisha *component* ya majitaka inaingizwa ili kuhakikisha tunaendana na Sera yetu ya maji safi na majitaka.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja nyingine kuhusu Mfuko wa Maji. Tumetengeneza kanuni ambazo zimesema wazi wazi angalau asilimia 65 ya fedha za Mfuko wa Maji lazima ziende vijijini. Kwa sababu vijijini ndiyo kwenye

changamoto kubwa sana ya maji. Bila kutatua tatizo la maji huko vijijini, itakuwa hatukuwasaidia Watanzania hasa wanaokaa vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuanzia mwezi Julai, 2018 mpaka mwezi Desemba, 2018 tumepokea takribani shilingi bilioni 88 za Mfuko wa Maji. Kati ya pesa hizo, shilingi bilioni 61.6 zimekwenda vijijini, yaani asilimia 70; na shilingi bilioni 26.4 asilimia 30 zimekwenda mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile tumepokea shilingi bilioni 4.73 kutoka pesa za nje kwa ajili ya miradi ya maji. Kwa ujumla, kutoka Julai mpaka Desemba mwaka 2018 tumepokea takribani shilingi bilioni 92.7. Kati ya pesa hizo, Mheshimiwa Pascal aliyosema, kule Jimboni kwake kuna mradi wa maji wa Mloo ambao unajengwa kwa shilingi takribani milioni 465 ambao hivi tunavyozungumza wananchi wanapata maji na Mkandarasi tumemlipa shilingi takriban 265. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna mradi mwingine wa maji kwenye Jimbo lake vilevile, mradi wa Isaka, Itewe unagharimu takribani shilingi bilioni 1.6 na kila akitoa mgao tunampelekea Mheshimiwa Mbunge kwa kuwa sisi hatuchagui Chama, Watanzania wote ni wamoja na nia yetu ni kuwapelekea Watanzania wote huduma majisafi na salama; kama wako mjini kama wako vijijini, kama wako Chadema au CCM, wote tutawapelekea majisafi na salama.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na *issue* iliyozungumzwa pia kuhusu madeni makubwa ya Taasisi za Serikali kwa mamlaka. Hili kweli ni changamoto, lakini tumepanga kuanzia sasa hivi, kila tunapopeleka kwenye huduma za maji hizi tunafuatia bili zetu na vile vile tumeamua sasa tuingize vifaa vya kisasa, yaani *Pre-paid meter* kuhakikisha kwamba kama hukulipa, inapofika mwisho wa mwezi maji yanakatika. Tunaamini tukiweka mfumo huu wa *pre-paid meters* Wizara zote na Taasisi zote zitaweza kulipa maji au bili za maji bila matatizo.

Mheshimiwa Spika, tunataka kuwekeza kwenye Wizara zote za Serikali; kwenye Mji wa Serikali, Ofisi zote tutaweka *pre-paid meters* ili tuhakikishe kwamba kama Waziri au Wizara haikulipia maji inakatiwa. Tunaamini tukifanya hivi, kila Wizara italipa bili zake kwa wakati bila kuchelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na suala lingine kuhusu taarifa ya mchakato wa kupeleka huduma ya maji miji 26 ambao unafadhiliwa na Benki ya *Exim Bank* ya India, ambao unagharimu takribani dola za Kimarekani milioni 500 sawa na shilingi za Kitanzania trilioni 1.2. Miji 26 hiyo ni Muheza, Korogwe, Makonda, Pangani, Ifakara, Kilwa Masoko, Makambako, Njombe, Songea, Chunya, Rujewa, Mafinga, Manyoni, Sikonge, Singida, Mpanda, Urambo, Kaliua, na mingineyo.

Mheshimiwa Spika, hatua tuliyofikia sasa hivi, kwanza mchakato ulianza tarehe 17 mwezi wa Nane mwaka 2018; na wakati huo tulitangaza *tender. Tender* hiyo ilitangazwa huko India na makampuni 10 ya India yaliomba kwa sababu huu ni mradi ambao unafadhiliwa kwa mkopo kutoka India. Mchakato ulifanyika na tukapata makampuni manne; na hivi sasa tumeshafungua zabuni kwa ajili ya kumpata Mkandarasi mmoja. Kesho wataendelea na mchakato wa kupitia *Financia Bill* kwa ajili ya *finally* ya kumpata Mkandarasi ambaye ataanza kufanya usanifu na kutengeneza *Tender Document* kwa ajili ya miji hiyo 26. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wajumbe wote hawa ama Wabunge wote...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante Profesa.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, la mwisho, Waheshimiwa Wabunge wote ambao wana miradi hii ya miji 26 tumetayarisha *group la WhatsApp,* kila

tunalofanya tunawapa taarifa na ninaamini Wabunge wote hawa wanajua nini Serikali inafanya kuhusu miradi hii na tutaendelea kuwafahamisha mpaka pale ambapo miradi hii utakapokamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja, ninai-*support* sana hoja ya Kamati yangu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Prof. Mbarawa. Sasa atafuata Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Hasunga. Nadhani naweza kuwa-*accomodate* kwa dakita 15. Jaribu kutumia dakika 15 tu.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba nichukue nafasi hii kukushukuru kwanza kwa kunipa hii nafasi, lakini nichukue nafasi hii pia kuwashukuru Wabunge wote ambao kwa namna moja ama nyingine mmechangia katika taarifa ya Kamati hii. Pia naomba niunge mkono taarifa ya Kamati zote mbili, lakini kipekee niwapongeze Wajumbe wa Kamati ya Kilimo. Ripoti yao imesheheni mambo mengi mazuri na ya msingi sana ambayo sisi kama Serikali tutayafanyia kazi na tutaona namna ya kuweza kushirikiana na Waheshimiwa Wabunge hawa ili tuweze kufikia hii azma ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee namshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pamoja na Viongozi wengine wote Wakuu pamoja na Mawaziri kwa kuendelea kukiunga mkono kilimo cha nchi hii. Hapa Waheshimiwa Wabunge wote naomba mniunge mkono kwa sababu ningi wote ni wadau wa kilimo. Kama muda ungetosha, najua mngepata nafasi ya kuzungumza. Wote hapa ni wadau wa kilimo, wote hapa tumekula chakula ndiyo maana tunaongea. Kwa hiyo, wote kwa namna moja ama nyingine ni wadau wa kilimo.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingi zimetolewa, lakini naomba nianze kwa hoja chache, bahati mbaya naona Mheshimiwa Zitto hayupo, lakini naomba nianze na

hii hoja yake. Hoja ya kwanza ambayo ameisema, ni kuhusu chanzo cha fedha ambacho Benki yetu ya Kilimo imepata, labda naomba niweke takwimu vizuri, siku fulani hapo juzi nilisema, Benki yoyote duniani inayoitwa Benki ya Biashara, benki yoyote inategemea mitaji yake katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kuna mtaji unaowekeza na wenye hisa na ukiangalia mtaji wa wenye hisa, ni mtaji ambao unawekezwa na ule mara nyingi ni kwa sababu ya taratibu za kibenki inakuwa kama dhamana; na mara nyingi unawekwa Benki Kuu. Benki baada ya kuanzishwa, iki-*comply* na zile taratibu za kuanzishwa, inatakiwa itafute fedha mahali popote zilipo nyingi ilete iweke na ipeleke mahali zinapotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitoe mfano, nianze na *CRDB.* Ukichukua mtaji wa *CRDB* wa wenye hisa, ni shilingi bilioni 65,296; lakini angalia mali walizonazo, wana mali zaidi ya shilingi trilioni 6,038,571. Wana shilingi trilioni sita, mtaji shilingi bilioni 65. Kwa hiyo, pale siyo kwamba wanafanya biashara kwa kutumia hela za mtaji, kazi yao ni ku *mobilize* fedha kutoka ziliko, wanakuja kufanya biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukichukua *NMB,* wana mtaji wa shilingi bilioni 20, lakini angalia mali zao walizonazo; *asset* za *NMB* ni zaidi ya shilingi trilioni tano. Ni shilingi trilioni 5,706,110. Kwa hiyo, ina maana hawa wanafanya kazi ya biashara. Vivyo hivyo Benki yetu ya Kilimo, ina mtaji mkubwa kuliko hata *NMB.* Benki yetu Serikali iliwekeza shilingi bilioni 60, nayo inaendelea kufanya kazi na kutafuta fedha na kuendesha na tunataka hii benki iendelee kutoa mikopo kwa wakulima wa nchi hii ili kilimo kiweze kusonga mbele.

**MBUNGE FULANI:** Shule hiyo!

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, kwa kuanzia ndiyo maana benki hii imetafuta fedha. Ilikopata mimi sijui, imetafuta. Ninachokijua, wametoa fedha kwenye Bodi yetu ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko. Wametoa mkopo; na

mkopo lazima ulipwe. Bodi yetu inalipa. Tumekopa Benki ya Kilimo ambayo kazi yake ni kufanya biashara.

Mheshimiwa Spika, nataka niseme kwamba kazi yetu sisi ni kukopa na hiyo Bodi yetu ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko imekopa, inaendelea kukopa, inafanya biashara, imenunua korosho, kazi yake ni kununua, kuchakata na kwenda kuziuza hizo korosho. Hiyo tutaifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu nilotaka kulizungumzia na bahati nzuri amesema Mheshimiwa Zitto na Waheshimiwa Wabunge wengine wamechangia, naomba niseme, Serikali yoyote duniani iko pale kwa mujibu wa Katiba na kwa mujibu wa sheria.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tusikilizane. Hii ni shule, msikilize vizuri. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, kazi ya Bunge ni kutunga sheria. Sheria hizo zikishatungwa, kazi ya Serikali ni kuzitekeleza hizo sheria. Sasa mwaka 2009, Bunge lako Tukufu lilitunga sheria inayohusu Zao la Korosho. Ilipotunga sheria, iliweka vifungu mbalimbali. Kwa sababu ya muda, naomba niweke vizuri ili tuelewane. Ukisoma hiyo Sheria ya Bodi ya Korosho, Kifungu cha 12 (1) kinasema hivi: "*every cashew nut dealer, being a buyer, processor, importer, exporter, wherehouse owner or operator shall be required to register with the Board.*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mtu yeyote anayegusa, anayeshughulika na korosho kwa namna yoyote ile, lazima kwanza aandikishwe na Bodi. Ukisoma Kifungu cha 15(4) kinasema hivi: "a person shall not buy," naomba Mheshimiwa Zitto uishike vizuri. *"A person shall not buy, sell, process, own or operate a wherehouse or exports any cashew nuts on commercial basis without a licence issued by the Board."* Huu ndiyo msingi ambao tunautumia sisi kusimamia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, unapokuja na hoja unasema sijui kuna Kangomba sijui wafanye nini, mwaruhusu, kazi yako ya kwanza kama Mbunge, itisha turekebishe hii sheria. Kama hatujarekebisha, sitaisimamia hii. Kama unataka korosho zinazotoka nje, zinazotoka popote zije, zifuate utaratibu ulioandikwa kwenye sheria. Kwa hiyo, huo ndiyo msimamo ambao sisi kama Serikali tutaendelea kuusimamia na tutaendelea kuhakikisha kwamba haya yote yanazingatiwa.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumzia kuhusu kilimo, nami nakubaliana kabisa. Zipo hoja za msingi mlizosema namna ya kuboresha kilimo chetu. Kilimo chetu hiki ili tuweze kukiboresha vizuri, jambo la kwanza ambalo lazima tuangalie ni mifumo yetu ya pembejeo nchini. Hilo nakubaliana na Kamati imetoa maoni, imeshauri, tutayafanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, inaendana na tija; ni ukweli usiofichika. Kwenye kilimo chetu, tija bado iko chini. Ukiangalia tija bado iko chini; ukiangalia upatikanaji wa mbegu bora, bado hata hatujakaa vizuri. Hili ndiyo suala tunalolifanyia kazi. Pembejeo viuatilifu na madawa mengine hivi vyote ndiyo msingi, lakini pia kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, watu wetu katika maeneo mengi, ukiangalia mashamba tunayolima yaliyo mengi, uzalishaji wake uko chini, tija iko chini, ndiyo maana tunaona kuna hasara. Kazi yetu kama Wizara, ni kuhakikisha kwamba tunafanya utafiti wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, labda niliseme hili, wengi wamesema kwa mfano kuhusu mbolea, nami nakubaliana. Wengi wanasema kuhusu pembejeo, lakini kazi ya kwanza ambayo tunatakiwa tuifanye na ambayo sasa tunaifanya, naomba niliambie Bunge lako hili, ni kufanya utafiti wa ardhi yote ya nchi hii ya kilimo ili kuiona ina virutubisho gani? Ina kitu gani kinachokosekana ili tujue aina sahihi ya pembejeo zinazohitajika kwenye lile eneo. Siyo suala la ku-*apply* tu mbolea, ni suala la lazima kufanyike utafiti.

Mheshimiwa Spika, Kituo chetu cha Mlingano kile cha Tanga karibu kinakamilisha hiyo kazi ya kufanya *mapping.* Tukishajua hilo, tutajua aina ya mbolea inayotakiwa, tutajua kumbe inawezekana siyo hiyo *CAN* tunayoisoma au siyo *DAP.* Lazima tuangalie ni madini gani yanakosekana pale, ndiyo tutengeneze, ndiyo tulete hiyo mbolea.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, mtazamo wa mbolea sasa hivi ndiyo ulioharibu ardhi kwa kiwango kikubwa katika nchi yetu. Sasa hivi wataalam wanasema, inawezekana tukifanya utafiti tutahitaji kuzalisha chokaa ya kutosha ambayo iko nyingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwapongeze, Dodoma kuna kiwanda kinazalisha chokaa. Ile chokaa tungekuwa na uwezo, baada ya kufanya utafiti wa ardhi yetu, tukaenda tukaitumia kwenye mashamba yetu, tusingehitaji kutumia mbolea hata siku moja. Kwa sababu kutumia mbolea maana yake nini? Ukisoma ile mbolea ni *sulpher* sijui *nitrogen;* ni madini yaliyokosekana kwenye ardhi.

Mheshimiwa Spika, maana yake nini? Maana yake uchachu *(acid)* uko juu. Sasa ili kuupunguza uchachu, unahitaji *alkaline.* Kwa sababu unahitaji *alkaline*, ile *lime* ndiyo inaweza ikapunguza hicho kitu chote kikapotea. Kwa kwa mantiki hiyo, inawezekana tusihitaji kabisa hizo mbolea, tutaweka mkazo katika kuhakikisha hiki kiwanda kinazalisha chokaa ya kutosha na tutoe elimu kwa wananchi ili waweze kuanza kujua kutumia chokaa badala ya kufikiria tu kununua mbolea.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana kwamba kilimo ndiyo kitatoa mchango mkubwa kwenye viwanda vyetu ambavyo tunasema, nasi kama Serikali tutaendelea kushirikiana kwa pamoja kuhakikisha kwamba viwanda vyetu vinapata malighafi. Sote tunajua, viwanda vyetu vinategemea asilimia 66.5 ya malighafi zinazotokana na kilimo.

Mheshimiwa Spika, kazi yetu sisi sasa Wizara ya Kilimo ni kukaa na wenzetu wa Viwanda ili watuambie ni aina gani

ya malighafi wanaihitaji yenye ubora wa kiwango gani kusudi tuhamasishe uzalishaji unaoendana na mahitaji ya soko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na wale wote waliosema kuhusu masoko, siku za nyuma hatukuweka mkazo wa kutosha, hatukuweka msisitizo wa kutosha kwenye upande wa masoko, na hapa ndiyo tatizo. Wananchi wengi walikuwa wanazalisha mazao lakini walikuwa hawajui wapi kwa kuuza. Ndiyo maana kama Wizara kwa kushirikiana na Wizara na taasisi nyingine sasa hivi tumeweka mkazo kwamba lazima suala la masoko lipewe kipaumbele ili kujua masoko ya kila zao yako wapi na wananchi wanapoambiwa kuzalisha basi tuwaambie hili soko liko huku na bei zake ziko hivi. Hiyo tutakuwa tayari tume-*link* pamoja uzalishaji na masoko yaliyoko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimesikitika mdogo wangu Mheshimiwa Haonga anaposema hatujashughulikia mazao, tumeshughulikia mazao yote. Tulipoingia tumesaini mkataba mkubwa wa tani 36,000 ambapo Mheshimiwa Rais wetu ameshuhudia wa kununua mahindi ambapo *WFP* wamenunua; lile lote ni soko la mahindi. Unaposema kwamba eti hatujashughulikia utakuwa unazungumza vitu vya ajabu. Wizara kila mahali tunatafuta masoko, sasa hivi tumepata soko DRC lakini tumepata vikwazo mahali pa kupitisha kule nchini Zambia ambapo tunaendelea na mazungumzo ili kusudi watu wetu waende kuuza kule nchini Kongo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wamezungumzia Tume ya Ushirika kwamba inawafanya kazi wachache, haina uwezo, nakubali kweli wafanyakazi ni wachache na kazi yetu kubwa ni kuijengea uwezo Tume ya Ushirika ili iweze kufanya kazi iliyokusudiwa kwasababu ndiyo tarajio la wakulima wengi wa nchi hii na ndiyo njia pekee ya kuweza kutatua changamoto zao mbalimbali. Haya matatizo tunayozungumzia kwenye mfumo wa usambazaji wa pembejeo na mambo mengine ni kwa sababu ushirika wetu

haujasimama imara. Ni imani yetu tukiusimamisha vizuri haya mambo yatapungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo basi, mwaka huu tunategemea kama mambo yataenda kama tulivyopanga tutapata watu 86 ambao tutawaajiri kule kwenye ushirika. Hata hivyo, bado tunaendelea kushauriana na TAMISEMI ili wale wanaushirika walioko chini ya TAMISEMI waweze kuhamishiwa kwetu kusudi waweze kufanya kazi za ushirika.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru lakini kama zitahitajika taarifa zaidi tuko tayari kutoa taarifa ili Bunge lako liweze kujua na takwimu nyingi bado tunazo. Nakushukuru sana kwa nafasi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Hasunga. Tunaendelea na Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla dakika 15 pia.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa fursa hii. Pia nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa fursa hii pia na naomba nitoe mchango wangu kwanza kwa kuunga mkono hoja iliyowekwa mbele yetu na Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii na kuwahakikishia kwamba kwa kuwa tunafanya kazi vizuri na kwa ukaribu, tutaendelea kushirikiana kuhakikisha mapendekezo yaliyotolewa na Kamati yao tunayafanyia kazi kwa wakati muafaka na kwa namna ambayo wenzetu Wajumbe wa Kamati na Bunge litaridhia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba nianze kwanza kwa kuchangia kuhusu mkakati wa Serikali ya Awamu ya Tano wa kufufua Shirika la Ndege, kujenga viwanja vya ndege nchini na namna ambavyo unaungana moja kwa moja na jitihada za kukuza utalii katika Taifa letu.

Jana zilizuka hoja nyingi kuhusu Uwanja wa Ndege wa Chato na unaweza ukazielezea kiurahisi sana kama utazungumzia Mkakati wa Serikali ya Awamu ya Tano wa kufungua kiutalii *Circuit* ya Magharibi na Kaskazini Magharibi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mkakati huu unaenda sambamba na mkakati wetu wa kufanya ukarabati na utanuzi wa Kiwanja cha Ndege cha Nduli, kilichopo pale Iringa na kujenga viwanja vingine viwili vya ndege pembezoni mwa Hifadhi ya Taifa ya Ruaha, ambayo kwa sasa ni hifadhi ya saba kwa ukubwa duniani na kwa Afrika inashika namba nne na kwa Tanzania ni hifadhi ya kwanza kwa ukubwa. Ndipo mahali pekee kwa haraka haraka ukienda kutembelea unaweza ukawaona *predators* wakiwa *in action.* Unaweza ukaona simba wakikimbiza mbogo, wakikamata na kula ni matukio ya kawaida kabisa ukiwa pale *Ruaha National Park*.

Mheshimiwa Spika, sambamba na mkakati huu, katika Awamu ya Tano tunakusudia kufungua pia *Circuit* ya Kusini kwa upande wa Selou kwa maana ya kujenga Kiwanja kingine cha Ndege cha kiwango cha sakafu ngumu Kaskazini mwa Pori la Akiba la Selou maeneo ya Matambwe, uzuri wewe ni mwenyeji sana kule ili kufungua utalii wa picha upande huo. Mikakati yote hii kwa ujumla wake inaenda sambamba na mikakati inayotekelezwa na Serikali ya kufufua Shirika la Ndege la Taifa kwa kununua ndege lakini pia kufungua safari za moja kwa moja kwenye masoko mbalimbali ya utalii na kuyaunganisha na Jiji letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikianza na jitihada zetu za kupandisha hadhi Mapori ya Akiba ya Burigi, Biharamulo, Kimisi, Ibanda na Rumanyika kwenda kwenye hadhi ya *National Park*, muda si mrefu tutafikisha mbele yako mapendekezo ya Serikali baada ya kukamilisha mchakato ambao tupo katika hatua za mwisho ili tupate ridhaa ya Bunge lako Tukufu kupandisha hadhi Mapori haya matatu na kuyaunganisha kuwa *National Park* moja ya *Burigi Chato National Park*, ambako itachukua yale maeneo yaliyokuwa Mapori ya Akiba ya Biharamulo, Burigi na Kimisi, pia

kupandisha hadhi Pori la Akiba la Ibanda ili kuwa *Ibanda National Park* na Pori la Akiba la Rumanyika ili kuwa *Rumanyika National Park*.

Mheshimiwa Spika, *Circuit* hii itakamilika kwa kuunganisha na Hifadhi ya Taifa ya Rubondo ambayo iko ndani ya Ziwa Victoria na Hifadhi ya Taifa ya Saanane na tutaweza kuiunganisha na *Circuit* ya Magharibi pamoja na Hifadhi ya Taifa ya Mahale na Hifadhi ya Taifa ya Gombe. Pia ndani ya Serikali tuko katika mchakato kuona kama tunaweza tukapandisha hadhi eneo la kiini cha Pori la Akiba la Moyowosi, Kigosi na Ugala pale pembezoni mwa mto ili pia yawe Hifadhi ya Taifa na tuweze kufanya utalii wa picha. *Circuit* hiyo sasa itakamilika kwa upande mmoja. Vilevile *Circuit* ya Kusini tutaweza kuiunganisha vizuri kwa kuwa na ndege ambazo zitaweza kutua na kufanya safari zake za kawaida kila siku kwenye maeneo ya Msambe, kama nilivyosema, upande wa Kaskazini Magharibi mwa Hifadhi ya Taifa ya Ruaha, pia katikati ya Hifadhi ya Taifa ya Mikumi pamoja na hiyo *Circuit* ya Kaskazini ya pori la akiba la Selou.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ukiangalia kwa undani sana unaweza ukaona tunapowekeza kwenye ndege na viwanja vya ndege ni kama vile tunatupa pesa nyingi sana kwenye jambo ambalo pengine haliwagusi wananchi moja kwa moja. Nimesikia michango ya Waheshimiwa Wabunge, hususan wanaotokea ng'ambo ya pili katika eneo hilo na mimi napenda kupingana nao na pengine kuwapa maelezo kwamba sekta ya utalii inachangia kuingiza pato la Taifa kwa asilimia 17.6 na ndiyo sekta inayoongoza kwa kuingiza fedha za kigeni hapa nchini kwa asilimia 25 ya fedha zote za kigeni zinazoingia nchini. Pia sekta hii inachangia Dola za Kimarekani bilioni 2.4 katika uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Utafiti wa Benki ya Dunia wa mwaka 2014 ulisema kama nchi yetu itafanya vizuri katika eneo la maliasili na utalii kufikia mwaka 2025 tutaweza ku-*tap* kutoka kwenye sekta hii mapato yanayofikia Dola za Kimarekani bilioni 16,000. Kipindi hicho inakadiriwa kwenye taarifa hiyo kubwa kabisa inayohusu Hali ya Uchumi wa

Tanzania ya Benki ya Dunia, kwamba watalii kwa mwaka huo watakuwa wamefikia kiasi cha milioni 8 leo hii tuko hapo karibia milioni 1.5.

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo, utaona Waheshimiwa Wabunge wengi wanachangia kwamba pengine jitihada za kutangaza vivutio hazijafanyika ipasavyo, pengine tunahitaji kujipanga zaidi; tunakubaliana nao lakini pia Serikali imeshachukua hatua nyingi sana katika kutangaza vivutio vyetu na ndiyo maana idadi ya watalii inaongezeka mwaka hata mwaka. Mwaka jana tu Mheshimiwa Waziri Mkuu alitufungulia *channel* maalum ya utalii *(Tanzania Safari Channel)* tumepokea mapendekezo ya Kamati kwamba tujitahidi kuifanya iweze kuonekana nje ya nchi na ndizo jitihada ambazo kweli kwa sasa tunaendelea kuzifanya ili iweze kuonekana kwa wingi zaidi nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwenda kwenye *show* mbalimbali ambazo tunawakilishwa na Bodi yetu ya Utalii bado tuna mikakati mingine mahsusi ya kukuza sekta ya utalii kwa kutumia watu mashuhuri wanaokuja hapa nchini. Pia kutangaza kwenye michezo kutangaza, vituo vya mabasi na treni kule nje, ni mikakati ambayo tunaiwekea hatua mbalimbali za utekelezaji. Pia kuweka mabango makubwa katika maeneo yote ambayo ni mageti ya kuingia katika nchi yetu kuanzia viwanja vya ndege na hata pale maeneo ya bandarini; tuna mradi huo ambao tuko katika hatua ya kuutekeleza na muda si mrefu kila sehemu utakuwa ukizunguka ukiangalia hivi unaona simba, tembo na kadhalika. Hata kwenye ile *round about* kubwa ya hapa Dodoma tunakusudia kuweka *television* kubwa kabisa ambayo itakuwa inaonesha *live* kila kinachoendelea ndani ya *creator*. Kwa hivyo, tukifanikiwa kufanya hilo, kila atakaye kuwa anaingia katika Jijini la Dodoma ataweza kuona vivutio vyetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, napenda pia kuzungumzia kuhusu Mradi wa *REGROW* ambapo wenzetu wanadhani kwamba unasuasua lakini pia Kamati yetu imezungumzia sana kuhusu ucheleweshaji wa utekelezaji wa

mradi huu. Mradi huu unatekelezwa kwa mkopo kutoka Benki ya Dunia ambapo nchi yetu inakopeshwa Dola za Kimarekani milioni 150. Fedha hizi ni nyingi na ni mkopo na mkopo maana yake ni lazima ulipwe.

Mheshimiwa Spika, nilipoteuliwa kuwa Waziri kwenye Wizara hii nilisoma lile andiko la mradi na nikaona kwamba haukukaa zaidi kibiashara. Kwa sababu ukiuangalia unaona haujahusisha ujenzi wa barabara kutoka *Nduli Airport* pale Iringa kwenda mpaka kwenye geti la Msambe kuingia *Ruaha National Park*, hakuna mradi wa kuukarabati Uwanja wa Ndege wa Nduli lakini pia ulikuwa ujenge viwanja vidogo vidogo vya hadhi ya changarawe katika maeneo yote hayo ambayo nimeyazungumzia ya *Circuit* hii ya utalii ya Kusini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wewe ni Mhifadhi unafahamu, kila mkitaka kukarabati viwanja vya changarawe lazima mchukue *material* humo humo ndani ya hifadhi yenyewe maana mnazidi kuharibu mazingira lakini pia mnajenga mwaka huu baada ya mwaka mmoja mnaanza ukarabati. Nikasema mradi ulipokuwa *designed* haukukwa *commercially sound* kwa kiasi kikubwa, kwa hivyo, tukasema lazima tuufanye huu mradi uwe wa kibiashara. Ili kuufanya mradi ule uwe wa kibiashara tuliona ni lazima pajengwe viwanja vya ndege ambavyo vina sakafu ngumu ambavyo vinaendana na uhifadhi wa mazingira kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo, tukasema badala ya viwanja 15 bora tupate vinne (4) ambavyo vitadumu kwa muda mrefu, havihitaji ukarabati lakini pia vitatuwezesha tupate watalii ambao kwa sasa wanatukwepa kutokana na masharti mbalimbali yaliyopo katika bima zao za maisha ama bima zao za *flight*. Mfano, wazee wanaokuja Tanzania hapa ambao wako zaidi ya miaka 65 ni asilimia 5 tu ya watalii wote lakini hili ndilo kundi kubwa ambalo linasafiri duniani kwa ajili ya kupumzika; wazee ambao wako kwenye pensheni, wana pesa za kutosha, wana bima za maisha wanahitaji kwenda kupumzika katika maeneo mbalimbali. Hawa wote wanakwenda *Kruger National Park* kule South

Africa kwa sababu wenzetu wana uwanja wa ndege ambao una sakafu ngumu na sisi tunaishia kupata asilimia 5 tu.

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo, tukijenga Viwanja vya Ndege kwa sasa maana yake tutaweza kupata hii *segment* ya soko la watalii ambao wana bima za maisha. Sababu ni moja tu, bima nyingi za maisha zinawataka watalii lazima wasafiri kwenye ndege ambayo ina injini mbili, ma-*pilot* wawili lakini pia atue kwenye sakafu ambayo ni ngumu, ambapo ikitokea ajali ataweza kulipwa hiyo bimavinginevyo hawezi kupata hiyo bima. Kwa hiyo, sasa tukaona ni bora ili kuufanya mradi uwe *commercially viable* tujenge viwanja vichache lakini vyenye sakafu ngumu tuweze kupata wageni hao. Kwa hivyo, tuliweka mguu tukasema hapana lazima mabadiliko yafanyike katika mradi huu ili mradi uwe *commercially viable,* tuongeze idadi ya watalii na pia tupate pesa kwa ajili ya kulipa deni ambalo linatokana na mradi wenyewe.

Mheshimiwa Spika, pia ikatokea maneno kidogo ambayo sasa hivi tungeweza kuyatatua kwamba tutatekeleza mradi katika eneo la Selou, kwa hivyo, tusiutekeleze kule Selou kwa sababu kuna uharibifu wa mazingira. Sisi tukasema hapana mradi utatekelezwa maeneo yote ama usitekelezwe kabisa kwa sababu hatuwezi kutekeleza nusu nusu tukaiacha *segment* ya mradi ambayo ipo katika Pori la Akiba la Selou. Bahati nzuri Benki ya Dunia sasa hivi wamekubali kwamba tutekeleze mradi na tutekeleze pia mradi wetu wa kufufua umeme katika Bonge la Mto Rufiji. Kwa hivyo, kwa sasa tumebaki tuna *negotiate* kwenye eneo hili moja la viwanja vya ndege.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ambayo napenda kuzungumzia ni kuhusu uwindaji wa kitalii. Uwindaji wa kitalii umekumbwa na dhoruba nyingi sana tangu mwaka 2008 mpaka leo. Uzuri wewe ulikuwepo Bungeni na ulikuwa kwenye Kamati inayosimamia maliasili hivyo unafahamu kilichotokea, sina haja ya kurudia hapa.

Mheshimiwa Spika, wakati mimi nateuliwa kuwa Waziri kwenye Wizara hii nilikuta mapato yameshuka mpaka

chini ya bilioni 10 kwa mwaka sasa hivi tumeweza kuyapandisha mpaka zaidi ya bilioni 40 na mwaka huu tunakusudia kuweka bajeti zaidi ya bilioni 60. Mapinduzi ambayo tumeyafanya kwenye sekta ya uwindaji wa kitalii ambayo mashuhuri yanajulikana kama *Hunt More for Less* yatatupeleka kuifufua sekta ya uwindaji wa kitalii na kupata mapato makubwa zaidi kuliko ilivyo sasa na pengine uwindaji wa kitalii nao ukachangia kwa kiasi kikubwa katika ukuaji wa uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru na naunga mkono hoja ya Kamati. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Sasa tunakuja kwa Waziri wa Mifugo, Mheshimiwa Mpina, dakika 15.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, nami nishukuru sana kwa nafasi hii ambayo umenipatia ili niweze kuchangia kuhusiana na mapendekezo na maazimio ya Kamati hizi zote mbili. Niipongeze sana Kamati yangu, Kamati ya Kilimo, Mifugo, Maji na Uvuvi kwa kazi nzuri sana waliyoifanya ikiongozwa na Mheshimiwa Mahmood Hassan Mgimwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utakubaliana na mimi kwamba hata ukisoma tu ripoti yao utajua kwamba hii Kamati ina Mwenyekiti makini na Wabunge makini sana wanaofanya kazi vizuri sana. Niwapongeze sana kwa pongezi walizotupa ukurasa wa 42 kwa kuanzisha Dawati la sekta binafsi kwenye Wizara, tunazipokea pongezi hizo. Dawati hilo limekuwa msaada mkubwa sana kwa wananchi wetu, wazalishaji, wenye viwanda na wafanyabiashara wote na wawekezaji hapa nchini. Pia wamealika vijana wa vyuo vikuu wakiongozwa na Ndugu Peter Nibonye, Rais wa Vyuo Vikuu *(TAHLISO)* ni mambo mazuri vijana hawa nao waweze kujifunza na kuona jinsi tunavyofanya shughuli zetu humu.

Mheshimiwa Spika, niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao mizuri sana. Kwa kuanzia

nianze kusema kwamba yale mapendekezo na Maazimio ya Kamati yaliyowekwa nakubaliana nayo asilimia 100 na sisi kama Serikali tutayasimamia kuhakikisha kwamba utekelezaji wake unafanyika vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wengi walipochangia waliniomba na waliniagiza kwenda kutembelea na kukutana na wavuvi hasa katika Ukanda wa Pwani. Napenda tu kusema kwamba nimekubali, nimeandaa ratiba ambayo nitatembelea eneo lote kuanzia Moa hadi Msimbati; kuhakikisha kwamba nakutana na wavuvi wote na kuzungumza nao na kuona changamoto zao na kuzitafutia majawabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati na Waheshimiwa Wabunge wengi na kwa muda mrefu wamezungumzia sana suala la kufufuliwa kwa Shirika la Uvuvi Tanzania (*TAFICO)*. Nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba Serikali ya Awamu ya Tano iko kwenye hatua nzuri sana za kulifufua hili Shirika. Moja, tayari mpaka sasa hivi, kama Kamati ilivyozungumza menejimenti tumeiweka, uhakiki wa mali unaendelea ambapo mpaka sasa hivi zaidi ya shilingi bilioni 141, samani, viwanja, maghala, ofisi na nyumba ambazo zilikuwa zinamilikiwa na watu kinyemela na nyingine walikuwa wamejimilikisha tumeshazitaifisha na sasa zimerudi mikononi mwa *TAFICO*, vitu vyenye thamani ya shilingi bilioni 118. Tunaendelea kwenye maeneo mengine kuhakikisha kwamba *assets* zote za shirika hili zinarejea.

Mheshimiwa Spika, vilevile tunakwenda kwa kasi kuandaa mipango ya biashara, nayo tunaenda vizuri. Mpaka sasa hivi tayari tumeshapata shilingi bilioni 4.3 kutoka Serikali ya Japan kwa ajili ya kufufua ile miundombinu yetu, kwa maana ya majokofu ya kuhifadhi samaki, gari la barafu, meli moja ya uvuvi na kujenga gati la kuegesha meli za *TAFICO,* kwa hiyo, tunaenda vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, katika huo mpango wetu wa biashara tunaoufanya tunajiandaa kununua meli mbili kubwa ambazo tutaingia kwenye uvuvi wa bahari kuu. Wabunge

kwa muda mrefu na mingi sana wamekuwa na kilio kikubwa sana, ya sisi kuingia kwenye maji ya bahari, nataka niwahakikishie Serikali ya Awamu ya Tano tunaingia kuvua katika uvuvi wa bahari kuu na mipango iko vizuri na ndio maana unaona sasa hivi kwa muda mfupi tu tumezipata hizi bilioni 4.3 ambazo zinaturahisishia sana safari yetu kuendelea.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa bandari kama nilivyosema tayari Mtaalam Mwelekezi sasa hivi anafanya anaendelea na zoezi ambalo ni miezi minane tu atakuwa amemaliza suala la upembuzi yakinifu ili tuanze ujenzi wa bandari. Hili nalo limezungumzwa miaka mingi, lakini sasa tunaenda kuanza, rasmi ujenzi wa bandari yetu ya uvuvi.

Mheshimiwa Spika, la nne, Wabunge wengi wamelalamika na nakubaliana nao kabisa, malalamiko yao ni ya haki juu ya viwanda vya kuchakata mazao ya mifugo, viwanda hivyo vingi havipo, ni kweli kabisa nakubaliana nao. Hata hivyo, nataka niwaambie Waheshimiwa Wabunge habari njema za Serikali ya Awamu ya Tano, mipango tuliyonayo, viwanda vingi, tunaenda kuvifufua na sasa hivi ninavyozungumza tunaenda kujenga kiwanda kikubwa sana pale Ruvu. Kiwanda ambacho kitakuwa na machinjio, kiwanda ambacho kitakuwa na uchakataji wa kusindika nyama, kiwanda ambacho kitasindika ngozi, kiwanda ambacho kitasindika mazao ya ngozi, maana yake ukiingiza ngozi mpaka unaenda kutoka na kiatu. Pia tutajenga mnada mkubwa sana wa Kimataifa pale Ruvu na hii mchana Bunge lilipoahirishwa Waziri mwenzangu kwa sababu kiwanda hiki kinajengwa baina ya Kampuni ya *NARCO* Tanzania na Kampuni ya Misri na fedha zipo. Tunatajia kwamba kuanzia Machi, ujenzi wa kiwanda hiki utaanza, matatizo ya wafugaji wa nchi hii yamefika mwisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kiwanda hicho kinajengwa na fedha tunazo. Leo kama ninavyozungumza Waziri mwenzangu wa Mifugo na Uvuvi kutoka Misri tumekutana na tumeazimia kwamba sasa ujenzi uanze kuanzia Machi na kuendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuna viwanda vingi vinajengwa, kipo Kiwanda kikubwa sana kinajengwa Longido, chenye uwezo wa kuchakata mifugo mingi kwa siku, tuna *Tan Choice* Kibaha, kinajengwa chenye uwezo wa kuchinja ng'ombe zaidi 1,000 mbuzi zaidi 4,000 na kiko kwenye hatua ya mwisho kukamilishwa, lakini kule Kahama, Chato tunajenga kiwanda kingine.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge napenda niwaambie, Serikali ya Awamu ya Tano, iko kazini, matatizo ya wananchi kukosa soko sasa yamefika mwisho na viwanda hivi, ni tegemeo kubwa sana la uchumi wa nchi yetu ambalo litawawezesha wananchi wetu kuwa na soko la uhakika litawawezesha wananchi wetu kupata manufaa ya mazao haya ya mifugo ambayo muda mrefu wameshindwa kunufaika nayo.

Mheshimiwa Spika, tumeenda tumefanya makubwa ambayo yalikuwa yamesimama kwa muda mrefu, kama uogeshaji wa mifugo, sasa hivi tunaogesha mifugo kila kona, mahali ambapo hawaogeshi mifugo ni mahali tu ambapo hawana josho lakini maeneo yote tumegawa dawa kwenye maeneo yote yenye majosho kwa ajili ya kuweza kuogesha. Kwenye majosho 1,409 yote ninavyozungumza hivi sasa wanaogesha mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeazimia kwamba uogeshaji wa mifugo utakuwa ni wa kila siku na Wizara itaendelea kutoa madawa kwa ajili ya uogeshaji. Wafugaji walikuwa wanateswa kuogesha ng'ombe mmoja unadumbukiza unalipa Sh.1,000, Sh.500, Sh.2000 tumesema hapana, watakuwa wanachangia gharama ndogondogo tu ya kujaza maji na kununua zile dawa ndogo ndogo na ng'ombe akiingia majini analipa Sh.50 tu na tutaweka mpaka kwenye Kanuni kwa sababu wafugaji wamedhulumiwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na hili tatizo kubwa hapa la muda ambalo ninalohangaika nalo, sasa nizungumzie hoja za Waheshimiwa Wabunge,

wamezungumza mambo mengi mazuri na hasa pia wakazungumzia suala la doria na wakazungumzia suala la operesheni. Waheshimiwa Wabunge hapa tuelewane, tunazungumza uwekezaji leo, hivi nani anayeweza kuja kwenye uwekezaji kwenye nchi ambayo haiwezi kulinda raslimali zake, hakuna. Nani atakayejenga Kiwanda leo hapa, cha Kusindika Samaki wakati samaki wakati samaki wote wanatoroshwa kwenda nje, bila hata kufata utaratibu unaokubalika, ni nani? Nani atakayekubali kuwekeza kuzalisha vifaranga kuzalisha kuku, kuzalisha ng'ombe wa maziwa katika nchi ambayo maziwa yanatoka nje ya nchi hayana vibali, hayajalipiwa kodi yoyote hayajapimwa ubora na yanauzwa na yanashindana na viwanda vya ndani, nani atakayejenga viwanda hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, pia nani atakayejenga viwanda katika nchi ambayo inaruhusu mpaka vitu vilivyokwisha muda wa matumizi, kuuzwa hapa nchini na kushindana na wazalishaji wa ndani, nani atakubali? Ni lazima tukubali, doria zinazoendelea, doria zinazoendelea hapa nchini zinalenga kuwalinda wazalishaji wa ndani ili waweze kuzalisha vizuri. Leo nenda kawaulize wazalishaji wa Viwanda vya maziwa, wameji-*commit* hata kuongeza uzalishaji kwa sababu kuna ulinzi madhubuti, hakuna mtu anaingiza leo mzaha kutoka nje, mzaha mzaha hapa nchini hakuna.

Mheshimiwa Spika, katika vitu ambavyo nilichukia kuliko vyote, ulikuwa Naibu Spika, lakini wewe ni kiongozi wangu wa muda mrefu nikiwa Mbunge wa kawaida, kitu kilichokuwa kinaniuzi na kupita vyote ni suala hili, watu wanaleta vitu hapa nchini vilivyokwisha muda wa matumizi wamepita njia za panya, halafu Waziri mhusika anakuja kuwasilisha naye analalamika juu ya mambo hayo, wakati yeye ndiyo ana uwezo wa kuwashika. Tutawashika na sisi hatutakubali raslimali zetu kuvuruga wawekezaji wetu hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, naomba tuungane pamoja tuzilinde hizi rasilimali kwa ajili ya wananchi wetu kwa sababu zikitoweka hata wao

hawawezi kunufanika, samaki wakitoweka majini yakabaki maji tu, nani anayewahurumia wavuvi? Mtu ambaye anaruhusu watu wakavue kwa nyavu haramu, halafu baadaye mvuvi anayeenda kuvua kwenye ziwa, anaenda na mafuta yake na gharama kubwa, halafu anarudi bila samaki, nani anayetetea wavuvi, ni yule ambaye analinda mwisho wavuvi wakienda kuvua wakarudi na samaki wengi ili wawe matajiri, ndiyo msingi hasa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninachokitaka nikiseme leo hii kwa Wabunge wenzangu, ni kitu kimoja, zipo baadhi ya changamoto mmezizungumza kwenye sharia nimeziona mimi na wenzangu, ndiyo maana tukaamua kuifumua Sheria ya Uvuvi, Na. 22 ya mwaka 2003 na Kanuni zake za mwaka 2009 ili kukaribisha mwanya wa wananchi wetu wachangie waone mambo yaliyopitwa na wakati tuyaondoe na mimi niko tayari.

Mheshimiwa Spika, nimesema tena kwenye Kanuni kwa sababu uwezo ni wa Waziri wakimaliza kunishauri mambo, nitatengeneza hata *task team* ya kutengeneza Kanuni haraka ili mambo yanayotukwaza kusonga mbele tuyafute, ili wananchi wetu waweze kunufaika na Sheria zingine ambazo nimeamua tuzifumue ni Sheria ya Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu, Sheria Na. 29 ya mwaka 1994 ili na yenyewe mambo ambayo yanakwaza wazalishaji, wavuvi wetu, wafanyabiashara wetu na wawekezaji wetu, tuyaondoe pamoja na Sheria za Bahari zote hizi ili kuhakikisha kwamba wananchi wetu tumewaweka vizuri, wanafanya biashara vizuri sana katika maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile kwenye mifugo nako wameshauri hapa shabaha ya kuwa na tozo za rasilimali za nchi, huwezi ukawa na rasilimali zako hapa zinavunwa, zinaenda nchi nyingine halafu Taifa linaachwa halina chochote, lazima tuweke tozo zinazolingana na thamani ya rasilimali zetu ili zinapozouzwa nje, Taifa linufaike, lakini inapotokea labda tumezidisha sana, ikawa maumivu kwa wafugaji wetu au kwa wafanyabiashara wetu, au kwa wawekezaji wetu, sisi hatuna tatizo, tunakaribisha mawazo

yenu, tutafanya *review;* kama kuna tozo zimezidi upande wa uvuvi au mifugo tutazi-*regulate.* Lengo letu, ni kuhakikisha kwamba hawa wafugaji wetu wanafuga vizuri, lakini na hawa wavuvi wanavua vizuri na wafanyabiashara na wawekezaji katika eneo hili wanafanya biashara vizuri, lakini bila kuyasahau maslahi ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi uliyonipa. (Makofi)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Uvuvi, Mheshimiwa Mpina, tunaenda vizuri, kwa upande wa muda, labda jambo moja Waziri wa Utalii wakati anazungumzia habari ya kuendeleza utalii, ametaja zile *Circuit* ya Kaskazini ya Kaskazini Magharibi, zile hifadhi mpya zitakazoanza Ibanda, Rumanyika na nyingine kule Kagera, Kusini na kadhalika, utaona Waziri wa Uvuvi naye alipozungumza amezungumzia habari ya Hifadhi za Baharini (*Marine Parks), Marine Parks* ziko kwa Waziri wa Uvuvi, *Terrestrial Parks* za Bara hizi ziko kwa Waziri wa Maliasili; majirani zetu Wakenya, hizi zote ziko pamoja. Kwa hiyo, katika *Circuit* ambayo angezungumzia Waziri wa Utalii angejikuta anazungumzia hizo zote pamoja na za baharini, sasa kwa sababu ni Wizara mbili tofauti, mipango inakuwa miwili tofauti. Kwa hiyo, Kamati ya Ardhi na Maliasili jambo hili ni vizuri kulitazama kama sisi tuko *right* au wenzetu majirani wako *right*. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tumalizie na Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Mheshimiwa Lukuvi, dakika kumi na tano.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa muda ulionipa. Nami nakupongeza sana kwa utendaji wako na usimamizi mkubwa wenye tija wa Bunge letu Tukufu, nawapongeza sana Kamati yangu ya Ardhi, Maliasili na Utalii kwa ushauri wao ambao wamekuwa wanatupa kila wakati, mimi na Naibu wangu tumefurahi, na tumenufaika sana na ushauri wa Kamati hii, tukiwa kwenye mikutano, tukiwa kwenye ziara, tumefaidika sana na Wajumbe wote kwa

pamoja wakiongozwa na aliyekuwa Mwenyekiti. Kwa hiyo nawapongeza sana na tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika utendaji wa kazi ambazo tumekabidhiwa mara zote sisi tunatekeleza kwa malengo ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Pili, tunatekeleza kwa maelekezo mahsusi, ya Mheshimiwa Rais na Viongozi Wakuu, Makamu na Waziri Mkuu maagizo ya *Cabinet* lakini pia maelekezo ya Bunge lako Tukufu. Maelekezo ya Bunge lenyewe lakini kupitia Kamati yetu ambayo tunayo kwa muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya shukrani hizi nafikiri niseme machache ambayo yamesemwa kwenye Kamati, naunga mkono sana, Kamati hii na maoni yake, lakini niseme mambo matatu yaliyogusiwa ndani ya ripoti hii, la kwanza nataka niseme, kwamba pamoja na kutekeleza kwa misingi niliyoisema lakini tunatekeleza kwa mujibu wa Sheria. Kwetu sisi Wizara ya Ardhi, Sheria kuu zaidi tunazozisimamia ni mbili kwa upande wa ardhi; Sheria Na. 4 na Na. 5 za mwaka 1999. Sheria Na. 4 inahusu zaidi ardhi hizi ambazo mara nyingi sana zinasimamiwa na kila anayemilika ardhi kwa kutumia sheria hii huwa tunampa karatasi hii, hati ya namna hii. Hii ni hati inayotolewa kwa kusimamiwa na Sheria Na. 4 ya mwaka 1999, inaitwa ardhi ya jumla.

Mheshimiwa Spika, tunaposema habari ya ufutaji wa ardhi wa hati unaoanzia kutoka kwenye Halmashauri kama alivyoeleza Mbunge wa Korogwe Vijijini ni hati hizi ndizo zinahusika na utaratibu ule lakini pia tunayo Sheria Na. 5 ya Sheria ya Ardhi ya mwaka 1999, inahusu ardhi ya vijiji. Kabla ardhi haijageuzwa haijahaulishwa kuja kutolewa hati hii, ardhi zote za vijiji zinatolewa hati ya namna inaitwa hati za kimila. Wanaopata ardhi hii hawana ukomo wa umiliki hawalipi kodi, lakini imeweka kiwango kila kijiji hakipaswi kutoa zaidi ya ekari 50. Kwa hiyo tuna ardhi zinatawaliwa na Sheria mbili, lakini na hati za utambulisho ziko mbili.

Mheshimiwa Spika, nimesema nianze na hii ili angalau Waheshimiwa Wabunge tuelewane. Sasa katika usimamizi

wa sheria kama nilivyosema Sheria ya Ardhi hii inayotawala Sheria ya Vijiji, mamlaka makubwa zimepewa Serikali za Vijiji zenyewe, ila inapozidi 50 uhaulishaji sasa inabidi ngazi ya Wilaya izungumze, ije kwetu Wizarani, tumpelekee Mheshimiwa Rais, ikimpendeza anakubali kuibadilisha ile ardhi ya kijiji kuja ardhi ya jumla na ndipo mtu anaweza akamiliki ardhi kwa hati kama hii, kama ni ekari 50 kwa matumizi yoyote, kama ardhi iko kijijini.

Mheshimiwa Spika, sasa hati hizi ziko nyingi sana, hatutozi kodi lakini tunaamini masikini wa Tanzania wanaopendwa sana Serikali ya Dkt. John Pombe Magufuli ndio wanatumia hati hizi na ndio maana hazitozwi Kodi. Wanaotumiwa hati hizi sasa hivi wanakaribia milioni moja katika vijiji vyetu, lakini hawa ni mashamba, wanakaribia milioni moja. Kwenye hati hizi wa mashamba wanakaribia 2,000, mashamba makubwa, wanaomiliki kwa hati hizi, yako mashamba yasiyopungua 2,000 yenye ekari zisizopungua milioni sita zinazotumika kwa shughuli mbalimbali za kilimo za ufugaji na wamilika hao 2,000 wanazo hati hizi.

Mheshimiw Spika, sasa moja ya jambo ambalo tumeshauriwa hapa na ambalo limezungumzwa na ndugu yangu Mheshimiwa Msigwa hapa, alitaka kuzungumza kwamba utekelezaji wa Sheria hii una mashaka na amefika mahali mpaka amemhusisha Rais, lakini nashukuru Waheshimiwa Wabunge wengi mmechangia hapa, kwamba utoaji wa ardhi au ufutaji wa hati hizi unafuata Sheria na hata siku moja, haijawahi kutokea Rais akaniagiza mimi nifute hati ya mtu fulani au nimpelekee hati ya mtu fulani afute, hajawahi kuniambia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wanaoanza kupendekeza ardhi hii kwanza, mnakumbuka tulipoanza Awamu ya Tano, mimi mwenyewe nilileta dodoso hapa kwa kila Mbunge kuuliza kero zenu, ninyi ndio mlijaza dodoso na kueleza kero zenu, tukatengeneza kitabu, asilimia 60 ya kero zile ilikuwa mashamba pori na migogoro ya ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, baada ya hapo tukatengeneza ratiba ya utekelezaji na ...

**MHE. ZITTO R. Z. KABWE:** Mheshimiwa Spika, kuna ushahidi wa maagizo ya Rais.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Wewe Zitto una kelele sana, sikiliza wenzako waseme.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Spika, achana naye huyo.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, ninyi mlipoleta zile kero ndipo tukatengeneza ratiba ya utekelezaji, kwa hiyo kutokana na maelekezo yenu, tumefuatilia, tumerudisha yale maelekezo yenu kule Wilayani, wamefuatilia. Katika uhakiki wa mashamba haya 2,000 mpaka sasa katika miaka mitatu hii, tumeshafuta mashamba 46 kwa mujibu wa Sheria, lakini chanzo ni ninyi, lakini pia *outcry* ya wananchi na Viongozi mbalimbali wamepita kwenye Kampeni wamesikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sababu ni moja tu, watu katika hawa 2,000 tuliowapa hizi hati, wanayo mashamba makubwa kama walivyosema Wajumbe Fulani. Hati hizi ukipewa kuna masharti ya matumizi huku nyuma, umri wa matumizi umeandikwa kwenye hati hizi, hati hizi hakuna umri wa matumizi, lakini unatakiwa ukipata ardhi ya shamba, angalau uhangaike moja ya nane kwa mwaka uendeleze. Kwa hiyo matarajio ya hati hii angalau katika kipindi cha miaka minane utakuwa umejiendeleza kumaliza hili shamba, lakini wako watu wengi, wengi sana, ambao wamepokea mashamba haya, matokeo yake siku zote hizi za nyuma walikuwa wanatumia kwa ajili ya kuweka rehani kupata mtaji wa biashara na kufanya biashara nyingine. (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa mbele yangu nimekuja na daftari hili, mimi nina *privilege* ya kujua siri zenu zote, humu

ndani kuna watu ambao wamepewa ardhi na wamechukua mkopo, hapa kuna zaidi ya trilioni moja nimeshika, kuna zaidi ya dola mia tano hapa na kuna fedha tasilimu zaidi ya bilioni 800 watu wamekopa, kwa rehani na hii ni taarifa ya Benki kuu, kwa rehani ya ardhi, lakini ninyi wenyewe mnajua, hivi kama kweli kilimo cha Tanzania kingewekeza zaidi ya trilioni moja si nchi ingetikisika, fedha ziko wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi tunao ushahidi baada ya kufanya uhakiki kwamba watu walichukua hizi fedha kwa sababu usimamizi ulikuwa hafifu, wamechukua kama kinga, wamechukua Benki, pamoja na kuandika madhumuni ya kuendeleza yale mashamba, lakini Benki hazifuatilii, Benki zinataka tu *return* ya biashara zao, wameenda kuwekeza Dubai, wamenunua *apartment*, wanawekeza biashara na kulipa papo kwa papo mashamba yamebaki pori, hayakuendelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hivi Wabunge mkisema kuna mashamba pori huku, watu wamekopa hela benki, lakini watu wanapambana kulima yale mashamba, halafu anatokea siku moja mtu anatishatisha hivi, miaka 10 au 20 yeye anaendelea kuongeza thamani ya Kampuni yake, kutokana na mtaji unaotokana na thamani ya ardhi, lakini kule kwenye shamba haendi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka kuwahakikishia kwamba kwa maelekezo ya Ilani, Chama cha Mapinduzi kimetuelekeza tufanye uhakiki na tuchukue mashamba haya na ndiyo maana tumefanya hivyo. Kwa sasa tumechukua mashamba 46 katika mikoa ifuatayo: Arusha (2); Kilimanjaro (1); Dar es Salaam (2); Morogoro (18) na Kilosa peke yake ni 12; Iringa (1); Pwani (4); Simiyu (2); Tanga (17); Kagera (1); Mara (1); Lindi (1) alilotaja Mheshimiwa Nnauye. Shamba limetoka kwenye Jimbo lake na bado namba 38, umetaja namba 37 na 38 tumepeleka. Kwa hiyo, huu ni utekelezaji wa maelekezo yenu kumbe tufanye nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ndugu zangu wakati mwingine, Mheshimiwa Peter hayuko hapa, huna sababu ya

kuunda Kamati Teule ya kwenda kuchunguza uhalali wa kazi aliyoifanya Rais kisheria. Ninyi mnaofikiria maneno haya hangaikeni na Majimbo yenu tu kwa sababu Mheshimiwa Rais ametimiza wajibu kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aliyesababisha hii ni ninyi, wananchi wana shida na tumetekeleza. Fikiria tumefanya uhakiki wa mashamba 2,000 tumegundua 46, kumbe tungefanya nini? Mashamba haya mnaachiwa wenyewe ili muwapangie wale wananchi walioko pale wanaitwa wavamizi ili nao wawe wamiliki wa mashamba hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka niseme tu kwa Waheshimiwa Wabunge tushirikiane, hili jambo ni jema, hakuna sababu ya kutafutiana maneno hapa, Mheshimiwa Rais anatekeleza wajibu wake na ni msikivu sana. Yeye hafuti, mapendekezo yanatoka huku.

Mheshimiwa Spika, mashamba yaliyotajwa ya *Mohamed Enterprises Company* hapa amesema Mheshimiwa Peter. *Mohamed Enterprises* anamiliki mashamba makubwa 21 nchi hii...

**WABUNGE FULANI:** Eeeee.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Yako Tukuyu, Rungwe, Mombo, Korogwe na Same.

**MBUNGE FULANI:** Efatha.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Hivi asipoendeleza tunafanyaje? Kwa hiyo, tumefanya uhakiki, kwanza niwaambie mashamba yaliyofutwa ni sita lakini onyo alipata mashamba 12. Baada ya kupata onyo, Afisa Ardhi pale akawa anachezacheza Naibu Waziri akamdhibiti amemuondoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo nilipomwagiza Naibu Waziri, tumepiga na picha na vielelezo vyote tunavyo,

tukagundua ukweli mashamba sita hana la kufanya. Nataka nimwambie hayo sita na yenyewe tumempa angalizo tunamtazamia, asipotekeleza tuliyomwambia nayo yako kwenye mstari mwekundu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka kuwaambia sheria itasimama na itachukua mkondo wake bila kumuonea mtu lakini bila kumuogopa mtu. Sisi tumeelekezwa kulinda rasilimali za Taifa. Kwa hiyo, naomba kama Wabunge tushirikiane, haya maneno madogo madogo ya watu wamechukua rushwa sijui wamefanya nini hayana maana, tushirikiane katika kusimamia mambo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru sana wote mliochangia na najua wengi mmesoma kwenye mitandao kwamba katika kutekeleza mambo haya mimi na Naibu wangu tumechukua rushwa. Kama tunaweza kuchukua rushwa na tukafuta basi hiyo nzuri. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Bado Rukwa.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, kule Rukwa kulikuwa na shamba kubwa ambalo lina mgogoro mkubwa na Nabii wa Efatha, Mheshimiwa Mwingira, kwa hiari yake mwenyewe amekubali kutoa ekari 3,000 na kuwarudishia wananchi wa vijiji vitatu. Kule Same Mheshimiwa Mama Kilango tumekwenda wenye mashamba makubwa wamekubali kutoa mashamba yao. Ulanga juzi wawekezaji wamekubali kuweka ekari 9,000 kwa wananchi ili angalau na wenyewe wasitazame tu macho kwenye ardhi ambayo inamilikiwa na wenye mashamba makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka kusema kwa kweli Wabunge wote tushirikiane kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi hii kubwa anayoifanya. Anafanya kwa ajili yenu, Wabunge wa CCM wote tumeahidi kwenye Ilani kwamba tutafanya jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, Mheshimiwa Rais mmempongeza sana ametangaza Wizara saba tushirikiane, tunataka kuwahakikishia kwamba Wizara saba tutafanya lile jambo ambalo ametuagiza Mheshimiwa Rais la kutokomeza migogoro. Nimemwomba Mheshimiwa Spika tuwashirikishe na ninyi Waheshimiwa Wabunge, mimi ndiyo Mwenyekiti. Tuwashirikishe na ninyi Wabunge kama mna ziada zaidi ya yale ambayo mlisema tuko hapa wiki hii. Mtu yeyote ambaye anafikiri ana kero ya ardhi ya ziada atuandikie ili tuongeze katika agenda tulizonazo na tumepewa muda mfupi sana tupeleke kwa Mheshimiwa Rais. Kwa hiyo, kwa niaba yake na kwa niaba yenu, tunashukuru sana kwamba angalau wazo hili la Mheshimiwa Rais mmelichukua na tumeona watu wote wananchi wenye nia njema wamefurahia jambo hili.

Mheshimiwa Spika, *National Housing* haina matatizo ya kulipa deni, ina uwezo wa kulipa deni na kila mwezi inalipa shilingi bilioni tano na milioni mia sita kutokana na fedha yake yenyewe. Kwa hiyo, ina uwezo wa ku-*service* madeni na ina mali ambayo zina thamani ya zaidi ya shilingi trilioni 5.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, nawashukuru sana Wabunge wote kwa kunisikiliza na kwa kuchangia hoja hii. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri Lukuvi. Sasa nimuite aliyetoa hoja ya Kamati, Mheshimiwa Dkt. Kiruswa kwa niaba ya Kamati ya Ardhi. Karibu sana uhitimishe hoja yako kwa dakika kumi na tano. *(Makofi)*

**MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII):** Mheshimiwa Spika, ninayo heshima tena kusimama mbele yako na mbele ya Bunge lako Tukufu jioni hii ili niweze kuhitimisha hoja ya Kamati yetu ya Ardhi, Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kutoa muhtasari wa yale ambayo yamejiri katika mjadala ulioendelea hapa, nitumie fursa hii kwa sababu asubuhi nilishikwa na taharuki baada ya kujiandaa kuwasilisha ile ripoti kwa nusu saa nikaambiwa tuna roba saa lakini najua sababu ni nini, kutanguliza shukrani za dhati kwa Kiongozi wa Taifa letu, Mheshimiwa Rais John Pombe Magufuli kwa sababu ya mambo makubwa na ya kupendeza anayoendelea kulitendea Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya jamii ya wafugaji na wakulima, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa tamko lake la juzi la kwamba Wizara husika zikakae ili ardhi zote ambazo zimekaa *idle* mfano mashamba na maeneo ya hifadhi ambayo yamepoteza hadhi yakapitiwe upya ili wananchi wanaoteseka waweze kupata maeneo ya kulima na kufugia. Kwa kweli amewafariji sana jamii ya wafugaji na wakulima hususani watu wa Kanda ya Kaskazini wamefarijika na wamefurahia sana suala hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nitumie dakika moja kusema ahsante sana kwa Wizara ya Kilimo, Mifugo na Umwagiliaji kwa taarifa ambayo nimeisikiliza hapa kidogo na Waziri akanigusa katika maslahi mazuri anayowawekea jamii ya kifugaji ya kuhakikisha kwamba masoko ya uhakika na viwanda yanakwenda kuanzishwa ili tuondokewe na hiyo kero ya kupeleka mifugo Kenya. Nimshukuru Waziri kwa operesheni alizozianzisha ambazo zimeleta kilio kikubwa kwa wananchi wa jamii za kifugaji hasa wa Wilaya ya Longido ambako mifugo yote ya Tanzania inayokwenda Kenya inapitia sasa itakuwa imetokomezwa.

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri zaidi kwa sababu ameniahidi kwamba tutakwenda kule kujaribu kuwapoza wananchi maana kuna unyanyasaji mkubwa umetokea hivi karibuni kwa namna operesheni ile ya kuzuia mifugo inakwenda Kenya inavyotekelezwa. Kwa sababu nimesimama hapa kutoa shukrani kwa jinsi ulivyotupa matumaini, naomba niishie hapo ili nirejee kwenye hoja yangu ya msingi ambayo nakuja kuhitimisha.

Mheshimiwa Spika, hizi Wizara mbili ambazo Kamati yetu inasimamia, kwanza nianze kuwashukuru wote ambao wamechangia hoja yetu na niwashukuru wajumbe wa Kamati maana wamefanya kazi kubwa na yenye tija ya kuandaa ripoti hii ambayo kwa jinsi mjadala ulivyoendelea inaonekana kwamba kwa kweli kwa asilimia zaidi ya 99 imeungwa mkono hata na wenzetu wa upande huu. Malalamiko yaliyojiri ni madogo sana na nitapitia yale machache ambayo yametamkwa ili nitoe msimamo wa Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kifupi ukiangalia katika Wizara ya Ardhi mambo ambayo yamejiri sanasana ni kuhusu Shirika la Nyumba la Taifa kwamba tulipofanya ziara tulikuta kwamba baadhi ya miradi yake imesimama kwa sababu walizuiwa kukopa fedha na wakawa wameacha miradi viporo. Sisi kama Kamati tulisema kwamba ingefaa sasa Serikali iwaruhusu kama bado wanahitaji hela ya mikopo, maana Waziri hapa ametuambia wana uwezo kabisa wa kulipa wala hakuna tatizo, hiyo miradi viporo imalizwe ili hizo nyumba ziendelee kuleta tija na mapato ya kuwezesha shirika kuendelea kujenga nyumba nyingine hasa zile za bei nafuu ambazo wananchi wanahitaji vijijini.

Mheshimiwa Spika, pia kulikuwa na mjadala ambao umejadiliwa na wengi kuhusu urejeshwaji wa mashamba makubwa yale yaliyotelekezwa. Hapa ndiyo mjumbe wangu mmoja wa Kamati, ndugu yetu Mheshimiwa Mchungaji Msigwa alikwenda katika hatua ambayo sisi hatukufikia kwenye Kamati ya kutaka kuundwa Tume. Kwa kweli sisi tulichofanya kwenye Kamati ni kuunga mkono tamko la Rais la kusema kwamba hayo mashamba yaliyotelekezwa na maeneo ya hifadhi yaliyopoteza hadhi yaende sasa yakafanyiwe mchakato ili warudishiwe wananchi ambao wanateseka. Huu ndiyo msimamo wa Kamati na yale mengine ambayo alisema tumekubaliana, tulichokubaliana sisi yote yameandikwa katika kijitabu cha taarifa yetu ambayo wote mnayo mkononi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia kwenye Wizara hiyo ya Ardhi, suala lingine lililojitokeza ni Programu ya Upangaji, Upimaji na Urasimishwaji wa Ardhi na mradi wa mfano ni ule wa Mkoa wa Morogoro ambapo kuna hizo Wilaya tatu za Kilombero, Ulanga na Malinyi ambazo huo mradi umeendelea kutekelezwa. Hoja iliyotokea kwa mmoja wa wachangiaji anaona kama *speed* ya hiyo kazi ni ndogo sana. Sisi pia mwanzoni tulishikwa na taharuki kwa sababu tuliona kama mradi hauendi lakini baada ya ziara yetu mwezi uliopita tuligundua kwamba ile timu sasa iko imara, wamepata uzoefu na kazi ile inakwenda kwa *speed* na hofu yetu ikabakia moja tu ambayo kwa niaba ya Kamati naomba niiseme.

Mheshimiwa Spika, hofu yetu ni kwamba fedha za wafadhili katika ule Mradi wa Upimaji na Umilikishaji Ardhi zimekwenda vizuri sana, wao wameshatoa asilimia 90 ya ile shilingi bilioni 28 ambayo ndiyo walitutengea lakini pesa ya Serikali, ile shilingi bilioni 7 mpaka sasa hivi wao wametoa tu asilimia 10. Kwa hiyo, rai yetu kama wajumbe wa Kamati tunaiomba sana Serikali kwamba wajitahidi na wao watimize ahadi yao, watenge fedha za kutosha kwenye bajeti kwa sababu hii misaada ya wafadhili itakapokoma itatukwamisha. Hofu yetu ni kwamba kwa sababu huu mradi unakwenda kufanikiwa kwa kasi na ufanisi mkubwa katika hizi wilaya tatu ni kwamba hatutaweza kunakili au ku-*reduplicate* katika Wilaya zote za nchi yetu kama sera inavyosema kwamba kila kipande cha ardhi ya nchi hii kitakwenda kupangwa, kupimwa na kumilikishwa. Sambamba na hilo, tulikuwa tunategemea katika zoezi la upangaji wa ardhi ambapo ni mpango wa matumizi bora ya ardhi kila jamii itatenga maeneo mahsusi ya akiba kwa ajili ya vizazi vya baadaye.

Mheshimiwa Spika, hayo ndiyo mambo makuu yaliyojitokeza katika mjadala kwenye Wizara ya Ardhi lakini pia kulikuwa na suala moja ambalo tuliliweka lakini halikuchangiwa ila naomba niseme kwa niaba ya Kamati kwamba, tulipokwenda kutembelea ile mipaka ya nchi yetu na nchi ya Uganda, tulijifunza kwamba alama zilizowekwa tangu enzi za kikoloni *(beacons)* pamoja na kwamba ni

kubwa na zinaonekana kwa mbali, lakini zimefukiwa, ziko mbalimbali na imesababisha raia wa nchi ya kigeni kuvamia ardhi yetu pengine hata pasipo kujua na kuishi kana kwamba wako katika ardhi ya nchi yao.

Mheshimiwa Spika, changamoto kubwa zaidi ambayo naiomba sana Serikali itilie maanani ni changamoto ya barabara za kuimarisha ulinzi wa mipaka ya nchi yetu. Kwa sababu hakuna barabara ya kuzungukia ile mipaka ili kuiweka madhubuti na kuihakiki na kuwasogeza watu wa nchi za jirani wanaovamia. Kwa hiyo, nimeona kwamba hilo ni pengo moja ambalo wachangiaji hawakuliona lakini sisi kama Kamati tumeliweka katika taarifa yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda, hayo ndiyo mambo ya msingi katika Wizara ya Ardhi lakini kwenye Wizara ya Maliasili mambo yaliyoibuka sana ni ule Mradi wa Kukuza Utalii wa Kanda za Kusini kupitia Mradi wa *REGROW* na masuala ya misitu. Hoja kubwa nyingine ambayo Wajumbe pia wamechangia na sisi tuliona ni hili la mtawanyiko wa mamlaka zinazosimamia misitu ya nchi yetu. Sasa hivi tuna karibu aina nne za misitu; kuna misitu ya Serikali Kuu, misitu ya Serikali za Mitaa na kuna misitu ambayo iko chini watu binafsi na mamlaka nyingine.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia misitu tuliyonayo asilimia 52 ziko mikononi mwa Serikali za Mitaa na asilimia 35 ndiyo ziko katika Serikali Kuu. Ukiangalia uharibifu katika misitu yetu, asilimia kubwa inatokea katika misitu iliyo katika utawala na usimamizi wa Serikali za Mitaa. Ndiyo maana Kamati katika ripoti yetu imeweka pendekezo kwamba ingependeza na ingefaa sasa na sisi katika Wizara hii tuanzishe mamlaka kamili ya kusimamia misitu badala ya kuwa na Wakala wa Misitu tuwe na Mamlaka ya Misitu kama tulivyo na Mamlaka ya Wanyamapori yaani iitwe *Tanzania Forest Authority.*

Mheshimiwa Spika, pia wajumbe walichangia kuhusu tozo za utalii na mazao ya misitu. Wazo kubwa ambalo limeungwa mkono ni hili la kusema kwamba tuwe na *one*

*stop payment center* na kodi zipunguzwe ili kuvutia utalii. Utalii hapa kwetu sasa hivi kwa kulinganisha na nchi za jirani umekuwa ghali na Tanzania *as a tourism destination*, imeonekana ni ghali ukilinganisha na nchi za jirani kama Msumbiji, Zambia, Afrika Kusini na hata wenzetu hapa Kenya.

Mheshimiwa Spika, pia suala la *WMA* limeibuka katika mjadala na wachangiaji walikuwa wanasisitiza kwamba *WMA* zitambulike kama ardhi ya jamii, ambapo jamii ndiyo ina mamlaka nayo juu ya matumizi yake na isiwe na utawala unaofanana na ule wa *National Parks* wa wananchi kufukuzwa na kusukumwa pale ambapo wamependelea kuishi na kufanyia shughuli zao za kibinadamu. Kubwa zaidi katika *WMA,* Serikali imekaa mbali nazo hata yale mapato ambayo yanakusanywa na Serikali Kuu inachukua muda sana kurudishiwa na hiyo ndiyo imesababisha *WMA* nyingi hadhi yake kushuka na pengine baadaye zitakuja kupoteza haki ya uhifadhi na kukosesha jamii mapato.

Mheshimiwa Spika, lakini suala lingine muhimu ambalo limetajwa ni hili la *single entry* wakati watalii wanapokuja kwenye hifadhi zinazopakana na maeneo ya jamii yenye utalii wa kitamaduni. Kuna malalamiko kwamba wanapoingia wakatamani kutoka na kurudi wanatozwa tena ada nyingine ambayo inawaumiza na inawakatisha tamaa na kuwakosesha wale walioko nje ya *parks* fursa ya wao nao kupata mgawo wa mkate wanaoleta watalii wanaokuja. Kwa hiyo, tunaomba sana hilo suala ama *double entry fee* liangaliwe ama uwepo utaratibu wa *biometric,* zile mashine za kusoma alama za vidole, mgeni akitoka abonyeze ionekane ametoka na ameingia saa ngapi ndani ya zile saa ambazo zinaruhusiwa.

Mheshimiwa Spika, pia hili suala la kuanzisha *Utalii Channel* tumeliunga mkono sana sisi kwenye Kamati yetu. Napenda tu kusema kwamba kinachohitajika sasa pale ni kutangaza katika lugha mbalimbali za kimataifa pamoja na lugha yetu ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa pia na suala la urudishwaji wa ardhi karibu na maeneo yaliyohifadhiwa. Kuna mwenzetu mmoja katika Wabunge waliochangia ambaye alikuwa anasema kwamba suala hili liangaliwe kwa makini kwa sababu tutakuja ku-*block wildlife corridors,* yale maeneo au mapito ya wanyamapori. Naungana naye kusema kwamba hilo ni suala la msingi na la muhimu sisi kama wahifadhi kuliangalia. Ni wazi Rais alivyosema kwamba Wizara zikakae ziweke mchakato pamoja na michakato mingine ni kuhakikisha kwamba wamezingatia maslahi ya maeneo ambayo bado yana hadhi ya uhifadhi, yana mapito ya wanyamapori na hawataweza kupangilia makazi ya watu katika maeneo ambayo bado yanatusaidia katika kudumisha rasilimali yetu ya maliasili.

Mheshimiwa Spika, kati ya wachangiaji wa leo, nimepokea michango ya maandishi wachangiaji wane na pia waliochangia kwa kutoa hoja hapa Bungeni wamefikia 16. Napenda kuwashukuru sana wote kwa sababu wamegusia mambo ya msingi ambayo nasi tulikuwa nayo kwenye ripoti yetu na sijapata mawazo yaliyokwenda kinyume na yale ambayo tumeyapendekeza zaidi tu ya kuboresha na kutilia mkazo na sisi tumepokea maoni yenu na naamini kwamba sisi kama Kamati tutakwenda kuyafanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, kuna moja ambalo limetokea ambalo sisi hatukuwa nalo kwenye ripoti, kuna mchangiaji mmoja ambaye ameleta kwa maandishi suala la hofu yake kuhusu upimaji wa miji katika ardhi ya wakulima. Akasema kwamba ardhi inapopimwa kwa sababu mji unapanuka na mkulima aliyekuwa anaotesha korosho, mahindi au maharage akaambiwa huwezi kulima tena kwa sababu sasa eneo hili linakwenda kuwa sehemu ya mji linaacha pengo ambapo yule mkulima anakosa mahali pa kuegemea maana mara nyingi anajikuta hawezi kuchukua vile viwanja na hapewi ardhi mbadala. Akasema Kamati katika kazi zake za siku zijazo iliangalie sana kwa makini suala hilo na mimi nalichukua tutaenda kulifanyia kazi. Tungefurahi kujua ni maeneo gani ya mashamba ambayo sasa hivi yanapimwa

kuwa miji ambayo wakulima au wakaaji wake wameathirika na jambo hili.

Mheshimiwa Spika, pamoja na maoni mengine yaliyotolewa ambayo yanafanana na yaliyopo kwenye ripoti yetu, naomba nihitimishe hoja yangu kutoka Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii kwa kusema kwamba naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Ahsante sana, unaweza ukaondoka sasa. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Dkt. Kiruswa kwa niaba ya Kamati kwa kufanya kazi hiyo nzuri sana. *(Makofi)*

Sasa nimuite Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji.

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii tena kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuhitimisha hoja yangu ya taarifa ya mwaka ya Kamati ya Kudumu ya Kilimo, Mifugo na Maji. Pia naomba nichukue fursa hii kuwashukuru sana Wajumbe wa Kamati yangu ya Kilimo, Mifugo na Maji kwa kuandaa taarifa nzuri ambayo imeungwa mkono na wachangiaji walio wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote kwa jinsi walivyokuwa wanafuatilia mijadala iliyokuwa inaendelea hapa Bungeni. Wabunge waliochangia walikuwa 19; 6 wamechangia kwa maandishi na 13 wamechangia kwa kusema.

Mheshimiwa Spika, katika michango ya Waheshimiwa Wabunge, wote wameonekana kuunga mkono mapendekezo na Maazimio ya Kamati. Kwa hiyo, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwamba kwenye mambo yote tuliyowasilisha wametuunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee, niwashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri; Mheshimiwa Hasunga, Mheshimiwa Prof. Mbarawa na Mheshimiwa Mpina, wote walipokuja kutoa maelezo yao hapa walionyesha hawana tofauti na Kamati na wamekubaliana na hoja zilizowasilishwa na Kamati. Wametuahidi mbele ya Bunge lako Tukufu watakuwa tayari kuzifanyia kazi hoja zote zilizowasilishwa na Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nijielekeze katika maeneo machache kabla sijahitimisha hoja ya mjadala huu. Eneo la kwanza, Kamati yangu inakuomba wewe kupitia Bunge lako Tukufu uandae Kamati Maalum itakayokuwa inashughulikia Maazimio yanayotokana na taarifa za Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kwa nini sisi kama Kamati tumeliona jambo hili? Hii ni kwa sababu kila mwaka tumekuwa na tabia ya kurudia hoja za Kamati, kwa hiyo, tunashindwa kuelewa ni hoja zipi ambazo zimeazimiwa na Bunge lako Tukufu zimetekelezwa na kama tungekuwa tunapata taarifa ya utekelezaji wa hoja hizo tungekuwa kwenye *position* ya kutozirudia tena. Kwa hiyo, sisi kama Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji tunakuomba sana uunde Kamati Maalum itakayokuwa inashughulikia hoja mahsusi kama ambavyo tunawasilisha wakati huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ambalo napenda kulitolea maelezo kidogo ni kuhusu Bodi ya Mazao Mchanganyiko. Tunaomba Bodi hii ipewe pesa ya kutosha kwa sababu ni eneo pekee ambalo Serikali imejiingiza kufanya biashara kisheria. Malalamiko yaliyokuwepo kwenye maeneo mengi ya wakulima wa mahindi, mbaazi na nafaka mbalimbali kama Bodi ya Mazao Mchanganyiko itapewa pesa za kutosha matatizo ya wakulima kwenye hayo maeneo hayatakuwepo.

Mheshimiwa Spika, pia pesa hizi wapewe kwa wakati. Unakuta safari hii Bodi ya Mazao Mchanganyiko imepewa pesa mwezi Desemba wakati mazao yanavunwa mwezi wa

Juni, kwa hiyo, tunaweka wakulima katika kipindi kigumu. Kwa hiyo, hata kama sasa hivi wanapata nafasi ya kwenda kununua mazao kwenye maeneo hayo, wakulima watakuwa na shida ya kuanza kulima upya katika msimu wa kilimo. Kwa hiyo, tunaomba Bodi ya Mazao Mchanganyiko ipewe pesa ya kutosha au itengenezewe utaratibu wa kupata mikopo kwa njia rahisi kusudi kuweza kununua mazao kutoka kwa wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili kwenye eneo la Bodi ya Mazao Mchanganyiko wawe na wafanyakazi wa kutosha. Sasa hivi asilimia 95 ya wafanyakazi wa Bodi ya Mazao Mchanganyiko wapo Mtwara, kwa hiyo, maeneo mengine hawawezi kupata zile huduma za Bodi ya Mazao Mchanganyiko. Hata utaratibu wa kununua nafaka kwenye maeneo mengine sasa hivi haupo, wamefanya *concentration* kwenye eneo moja tu la korosho, hakuna wafanyakazi wowote ambao wamewaweka kwa ajili ya kununua nafaka kwenye maeneo mengine. Naomba hili tuliangalie na waongezewe vifaa kwa maana ya magari. Mara ya mwisho wamepewa magari nane (8) lakini hayakidhi kutokana na hali halisi kwa sababu ni eneo pekee ambalo litamsaidia mkulima aweze kufanya kazi zake ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Benki ya Maendeleo ya Kilimo ilianzishwa kwa ajili ya kuwasaidia wakulima, kwa hiyo, ifanye kazi *specific* kwa sheria iliyoanzisha benki hii. Pale katikati Benki ya Kilimo nayo ilikuwa inaanza kutengeneza utaratibu wa kukopesha hela kwa watu wengine, ifungue matawi kwa ajili ya wakulima, wavuvi pamoja na wafugaji waweze kupata hela kwa riba nafuu ingeweza kuwasaidia sana watu kwenye maeneo yetu. Kusudi twende kwenye viwanda lazima tuhakikishe tunawawezesha sana watu wetu kwenye maeneo haya.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mpina na Naibu wake Mheshimiwa Ulega, kwanza wamekuwa wasikivu sana. Kutokana na changamoto zilizojitokeza katika Operesheni

Sangara wameamua kuanzisha mchakato wa marekebisho ya Sheria Na.22 ya mwaka 2003 pamoja na Kanuni zake za 2009. Kama tutaendelea kuwa na malalamiko bila kurekebisha sheria tutaendelea kuwalaumu Mawaziri hawa lakini nawashukuru wamekubali, wamesikiliza hoja za Wabunge na leo hii Waziri ametamka wazi kwamba watahakikisha huo mchakato wa kubadilisha Sheria Na. 22 ya mwaka 2003 pamoja na Kanuni zake unafanyika kabla ya mwezi Julai, 2019. Kama sheria zile zitarekebishwa mapema, malalamiko yote ambayo yapo kwa wavuvi hayatakuwepo kwa sababu wavuvi nao watakuwa wana haki ya kusema zile changamoto ambazo zinawakuta kwenye maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo napenda niwapongeze wenzetu hawa sekta ya mifugo na uvuvi ni kuanzisha Dawati la Sekta Binafsi. Hapa wananchi wanapata nafasi ya ku-*chip in.* Taasisi nyingi zimejihusisha kwenye sekta hii, kwa hiyo matatizo yote ya wafugaji na wavuvi yanaweza kutatuliwa kwenye Dawati hili na tumeliona hili jambo, ndiyo maana wamekuwa tayari hadi kuanzisha mchakato wa marekebisho ya sheria.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii tena kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Maji kwa kuleta Bungeni Muswada wa Sheria ya Huduma ya Majisafi na Usafi wa Mazingira ya mwaka 2018. Sheria hii itakaposainiwa na Mheshimiwa Rais itaboresha upatikanaji wa huduma ya majisafi na majitaka ambalo lilikuwa tatizo kubwa katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni imani yangu kuwa safari hii Serikali itakubaliana na mapendekezo ya Wabunge ya kuongeza shilingi 50 kwenye kila lita ya mafuta kwa maana ya petroli pamoja na dizeli. Tukiongeza shilingi 50 kwenye huu Mfuko wa Maji wa Taifa tutaweza kutunisha fedha zake ambapo utasaidia watu wengi katika vijiji waweze kupata maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii tena kuipongeza Serikali chini ya Rais wetu mzalendo Dkt. John Pombe Magufuli kwa hatua madhubuti alizochukua katika kuimarisha tasnia ya korosho. Ni matumaini yangu kuwa Wizara yenye dhamana itaendelea kushughulikia changamoto zilizobainika pamoja na ushauri wa Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hakuna jambo lolote muhimu katika nchi linaloweza kuendelea bila *research*. Ni wakati muafaka sasa hivi wa Serikali kutenga asilimia 1 ya *DGP* kwa ajili ya *research.* Kwenye eneo hili tunaiomba sana Serikali iondoe kigugumizi kwa sababu kumekuwa na malumbano katika *research.* Hakuna mtu anayekataza *research,* wafanye *research* na watuasaidie kuweka wazi kusudi tuweze kuwasaidia wakulima wetu katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba Bunge lako Tukufu liazimie hoja na Maazimio ya Kamati kama yalivyowasilishwa na Kamati.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Nakushukuru sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Mgimwa. *(Makofi)*

Kuna mambo mawili katika mapendekezo yenu, mojawapo ni la kuiomba Serikali huko tunakoenda kukubali ile hoja ya shilingi 50 kwenye mafuta ili tuingize kwenye Mfuko wa Maji. Tutakapofika kwenye bajeti Bunge lijalo basi Serikali ijue ni moja ya Maazimio ambayo tunaenda kuyaamulia sasa ili lifanyiwe kazi kwa sababu lengo lake ni jema kwa kweli ili tuwe na Mfuko wa Maji ambapo hakuna kusuasua. *(Makofi)*

La pili mmependekeza kwamba tuunde utaratibu fulani wa ufuatiliaji wa ahadi za Serikali. Ni kweli katika Mabunge ya wenzetu huwa kuna Kamati Maalum kabisa,

Kamati mojawapo ya Bunge inakuwa ni Kamati inayoitwa Kamati ya Ufuatiliaji wa Ahadi za Serikali; ahadi za Maazimio kama haya lakini Mawaziri wanapojibu maswali Bungeni na *forum* nyingine zozote ndani ya Bunge ahadi inatolewa, kazi ya Kamati ile ni kufuatilia utekelezaji wa ahadi zile. Kwa hiyo, tutaangalia na sisi kwetu kama awamu hii au tutakapobadili Kanuni basi ianze na Bunge la wenzetu litakalofuata. *(Makofi)*

Nizishukuru sana Kamati zote mbili kwa kazi nzuri ambayo wamefanya pia Waheshimiwa Mawaziri kwa uchangiaji mzuri mlioufanya. Sasa baada ya hoja hizi mbili kutolewa lazima tuzifanyie maamuzi. Kwa hiyo, ningependa niwahoji kama mnapokea taarifa hizi mbili pamoja na maoni na mapendekezo yake yapite kama Maazimio ya Bunge.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii na Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu Shughuli za Kamati kwa mwaka 2018 zilipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge wote wamekubaliana na maoni na mapendekezo ya Kamati zetu na kwa hiyo sasa ni Maazimio ya Bunge ambayo tunawapa wenzetu Serikalini ili sasa waangalie utekelezaji wa Maazimio hayo. *(Makofi)*

Vinginevyo niwashukuru tena Waheshimiwa Mawaziri na timu kutoka Wizara zote ambazo leo mlikuwa mnahusika na Kamati hizi mbili. Makatibu Wakuu na Wasaidizi wenu wote tunawashukuru sana. Mambo mengi yamejadiliwa hapa, naamini mmepata machagizo mapya ya kuweza kuyafanyia kazi yatakayowasaidia ili kuweza kutatua matatizo ya wananchi. Niwashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri, Naibu Mawaziri kwa kazi kubwa ambayo mmekuwa mkifanya mwaka mzima na Kamati zangu hizi na mmefika leo mpaka tumehitimisha jambo hili, ni jambo la kushukuru sana.

Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa kalenda ya leo imekamilika, nichukue nafasi hii sasa kusitisha shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 1.30 Usiku Bunge liliahirishwa hadi siku ya Jumanne, Tarehe 6 Februari, 2019, Saa Tatu Kamili Asubuhi)*